JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA KATIKA MWAKA 2023

Wizara ya Fedha
Dodoma-Tanzania
Juni, 2024

# YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... **viii**
**KIREFU/TAFSIRI YA MANENO** .......... **xii**
**MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KATIKA MWAKA 2023** .......... **xvi**
**SURA YA 1** .......... **1**
**HALI YA UCHUMI WA TAIFA** .......... **1**
Ukuaji wa Uchumi .......... 1
Mwenendo wa Mfumuko wa Bei .......... 7
Ukuzaji Rasilimali .......... 10
**SURA YA 2** .......... **36**
**FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA** .......... **36**
Ujazi wa Fedha .......... 36
Mikopo kwa Sekta Binafsi .......... 36
Amana katika Benki za Biashara .......... 38
Mwenendo wa Viwango vya Riba .......... 38
Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania .......... 38
**MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA** .......... **39**
Huduma za Benki .......... 39
Huduma za Mawakala wa Benki .......... 40
Mwenendo wa Viashiria vya Sekta ya Benki .......... 40
Maboresho katika Sekta ya Benki .......... 40
Huduma Ndogo za Fedha .......... 41
Huduma Jumuishi za Fedha .......... 41
Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana .......... 41
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma .......... 44
Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii .......... 45
Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi .......... 45
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya .......... 46
Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa .......... 48
Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania .......... 48
Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania .......... 50
**SURA YA 3** .......... **55**
**FEDHA ZA SERIKALI** .......... **55**
Utangulizi .......... 55
Mwenendo wa Mapato .......... 55
Mapato ya Ndani .......... 55
Mwenendo wa Matumizi .......... 57
Deni la Serikali .......... 58
Deni la Nje .......... 59
Deni la Ndani .......... 60
Tathmini ya Uhimilivu wa Deni .......... 60
**SURA YA 4** .......... **67**
**SEKTA YA NJE** .......... **67**
Bidhaa Zilizouzwa Nje .......... 67
Bidhaa Asilia .......... 67

Bidhaa Zisizo Asilia ........ 68
Mapato ya Huduma ........ 71
Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi ........ 71
Malipo ya Huduma ........ 72
Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali ........ 73
Mizania ya Malipo na Nchi za Nje ........ 78
Akiba ya Fedha za Kigeni ........ 79
**SURA YA 5 ........ 89**
**HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA ........ 89**
HALI YA UCHUMI WA DUNIA ........ 89
Mwenendo wa Biashara Duniani ........ 93
Ushirikiano wa Uchumi Kimataifa ........ 94
Ushirikiano wa Kiuchumi Barani Afrika ........ 96
Ushirikiano wa Kiuchumi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ........ 96
Ushirikiano wa Kiuchumi Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ........ 97
**SURA YA 6 ........ 99**
**RASILIMALI WATU ........ 99**
Idadi ya Watu ........ 99
Mgawanyiko wa Watu Kimkoa ........ 99
Mgawanyo wa Watu kwa Umri ........ 101
Nguvu Kazi na Ajira ........ 103
**SURA YA 7 ........ 106**
**KILIMO NA USHIRIKA ........ 106**
**UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO ........ 106**
Mazao ya Chakula ........ 106
Miundombinu ya Hifadhi ya Chakula ........ 106
Mazao ya Biashara ........ 107
Mazao ya Mbegu za Mafuta ........ 108
Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo ........ 108
Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao ........ 110
Huduma za Ugani ........ 111
Utafiti katika Uzalishaji wa Mazao ........ 112
Mafunzo ya Kilimo ........ 113
Umwagiliaji ........ 113
**MIFUGO ........ 113**
Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake ........ 113
Biashara ya Mifugo na Mazao yake ........ 115
Uzalishaji wa Chanjo za Mifugo ........ 117
Uzalishaji wa Malisho na Utengenezaji wa Vyakula vya Mifugo ........ 117
Mafunzo ya Mifugo ........ 118
Utafiti wa Mifugo ........ 118
**UVUVI ........ 119**
Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ........ 119
Ukuzaji Viumbe Maji ........ 120
Uvunaji wa Samaki ........ 121
Mwenendo wa Uuzaji na Uagizaji wa Mazao ya Uvuvi Nje ya Nchi ........ 122

Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi ... 122
Mafunzo ya Uvuvi ... 123
**MAENDELEO YA USHIRIKA ... 123**
**SURA YA 8 ... 134**
MISITU, WANYAMAPORI NA UTALII ... 134
Misitu na Nyuki ... 134
Upandaji wa Miti ... 134
Mauzo ya Bidhaa za Misitu Nje ya Nchi ... 135
Wanyamapori ... 136
Uwindaji wa Kitalii ... 137
Malikale ... 139
**SURA YA 9 ... 146**
**MADINI ... 146**
Leseni za Utafutaji na Uchimbaji wa Madini ... 146
Vibali vya Uuzaji wa Madini ... 146
Dhahabu ... 146
Almasi ... 147
Vito vya Thamani ... 147
Tanzanite ... 147
Makaa ya Mawe ... 147
Madini ya Jasi ... 147
Madini Mengine ... 148
Masoko ya Madini ... 148
**SURA YA 10 ... 152**
**VIWANDA NA BIASHARA ... 152**
Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani ... 152
Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ... 152
Usajili wa Biashara na Viwanda ... 154
Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa ... 155
Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo ... 155
Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia ... 157
Shirika la Maendeleo la Taifa ... 157
**SURA YA 11 ... 165**
**UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI ... 165**
**UJENZI ... 165**
Mtandao wa Barabara Nchini ... 165
Barabara, Madaraja, Vivuko na Magari ... 167
Mfuko wa Barabara ... 168
Nyumba na Majengo ya Serikali ... 168
Usajili wa Makandarasi ... 168
Usajili wa Wahandisi ... 169
Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ... 170
Baraza la Taifa la Ujenzi ... 170
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ... 171
**MAENDELEO YA ARDHI ... 171**
Utayarishaji wa Hatimiliki, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Utatuzi wa Migogoro ... 171

Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria ... 171
Uthamini wa Mali na Upimaji wa Mashamba na Viwanja ... 172
Mipango ya Matumizi ya Ardhi ... 173
Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa ... 176
Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ... 176
Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara ... 176
**SURA YA 12 ... 177**
**UCHUKUZI NA UHIFADHI MIZIGO ... 177**
Usafiri wa Barabara ... 177
Usafiri wa Anga ... 179
Usafiri wa Majini ... 180
Uchukuzi Kwenye Maziwa ... 184
Huduma za Hali ya Hewa ... 184
**SURA YA 13 ... 187**
**HABARI NA MAWASILIANO & SANAA NA BURUDANI ... 187**
MAWASILIANO ... 187
Huduma za Posta ... 187
Huduma za Simu ... 188
Huduma za Intaneti ... 188
Huduma za Utangazaji ... 189
Utoaji wa Leseni za Mawasiliano ... 189
Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ... 190
HABARI ... 190
SANAA NA BURUDANI ... 191
Maendeleo ya Sanaa ... 193
Maendeleo ya Michezo ... 195
**SURA YA 14 ... 198**
**NISHATI ... 198**
Ufuaji wa Umeme ... 198
Gesi Asilia ... 199
Uagizaji Mafuta ... 200
Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani ... 201
Mwenendo wa Bei za Mafuta ... 202
Nishati Jadidifu ... 204
Nishati mbadala ya Gesi inayotokana na Petroli ... 204
**SURA YA 15 ... 208**
**MAJI ... 208**
Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji ... 208
Ubora wa Maji ... 208
Huduma ya Maji Vijijini ... 209
Huduma ya Maji Mijini ... 210
Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa ... 212
Uondoaji wa Majitaka ... 212
**SURA YA 16 ... 216**
**ELIMU MAFUNZO YA UFUNDI NA TEKNOLOJIA ... 216**
Elimu ya Awali ... 216

Elimu ya Msingi ..... 216
Elimu ya Sekondari ..... 217
Elimu katika Vyuo vya Ualimu ..... 218
Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu ..... 218
Elimu ya Ufundi na Mafunzo ..... 219
Elimu ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ..... 219
Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ..... 220
Elimu ya Juu ..... 221
**SURA YA 17 ..... 227**
**AFYA NA MAENDELEO YA JAMII ..... 227**
**AFYA ..... 227**
Vituo vya Kutolea Huduma za Afya ..... 227
Dawa na Vifaa Tiba ..... 228
Afya ya Uzazi na Mtoto ..... 228
Huduma za Chanjo kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja ..... 229
Huduma za Matibabu ya Kibingwa ..... 229
Udhibiti wa Malaria ..... 230
Udhibiti wa Kifua Kikuu ..... 231
Lishe ..... 231
Mafunzo katika Kada za Afya ..... 231
**MAENDELEO YA JAMII ..... 232**
Ustawi wa Jamii ..... 232
Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ..... 232
Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ..... 233
Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto ..... 233
Ukatili wa kijinsia ..... 234
Huduma za Ustawi kwa Wazee ..... 234
Mashirika yasiyo ya kiserikali ..... 235
**SURA YA 18 ..... 239**
**MASUALA MTAMBUKA ..... 239**
Mazingira ..... 239
Ulinzi na Usalama wa Raia ..... 240
Utambuzi na Usajili wa Watu ..... 241
Udhibiti wa Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu ..... 242
Usajili, Ufilisi na Udhamini ..... 242
Maendeleo ya Sheria na Mahakama ..... 243
Utawala Bora ..... 244
**HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU ..... 245**
Jitihada za Kupunguza Umaskini ..... 245
Maendeleo ya Watu ..... 247
**SURA YA 19 ..... 248**
**UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI ..... 248**
Usajili wa Miradi ya Uwekezaji ..... 248
Mgawanyiko wa Usajili wa Miradi Kisekta ..... 248
Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa ..... 249
Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje ..... 250

Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje ........ 250
Mazingira ya Biashara na Uwekezaji ........ 252
Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ........ 254
Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati ........ 256
Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ........ 257
**SURA YA 20 ........ 260**
Utangulizi ........ 260
Mfumo wa Elimu Kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ........ 260
Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ........ 261
Utofauti wa Idadi ya Wahitimu na Fursa za Ajira ........ 268
Changamoto za Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ........ 269
Malengo na Mahitaji ya Kuboresha Sera ya Elimu ........ 269
Malengo ya Kuboresha Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ........ 269
Mahitaji ya Kuboresha Sera ya Elimu 2014 ........ 270
Maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ........ 270
Hatua za Utekelezaji wa Maboresho ya Mfumo wa Elimu ........ 273
Utaratibu wa Utekelezaji wa Maboresho ya Mfumo wa Elimu ........ 273
Umuhimu wa Maboresho ya Mfumo wa Elimu katika Kujenga Nchi ........ 274
Hitimisho ........ 275

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Ukurasa**

Jedwali A: TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA....................xvii
Jedwali B: MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI MKUU NA BAJETI............xviii
Jedwali Na. 1: PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA) ..................................................12
Jedwali Na. 2: PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA).........................................................................................13
Jedwali Na. 3: PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA) ..................................................14
Jedwali Na. 4: PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA).........................................................................................15
Jedwali Na. 5: PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO (KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)...........................................................................16
Jedwali Na. 6: PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI (BEI ZA MWAKA 2015)...................................................................................................17
Jedwali Na. 7: PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (BEI ZA MWAKA 2015)......18
Jedwali Na. 8: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI (BEI ZA MWAKA 2015)..........................................................................................19
Jedwali Na. 9: PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (BEI ZA MWAKA 2015)......21
Jedwali Na. 10: PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO (BEI ZA MWAKA 2015)..........................................................................................22
Jedwali Na. 11: UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI ( BEI YA MIAKA INAYOHUSIKA).........................................................................................23
Jedwali Na. 12: UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (BEI ZA MWAKA 2015)...................................................................................................24
Jedwali Na. 13: MCHANGO KATIKA RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA) ..................................................................25
Jedwali Na. 14: UKUZAJI WA RASILIMALI KATIKA SEHEMU ZA UCHUMI WA KITAIFA NA BINAFSI (KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA) .........................26
Jedwali Na. 15: FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA YA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (Des. 2015=100) ...27
Jedwali Na. 16: FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIKAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 = 100) ......28

Jedwali Na. 17: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (Des 2015 =100)................29
Jedwali Na. 18: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 =100).........30
Jedwali Na. 19: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 =100)...........31
Jedwali Na. 20: FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Des. 2015=100) ............................................................32
Jedwali Na. 21: FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Des. 2020=100).....................33
Jedwali Na. 22: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Des 2015 = 100) ......................34
Jedwali Na. 23: FAHIRISI ZA BEI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA ( Des. 2015=100) ....................................................................................................35
Jedwali Na. 24: MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA.....................................................................................................51
Jedwali Na. 25: VIWANGO VYA UKUAJI WA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA ..................................................................................................................52
Jedwali Na. 26: MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI.......................................................................53
Jedwali Na. 27: MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA ................53
Jedwali Na. 28: VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA .....................................................54
Jedwali Na. 29: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI ..................63
Jedwali Na. 30: MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI............................................................................................................65
Jedwali Na. 31: THAMANI YA BIASHARA YA BIDHAA BAINA YA TANZANIA NA NCHI NYINGINE..........................................................................................80
Jedwali Na. 32: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE .........81
Jedwali Na. 33: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE ......................................................................82
Jedwali Na. 34: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE ..................................................................................................................85
Jedwali Na. 35: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI ..................................................................................................................86
Jedwali Na. 36: MIZANIA YA MALIPO MWAKA 2019 - 2023 ...........................................87
Jedwali Na. 37: IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA MWAKA 2017 - 2023 ................................................................................................................104
Jedwali Na. 38: UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI .......................................125
Jedwali Na. 39: PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI .................................126

Jedwali Na. 40: ENEO LILILOPANDWA CHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA ........................................................... 127
Jedwali Na. 41: KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI ............................. 128
Jedwali Na. 42: ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA .... 129
Jedwali Na. 43: MAUA YA PARETO YALIYONUNULIWA NA MAUZO YA BIDHAA ZA PARETO NCHINI ........................................................... 130
Jedwali Na. 44: UZALISHAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI MWAKA 2010 - 2023 ......... 131
Jedwali Na. 45: MWENENDO WA UUZAJI WA SAMAKI NJE YA NCHI ....................... 132
Jedwali Na. 46: MAUZO YA SANGARA NJE YA NCHI MWAKA 2008 - 2023 ............... 133
Jedwali Na. 47: WATALII WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA KATIKA MWAKA 2010 - 2023 ........................................................... 142
Jedwali Na. 48: MAUZO YA BIDHAA ZA MISITU KATIKA MASOKO YA NCHI ZA NJE KWA MWAKA 2023 ........................................................... 143
Jedwali Na. 49: MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII 2016 - 2023 .......................... 144
Jedwali Na. 50: WATALII WALIOTEMBELEA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO ........................................................... 145
Jedwali Na. 51: UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA ....................... 150
Jedwali Na. 52: THAMANI YA MADINI YALIYOTOLEWA VIBALI KWA AJILI YA KUUZWA NJE YA NCHI ........................................................... 151
Jedwali Na. 53: MATUMIZI YA SARUJI NCHINI ........................................................... 159
Jedwali Na. 54: UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI ........................ 160
Jedwali Na. 55: VIWANDA: IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA .................................. 161
Jedwali Na. 56: VIWANDA: GHARAMA ZA KAZI ........................................................... 162
Jedwali Na. 57:VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO ............................................. 163
Jedwali Na. 58: VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA ........................... 164
Jedwali Na. 59: SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)+ ............................................ 186
Jedwali Na. 60: HUDUMA ZA POSTA ........................................................... 196
Jedwali Na. 61: IDADI YA KADI ZA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI ..................... 197
Jedwali Na. 62: UWEZO WA MITAMBO YA KUFUA UMEME NCHINI NA UPATIKANAJI WA UMEME MWAKA 2023 ........................................... 205
Jedwali Na. 63: MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI MWAKA 2023 (Saa za Gigawati) ........................................................... 206
Jedwali Na. 64: MAUZO YA UMEME KWA MIKOA MWAKA 2023 (GWh) .................. 207
Jedwali Na. 65: UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYONA MAJI MIJINI ........................................................... 213
Jedwali Na. 66: MAHITAJI NA KIWANGO CHA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI MWAKA 2023 ........................................................... 215
Jedwali Na. 67: SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO ........................................................... 223

Jedwali Na. 68: SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO....224
Jedwali Na. 69: IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA ....225
Jedwali Na. 70: IDADI YA TAASISI ZA ELIMU....226
Jedwali Na. 71: IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA....236
Jedwali Na. 72: IDADI YA VITANDA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NCHINI ....237
Jedwali Na. 73: KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA: MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA MWAKA 2022 - 2023 ....258

## KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

| | |
|---|---|
| AfCFTA | African Continental Free Trade Area (Eneo Huru la Biashara Afrika) |
| AGTIF | Agricultural Input Trust Fund (Mfuko wa Pembejeo za Kilimo) |
| ASA | Agricultural Seed Agency (Wakala wa Mbegu za Kilimo) |
| ATCL | Air Tanzania Company Limited (Kampuni ya Ndege Tanzania) |
| AWCCSP | African Women Clean Cooking Support Programme (Mpango wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa Wanawake wa Afrika) |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| BASATA | Baraza la Sanaa la Taifa |
| BMT | Baraza la Michezo la Taifa |
| BRELA | Business Registrations and Licensing Agency (Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni) |
| CAMARTEC | Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology (Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini) |
| CBE | College of Business Education (Chuo cha Elimu ya Biashara) |
| COASCO | Co-operative Audit and Supervision Corporation (Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika) |
| COSOTA | Chama cha Hakimiliki Tanzania |
| DSE | Dar es Salaam Stock Exchange (Soko la Hisa la Dar es Salaam) |
| EAC | The East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki) |
| FETA | Fisheries Education and Training Agency (Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi) |
| GDP | Gross Domestic Product (Pato la Taifa) |
| GWh | Gigawatt hour (Saa za Gigawati) |
| iCHF | Improved Community Health Fund (Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa) |
| IMF | International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa) |
| FCC | The Fair Competition Commission (Tume ya Ushindani) |

| | |
|---|---|
| LATRA | Land Transport Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini) |
| LPG | Liquified Petroleum Gas (Gesi inayotokana na Petroli) |
| HDI | Human Development Index (Fahirisi ya Maendeleo ya Watu) |
| M1 | Narrow Money Supply (Ujazi wa fedha kwa Tafsiri Finyu) |
| M2 | Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana) |
| M3 | Extended Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi) |
| MKUMBI | Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara |
| MPRU | Marine Parks and Reserves Tanzania (Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu) |
| MSCL | Marine Services Company Limited (Kampuni ya Huduma za Meli) |
| NACTVET | The National Council for Technical and Vocational Education and Training (Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi) |
| NDC | The National Development Corporation (Shirika la Maendeleo la Taifa) |
| NEDF | National Entrepreneurship Development Fund (Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali) |
| NFRA | National Food Reserve Agency (Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula) |
| NSSF | National Social Security Fund (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii) |
| NTB | Non-tariff Barriers (Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Kiforodha) |
| OPV | Oral Polio Vaccine |
| PPP | Public Private Partnership (Ubia kati ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi) |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma) |
| SADC | The Southern African Development Community (Jumuiya ya maendeleo Kusini mwa Afrika) |
| SIDO | Small Industries Development Organization (Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo) |
| TADB | Tanzania Agricultural Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania) |

| | |
|---|---|
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TMA | Tanzania Meteorological Authority (Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania) |
| TANESCO | Tanzania Electricity Supply Company (Shirika la Ugamvi wa Umeme Tanzania) |
| TANIPAC | Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination (Mradi wa Kuzuia Sumu Kuvu) |
| TANROADS | Tanzania National Roads Agency (Wakala wa Barabara Tanzania) |
| TARI | Tanzania Agricultural Research Institute (Taaasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania) |
| TARURA | Tanzania Rural and Urban Roads Agency (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini) |
| TASAC | Tanzania Shipping Agency Corporation (Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania) |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund (Mfuko wa Maendeleo ya Jamii) |
| TAZARA | Tanzania Zambia Railway Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia) |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards (Shirika la Viwango Tanzania) |
| TCAA | Tanzania Civil Aviation Authority (Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania) |
| TDCs | Technology Development Centres (Vituo vya Uendelezaji Teknolojia) |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TelW | Tanzania Electronic Investment Window (Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji) |
| TEMDO | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation (Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania) |
| TEMESA | Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency (Wakala wa Ufundi na Umeme) |
| TIC | Tanzania Investment Centre (Kituo cha Uwekezaji Tanzania) |
| TIRDO | Tanzania Industrial Research and Development Organization (Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania) |

| | |
|---|---|
| TMX | Tanzania Merchantile Exchange (Soko la Bidhaa Tanzania) |
| TNBC | Tanzania National Business Council (Baraza la Taifa la Biashara) |
| TanTrade | Tanzania Trade Development Authority (Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania) |
| TOSCI | Tanzania Official Seed Certification Institute (Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania) |
| TPA | Tanzania Ports Authority (Mamlaka ya Bandari Tanzania) |
| TRA | Tanzania Revenue Authority (Mamlaka ya Mapato Tanzania) |
| TRC | Tanzania Railway Corporation (Shirika la Reli Tanzania) |
| TVLA | Tanzania Veterinary Laboratory Agency (Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania) |
| UCSAF | The Universal Communications Service Access Fund (Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote) |
| UNDP | United Nations Development Programme (Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa) |
| VETA | Vocational Education and Training Authority (Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi) |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |
| WCF | Workers Compensation Fund (Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi) |
| WEO | World Economic Outlook |
| WMA | Weight and Measurement Agency (Wakala wa Vipimo) |
| WTO | The World Trade Organization (Shirika la Biashara Duniani) |
| WTTC | The World Travel & Tourism Council (Baraza la Wasafiri na Utalii Duniani) |

## MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KATIKA MWAKA 2023

| Na. | Tarehe | Mwezi | Tukio |
|---|---|---|---|
| 1. | 18 | Machi | Kufanyika kwa mara ya kwanza kwa zoezi la tathmini ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni (Crediting Rating) na kampuni za kimataifa za *Moody's Investors Services* na *Fitch Ratings.* |
| 2. | 03 | Aprili | Mchakato wa kuandaa Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo (Vision 2050) ulizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philipo Isdor Mpango. |
| 3. | 15 | Juni | Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2023/24. |
| 4. | 16 | Juni | Benki Kuu ya Marekani yatangaza rasmi kupandisha riba kwa ajili ya kukabiliana na mfumuko wa bei za huduma na bidhaa. Hatua hiyo ilichangia kuongezeka kwa gharama za mikopo katika masoko ya fedha ya kimataifa. |
| 5. | 5 - 8 | Septemba | Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika Mwaka 2023 (Africa's Food Systems Forum 2023), chini ya Uenyekiti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. |
| 6. | 25 | Septemba | Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilianza kutekeleza Mpango wa Ndani wa Ununzi wa Dhahabu kwa ajili ya kuimarisha hifadhi ya fedha za kigeni. |
| 7. | 01 | Novemba | Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote wa Mwaka 2022. |
| 8. | 02 | Novemba | Kuidhinishwa kwa Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 na Mitaala ya Elimu Ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu. |

## Jedwali A: TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA

| Maelezo | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watu Tanzania Bara (Milioni) | 52.6 | 54.3 | 55.9 | 57.7 | 59.9 | 61.7 | 3.0 |
| Pato la Taifa kwa Bei za miaka inayohusika (Sh. Milioni)* | 123,997,772 | 134,540,194 | 145,384,353 | 156,167,137 | 170,820,032 | 188,588,052 | 10.4 |
| Pato la Taifa kwa Bei za mwaka 2015 (Sh. Milioni) | 115,174,468 | 123,193,239 | 128,723,538 | 134,951,513 | 141,247,193 | 148,399,757 | 5.1 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika (Sh.) | 2,452,406 | 2,573,324 | 2,653,790 | 2,708,999 | 2,854,072 | 3,055,606 | 7.1 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za 2015 (Sh.) | 2,188,195 | 2,269,888 | 2,306,682 | 2,346,983 | 2,370,418 | 2,405,182 | 1.5 |
| Kasi ya Upandaji Bei (asilimia) | 3.5 | 3.4 | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8 | -11.6 |
| Urari wa Biashara ya Bidhaa (US$ milioni) | -4,227.00 | -3,237.60 | -1,460.00 | -3,247.70 | (6,984.9) | (6,032.3) | -13.6 |
| Saruji Iliyotumika (Tani ) | 4,577,117 | 6,104,108 | 5,887,775 | 6,863,004 | 7,532,173 | 7,950,515 | 5.6 |
| Umeme Uliouzwa (GWH)* | 6,290.7 | 6,642.6 | 6,674.3 | 7,313.20 | 7,729.60 | 8,232.00 | 6.5 |
| Utalii (Mapato US$ milioni) | 2,433 | 2,604 | 715 | 1,248 | 2,527.8 | 3,373.8 | 33.5 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Msingi ('000) * | 10,112 | 10,605 | 10,925 | 11,196.80 | 11,420.97 | 11,425.48 | 0.0 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Sekondari ('000) * | 2,149 | 2,338 | 2,473 | 2,671.90 | 2,823.60 | 3,077.36 | 9.0 |
| Hospitali: Idadi ya Vitanda | 62,203 | 80,164 | 84,162 | 86,131 | 104,687 | 125,500 | 19.9 |
| **Mauzo Nje ya Mazao Muhimu ya Biashara (Mil. US$)** | | | | | | | |
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | |
| Kahawa | 148 | 152.2 | 145 | 155.2 | 161.2 | 227.9 | 41.4 |
| Pamba | 68.38 | 91.8 | 87.5 | 81.3 | 103.4 | 101.9 | -1.5 |
| Katani | 32.54 | 19.3 | 17.6 | 20.2 | 24.3 | 20.4 | -16.0 |
| Chai | 45.82 | 45.7 | 32.4 | 32.9 | 30.0 | 31.1 | 3.7 |
| Tumbaku | 269.95 | 146.5 | 148.7 | 127.5 | 178.5 | 340.4 | 90.7 |
| Korosho | 109.56 | 353.1 | 359.6 | 159 | 226.9 | 206.4 | -9.0 |
| Karafuu | 0.36 | 9.1 | 17.1 | 51.8 | 42.1 | 25.1 | -40.4 |
| **Bidhaa zisizo Asilia** | | | | | | | |
| Madini | 1615.4 | 2,326.70 | 3369.1 | 3,116.4 | 3,395.3 | 3,551.4 | 4.6 |
| Bidhaa za Viwanda | 894.29 | 851.8 | 908.6 | 1,200.0 | 1,419.2 | 1,363.3 | -3.9 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | 181.85 | 168 | 139.6 | 164.3 | 168.2 | 164.0 | -2.5 |
| Mazao ya Mboga na Maua | 147.7 | 202.4 | 274.1 | 378.6 | 289.6 | 417.2 | 44.1 |
| Bidhaa zilizouzwa tena (Re-export) | 186.71 | 242.8 | 87.7 | 90.2 | 131.2 | 135.2 | 3.0 |
| Bidhaa nyinginezo | 340.4 | 394.3 | 474.2 | 813.5 | 654.9 | 690.5 | 5.4 |
| **Ujazi wa Fedha** | | | | | | | |
| Ujazi wa Fedha - M3 (Sh. bilioni) | 25,823.50 | 28,313.10 | 29,920.60 | 34,558.00 | 38,580.00 | 44,002.60 | 14.1 |
| Karadha (Sh. bilioni) | 26,249.30 | 28,103.30 | 26,139.60 | 30,030.50 | 37,557.30 | 43,411.50 | 15.6 |
| **Fedha za Serikali** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24P** | **Badiliko (Asilimia)** |
| Mapato ya Ndani ya Serikali (Sh. milioni) | 18,527,293 | 21,051,755 | 20,594,735 | 24,395,567 | 27,053,777 | 30,503,027 | 12.7 |
| Matumizi ya Kawaida ya Serikali (Sh. milioni) | -13,811,190 | -14,201,148 | -14,883,723 | -15,817,056 | -19,043,025 | -23,872,264 | 25.4 |
| Matumizi ya Maendeleo ya Serikali (Sh. milioni) | -8,454,182 | -9,926,993 | -11,701,584 | -15,080,341 | -15,006,002 | -13,331,811 | -11.2 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha
*Takwimu zimeboreshwa

## Jedwali B: MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI MKUU NA BAJETI

| **Mwaka wa Kalenda** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **PATO LA TAIFA** | | | | | | |
| Ukuaji halisi wa Pato la Taifa (mp) | 7.0% | 6.9% | 4.5% | 4.8% | 4.7% | 5.1% |
| Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika (mp) | 4.4% | 8.5% | 8.1% | 7.4% | 9.4% | 10.4% |
| Uwiano wa Uwekezaji na Pato la Taifa (Investment/GDP)* | 32.8% | 34.3% | 38.5% | 40.8% | 39.3% | 37.8% |
| Uwiano wa Akiba kwenye Benki na Pato la Taifa (Savings/GDP) | 20.5% | 21.0% | 20.9% | 21.1% | 20.9% | 24.3% |
| **MWENENDO WA BEI NA VIWANGO VYA RIBA** | | | | | | |
| Kasi ya Upandaji wa Bei (mwisho wa kipindi) | 3.3% | 3.8% | 3.2% | 4.2% | 4.8% | 3.0% |
| Kasi ya Upandaji wa Bei (wastani wa mwaka) | 3.5% | 3.4% | 3.3% | 3.7% | 4.3% | 3.8% |
| GDP deflator Inflation (bp) | -2.1% | 2.0% | 3.0% | 2.3% | 4.2% | 3.9% |
| GDP deflator Inflation (MP) | -2.4% | 1.5% | 3.4% | 2.5% | 4.5% | 6.7% |
| Riba za Mikopo (mwaka mmoja) | 18.3% | 18.2% | 16.7% | 15.7% | 16.4% | 16.8% |
| Riba za Amana za muda maalum (miezi 12) | 11.7% | 8.8% | 8.8% | 8.3% | 8.3% | 8.5% |
| Tofauti ya riba za amana na za mikopo (mwaka) | 6.6% | 9.5% | 7.9% | 7.5% | 8.1% | 8.3% |
| Thamani ya Tshs/Dola (wastani wa mwaka) | 2,275.4 | 2,299.79 | 2,305.6 | 2,309.2 | 2,314.5 | 2,395.7 |
| **UJAZI WA FEDHA** | | | | | | |
| Kiwango cha ukuaji wa M3 | 4.5% | 9.6% | 5.7% | 15.5% | 11.6% | 14.1% |
| Kiwango cha ukuaji wa M2 | 3.8% | 11.8% | 8.2% | 17.6% | 12.1% | 11.9% |
| Mikopo Chechefu | 10.7% | 9.8% | 9.8% | 8.5% | 5.8% | 4.3% |
| Kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi | 4.9% | 11.1% | 3.1% | 10.0% | 22.5% | 17.1% |
| **UWIANO WA MIZANIA YA MALIPO YA NJE NA PATO LA TAIFA** | | | | | | |
| Bidhaa zilizouzwa nje | 8.1% | 7.2% | 8.5% | 9.4% | 9.1% | 8.8% |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 15.0% | 14.0% | 15.2% | 12.6% | 13.3% | 14.6% |
| Bidhaa zilizonunuliwa kutoka nje | 13.1% | 14.3% | 13.6% | 11.5% | 13.5% | 17.4% |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 16.7% | 17.6% | 16.4% | 13.4% | 15.6% | 20.4% |
| Urari wa malipo ya kawaida | -2.7% | -3.9% | -2.1% | -2.1% | -3.2% | -6.8% |
| Akiba ya fedha za kigeni (miezi) | 4.6 | 5.9 | 5.3 | 6.2 | 4.7 | 4.5 |
| **UWIANO WA BAJETI YA SERIKALI NA PATO LA TAIFA** | | | | | | |
| **Mwaka wa fedha** | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** |
| Mapato ya ndani | 14.8% | 14.3% | 15.0% | 13.7% | 14.9% | 14.6% |
| Mapato ya kodi | 12.4% | 11.9% | 12.5% | 11.5% | 12.3% | 11.9% |
| Matumizi (Bila rollover) | 16.8% | 17.2% | 17.2% | 17.6% | 19.0% | 19.2% |
| Matumizi ya kawaida | 10.2% | 10.7% | 10.1% | 9.9% | 9.8% | 11.4% |
| Matumizi ya maendeleo | 6.6% | 6.5% | 7.1% | 7.8% | 9.2% | 7.8% |
| Misaada | 0.8% | 0.4% | 0.7% | 0.5% | 0.4% | 0.3% |
| Nakisi (kabla ya misaada) | -2.7% | -3.6% | -2.6% | -4.5% | -4.1% | -4.6% |
| Nakisi (baada ya misaada) | -1.9% | -3.3% | -1.9% | -4.0% | -3.6% | -4.3% |
| Mikopo ya nje | 1.4% | 0.9% | 1.7% | 1.8% | 1.9% | 1.7% |
| Mikopo ya ndani (kutoka benki) | -0.3% | 1.8% | -0.3% | 1.2% | 1.1% | 0.8% |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha



## Sehemu ya Kwanza

# Maendeleo ya Uchumi Jumla

## SURA YA 1


## HALI YA UCHUMI WA TAIFA

**Ukuaji wa Uchumi**

1. Mwaka 2023, Pato halisi la Taifa lilifikia shilingi bilioni 148,399.76 kutoka shilingi bilioni 141,247.19 mwaka 2022, sawa na ukuaji wa asilimia 5.1 ikilinganishwa na asimilia 4.7 mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na: jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ikiwemo mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Ukraine na Urusi pamoja na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu na usafirishaji; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe; na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi iliyochachua shughuli za kiuchumi. Hata hivyo, kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa cha asilimia 5.1 mwaka 2023 kipo chini ya lengo la mwaka la asilimia 5.2. Hii ilitokana na: kupanda kwa gharama za uzalishaji katika baadhi ya sekta; mabadiliko ya tabianchi yaliyoathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa baadhi ya maeneo nchini na kuharibu miundombinu ikiwemo madaraja na barabara; pamoja na hatua zilizochukuliwa na nchi zilizoendelea katika kukabiliana na mfumuko wa bei zilizosababisha kuongezeka kwa gharama za mikopo kutoka masoko ya kimataifa ya fedha na hivyo kuathiri shughuli za uzalishaji.


**Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi na Mchango wa Ukuaji katika kila Robo Mwaka (2019 - 2023)**

**Asilimia**




2. Mwaka 2023, sekta ya sanaa na burudani iliongoza kwa kuwa na ukuaji wa asilimia 17.7 ikifuatiwa na sekta ya fedha na bima asilimia 12.2, madini asilimia 11.3, malazi na huduma za chakula asilimia 8.3 pamoja na habari na mawasiliano asilimia 7.6 **(Kielelezo Na. 1.2).** Aidha, shughuli ya kilimo iliongoza kwa kuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa wa asilimia 26.5 ikifuatiwa na ujenzi asilimia 13.2, madini asilimia 9.0 na biashara na matengenezo asilimia 8.3 **(Kielelezo Na. 1.3).**

**Kielelezo Na. 1.2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi (Asilimia)**





**Kielelezo Na. 1.3: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa Mwaka 2023 (Asilimia)**



3. Licha ya kuwa na ukuaji mkubwa, shughuli za sanaa na burudani zilikuwa na mchango mdogo katika ukuaji wa Pato la Taifa. Hii imetokana na kuwa sekta hii imeajiriri watu wachache wanaojishughulisha na kazi mbalimbali za sanaa ikilinganishwa na shughuli nyingine za uchumi. Kazi hizo ni pamoja na maigizo, tamthilia, muziki, uchongaji, uchoraji, na ushonaji. Aidha, shughuli za kilimo, madini, ujenzi na fedha na bima zimeendelea kuwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi kutokana na shughuli hizo kuwa na pato kubwa na kuhusisha sehemu kubwa ya jamii mijini na vijijini. Mchango wa shughuli za uchumi katika ukuaji wa Pato la Taifa ni kama unavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.4.**

**Kielelezo Na. 1.4: Mchango wa Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa Mwaka 2023**




4. Mwaka 2023, Pato ghafi la Taifa (kwa bei za mwaka husika) lilikuwa shilingi bilioni 188,588.05 ikilinganishwa na shilingi bilioni 170,820.03 mwaka 2022. Aidha, Tanzania Bara ilikuwa na wastani wa watu 61,718,700 mwaka 2023 ikilinganishwa na watu 59,851,347 mwaka 2022. Hivyo, Pato la Taifa kwa Mtu (GDP per capita) mwaka 2023 lilikuwa wastani wa shilingi 3,055,606 ikilinganishwa na shilingi 2,854,072 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Kiasi hicho ni sawa na dola za Marekani 1,275.5 kwa mtu mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,233.1 kwa mtu mwaka 2022.

5. Mwaka 2023, ukuaji wa shughuli za kilimo ambazo zinajumuisha kilimo cha mazao, mifugo, misitu na uvuvi ulikuwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kutoa ruzuku ya mbolea na hivyo kuwezesha wakulima kupata mbolea kwa bei nafuu pamoja na upatikanaji wa mvua za kutosha na za wakati katika maeneo mengi ya uzalishaji. Aidha, shughuli za mifugo zilikuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji cha asilimia 5.0 ikifuatiwa na misitu (asilimia 4.3), uzalishaji mazao

(asilimia 4.2) na uvuvi (asilimia 1.4) ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0, asilimia 3.1, asilimia 2.7 na asilimia 1.9 mtawalia mwaka 2022.

6. Mwaka 2023, shughuli za kilimo sehemu ya kuuza ilikuwa na ukuaji wa asilimia 4.2 na sehemu isiyo ya kuuza asilimia 4.5 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.3 kwa sehemu ya kuuza na asilimia 3.5 sehemu isiyo ya kuuza mwaka 2022. Aidha, sehemu ya kuuza kwa shughuli za mifugo ilikua kwa asilimia 5.0, misitu asilimia 4.3, uzalishaji mazao asilimia 4.2 na uvuvi asilimia 1.4 kama ilivyokuwa kwa sehemu isiyo ya kuuza.

7. Mwaka 2023, mchango wa shughuli za kilimo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 26.5 ikilinganishwa na asilimia 26.2 mwaka 2022. Aidha, shughuli ndogo za mazao zilichangia asilimia 16.1 katika Pato la Taifa, mifugo (asilimia 6.2), misitu (asilimia 2.5) na uvuvi (asilimia 1.7) mwaka 2023 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 15.0, asilimia 6.7, asilimia 2.7 na asilimia 1.8 mtawalia mwaka 2022.

8. Mwaka 2023, kiwango cha ukuaji wa shughuli za uchimbaji madini na mawe kilikuwa asilimia 11.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 10.8 mwaka 2022. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan makaa ya mawe, jasi, chumvi, almasi, mawe ya chokaa na shaba. Aidha, mchango wa shughuli za uchimbaji madini na mawe kwenye Pato la Taifa ulikuwa asilimia 9.0 mwaka 2023 kama ilivyokuwa mwaka 2022.

9. Mwaka 2023, kiwango cha ukuaji wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani kilikuwa asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za viwandani hususan katika soko la ndani kufuatia mwitikio wa wananchi kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini. Aidha, mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.0 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2022.

10. Mwaka 2023, kiwango cha ukuaji wa shughuli za ufuaji, usafirishaji na usambazaji umeme kilikuwa asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 7.6 mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na uchakavu wa njia za kusambaza umeme zilizosababisha upotevu wa umeme wakati wa usafirishaji pamoja na kuzimwa kwa baadhi ya mitambo ili kupisha ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji. Mchango wa shughuli za umeme kwenye Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.02 ikilinganishwa na asilimia 0.15 mwaka 2022.

11. Mwaka 2023, kiwango cha ukuaji wa shughuli za usambazaji maji na udhibiti majitaka kilikuwa asilimia 2.5 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2022. Hii ilichangiwa na uharibifu wa miundombinu ya maji kutokana na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha mvua zilizozidi wastani katika baadhi ya maeneo. Mchango wa shughuli za usambazaji maji na udhibiti majitaka katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.5 mwaka 2023 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Aidha, shughuli za usambazaji maji na udhibiti wa majitaka kwa sehemu

inayouzika na isiyouzika zilikua kwa asilimia 2.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.5 mwaka 2022.

12. Mwaka 2023, shughuli za ujenzi zilikua kwa asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 3.9 mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na kuendelea kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege, reli, ofisi za Serikali, madarasa, vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na nyumba za makazi na biashara. Kwa upande mwingine, shughuli za ujenzi sehemu inayouzika ilikua kwa asilimia 3.7 na sehemu isiyouzika ilikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.6 mwaka 2023. Pamoja na kasi ndogo ya ukuaji, shughuli za ujenzi ni za pili kwa kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa wa asilimia 13.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 13.7 mwaka 2022.

13. Mwaka 2023, kiwango cha ukuaji wa shughuli za biashara na matengenezo kilikuwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na asilimia 3.9 mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya ufanyaji biashara nchini, kuimarika kwa upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi pamoja na kuimarika kwa biashara za kikanda baada ya kulegezwa kwa vikwazo vya kibiashara. Aidha, mchango wa shughuli za biashara na matengenezo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2022.

14. Mwaka 2023, shughuli za huduma za malazi na chakula zilikua kwa asilimia 8.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.0 mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, hususan utalii kufuatia hatua zilizoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo utangazaji wa utalii kupitia Programu ya Tanzania - The Royal Tour na uboreshwaji wa miundombinu ya utalii. Aidha, mchango wa shughuli za huduma za malazi na chakula katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 1.1 mwaka 2022.

15. Mwaka 2023, shughuli za usafirishaji na uhifadhi mizigo zilikua kwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2022. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa abiria na shehena za mizigo iliyohudumiwa katika bandari na kusafirishwa kwa njia ya barabara, reli na anga. Mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 7.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2022.

16. Shughuli za habari na mawasiliano zinajumuisha huduma za utayarishaji, uchapishaji na usambazaji wa taarifa mbalimbali kupitia vyombo vya habari kama vile radio, magazeti, luninga, tovuti pamoja na huduma za mawasiliano kwa njia ya simu. Mwaka 2023, shughuli hizo zilikua kwa asilimia 7.6 ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2022. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za simu za viganjani na mitandao ya

kijamii nchini katika kuwasiliana na kupata habari na matukio mbalimbali, kuongezeka kwa matumizi ya njia za mitandao katika kufanya mikutano, pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wateja waliopata huduma za fedha kupitia mitandao ya simu na huduma za utangazaji na inteneti. Aidha, mchango wa shughuli hizi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2022.

17. Mwaka 2023, shughuli za huduma za fedha na bima zilikua kwa asilimia 12.2 ikilinganishwa na asilimia 9.2 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa kiwango cha amana na mikopo kwa sekta binafsi, kupungua kwa mikopo chechefu, kupanuka kwa huduma za shughuli za bima pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kulikochangia kuongezeka mahitaji ya huduma za fedha. Mchango wa shughuli za huduma za fedha na bima katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 4.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2022.

18. Mwaka 2023, shughuli za upangishaji majengo zilikua kwa asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2022. Ukuaji huo ulitokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya nyumba kwa ajili ya makazi, biashara na ofisi, hususan maeneo ya mijini. Aidha, shughuli za upangishaji majengo kwa sehemu inayouzika na sehemu isiyouzika zilikua kwa asilimia 4.3 mwaka 2023. Vile vile, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.8 mwaka 2022.

19. Mwaka 2023, shughuli za utawala wa umma na ulinzi zilikua kwa asilimia 5.5 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2022. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa ulipaji wa malimbikizo ya madai ya wafanyakazi, utekelezaji wa kazi za ulinzi na usalama na uendeshaji wa shughuli za Serikali. Hata hivyo, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulipungua kufikia wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2022.

20. Mwaka 2023, ukuaji wa shughuli za huduma za utawala na usaidizi ulikuwa asilimia 5.0 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2022. Shughuli hizo zinajumuisha ukodishaji wa vifaa, mashine na mitambo, utafutaji wa ajira, huduma za utalii, utoaji huduma ofisini, uwakala wa kampuni za usafiri na haki ya kutumia matokeo ya kitaaluma. Mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.5 mwaka 2022.

21. Mwaka 2023, ukuaji wa shughuli za utoaji huduma za elimu ulikuwa asilimia 6.2 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2022. Ukuaji huo ulitokana na juhudi za Serikali kwa kushirikiana na wadau katika kuboresha miundombinu ya elimu, kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari pamoja na kuajiri waalimu. Aidha, shughuli za huduma za elimu zilichangia asilimia 2.2 katika Pato la Taifa mwaka 2023 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Kwa upande mwingine, shughuli za kitaaluma, sayansi na

ufundi zilikua kwa asilimia 5.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2022. Vile vile, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.7 mwaka 2023 kama ilivyokuwa mwaka 2022.

22. Shughuli za huduma za afya na maendeleo ya jamii zilikua kwa asilimia 6.0 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2022. Ukuaji huo ulitokana na kuendelea kuboreshwa kwa utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote za kutolea huduma. Aidha, mchango wa shughuli za huduma za afya na maendeleo ya jamii katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.4 mwaka 2023 kama ilivyokuwa mwaka 2022.

23. Mwaka 2023, shughuli za sanaa na burudani ndizo zilikuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji wa asilimia 17.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 19.0 mwaka 2022. Ukuaji huo ulitokana na kuendelea kuimarika kwa mauzo ya bidhaa za kitamaduni kwa watalii na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara ya tasnia ya burudani. Aidha, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.4 mwaka 2023 kama ilivyokuwa mwaka 2022.

24. Mwaka 2023, ukuaji wa shughuli za kaya binafsi katika kuajiri ulikuwa asilimia 3.1 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Aidha, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.2 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Kwa upande mwingine, shughuli za huduma nyingine zilikua kwa asilimia 6.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.7 mwaka 2022. Mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 0.9 mwaka 2022.

**Mwenendo wa Mfumuko wa Bei**

25. Mwaka 2023, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.8 ikilinganishwa na asilimia 4.3 mwaka 2022. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulichangiwa na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani pamoja na kuimarika kwa bei ya mafuta katika soko la dunia. Kiwango cha mfumuko wa bei kipo ndani ya lengo la nchi la muda wa kati (asilimia 3.0 - 5.0) na kinakidhi vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (asilimia isiyozidi 8.0) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (asilimia 3.0 - 7.0).

26. Mwaka 2023, kundi la chakula na vinywaji baridi lilikuwa na mfumuko wa bei mkubwa zaidi wa wastani wa asilimia 6.8 ikilinganishwa na makundi mengine. Hata hivyo, kiwango hicho ni kidogo ikilinganishwa na asilimia 7.3 mwaka 2022. Hii ilitokana na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuimarisha upatikanaji wa chakula nchini ikiwemo, kutoa ruzuku ya mbolea pamoja na kujenga na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji ili kupunguza utegemezi wa mvua katika uzalishaji wa mazao ya chakula. Kwa upande mwingine, kundi la huduma za fedha na bima lilikuwa na mfumuko wa bei mdogo zaidi wa wastani asilimia 0.1 mwaka 2023 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Kundi la makazi, maji, umeme, gesi na nishati nyingine lilifuatia kwa kuwa na mfumuko wa bei

mdogo wa wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2022. Jedwali Na. 1.1 linaonesha mwenendo wa bei kwa makundi makuu ya bidhaa na huduma.


27. Mwaka 2023, mfumuko wa bei wa msingi (core inflation) ulipungua hadi wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2023 kutoka asilimia 3.0 mwaka 2022. Aidha, Mfumuko wa bei kwa kundi la nishati, mafuta na ankara za maji ulikuwa asilimia 2.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 9.1 mwaka 2022. Hii ilichangiwa na kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei ya bidhaa za petroli katika soko la dunia **(Kielelezo Na. 1.5).** Vile vile, mfumuko wa bei za bidhaa na huduma ulikuwa wastani wa asilimia 4.6 na asilimia 2.5 mwaka 2023, kutoka asilimia 5.3 na asilimia 2.8 mtawalia mwaka 2022.

**Jedwali Na. 1.1: Fahirisi za Kitaifa za Bei ya Mtumiaji (NCPI) na Viwango vya Mfumuko wa Bei (Kizio 2020 = 100)**

| | | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Uzito** | | 28.2 | 1.9 | 10.8 | 15.1 | 7.9 | 2.5 | 14.1 | 5.4 | 1.6 | 2.0 | 6.6 | 2.1 | 2.1 | 100.0 |
| **2017** | **Fahirisi za Bei** | 91 | 96 | 92 | 77 | 92 | 96 | 93 | 101 | 99 | 95 | 93 | 96 | 95 | 90 |
| **2018** | | 93 | 98 | 95 | 86 | 95 | 97 | 96 | 100 | 98 | 97 | 95 | 97 | 97 | 94 |
| **2019** | | 96 | 100 | 98 | 93 | 98 | 99 | 99 | 100 | 100 | 99 | 98 | 100 | 99 | 97 |
| **2020** | | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 |
| **2021** | | 104 | 102 | 105 | 104 | 103 | 103 | 103 | 102 | 103 | 101 | 105 | 100 | 103 | 104 |
| **2022** | | 112 | 103 | 107 | 108 | 107 | 104 | 110 | 103 | 104 | 102 | 107 | 100 | 105 | 108 |
| **2023** | | 120 | 106 | 110 | 110 | 110 | 106 | 113 | 105 | 107 | 105 | 112 | 100 | 108 | 112 |
| **2017** | **Mfumuko wa Bei** | 9.1 | 3.3 | 3.5 | 7.6 | 2.9 | 2.6 | 0.5 | -0.7 | 2.4 | 0.9 | 1.2 | 1.4 | 3.3 | 5.3 |
| **2018** | | 3.0 | 1.6 | 2.9 | 12.0 | 2.5 | 1.3 | 2.5 | -1.2 | -0.9 | 2.4 | 1.3 | 1.3 | 1.7 | 3.5 |
| **2019** | | 2.9 | 2.4 | 3.0 | 7.9 | 3.9 | 1.8 | 3.1 | 0.1 | 1.5 | 1.8 | 4.2 | 2.8 | 2.4 | 3.4 |
| **2020** | | 4.1 | -0.1 | 2.2 | 7.6 | 1.8 | 0.8 | 1.4 | 0.4 | 0.1 | 1.3 | 1.5 | 0.0 | 1.0 | 3.3 |
| **2021** | | 4.3 | 2.2 | 4.6 | 4.1 | 3.2 | 2.7 | 3.3 | 1.8 | 2.7 | 1.1 | 4.9 | 0.3 | 2.8 | 3.7 |
| **2022** | | 7.3 | 1.2 | 2.5 | 3.6 | 3.5 | 1.4 | 6.1 | 0.9 | 1.5 | 0.6 | 2.3 | 0.1 | 2.3 | 4.3 |
| **2023** | | 6.8 | 2.4 | 3.0 | 1.6 | 3.2 | 1.7 | 2.8 | 1.7 | 2.2 | 3.4 | 4.3 | 0.1 | 2.9 | 3.8 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo Na. 1.5: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Baadhi ya Makundi Mwaka 2012 - 2023**




| | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfumuko wa bei | 16.0 | 7.9 | 6.1 | 5.6 | 5.2 | 5.3 | 3.5 | 3.4 | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8 |
| Chakula | 22.0 | 8.6 | 7.7 | 8.6 | 7.6 | 9.6 | 3.7 | 4.3 | 5.0 | 4.3 | 7.3 | 6.8 |
| Nishati | 30.9 | 12.8 | 12.1 | -0.9 | 6.3 | 10.5 | 17.2 | 9.0 | 5.0 | 3.1 | 9.1 | 2.3 |
| Msingi | 12.8 | 4.5 | 3.7 | 2.3 | 2.6 | 2.0 | 1.9 | 3.0 | 2.3 | 4.1 | 3.0 | 2.3 |

28. Mwaka 2023, mfumuko wa bei kwa matabaka ya kipato cha kati na juu ulipungua hadi asilimia 4.9 na asilimia 2.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.8 na asilimia 3.8, mtawalia mwaka 2022. Hata hivyo, mfumuko wa bei kwa tabaka la kipato cha chini uliongezeka hadi asilimia 5.2 mwaka 2023 kutoka asilimia 4.7 mwaka 2023 kutokana na ongezeko kubwa la bei katika makundi ya burudani, michezo na utamaduni asilimia 13.8, vyakula na vinywaji baridi asilimia 9.8 pamoja na afya asilimia 9.1. **Jedwali Na. 1.2** linaonesha mwenendo mfumuko wa bei za bidhaa na huduma kulingana na tabaka la walaji.

**Jedwali Na. 1.2: Mfumuko wa Bei za Bidhaa na Huduma Zitumiwazo na Walaji Kulingana na Tabaka la Kipato (Msingi 2020 = 100) Mwaka 2018 - 2023**

| Mwaka | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **WAKAZI WENYE KIPATO CHA CHINI** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2018** | 4.3 | 0.1 | 3.1 | 7.7 | 1.9 | 0.1 | 0.4 | 0.0 | 0.9 | 2.7 | 0.1 | 2.2 | 1.5 | 3.0 |
| **2019** | 4.3 | 0.8 | 4.0 | 5.3 | 1.9 | 3.1 | 0.2 | 1.0 | 3.4 | 0.0 | 2.2 | 4.0 | 2.2 | 3.3 |
| **2020** | 1.3 | 0.0 | 1.2 | 10.1 | 0.6 | 0.9 | -0.1 | 0.2 | -0.4 | 0.0 | 0.6 | 0.0 | 0.3 | 2.2 |
| **2021** | 0.6 | 7.3 | 3.1 | 2.9 | 3.9 | 1.9 | -7.4 | 1.4 | 3.8 | 10.3 | 5.5 | 0.0 | 0.7 | 2.4 |
| **2022** | 7.5 | 0.5 | 3.7 | 3.9 | 6.3 | 2.9 | -2.1 | 1.8 | 13.3 | 2.3 | 3.0 | 0.0 | 3.5 | 4.7 |
| **2023** | 9.8 | 0.7 | 2.4 | 3.4 | 5.3 | 9.1 | -8.4 | 1.0 | 13.8 | 4.4 | 1.9 | 0.0 | 3.5 | 5.2 |
| **WAKAZI WENYE KIPATO CHA KATI** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2018** | 7.6 | -0.1 | 2.1 | 1.8 | 1.3 | 0.3 | 1.9 | 0.0 | -1.0 | 8.6 | 0.1 | 2.2 | 1.5 | 3.5 |
| **2019** | 5.4 | 0.4 | 3.5 | 6.8 | 2.2 | 4.5 | 0.1 | 1.5 | 1.8 | 0.0 | 2.7 | 4.0 | 2.4 | 4.0 |
| **2020** | 4.5 | 0.1 | 1.3 | 8.6 | 0.5 | 0.7 | -0.7 | 0.5 | -0.6 | 0.0 | 0.7 | 0.0 | 0.2 | 3.3 |
| **2021** | 1.2 | 4.2 | 0.7 | -1.1 | 4.1 | 4.0 | 2.7 | 1.3 | 0.5 | 5.4 | 10.1 | 0.4 | 0.7 | 2.4 |
| **2022** | 9.5 | 0.5 | 2.6 | 5.0 | 4.5 | 1.8 | 7.3 | 0.2 | 16.5 | 1.2 | 3.7 | 0.1 | 3.4 | 5.8 |
| **2023** | 9.9 | 4.0 | 3.0 | 2.5 | 3.8 | 3.5 | 1.2 | 0.0 | 6.4 | 2.8 | 2.9 | -0.1 | 3.5 | 4.9 |
| **WAKAZI WENYE KIPATO CHA JUU** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2018** | 6.8 | 0.2 | 2.5 | 5.6 | 1.1 | 0.1 | 6.4 | 0.7 | -0.4 | 7.8 | 1.0 | 2.1 | 0.6 | 4.6 |
| **2019** | 4.3 | 0.0 | 2.4 | 8.1 | 2.0 | 4.1 | 2.8 | 1.3 | -0.6 | 1.5 | 3.7 | 4.1 | 0.1 | 3.5 |
| **2020** | 7.6 | 0.2 | 1.4 | 7.0 | 0.5 | 0.6 | -1.8 | 0.5 | -0.7 | 0.0 | 0.6 | 0.0 | -0.1 | 2.4 |
| **2021** | 3.9 | 11.2 | 3.4 | 0.1 | 8.2 | 3.3 | 1.8 | 1.3 | -1.3 | 3.0 | 7.0 | 0.2 | 1.5 | 3.0 |
| **2022** | 4.8 | 2.3 | 3.1 | 3.4 | 2.5 | 2.0 | 5.9 | 1.1 | 2.3 | 0.8 | 4.0 | 0.0 | 2.3 | 3.8 |
| **2023** | 4.0 | 1.8 | 2.9 | 2.4 | 2.0 | 4.9 | 0.8 | 0.6 | 3.7 | 1.2 | 4.2 | -0.1 | 7.4 | 2.5 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Ukuzaji Rasilimali

29. Mwaka 2023, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2015 ulikuwa shilingi bilioni 62,629.85 ikilinganishwa na shilingi bilioni 61,112.75 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 2.5. Aidha, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka husika ulikuwa shilingi bilioni 71,248.41 ikilinganishwa na shilingi bilioni 67,065.81 mwaka 2022. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulipungua kidogo kufikia asilimia 37.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 39.3 mwaka 2022.

30. Mwaka 2023, ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za mwaka husika ulikuwa shilingi bilioni 74,222.05 ikilinganishwa na shilingi bilioni 68,247.46 mwaka 2022. Rasilimali za kudumu zinajumuisha, majengo, vifaa vya usafiri, mitambo na vifaa, rasilimali za mazao ya mifugo, haki za umiliki, utafiti na maendeleo pamoja na huduma za kitaalamu. Aidha, ukuzaji rasilimiali za kudumu kwa bei za mwaka 2015 uliongezeka kwa asilimia 4.8 na kufikia shilingi bilioni 66,300.06 mwaka 2023 kutoka shilingi bilioni 63,270.61 mwaka 2022. Kwa upande mwingine, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za mwaka 2015 ilipungua kwa shilingi bilioni 3,670.21 mwaka 2023 ikilinganishwa na upungufu wa

thamani wa shilingi bilioni 2,157.86 mwaka 2022. Aidha, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za mwaka husika ilipungua kwa shilingi bilioni 2,973.64 mwaka 2023 ikilinganishwa na upungufu wa thamani wa shilingi bilioni 1,181.65 mwaka 2022.

31. Ukuzaji rasilimali katika sekta ya umma kwa bei za mwaka husika uliongezeka kwa asilimia 13.4 na kufikia shilingi bilioni 22,934.61 mwaka 2023 kutoka shilingi bilioni 20,231.10 mwaka 2022. Aidha, ukuzaji rasilimali katika sekta binafsi kwa bei za mwaka husika ulikuwa shilingi bilioni 51,287.44 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 48,016.36 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Sekta ya umma ilichangia asilimia 30.9 ya rasilimali zote za kudumu na sekta binafsi asilimia 69.1 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 1: PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***33,916,201*** | ***36,447,871*** | ***38,760,377*** | ***41,851,196*** | ***44,670,628*** | ***49,979,019*** |
| Kilimo cha Mazao | 19,060,478 | 20,066,646 | 21,920,177 | 23,549,769 | 25,580,490 | 30,378,157 |
| Mifugo | 9,251,173 | 10,357,287 | 10,622,499 | 11,269,820 | 11,479,664 | 11,678,978 |
| Misitu | 3,383,160 | 3,641,955 | 3,720,575 | 4,191,340 | 4,603,883 | 4,804,019 |
| Uvuvi | 2,221,390 | 2,381,982 | 2,497,126 | 2,840,267 | 3,006,591 | 3,117,865 |
| ***Viwanda na Ujenzi*** | ***33,410,922*** | ***37,385,883*** | ***42,476,524*** | ***45,334,983*** | ***52,068,150*** | ***55,985,595*** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 6,455,878 | 7,164,222 | 9,867,293 | 11,471,365 | 15,436,227 | 16,903,691 |
| Viwanda | 9,811,013 | 10,512,034 | 11,207,276 | 11,237,325 | 12,170,060 | 13,182,066 |
| Umeme | 345,775 | 369,917 | 398,084 | 378,691 | 248,139 | 34,392 |
| Maji safi na Maji taka | 554,536 | 590,324 | 635,959 | 746,403 | 893,174 | 908,275 |
| Ujenzi | 16,243,719 | 18,749,387 | 20,367,912 | 21,501,198 | 23,320,549 | 24,957,172 |
| ***Huduma*** | ***46,875,694*** | ***50,952,480*** | ***54,021,848*** | ***57,604,454*** | ***61,343,645*** | ***69,818,428*** |
| Biashara na Matengenezo | 11,067,502 | 12,286,407 | 12,958,573 | 13,789,132 | 14,006,738 | 15,678,782 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 8,381,276 | 9,622,792 | 10,701,520 | 10,860,302 | 11,397,028 | 13,523,735 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1,653,792 | 1,680,222 | 1,371,161 | 1,601,506 | 1,892,459 | 2,196,214 |
| Habari na Mawasiliano | 1,948,180 | 2,052,242 | 2,196,753 | 2,375,155 | 2,605,849 | 2,726,854 |
| Fedha na Bima | 4,823,101 | 4,927,613 | 5,013,181 | 5,380,249 | 6,313,664 | 8,425,562 |
| Upangishaji Majengo | 3,553,630 | 3,869,528 | 4,348,618 | 4,581,584 | 4,784,774 | 5,086,175 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 711,807 | 753,302 | 822,440 | 1,088,002 | 1,175,442 | 1,264,549 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,078,145 | 3,340,939 | 3,692,864 | 4,022,127 | 4,297,339 | 4,937,308 |
| Utawala na Ulinzi | 5,131,630 | 5,354,893 | 5,530,738 | 5,875,519 | 6,243,146 | 6,581,823 |
| Elimu | 3,081,718 | 3,322,028 | 3,440,525 | 3,649,124 | 3,838,330 | 4,130,679 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1,816,738 | 1,932,964 | 2,060,600 | 2,213,486 | 2,392,940 | 2,601,798 |
| Sanaa na Burudani | 374,924 | 427,887 | 416,049 | 513,448 | 623,721 | 749,446 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1,037,687 | 1,140,417 | 1,217,190 | 1,358,754 | 1,465,396 | 1,594,457 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 215,564 | 241,246 | 251,635 | 296,065 | 306,818 | 321,046 |
| ***Jumla ya Ongezeko la Thamani*** | ***114,202,816*** | ***124,786,234*** | ***135,258,749*** | ***144,790,632*** | ***158,082,423*** | ***175,783,042*** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 9,794,956 | 9,753,960 | 10,125,604 | 11,376,505 | 12,737,610 | 12,805,009 |
| **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **123,997,772** | **134,540,194** | **145,384,353** | **156,167,137** | **170,820,032** | **188,588,052** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 2: PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **A:SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **110,217,651** | **119,842,758** | **129,664,277** | **139,270,744** | **152,694,776** | **168,077,940** |
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***21,296,288*** | ***22,959,097*** | ***24,314,330*** | ***26,295,327*** | ***27,969,535*** | ***30,942,993*** |
| Kilimo cha Mazao | 10,307,806 | 10,851,760 | 11,854,269 | 12,735,397 | 13,833,046 | 16,427,129 |
| Mifugo | 6,674,010 | 7,471,864 | 7,663,285 | 8,130,184 | 8,281,247 | 8,424,859 |
| Misitu | 2,181,786 | 2,348,644 | 2,399,374 | 2,702,937 | 2,968,865 | 3,097,862 |
| Uvuvi | 2,132,686 | 2,286,828 | 2,397,402 | 2,726,809 | 2,886,377 | 2,993,141 |
| ***Viwanda na Ujenzi*** | ***32,392,034*** | ***36,331,105*** | ***41,375,431*** | ***44,176,658*** | ***50,834,268*** | ***54,713,777*** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 6,455,878 | 7,164,222 | 9,867,293 | 11,471,365 | 15,436,227 | 16,903,691 |
| Viwanda | 9,811,013 | 10,512,034 | 11,207,276 | 11,237,325 | 12,170,060 | 13,182,066 |
| Umeme | 345,775 | 369,917 | 398,084 | 378,691 | 248,139 | 34,392 |
| Maji safi na Maji taka | 387,408 | 412,410 | 448,050 | 525,861 | 629,265 | 639,904 |
| Ujenzi | 15,391,959 | 17,872,522 | 19,454,727 | 20,563,416 | 22,350,577 | 23,953,725 |
| ***Huduma*** | ***46,734,373*** | ***50,798,596*** | ***53,848,912*** | ***57,422,253*** | ***61,153,364*** | ***69,616,161*** |
| Biashara na Matengenezo | 11,067,502 | 12,286,407 | 12,958,573 | 13,789,132 | 14,006,738 | 15,678,782 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 8,381,276 | 9,622,792 | 10,701,520 | 10,860,302 | 11,397,028 | 13,523,735 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1,653,792 | 1,680,222 | 1,371,161 | 1,601,506 | 1,892,459 | 2,196,214 |
| Habari na Mawasiliano | 1,948,180 | 2,052,242 | 2,196,753 | 2,375,155 | 2,605,849 | 2,726,854 |
| Fedha na Bima | 4,823,101 | 4,927,613 | 5,013,181 | 5,380,249 | 6,313,664 | 8,425,562 |
| Upangishaji Majengo | 3,412,309 | 3,715,644 | 4,175,682 | 4,399,384 | 4,594,494 | 4,883,908 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 711,807 | 753,302 | 822,440 | 1,088,002 | 1,175,442 | 1,264,549 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,078,145 | 3,340,939 | 3,692,864 | 4,022,127 | 4,297,339 | 4,937,308 |
| Utawala na Ulinzi | 5,131,630 | 5,354,893 | 5,530,738 | 5,875,519 | 6,243,146 | 6,581,823 |
| Elimu | 3,081,718 | 3,322,028 | 3,440,525 | 3,649,124 | 3,838,330 | 4,130,679 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1,816,738 | 1,932,964 | 2,060,600 | 2,213,486 | 2,392,940 | 2,601,798 |
| Sanaa na Burudani | 374,924 | 427,887 | 416,049 | 513,448 | 623,721 | 749,446 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1,037,687 | 1,140,417 | 1,217,190 | 1,358,754 | 1,465,396 | 1,594,457 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 215,564 | 241,246 | 251,635 | 296,065 | 306,818 | 321,046 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **100,422,695** | **110,088,798** | **119,538,673** | **127,894,238** | **139,957,166** | **155,272,931** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 9,794,956 | 9,753,960 | 10,125,604 | 11,376,505 | 12,737,610 | 12,805,009 |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **13,780,121** | **14,697,436** | **15,720,076** | **16,896,394** | **18,125,257** | **20,510,111** |
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***12,619,912*** | ***13,488,774*** | ***14,446,046*** | ***15,555,869*** | ***16,701,094*** | ***19,036,026*** |
| Mazao | 8,749,506 | 9,211,537 | 10,062,319 | 10,810,523 | 11,743,616 | 13,947,057 |
| Mifugo | 2,578,812 | 2,887,197 | 2,961,106 | 3,141,595 | 3,200,334 | 3,256,111 |
| Misitu | 1,201,483 | 1,293,414 | 1,321,325 | 1,488,533 | 1,635,169 | 1,706,362 |
| Uvuvi | 90,110 | 96,626 | 101,296 | 115,218 | 121,974 | 126,496 |
| ***Viwanda na Ujenzi*** | ***1,018,888*** | ***1,054,778*** | ***1,101,094*** | ***1,158,324*** | ***1,233,882*** | ***1,271,818*** |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 167,128 | 177,914 | 187,909 | 220,543 | 263,910 | 268,372 |
| Ujenzi | 851,760 | 876,864 | 913,184 | 937,781 | 969,972 | 1,003,447 |
| ***Huduma*** | ***141,321*** | ***153,883*** | ***172,936*** | ***182,200*** | ***190,281*** | *202,267* |
| Upangishaji Majengo | 141,321 | 153,883 | 172,936 | 182,200 | 190,281 | 202,267 |
| **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **123,997,772** | **134,540,194** | **145,384,353** | **156,167,137** | **170,820,032** | **188,588,052** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 3: PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

**Asilimia**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***27.4*** | ***27.1*** | ***26.7*** | ***26.8*** | ***26.2*** | ***26.5*** |
| Kilimo cha Mazao | 15.4 | 14.9 | 15.1 | 15.1 | 15.0 | 16.1 |
| Mifugo | 7.5 | 7.7 | 7.3 | 7.2 | 6.7 | 6.2 |
| Misitu | 2.7 | 2.7 | 2.6 | 2.7 | 2.7 | 2.5 |
| Uvuvi | 1.8 | 1.8 | 1.7 | 1.8 | 1.8 | 1.7 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 5.2 | 5.3 | 6.8 | 7.3 | 9.0 | 9.0 |
| Viwanda | 7.9 | 7.8 | 7.7 | 7.2 | 7.1 | 7.0 |
| Umeme | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.2 | 0.1 | 0.0 |
| Maji safi na Maji taka | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.5 | 0.5 | 0.5 |
| Ujenzi | 13.1 | 13.9 | 14.0 | 13.8 | 13.7 | 13.2 |
| Biashara na Matengenezo | 8.9 | 9.1 | 8.9 | 8.8 | 8.2 | 8.3 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 6.8 | 7.2 | 7.4 | 7.0 | 6.7 | 7.2 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1.3 | 1.2 | 0.9 | 1.0 | 1.1 | 1.2 |
| Habari na Mawasiliano | 1.6 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.4 |
| Fedha na Bima | 3.9 | 3.7 | 3.4 | 3.4 | 3.7 | 4.5 |
| Upangishaji Majengo | 2.9 | 2.9 | 3.0 | 2.9 | 2.8 | 2.7 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.7 | 0.7 | 0.7 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 2.5 | 2.5 | 2.5 | 2.6 | 2.5 | 2.6 |
| Utawala na Ulinzi | 4.1 | 4.0 | 3.8 | 3.8 | 3.7 | 3.5 |
| Elimu | 2.5 | 2.5 | 2.4 | 2.3 | 2.2 | 2.2 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1.5 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 |
| Sanaa na Burudani | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.4 | 0.4 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.9 | 0.9 | 0.8 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **92.1** | **92.8** | **93.0** | **92.7** | **92.5** | **93.2** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 7.9 | 7.2 | 7.0 | 7.3 | 7.5 | 6.8 |
| **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 4: PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

**Asilimia**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **A:SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | | | | | | |
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***17.2*** | ***17.1*** | ***16.7*** | ***16.8*** | ***16.4*** | ***16.4*** |
| Kilimo cha Mazao | 8.3 | 8.1 | 8.2 | 8.2 | 8.1 | 8.7 |
| Mifugo | 5.4 | 5.6 | 5.3 | 5.2 | 4.8 | 4.5 |
| Misitu | 1.8 | 1.7 | 1.7 | 1.7 | 1.7 | 1.6 |
| Uvuvi | 1.7 | 1.7 | 1.6 | 1.7 | 1.7 | 1.6 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 5.2 | 5.3 | 6.8 | 7.3 | 9.0 | 9.0 |
| Viwanda | 7.9 | 7.8 | 7.7 | 7.2 | 7.1 | 7.0 |
| Umeme | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.2 | 0.1 | 0.0 |
| Maji safi na Maji taka | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.4 | 0.3 |
| Ujenzi | *12.4* | *13.3* | *13.4* | *13.2* | *13.1* | *12.7* |
| Biashara na Matengenezo | 8.9 | 9.1 | 8.9 | 8.8 | 8.2 | 8.3 |
| Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 6.8 | 7.2 | 7.4 | 7.0 | 6.7 | 7.2 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1.3 | 1.2 | 0.9 | 1.0 | 1.1 | 1.2 |
| Habari na Mawasiliano | 1.6 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.4 |
| Fedha na Bima | 3.9 | 3.7 | 3.4 | 3.4 | 3.7 | 4.5 |
| Upangishaji Majengo | 2.8 | 2.8 | 2.9 | 2.8 | 2.7 | 2.6 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.7 | 0.7 | 0.7 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 2.5 | 2.5 | 2.5 | 2.6 | 2.5 | 2.6 |
| Utawala na Ulinzi | 4.1 | 4.0 | 3.8 | 3.8 | 3.7 | 3.5 |
| Elimu | 2.5 | 2.5 | 2.4 | 2.3 | 2.2 | 2.2 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1.5 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 |
| Sanaa na Burudani | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.4 | 0.4 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.9 | 0.9 | 0.8 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **81.0** | **81.8** | **82.2** | **81.9** | **81.9** | **82.3** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 7.9 | 7.2 | 7.0 | 7.3 | 7.5 | 6.8 |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **11.1** | **10.9** | **10.8** | **10.8** | **10.6** | **10.9** |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 10.2 | 10.0 | 9.9 | 10.0 | 9.8 | 10.1 |
| Mazao | 7.1 | 6.8 | 6.9 | 6.9 | 6.9 | 7.4 |
| Mifugo | 2.1 | 2.1 | 2.0 | 2.0 | 1.9 | 1.7 |
| Misitu | 1.0 | 1.0 | 0.9 | 1.0 | 1.0 | 0.9 |
| Uvuvi | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.2 | 0.1 |
| Ujenzi | 0.7 | 0.7 | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.5 |
| Upangishaji Majengo | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 5: PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO (KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

**Shilingi Milioni**

| **Aina ya Matumizi** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko(GDPmp)** | **123,997,772** | **134,540,194** | **145,384,353** | **156,167,137** | **170,820,032** | **188,588,052** |
| **Matumizi ya Mwisho(Final consumption)** | **87,527,611** | **92,439,966** | **100,179,732** | **107,062,882** | **115,880,862** | **124,053,492** |
| Serikali | 10,468,313 | 10,864,652 | 11,263,617 | 11,862,430 | 12,455,979 | 13,031,657 |
| Binafsi | 76,759,564 | 81,252,021 | 88,581,903 | 94,824,443 | 103,000,650 | 110,544,782 |
| Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii | 299,734 | 323,293 | 334,212 | 376,009 | 424,233 | 477,052 |
| **Ukuzaji rasilimali** | **40,639,844** | **46,103,604** | **55,949,293** | **63,708,208** | **67,065,806** | **71,248,413** |
| Rasilimali za kudumu | 41,141,962 | 50,010,814 | 60,119,039 | 67,221,823 | 68,247,459 | 74,222,050 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani ***(changes in Valuables)*** | 1,215,104 | 1,273,337 | 1,838,290 | 1,954,173 | 1,916,891 | 1,981,135 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | -1,717,221 | -5,180,547 | -6,008,036 | -5,467,787 | -3,098,544 | -4,954,772 |
| Mauzo nje | **18,810,172** | **22,101,293** | **19,629,078** | **22,686,817** | **27,609,312** | **32,402,976** |
| Bidhaa-fob | 9,720,088 | 12,305,450 | 14,620,151 | 15,523,687 | 16,639,963 | 17,380,770 |
| Huduma | 9,090,084 | 9,795,843 | 5,008,927 | 7,163,130 | 10,969,349 | 15,022,206 |
| Uagizaji | **23,653,216** | **23,806,198** | **20,992,737** | **26,675,720** | **38,409,637** | **38,350,922** |
| Bidhaa-fob | 19,294,815 | 19,713,653 | 17,967,329 | 22,983,447 | 32,730,313 | 32,795,993 |
| Huduma | 4,358,401 | 4,092,545 | 3,025,408 | 3,692,272 | 5,679,323 | 5,554,928 |
| Makosa na Mapungufu | 673,361 | -2,298,472 | -9,381,013 | -10,615,051 | -1,326,310 | -765,908 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 6: PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI (BEI ZA MWAKA 2015)**

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***29,504,236*** | ***30,802,622*** | ***32,323,673*** | ***33,588,777*** | ***34,711,277*** | ***36,184,322*** |
| Kilimo cha Mazao | 15,679,338 | 16,372,351 | 17,196,815 | 17,818,276 | *18,295,700* | *19,064,330* |
| Mifugo | 8,276,692 | 8,687,238 | 9,119,559 | 9,574,892 | *10,054,947* | *10,560,054* |
| Misitu | 3,339,085 | 3,499,684 | 3,612,827 | 3,739,795 | *3,857,006* | *4,021,644* |
| Uvuvi | 2,209,121 | 2,243,349 | 2,394,472 | 2,455,814 | *2,503,624* | *2,538,294* |
| ***Viwanda na Ujenzi*** | ***31,344,128*** | ***34,912,847*** | ***37,251,857*** | ***39,085,652*** | ***41,147,936*** | ***43,234,380*** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 4,659,195 | 5,485,112 | 5,887,452 | 6,442,881 | *7,138,149* | *7,945,921* |
| Viwanda | 9,623,501 | 10,184,558 | 10,646,279 | 11,155,762 | *11,624,144* | *12,128,562* |
| Umeme | 928,174 | 994,879 | 1,049,610 | 1,154,204 | *1,242,132* | *1,290,960* |
| Maji safi na Maji taka | 477,510 | 510,411 | 540,159 | 575,213 | *606,754* | *621,827* |
| Ujenzi | 15,655,747 | 17,737,886 | 19,128,358 | 19,757,591 | *20,536,757* | *21,247,110* |
| ***Huduma*** | ***45,453,302*** | ***48,133,895*** | ***50,196,792*** | ***52,618,667*** | ***55,393,899*** | ***58,615,193*** |
| Biashara na Matengenezo | 10,480,204 | 10,984,480 | 11,216,401 | 11,578,146 | *12,031,598* | 12,542,371 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 8,736,561 | 9,493,191 | 10,293,276 | 10,658,344 | *11,061,950* | 11,510,657 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1,604,391 | 1,645,950 | 1,419,654 | 1,514,711 | *1,651,099* | 1,788,242 |
| Habari na Mawasiliano | 1,989,717 | 2,133,312 | 2,313,032 | 2,524,610 | *2,712,411* | 2,917,297 |
| Fedha na Bima | 4,094,972 | 4,281,167 | 4,412,967 | 4,599,677 | *5,024,301* | 5,639,079 |
| Upangishaji Majengo | 3,354,518 | 3,505,485 | 3,663,972 | 3,827,460 | *3,997,460* | 4,168,722 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 763,332 | 821,636 | 881,833 | 942,013 | *996,609* | 1,051,696 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,054,288 | 3,311,753 | 3,569,800 | 3,817,047 | *3,993,799* | 4,191,805 |
| Utawala na Ulinzi | 5,064,968 | 5,238,491 | 5,438,146 | 5,713,411 | *6,024,203* | 6,358,312 |
| Elimu | 3,046,789 | 3,257,406 | 3,365,355 | 3,537,611 | *3,724,729* | 3,955,485 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1,746,731 | 1,833,514 | 1,953,479 | 2,065,349 | *2,176,986* | 2,308,205 |
| Sanaa na Burudani | 350,027 | 389,225 | 372,120 | 444,488 | *528,722* | 622,264 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 971,690 | 1,037,083 | 1,089,265 | 1,181,814 | *1,249,425* | 1,333,612 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 195,113 | 201,203 | 207,492 | 213,987 | *220,607* | 227,445 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **106,301,666** | **113,849,364** | **119,772,323** | **125,293,096** | **131,253,112** | **138,033,894** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 8,872,802 | 9,289,875 | 8,951,215 | 9,658,417 | *9,994,080* | *10,365,863* |
| **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **115,174,468** | **123,139,239** | **128,723,538** | **134,951,513** | **141,247,193** | **148,399,757** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 7: PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (BEI ZA MWAKA 2015)

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **110,243,681** | **117,953,902** | **123,282,166** | **129,347,848** | **135,459,199** | **142,421,811** |
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***25,671,369*** | ***26,821,324*** | ***28,173,634*** | ***29,292,547*** | ***30,264,345*** | ***31,539,362*** |
| Kilimo cha Mazao | 13,381,343 | 13,996,558 | 14,711,216 | 15,252,963 | 15,658,987 | 16,316,897 |
| Mifugo | 7,090,719 | 7,446,156 | 7,832,125 | 8,233,750 | 8,646,525 | 9,080,909 |
| Misitu | 3,007,003 | 3,152,322 | 3,253,511 | 3,368,590 | 3,474,151 | 3,622,458 |
| Uvuvi | 2,192,305 | 2,226,288 | 2,376,783 | 2,437,243 | 2,484,681 | 2,519,097 |
| ***Viwanda na Ujenzi*** | ***30,352,531*** | ***33,819,773*** | ***36,076,540*** | ***37,899,047*** | ***39,933,072*** | ***42,032,997*** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 4,659,195 | 5,485,112 | 5,887,452 | 6,442,881 | 7,138,149 | 7,945,921 |
| Viwanda | 9,623,501 | 10,184,558 | 10,646,279 | 11,155,762 | 11,624,144 | 12,128,562 |
| Umeme | 928,174 | 994,879 | 1,049,610 | 1,154,204 | 1,242,132 | 1,290,960 |
| Maji safi na Maji taka | 369,545 | 396,149 | 420,891 | 448,945 | 473,562 | 485,327 |
| Ujenzi | 14,772,116 | 16,759,074 | 18,072,308 | 18,697,255 | 19,455,085 | 20,182,229 |
| ***Huduma*** | ***45,346,979*** | ***48,022,931*** | ***50,080,777*** | ***52,497,837*** | ***55,267,702*** | ***58,483,589*** |
| Biashara na Matengenezo | 10,480,204 | 10,984,480 | 11,216,401 | 11,578,146 | 12,031,598 | 12,542,371 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 8,736,561 | 9,493,191 | 10,293,276 | 10,658,344 | 11,061,950 | 11,510,657 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1,604,391 | 1,645,950 | 1,419,654 | 1,514,711 | 1,651,099 | 1,788,242 |
| Habari na Mawasiliano | 1,989,717 | 2,133,312 | 2,313,032 | 2,524,610 | 2,712,411 | 2,917,297 |
| Fedha na Bima | 4,094,972 | 4,281,167 | 4,412,967 | 4,599,677 | 5,024,301 | 5,639,079 |
| Upangishaji Majengo | 3,248,194 | 3,394,521 | 3,547,957 | 3,706,630 | 3,871,263 | 4,037,119 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 763,332 | 821,636 | 881,833 | 942,013 | 996,609 | 1,051,696 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,054,288 | 3,311,753 | 3,569,800 | 3,817,047 | 3,993,799 | 4,191,805 |
| Utawala na Ulinzi | 5,064,968 | 5,238,491 | 5,438,146 | 5,713,411 | 6,024,203 | 6,358,312 |
| Elimu | 3,046,789 | 3,257,406 | 3,365,355 | 3,537,611 | 3,724,729 | 3,955,485 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1,746,731 | 1,833,514 | 1,953,479 | 2,065,349 | 2,176,986 | 2,308,205 |
| Sanaa na Burudani | 350,027 | 389,225 | 372,120 | 444,488 | 528,722 | 622,264 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 971,690 | 1,037,083 | 1,089,265 | 1,181,814 | 1,249,425 | 1,333,612 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 195,113 | 201,203 | 207,492 | 213,987 | 220,607 | 227,445 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **101,370,879** | **108,664,027** | **114,330,951** | **119,689,431** | **125,465,119** | **132,055,949** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 8,872,802 | 9,289,875 | 8,951,215 | 9,658,417 | 9,994,080 | 10,365,863 |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **4,930,787** | **5,185,336** | **5,441,372** | **5,603,665** | **5,787,994** | **5,977,946** |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 3,832,866 | 3,981,298 | 4,150,038 | 4,296,231 | 4,446,932 | 4,644,960 |
| Mazao | 2,297,609 | 2,375,410 | 2,485,190 | 2,564,893 | 2,636,294 | 2,746,997 |
| Mifugo | 1,185,810 | 1,240,908 | 1,287,262 | 1,340,971 | 1,408,250 | 1,478,965 |
| Misitu | 332,233 | 347,517 | 359,470 | 371,362 | 383,014 | 399,356 |
| Uvuvi | 17,215 | 17,464 | 18,116 | 19,004 | 19,375 | 19,643 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **991,597** | **1,093,074** | **1,175,318** | **1,186,604** | **1,214,865** | **1,201,382** |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 107,966 | 114,262 | 119,268 | 126,268 | 133,192 | 136,501 |
| Ujenzi | 883,632 | 978,812 | 1,056,050 | 1,060,336 | 1,081,673 | 1,064,881 |
| **Huduma** | **106,323** | **110,964** | **116,016** | **120,830** | **126,197** | 131,603 |
| Upangishaji Majengo | 106,323 | 110,964 | 116,016 | 120,830 | 126,197 | 131,603 |
| **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **115,174,468** | **123,139,239** | **128,723,538** | **134,951,513** | **141,247,193** | **148,399,757** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu


## Jedwali Na. 8: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI (BEI ZA MWAKA 2015)

**Asilimia**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | **5.4** | 4.4 | 4.9 | 3.9 | 3.3 | 4.2 |
| Kilimo cha Mazao | 5.2 | 4.4 | 5.0 | 3.6 | 2.7 | 4.2 |
| Mifugo | 4.9 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 |
| Misitu | 4.9 | 4.8 | 3.2 | 3.5 | 3.1 | 4.3 |
| Uvuvi | 9.2 | 1.5 | 6.7 | 2.6 | 1.9 | 1.4 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 1.5 | 17.7 | 7.3 | 9.4 | 10.8 | 11.3 |
| Viwanda | 8.3 | 5.8 | 4.5 | 4.8 | 4.2 | 4.3 |
| Umeme | 5.8 | 7.2 | 5.5 | 10.0 | 7.6 | 3.9 |
| Maji safi na Maji taka | 7.4 | 6.9 | 5.8 | 6.5 | 5.5 | 2.5 |
| Ujenzi | 13.8 | 13.3 | 7.8 | 3.3 | 3.9 | 3.5 |
| Biashara na Matengenezo | 5.9 | 4.8 | 2.1 | 3.2 | 3.9 | 4.2 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 11.8 | 8.7 | 8.4 | 3.5 | 3.8 | 4.1 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 5.2 | 2.6 | -13.7 | 6.7 | 9.0 | 8.3 |
| Habari na Mawasiliano | 9.1 | 7.2 | 8.4 | 9.1 | 7.4 | 7.6 |
| Fedha na Bima | -0.5 | 4.5 | 3.1 | 4.2 | 9.2 | 12.2 |
| Upangishaji Majengo | 4.4 | 4.5 | 4.5 | 4.5 | 4.4 | 4.3 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 9.9 | 7.6 | 7.3 | 6.8 | 5.8 | 5.5 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 5.6 | 8.4 | 7.8 | 6.9 | 4.6 | 5.0 |
| Utawala na Ulinzi | 3.2 | 3.4 | 3.8 | 5.1 | 5.4 | 5.5 |
| Elimu | 6.6 | 6.9 | 3.3 | 5.1 | 5.3 | 6.2 |
| Afya na Huduma za Jamii | 8.4 | 5.0 | 6.5 | 5.7 | 5.4 | 6.0 |
| Sanaa na Burudani | 13.7 | 11.2 | -4.4 | 19.4 | 19.0 | 17.7 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 6.5 | 6.7 | 5.0 | 8.5 | 5.7 | 6.7 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **6.9** | **7.1** | **5.2** | **4.6** | **4.8** | **5.2** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 6.3 | 4.7 | -3.6 | 7.9 | 3.5 | 3.7 |
| **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **7.0** | **6.9** | **4.5** | **4.8** | **4.7** | **5.1** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo Na. 1.6: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI (BEI ZA MWAKA 2015)**



## Jedwali Na. 9: PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (BEI ZA MWAKA 2015)

**Asilimia**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | | | | | | |
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | **5.4** | **4.5** | **5.0** | **4.0** | **3.3** | **4.2** |
| Kilimo cha Mazao | 5.6 | 4.6 | 5.1 | 3.7 | 2.7 | 4.2 |
| Mifugo | 4.2 | 5.0 | 5.2 | 5.1 | 5.0 | 5.0 |
| Misitu | 5.2 | 4.8 | 3.2 | 3.5 | 3.1 | 4.3 |
| Uvuvi | 9.2 | 1.6 | 6.8 | 2.5 | 1.9 | 1.4 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 1.5 | 17.7 | 7.3 | 9.4 | 10.8 | 11.3 |
| Viwanda | 8.3 | 5.8 | 4.5 | 4.8 | 4.2 | 4.3 |
| Umeme | 5.8 | 7.2 | 5.5 | 10.0 | 7.6 | 3.9 |
| Maji safi na Maji taka | 5.6 | 7.2 | 6.2 | 6.7 | 5.5 | 2.5 |
| Ujenzi | 13.8 | 13.5 | 7.8 | 3.5 | 4.1 | 3.7 |
| Biashara na Matengenezo | 6.6 | 4.8 | 2.1 | 3.2 | 3.9 | 4.2 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 11.8 | 8.7 | 8.4 | 3.5 | 3.8 | 4.1 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 5.2 | 2.6 | -13.7 | 6.7 | 9.0 | 8.3 |
| Habari na Mawasiliano | 9.1 | 7.2 | 8.4 | 9.1 | 7.4 | 7.6 |
| Fedha na Bima | -0.5 | 4.5 | 3.1 | 4.2 | 9.2 | 12.2 |
| Upangishaji Majengo | 4.3 | 4.5 | 4.5 | 4.5 | 4.4 | 4.3 |
| Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 9.9 | 7.6 | 7.3 | 6.8 | 5.8 | 5.5 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 5.6 | 8.4 | 7.8 | 6.9 | 4.6 | 5.0 |
| Utawala na Ulinzi | 3.2 | 3.4 | 3.8 | 5.1 | 5.4 | 5.5 |
| Elimu | 6.6 | 6.9 | 3.3 | 5.1 | 5.3 | 6.2 |
| Afya na Huduma za Jamii | 8.4 | 5.0 | 6.5 | 5.7 | 5.4 | 6.0 |
| Sanaa na Burudani | 13.7 | 11.2 | -4.4 | 19.4 | 19.0 | 17.7 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 6.5 | 6.7 | 5.0 | 8.5 | 5.7 | 6.7 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **7.1** | **7.2** | **5.2** | **4.7** | **4.8** | **5.3** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 6.3 | 4.7 | -3.6 | 7.9 | 3.5 | 3.7 |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | 6.5 | 5.2 | 4.9 | 3.0 | 3.3 | 3.3 |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 5.0 | 3.9 | 4.2 | 3.5 | 3.5 | 4.5 |
| Mazao | 3.1 | 3.4 | 4.6 | 3.2 | 2.8 | 4.2 |
| Mifugo | 9.8 | 4.6 | 3.7 | 4.2 | 5.0 | 5.0 |
| Misitu | 1.7 | 4.6 | 3.4 | 3.3 | 3.1 | 4.3 |
| Uvuvi | 9.2 | 1.4 | 3.7 | 4.9 | 2.0 | 1.4 |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 14.1 | 5.8 | 4.4 | 5.9 | 5.5 | 2.5 |
| Ujenzi | 12.5 | 10.8 | 7.9 | 0.4 | 2.0 | -1.6 |
| Upangishaji Majengo | 9.9 | 4.4 | 4.6 | 4.1 | 4.4 | 4.3 |
| **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **7.0** | **6.9** | **4.5** | **4.8** | **4.7** | **5.1** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali Na. 10: PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO (BEI ZA MWAKA 2015)

**Shilingi Milioni**

| Aina ya Matumizi | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pato la Taifa kwa Gharama zake (GDPbp)** | **106,301,666** | **113,849,364** | **119,772,323** | **125,293,096** | **131,253,112** | **138,033,894** |
| **Kodi za uzalishaji** | **8,872,802** | **9,289,875** | **8,951,215** | **9,658,417** | **9,994,080** | **10,365,863** |
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)** | **115,174,468** | **123,139,239** | **128,723,538** | **134,951,513** | **141,247,193** | **148,399,757** |
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko(GDPmp)** | **115,174,468** | **123,139,239** | **128,723,538** | **134,951,513** | **141,247,193** | **148,399,757** |
| **Matumizi ya Mwisho (Final consumption)** | **77,496,083** | **79,584,578** | **83,532,038** | **87,480,181** | **89,503,360** | **91,967,299** |
| Serikali | 9,965,992 | 10,196,780 | 10,457,021 | 10,804,144 | 11,149,850 | 11,479,516 |
| Binafsi | 67,252,169 | 69,096,209 | 72,777,412 | 76,351,978 | 77,997,028 | 80,099,263 |
| Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii | 277,922 | 291,589 | 297,605 | 324,059 | 356,482 | 388,521 |
| **Ukuzaji rasilimali** | **45,155,626** | **48,650,734** | **51,210,017** | **54,636,423** | **61,112,749** | **62,629,847** |
| Rasilimali za kudumu | 46,824,212 | 53,293,526 | 56,436,601 | 58,860,660 | 63,270,605 | 66,300,057 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani ***(changes in Valuables)*** | 776,123 | 925,034 | 1,096,591 | 1,161,299 | 1,043,459 | 1,011,385 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | -2,444,709 | -5,567,827 | -6,323,175 | -5,385,536 | -3,201,316 | -4,681,595 |
| Mauzo nje | **15,273,479** | **18,015,712** | **14,958,602** | **17,301,312** | **20,307,688** | **22,703,984** |
| Bidhaa-fob | 7,559,698 | 9,941,744 | 10,400,109 | 11,030,299 | 11,055,648 | 10,787,776 |
| Huduma | 7,713,780 | 8,073,968 | 4,558,493 | 6,271,013 | 9,252,039 | 11,916,209 |
| Uagizaji | **20,850,950** | **21,717,641** | **19,867,913** | **24,412,030** | **32,068,975** | **30,664,707** |
| Bidhaa-fob | 17,374,220 | 18,560,540 | 17,441,130 | 21,500,877 | 27,899,126 | 26,674,466 |
| Huduma | 3,476,730 | 3,157,101 | 2,426,783 | 2,911,153 | 4,169,849 | 3,990,241 |
| Makosa na Mapungufu | -181,441 | -1,394,144 | -1,109,207 | -54,373 | 2,392,371 | 1,763,333 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 11: UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI ( BEI YA MIAKA INAYOHUSIKA)**

**Shilingi Milioni**

| **Aina** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 34,044,435 | 42,221,028 | 49,747,719 | 55,339,606 | 56,289,401 | 61,417,776 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,439,945 | 1,626,468 | 2,104,131 | 2,525,856 | 2,566,601 | 2,597,729 |
| Mitambo na Vifaa | 2,776,908 | 2,951,572 | 4,057,780 | 4,577,241 | 4,591,367 | 5,009,674 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 1,378,753 | 1,501,925 | 2,014,715 | 2,322,447 | 2,279,644 | 2,487,336 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 417,015 | 476,835 | 609,366 | 729,533 | 726,652 | 752,314 |
| Haki ya Umiliki,Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 1,084,906 | 1,232,987 | 1,585,327 | 1,727,139 | 1,793,793 | 1,957,221 |
| Rasilimali za kudumu | 41,141,962 | 50,010,814 | 60,119,039 | 67,221,823 | 68,247,459 | 74,222,050 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 1,215,104 | 1,273,337 | 1,838,290 | 1,954,173 | 1,916,891 | 1,981,135 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | -1,717,221 | -5,180,547 | -6,008,036 | -5,467,787 | -3,098,544 | -4,954,772 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **40,639,844** | **46,103,604** | **55,949,293** | **63,708,208** | **67,065,806** | **71,248,413** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 12: UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (BEI ZA MWAKA 2015)**

**Shilingi Milioni**

| **Aina** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 38,689,032 | 44,798,699 | 46,631,376 | 48,634,282 | 52,329,858 | 54,781,168 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,782,710 | 2,108,988 | 2,148,677 | 2,143,604 | 2,365,663 | 2,414,535 |
| Mitambo na Vifaa | 3,144,371 | 3,048,264 | 3,789,868 | 4,050,012 | 4,245,799 | 4,561,893 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 1,529,393 | 1,549,217 | 1,843,357 | 1,925,453 | 2,103,267 | 2,168,811 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 435,253 | 468,173 | 524,605 | 548,111 | 586,026 | 617,387 |
| Haki ya Umiliki,Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 1,243,454 | 1,320,184 | 1,498,719 | 1,559,197 | 1,639,992 | 1,756,264 |
| Rasilimali za kudumu | 46,824,212 | 53,293,526 | 56,436,601 | 58,860,660 | 63,270,605 | 66,300,057 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 776,123 | 925,034 | 1,096,591 | 1,161,299 | 1,043,459 | 1,011,385 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | -2,444,709 | -5,567,827 | -6,323,175 | -5,385,536 | -3,201,316 | -4,681,595 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **45,155,626** | **48,650,734** | **51,210,017** | **54,636,423** | **61,112,749** | **62,629,847** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 13: MCHANGO KATIKA RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

**Asilimia**

| **Aina** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 83.8 | 91.6 | 88.9 | 86.9 | 83.9 | 86.2 |
| Vifaa vya Usafiri | 3.5 | 3.5 | 3.8 | 4.0 | 3.8 | 3.6 |
| Mitambo na Vifaa | 6.8 | 6.4 | 7.3 | 7.2 | 6.8 | 7.0 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 3.4 | 3.3 | 3.6 | 3.6 | 3.4 | 3.5 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 1.0 | 1.0 | 1.1 | 1.1 | 1.1 | 1.1 |
| Haki ya Umiliki,Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 2.7 | 2.7 | 2.8 | 2.7 | 2.7 | 2.7 |
| Rasilimali za kudumu | 101.2 | 108.5 | 107.5 | 105.5 | 101.8 | 104.2 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 3.0 | 2.8 | 3.3 | 3.1 | 2.9 | 2.8 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | -4.2 | -11.2 | -10.7 | -8.6 | -4.6 | -7.0 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 14: UKUZAJI WA RASILIMALI KATIKA SEHEMU ZA UCHUMI WA KITAIFA NA BINAFSI (KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA)**

**Shilingi Milioni**

| **Sekta** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A. Rasilimali za kudumu | 41,141,962 | 50,010,814 | 60,119,039 | 67,221,823 | 68,247,459 | 74,222,050 |
| 1. Serikali: | 10,716,619 | 12,602,717 | 15,570,831 | 16,939,888 | 16,738,193 | 19,223,511 |
| 2. Mashirika: | 903,317 | 1,050,226 | 1,442,857 | 1,645,300 | 1,744,776 | 1,781,329 |
| 3. Taasisi: | 862,257 | 1,200,259 | 1,563,095 | 1,749,614 | 1,748,131 | 1,929,773 |
| 4. Sekta binafsi | 28,659,770 | 35,157,613 | 41,542,256 | 46,887,021 | 48,016,360 | 51,287,437 |
| C: Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 1,215,104 | 1,273,337 | 1,838,290 | 1,954,173 | 1,916,891 | 1,981,135 |
| D. Ongezeko la Limbikizo | -1,717,221 | -5,180,547 | -6,008,036 | -5,467,787 | -3,098,544 | -4,954,772 |
| **E. Jumla la Ukuzaji Rasilimali** | **40,639,844** | **46,103,604** | **55,949,293** | **63,708,208** | **67,065,806** | **71,248,413** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 15: FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA YA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (Des. 2015=100)**

| MWAKA | BIDHAA ZOTE | | ***VYAKULA NA VINYWAJI BARIDI | |
|---|---|---|---|---|
| | FAHIRISI | BADILIKO ASILIMIA | FAHIRISI | BADILIKO ASILIMIA |
| 2010 | 61.89 | 13.2 | 58.99 | 18.0 |
| 2011 | 66.48 | 7.4 | 63.16 | 7.1 |
| 2012 | 78.96 | 18.8 | 77.83 | 23.2 |
| 2013 | 86.34 | 9.3 | 85.98 | 10.5 |
| 2014 | 92.95 | 7.7 | 92.22 | 7.3 |
| 2015* | 97.97 | 5.4 | 97.67 | 5.9 |
| 2016 | 102.21 | 4.3 | 101.19 | 3.6 |
| 2017 | 104.10 | 1.9 | 104.67 | 3.4 |
| 2018 | 106.15 | 2.0 | 109.36 | 4.5 |
| 2019 | 110.13 | 3.8 | 114.38 | 4.6 |
| 2020 | 112.39 | 2.1 | 115.62 | 1.1 |
| **FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (Jan - Des. 2020 =100)** | | | | |
| 2016 | 90.9 | | 87.52 | |
| 2017 | 92.6 | 1.9 | 90.53 | 3.4 |
| 2018 | 94.4 | 2.0 | 94.59 | 4.5 |
| 2019 | 98.0 | 3.8 | 98.93 | 4.6 |
| **2020 | 100.00 | 2.1 | 100.00 | 1.1 |
| 2021 | 102.37 | 2.4 | 100.58 | 0.6 |
| 2022 | 107.16 | 7.2 | 108.16 | 7.5 |
| 2023 | 112.77 | 10.2 | 118.78 | 9.8 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Des. 2020 = 100)
***Jina limebadilika kutoka Kundi la chakula; toka des 2020 linasomeka vyakula na vinywaji baridi

**Jedwali Na. 16: FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIKAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 = 100)**

| Mwaka | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2016 | 87.52 | 96.37 | 90.95 | 81.16 | 92.80 | 94.57 | 109.22 | 98.54 | 95.16 | 91.47 | 96.60 | 91.76 | 95.45 | 90.94 |
| 2017 | 90.53 | 99.20 | 92.14 | 81.89 | 95.71 | 96.03 | 109.11 | 98.91 | 96.76 | 95.02 | 97.12 | 94.10 | 96.08 | 92.63 |
| 2018 | 94.59 | 99.20 | 95.03 | 86.58 | 97.53 | 96.10 | 95.51 | 98.82 | 97.84 | 100.22 | 97.23 | 96.17 | 97.49 | 94.44 |
| 2019 | 98.93 | 99.98 | 98.79 | 91.42 | 99.42 | 99.13 | 100.23 | 99.79 | 100.13 | 100.12 | 99.36 | 100.00 | 99.66 | 97.99 |
| 2020 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 |
| 2021 | 100.58 | 107.27 | 103.06 | 102.93 | 103.91 | 101.93 | 92.55 | 101.39 | 103.83 | 110.34 | 105.46 | 100.00 | 100.71 | 102.37 |
| 2022 | 108.16 | 107.86 | 106.86 | 106.97 | 110.42 | 104.89 | 90.61 | 103.25 | 117.66 | 112.84 | 108.58 | 100.00 | 104.23 | 107.16 |
| 2023 | 118.78 | 108.60 | 109.45 | 110.63 | 116.24 | 114.46 | 82.97 | 104.32 | 133.86 | 117.78 | 110.68 | 99.97 | 107.88 | 112.77 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 17: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (Des 2015 =100)**

| Mwaka | Miezi/ Robo-Mwaka | | | | | Badiliko Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | Wastani | |
| 2010 | 63.9 | 64.6 | 65.1 | 65.6 | 64.8 | 10.0 |
| 2011 | 67.9 | 69.3 | 70.3 | 72.1 | 69.9 | 7.9 |
| 2012 | 78.4 | 81.6 | 82.7 | 83.4 | 81.5 | 16.6 |
| 2013 | 87.6 | 88.6 | 88.5 | 88.4 | 88.3 | 8.3 |
| 2014 | 92.8 | 94.2 | 94.5 | 93.5 | 93.7 | 6.2 |
| 2015* | 96.5 | 98.9 | 100.6 | 100.0 | 99.0 | 5.6 |
| 2016 | 102.05 | 104.35 | 103.81 | 103.79 | 103.50 | 4.5 |
| 2017 | 104.48 | 106.72 | 106.65 | 107.02 | 106.22 | 2.6 |
| 2018 | 105.75 | 108.50 | 108.73 | 109.82 | 108.20 | 1.9 |
| 2019 | 111.91 | 113.48 | 112.96 | 113.96 | 113.08 | 4.5 |
| 2020 | 116.89 | 117.03 | 117.35 | 116.91 | 117.05 | 3.5 |
| **FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (Jan - Des. 2020=100)** | | | | | | |
| 2016 | 87.19 | 89.15 | 88.69 | 88.672602 | 88.43 | |
| 2017 | 89.3 | 91.2 | 91.1 | 91.4 | 90.75 | 2.6 |
| 2018 | 90.35 | 92.69 | 92.89 | 93.83 | 92.44 | 1.9 |
| 2019 | 95.62 | 96.95 | 96.51 | 97.36 | 96.61 | 4.5 |
| **2020 | 99.69 | 99.96 | 100.42 | 99.92 | 100.00 | 3.5 |
| 2021 | 101.71 | 102.57 | 101.87 | 103.45 | 102.40 | 2.4 |
| 2022 | 105.12 | 108.89 | 109.48 | 110.01 | 108.38 | 5.8 |
| 2023 | 112.37 | 113.39 | 113.78 | 113.63 | 113.72 | 4.9 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Des. 2020 = 100)
***Jina limebadilika kutoka Kundi la chakula; toka des 2020 linasomeka vyakula na vinywaji baridi

## Jedwali Na. 18: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 =100)

| | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2018 Robo ya kwanza | 87.41 | 99.43 | 93.46 | 82.62 | 96.44 | 94.88 | 94.15 | 98.17 | 97.69 | 100.03 | 96.12 | 100.00 | 95.48 | 90.35 |
| Robo ya pili | 92.18 | 99.43 | 94.58 | 84.42 | 97.15 | 95.01 | 94.50 | 98.07 | 98.37 | 100.03 | 96.12 | 100.00 | 96.96 | 92.69 |
| Robo ya tatu | 91.69 | 99.43 | 96.00 | 85.55 | 97.52 | 95.08 | 94.95 | 98.02 | 98.17 | 100.03 | 96.66 | 100.00 | 97.39 | 92.89 |
| Robo ya nne | 91.00 | 99.57 | 97.63 | 89.50 | 98.39 | 95.20 | 98.33 | 98.07 | 98.72 | 100.03 | 97.90 | 100.00 | 98.28 | 93.83 |
| 2019 Robo ya kwanza | 93.66 | 99.85 | 98.02 | 90.52 | 99.33 | 98.34 | 100.45 | 99.40 | 99.92 | 100.03 | 99.34 | 100.00 | 99.95 | 95.62 |
| Robo ya pili | 96.72 | 99.85 | 98.57 | 90.39 | 99.55 | 99.59 | 101.06 | 99.87 | 100.12 | 100.03 | 99.47 | 100.00 | 100.03 | 96.95 |
| Robo ya tatu | 95.12 | 99.85 | 99.20 | 91.58 | 99.39 | 99.60 | 101.06 | 99.15 | 101.01 | 100.03 | 99.45 | 100.00 | 99.44 | 96.51 |
| Robo ya nne | 97.19 | 99.85 | 99.17 | 92.21 | 99.71 | 99.69 | 100.61 | 99.30 | 99.70 | 100.03 | 99.04 | 100.00 | 99.67 | 97.36 |
| **2020 Robo ya kwanza | 101.46 | 99.85 | 99.85 | 96.53 | 99.93 | 99.71 | 100.93 | 99.54 | 99.97 | 100.00 | 99.05 | 100.00 | 99.25 | 99.87 |
| Robo ya pili | 99.72 | 99.85 | 99.96 | 101.49 | 99.99 | 100.04 | 99.31 | 100.15 | 99.99 | 100.00 | 99.05 | 100.00 | 99.88 | 99.99 |
| Robo ya tatu | 99.38 | 99.85 | 99.95 | 102.39 | 100.04 | 100.12 | 99.53 | 100.15 | 100.02 | 100.00 | 100.95 | 100.00 | 100.30 | 100.26 |
| Robo ya nne | 99.44 | 100.44 | 100.24 | 99.59 | 100.03 | 100.12 | 100.23 | 100.15 | 100.02 | 100.00 | 100.95 | 100.00 | 100.57 | 99.89 |
| 2021 Robo ya kwanza | 100.68 | 104.06 | 100.68 | 99.92 | 102.79 | 103.70 | 100.91 | 101.36 | 100.06 | 104.76 | 107.20 | 100.00 | 100.21 | 101.71 |
| Robo ya pili | 102.03 | 104.31 | 99.99 | 97.98 | 104.06 | 103.97 | 102.50 | 101.24 | 100.64 | 105.60 | 110.88 | 100.57 | 100.75 | 102.57 |
| Robo ya tatu | 99.63 | 103.90 | 100.16 | 97.71 | 104.07 | 103.97 | 103.47 | 101.25 | 100.57 | 105.53 | 110.88 | 100.57 | 100.69 | 101.87 |
| Robo ya nne | 102.36 | 104.56 | 101.79 | 99.97 | 105.36 | 104.32 | 103.99 | 101.54 | 100.55 | 105.54 | 111.53 | 100.57 | 100.99 | 103.45 |
| 2022 Robo ya kwanza | 104.28 | 104.70 | 102.85 | 103.83 | 107.30 | 104.48 | 104.25 | 101.62 | 115.16 | 105.54 | 112.88 | 100.57 | 102.20 | 105.12 |
| Robo ya pili | 111.70 | 104.70 | 102.92 | 105.35 | 107.68 | 105.19 | 111.04 | 101.59 | 116.25 | 106.11 | 114.50 | 100.55 | 104.65 | 108.89 |
| Robo ya tatu | 112.07 | 104.98 | 103.70 | 102.76 | 108.73 | 106.41 | 116.39 | 101.55 | 118.18 | 107.27 | 114.05 | 100.50 | 104.76 | 109.48 |
| Robo ya nne | 115.03 | 104.70 | 103.78 | 103.51 | 111.09 | 107.18 | 109.37 | 101.56 | 118.64 | 107.38 | 115.53 | 100.46 | 104.89 | 110.01 |
| 2023 Robo ya kwanza | 121.13 | 104.70 | 104.57 | 103.76 | 111.53 | 107.83 | 109.30 | 101.54 | 120.57 | 109.58 | 116.90 | 100.49 | 105.45 | 112.37 |
| Robo ya pili | 123.48 | 104.70 | 104.99 | 105.94 | 111.20 | 107.82 | 108.40 | 101.42 | 123.91 | 109.58 | 117.24 | 100.45 | 105.68 | 113.39 |
| Robo ya tatu | 120.59 | 112.05 | 106.94 | 106.05 | 113.29 | 111.18 | 113.17 | 101.55 | 126.12 | 109.58 | 117.83 | 100.41 | 110.01 | 113.78 |
| Robo ya nne | 121.68 | 114.61 | 109.24 | 109.89 | 115.50 | 111.20 | 115.27 | 101.69 | 127.72 | 109.58 | 118.07 | 100.52 | 110.03 | 115.33 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Des. 2020 = 100)

## Jedwali Na. 19: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 =100)

| | **Vyakula na Vinywaji Baridi** | **Vinywaji Vikali na Tumbaku** | **Mavazi na Viatu** | **Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo** | **Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi** | **Afya** | **Usafiri** | **Habari na Mawasiliano** | **Burudani, Michezo na Utamaduni** | **Huduma za Elimu** | **Migahawa na Huduma za Malazi** | **Huduma za Bima na Fedha** | **Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko** | **FAHIRISI BIDHAA ZOTE** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2018 Robo ya kwanza | 87.9 | 100.0 | 94.8 | 84.5 | 96.7 | 95.5 | 96.4 | 97.9 | 98.9 | 94.3 | 94.8 | 100.0 | 98.3 | 92.6 |
| Robo ya pili | 88.9 | 100.0 | 95.8 | 86.4 | 97.6 | 95.5 | 98.7 | 98.0 | 99.5 | 100.0 | 95.0 | 100.0 | 99.7 | 94.1 |
| Robo ya tatu | 89.8 | 99.6 | 97.0 | 87.1 | 97.9 | 95.5 | 99.8 | 98.0 | 99.8 | 100.0 | 95.6 | 100.0 | 100.6 | 94.9 |
| Robo ya nne | 89.5 | 99.7 | 97.6 | 88.7 | 98.2 | 95.4 | 101.4 | 98.0 | 99.3 | 100.0 | 97.7 | 100.0 | 100.8 | 95.6 |
| 2019 Robo ya kwanza | 90.9 | 99.8 | 97.9 | 89.1 | 99.3 | 98.4 | 101.5 | 99.4 | 99.8 | 100.0 | 99.6 | 100.0 | 100.8 | 96.4 |
| Robo ya pili | 93.6 | 99.8 | 98.5 | 94.5 | 99.6 | 99.8 | 102.3 | 99.9 | 100.4 | 100.0 | 99.7 | 100.0 | 100.8 | 98.1 |
| Robo ya tatu | 92.9 | 99.8 | 99.0 | 95.3 | 99.5 | 99.7 | 102.0 | 99.1 | 101.0 | 100.0 | 98.9 | 100.0 | 100.4 | 97.9 |
| Robo ya nne | 94.3 | 99.8 | 99.2 | 95.9 | 99.7 | 99.7 | 101.6 | 99.3 | 99.2 | 100.0 | 99.3 | 100.0 | 99.0 | 98.2 |
| **2020 Robo ya kwanza | 99.6 | 99.8 | 99.9 | 97.9 | 99.9 | 99.7 | 101.8 | 99.5 | 100.0 | 100.0 | 99.4 | 100.0 | 98.7 | 100.0 |
| Robo ya pili | 99.1 | 99.8 | 100.0 | 100.8 | 100.0 | 100.1 | 99.4 | 100.2 | 100.0 | 100.0 | 99.4 | 100.0 | 100.2 | 99.7 |
| Robo ya tatu | 100.0 | 99.8 | 100.0 | 101.4 | 100.1 | 100.1 | 99.4 | 100.2 | 100.0 | 100.0 | 100.6 | 100.0 | 100.5 | 100.1 |
| Robo ya nne | 101.3 | 100.7 | 100.2 | 99.8 | 100.1 | 100.1 | 99.5 | 100.2 | 100.0 | 100.0 | 100.6 | 100.0 | 100.6 | 100.3 |
| 2021 Robo ya kwanza | 102.8 | 104.6 | 102.6 | 100.3 | 107.1 | 102.9 | 100.6 | 101.3 | 98.6 | 102.4 | 105.4 | 100.0 | 100.7 | 102.2 |
| Robo ya pili | 104.7 | 113.5 | 103.1 | 99.7 | 108.1 | 103.3 | 101.7 | 101.0 | 98.6 | 103.6 | 107.4 | 100.2 | 101.6 | 103.1 |
| Robo ya tatu | 102.7 | 113.2 | 103.1 | 99.6 | 108.1 | 103.3 | 102.3 | 101.0 | 98.6 | 103.0 | 107.3 | 100.2 | 101.5 | 102.8 |
| Robo ya nne | 105.5 | 113.7 | 104.8 | 101.0 | 109.3 | 103.7 | 102.7 | 102.0 | 99.0 | 103.0 | 108.1 | 100.2 | 102.1 | 104.0 |
| 2022 Robo ya kwanza | 108.0 | 113.9 | 106.0 | 103.0 | 110.2 | 103.9 | 103.1 | 102.4 | 99.7 | 103.0 | 109.7 | 100.2 | 102.7 | 105.3 |
| Robo ya pili | 111.2 | 113.9 | 106.1 | 103.9 | 110.4 | 104.3 | 108.4 | 102.4 | 99.7 | 103.5 | 111.7 | 100.2 | 103.3 | 107.4 |
| Robo ya tatu | 107.9 | 113.9 | 107.0 | 103.0 | 110.7 | 105.6 | 113.1 | 102.3 | 101.9 | 104.3 | 111.3 | 100.1 | 103.6 | 107.8 |
| Robo ya nne | 108.5 | 113.5 | 107.6 | 104.1 | 112.0 | 107.7 | 106.9 | 102.5 | 102.5 | 104.4 | 112.5 | 100.0 | 105.7 | 107.1 |
| 2023 Robo ya kwanza | 112.9 | 113.6 | 108.2 | 104.6 | 112.3 | 109.2 | 107.2 | 102.8 | 102.5 | 105.0 | 115.1 | 100.1 | 106.2 | 108.5 |
| Robo ya pili | 114.0 | 113.6 | 108.4 | 105.4 | 112.1 | 109.3 | 106.6 | 102.8 | 102.3 | 105.0 | 115.7 | 100.0 | 107.4 | 108.8 |
| Robo ya tatu | 112.4 | 117.0 | 110.1 | 105.7 | 113.3 | 111.9 | 110.4 | 103.5 | 105.6 | 105.0 | 116.4 | 100.0 | 115.5 | 110.0 |
| Robo ya nne | 114.0 | 118.9 | 112.5 | 108.3 | 114.4 | 111.9 | 110.8 | 103.0 | 108.2 | 105.0 | 116.8 | 100.2 | 117.0 | 111.3 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Des. 2020 = 100)

**Jedwali Na. 20: FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Des. 2015=100)**

| Mwaka | Robo-Mwaka | | | | Wastani | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | | |
| 2010 | 63.41 | 64.89 | 65.82 | 66.29 | 65.10 | 8.1 |
| 2011 | 68.73 | 70.77 | 72.83 | 75.67 | 72.00 | 10.6 |
| 2012 | 78.04 | 79.50 | 80.40 | 82.20 | 80.04 | 11.2 |
| 2013 | 85.48 | 85.58 | 86.64 | 87.93 | 86.41 | 8.0 |
| 2014 | 90.61 | 90.68 | 91.84 | 93.27 | 91.60 | 6.0 |
| 2015* | 95.14 | 96.78 | 98.27 | 100.00 | 97.55 | 6.5 |
| 2016 | 101.02 | 102.52 | 102.43 | 102.81 | 102.20 | 4.8 |
| 2017 | 104.01 | 105.76 | 107.37 | 108.93 | 106.52 | 4.2 |
| 2018 | 109.52 | 111.24 | 112.15 | 113.00 | 111.48 | 4.7 |
| 2019 | 113.92 | 115.99 | 115.74 | 116.09 | 115.44 | 3.6 |
| 2020 | 118.15 | 117.85 | 118.31 | 118.52 | 118.21 | 2.4 |
| **FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Jan - Des. 2020 =100)** | | | | | | |
| 2016 | 85.46 | 86.73 | 86.65 | 86.98 | 86.45 | |
| 2017 | 87.99 | 89.47 | 90.83 | 92.16 | 90.11 | 4.2 |
| 2018 | 92.65 | 94.11 | 94.87 | 95.59 | 94.31 | 4.7 |
| 2019 | 96.37 | 98.13 | 97.92 | 98.21 | 97.66 | 3.6 |
| **2020 | 99.96 | 99.70 | 100.08 | 100.26 | 100.00 | 2.4 |
| 2021 | 102.17 | 103.08 | 102.81 | 104.03 | 103.02 | 3.0 |
| 2022 | 105.30 | 107.39 | 107.81 | 107.14 | 106.91 | 3.8 |
| 2023 | 108.47 | 108.78 | 110.02 | 111.25 | 109.63 | 2.5 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Des. 2020 = 100)

## Jedwali Na. 21: FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Des. 2020=100)

| Mwaka | Robo za Mwaka | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2018 | Robo ya kwanza | 94.0 | 97.4 | 94.0 | 81.5 | 93.4 | 97.2 | 94.4 | 100.9 | 99.1 | 96.7 | 94.1 | 96.5 | 95.7 | 92.9 |
| | Robo ya pili | 95.6 | 97.1 | 94.6 | 85.8 | 94.4 | 97.4 | 95.1 | 100.2 | 98.2 | 96.9 | 94.2 | 97.0 | 96.7 | 94.3 |
| | Robo ya tatu | 92.7 | 97.8 | 95.5 | 87.6 | 95.0 | 97.6 | 95.5 | 98.5 | 98.1 | 97.2 | 94.5 | 97.0 | 96.9 | 93.6 |
| | Robo ya nne | 91.1 | 98.8 | 96.2 | 89.6 | 95.6 | 97.8 | 97.5 | 98.5 | 98.4 | 97.2 | 95.4 | 98.6 | 97.3 | 93.6 |
| 2019 | Robo ya kwanza | 94.4 | 100.0 | 97.3 | 91.6 | 97.3 | 98.5 | 98.0 | 99.3 | 98.9 | 98.6 | 97.5 | 100.0 | 98.3 | 95.7 |
| | Robo ya pili | 97.3 | 100.6 | 97.8 | 94.2 | 98.3 | 99.4 | 99.0 | 100.0 | 101.6 | 98.8 | 98.7 | 100.0 | 99.1 | 97.6 |
| | Robo ya tatu | 96.0 | 100.1 | 98.1 | 93.1 | 98.6 | 99.4 | 98.7 | 99.5 | 99.8 | 98.8 | 98.8 | 100.0 | 99.3 | 96.9 |
| | Robo ya nne | 96.4 | 99.9 | 98.4 | 93.1 | 98.9 | 99.4 | 98.7 | 99.5 | 99.4 | 98.8 | 99.0 | 100.0 | 99.3 | 97.1 |
| 2020* | Robo ya kwanza | 98.8 | 99.5 | 99.5 | 98.1 | 99.4 | 99.4 | 101.1 | 99.1 | 100.5 | 99.9 | 99.5 | 100.0 | 99.6 | 99.2 |
| | Robo ya pili | 101.2 | 99.9 | 100.1 | 100.6 | 100.0 | 99.9 | 101.3 | 100.0 | 100.6 | 100.0 | 99.7 | 100.0 | 100.2 | 100.7 |
| | Robo ya tatu | 100.1 | 100.3 | 100.1 | 100.6 | 100.3 | 100.3 | 98.7 | 100.2 | 100.1 | 100.0 | 100.4 | 100.0 | 100.2 | 100.0 |
| | Robo ya nne | 99.9 | 100.3 | 100.3 | 100.8 | 100.3 | 100.4 | 98.9 | 100.7 | 98.8 | 100.1 | 100.5 | 100.0 | 99.9 | 100.1 |
| 2021 | Robo ya kwanza | 102.3 | 101.4 | 103.7 | 103.1 | 102.6 | 102.0 | 101.9 | 101.2 | 102.5 | 100.9 | 103.5 | 100.2 | 102.3 | 102.5 |
| | Robo ya pili | 106.0 | 102.3 | 104.5 | 104.2 | 103.0 | 102.5 | 103.1 | 101.8 | 102.9 | 101.2 | 105.1 | 100.3 | 102.6 | 104.2 |
| | Robo ya tatu | 104.3 | 102.5 | 104.8 | 104.5 | 103.3 | 103.1 | 103.9 | 102.0 | 103.0 | 101.2 | 105.3 | 100.3 | 103.0 | 103.9 |
| | Robo ya nne | 104.3 | 102.8 | 105.3 | 104.7 | 103.9 | 103.3 | 104.5 | 102.3 | 102.6 | 101.2 | 105.6 | 100.3 | 103.3 | 104.2 |
| 2022 | Robo ya kwanza | 108.7 | 103.2 | 106.5 | 106.6 | 105.6 | 103.6 | 105.6 | 102.4 | 104.0 | 101.4 | 106.5 | 100.4 | 104.6 | 106.3 |
| | Robo ya pili | 112.4 | 103.5 | 106.8 | 108.6 | 106.3 | 103.9 | 110.0 | 102.5 | 104.0 | 101.6 | 107.2 | 100.5 | 105.2 | 108.4 |
| | Robo ya tatu | 112.2 | 103.5 | 107.3 | 108.3 | 107.2 | 104.4 | 112.4 | 102.7 | 104.4 | 101.9 | 107.3 | 100.5 | 105.3 | 108.8 |
| | Robo ya nne | 114.2 | 103.6 | 107.9 | 107.9 | 108.0 | 104.9 | 110.5 | 103.5 | 104.7 | 101.9 | 108.3 | 100.1 | 105.8 | 109.3 |
| 2023 | Robo ya kwanza | 119.35 | 103.76 | 109.16 | 108.19 | 108.67 | 105.39 | 111.89 | 104.06 | 105.28 | 104.65 | 109.62 | 100.28 | 106.46 | 111.40 |
| | Robo ya pili | 121.89 | 104.86 | 110.25 | 109.44 | 109.33 | 105.56 | 111.84 | 104.33 | 105.94 | 105.10 | 111.90 | 100.09 | 107.22 | 112.69 |
| | Robo ya tatu | 118.66 | 107.31 | 110.81 | 109.66 | 111.01 | 106.34 | 113.18 | 104.73 | 107.02 | 105.32 | 112.85 | 100.74 | 109.44 | 112.42 |
| | Robo ya nne | 118.16 | 107.66 | 111.26 | 110.72 | 111.77 | 106.38 | 113.95 | 104.88 | 108.07 | 105.48 | 113.21 | 100.74 | 109.85 | 112.73 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Des. 2020 = 100)

**Jedwali Na. 22: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Des 2015 = 100)**

| Mwaka | Robo ya Mwaka | | | | Wastani wa Fahirisi | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya pili | Robo ya tatu | Robo ya nne | | |
| 2010 | 61.3 | 62.1 | 61.9 | 62.4 | 61.9 | 5.5 |
| 2011 | 65.8 | 68.2 | 71.0 | 74.2 | 69.8 | 12.7 |
| 2012 | 78.58 | 80.51 | 81.42 | 83.38 | 80.97 | 16.0 |
| 2013 | 86.71 | 87.31 | 86.94 | 88.42 | 87.35 | 7.9 |
| 2014 | 91.94 | 92.90 | 92.70 | 93.27 | 92.70 | 6.1 |
| 2015* | 95.75 | 97.83 | 98.54 | 99.42 | 97.88 | 5.6 |
| 2016 | 101.36 | 102.97 | 103.28 | 104.18 | 102.95 | 5.2 |
| 2017 | 107.11 | 109.13 | 108.60 | 108.85 | 108.42 | 5.3 |
| 2018 | 111.39 | 113.08 | 112.19 | 112.25 | 112.23 | 3.5 |
| 2019 | 114.75 | 117.03 | 116.18 | 116.44 | 116.10 | 3.4 |
| 2020 | 118.91 | 120.78 | 119.97 | 120.02 | 119.92 | 3.3 |
| **FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Jan - Des. 2020 = 100)** | | | | | | |
| **2020 | 99.16 | 100.72 | 100.04 | 100.08 | 100.00 | |
| 2021 | 102.46 | 104.16 | 103.94 | 104.20 | 103.69 | 3.7 |
| 2022 | 106.29 | 108.41 | 108.80 | 109.30 | 108.20 | 4.3 |
| 2023 | 111.40 | 112.69 | 112.42 | 112.73 | 112.31 | 3.8 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Des. 2020 = 100)

**Jedwali Na. 23: FAHIRISI ZA BEI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA ( Des. 2015=100)**

| Mwaka | FAHIRISI | | | WAKAZI MIJINI TANZ. BARA | BADILIKO% | | | WAKAZI MIJINI TANZ. BARA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KIPATO CHA | | | | KIPATO CHA | | | |
| | CHINI | KATI | JUU | | CHINI | KATI | JUU | |
| 2010* | 61.9 | 64.8 | 65.1 | 61.9 | 13.2 | 10.0 | 8.1 | 5.5 |
| 2011 | 66.5 | 69.9 | 72.0 | 69.8 | 7.4 | 7.9 | 10.6 | 12.7 |
| 2012 | 79.0 | 81.5 | 80.0 | 81.0 | 18.8 | 16.6 | 11.2 | 16.0 |
| 2013 | 86.3 | 88.3 | 86.4 | 87.3 | 9.3 | 8.3 | 8.0 | 7.9 |
| 2014 | 93.0 | 93.7 | 91.6 | 92.7 | 7.7 | 6.2 | 6.0 | 6.1 |
| 2015* | 98.0 | 99.0 | 97.5 | 97.9 | 5.4 | 5.6 | 6.5 | 5.6 |
| 2016 | 102.2 | 103.5 | 102.2 | 102.9 | 4.3 | 4.5 | 4.8 | 5.2 |
| 2017 | 104.1 | 106.2 | 106.5 | 108.4 | 1.9 | 2.6 | 4.2 | 5.3 |
| 2018 | 106.1 | 108.2 | 111.5 | 112.2 | 2.0 | 1.9 | 4.7 | 3.5 |
| 2019 | 110.1 | 113.1 | 115.4 | 116.1 | 3.8 | 4.5 | 3.6 | 3.4 |
| 2020 | 112.4 | 117.0 | 118.2 | 119.9 | 2.1 | 3.5 | 2.4 | 3.3 |
| **FAHIRISI ZA BEI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA ( Jan - Des. 2020 =100)** | | | | | | | | |
| **2020 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | | | | |
| 2021 | 102.37 | 102.40 | 103.02 | 103.69 | 2.4 | 2.4 | 3.0 | 3.7 |
| 2022 | 107.16 | 108.38 | 106.91 | 108.20 | 4.7 | 5.8 | 3.8 | 4.3 |
| 2023 | 112.77 | 113.72 | 109.63 | 112.31 | 5.2 | 4.9 | 2.5 | 3.8 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Des. 2020 = 100)


## SURA YA 2

## FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA

**Ujazi wa Fedha**

32. Mwaka 2023, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha kwa lengo la kupunguza ongezeko la ukuaji wa ukwasi katika uchumi, kudhibiti mfumuko wa bei uliotokana na kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na kuendelea kuchangia ukuaji wa uchumi. Katika kipindi hicho, ukuaji wa ujazi wa fedha ulikuwa sambamba na mahitaji ya shughuli za kiuchumi ambapo ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 14.1 na kufikia shilingi bilioni 44,002.6 mwaka 2023 kutoka shilingi bilioni 38,580.0 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 11.9 na kufikia shillingi billioni 34,001.7 mwaka 2023 kutoka shilingi billioni 30,378.9 mwaka 2022. Vile vile, ujazi wa fedha kwa tasfiri finyu (M1) uliongezeka kwa asilimia 8.7 na kufikia shilingi bilioni 20,601.6 mwaka 2023 kutoka shilingi bilioni 18,948.2 mwaka 2022.

**Kielelezo Na. 2.1: Ukuaji wa Ujazi wa Fedha Mwaka 2018 - 2023**




**Mikopo kwa Sekta Binafsi**

33. Mwaka 2023, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 32,057.6 kutoka shilingi bilioni 27,372.5 mwaka 2022, sawa na ukuaji wa asilimia 17.1 ikilinganishwa na lengo la asilimia 16.4. Ukuaji huo ulitokana na maboresho katika mazingira ya biashara na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini. Katika kipindi hicho, mikopo katika sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 43.5 kutokana na matokeo ya hatua za kisera zilizochukuliwa Julai 2021 zilizolenga kuongeza mikopo na kushusha viwango vya


riba katika sekta ya kilimo. Aidha, mikopo katika sekta ya uchimbaji madini ilikua kwa asilimia 36.4, ujenzi asilimia 23.5 na mikopo kwa shughuli binafsi asilimia 18.1. Kwa upande mwingine, sehemu kubwa ya mikopo iliendelea kuelekezwa katika shughuli binafsi (ikihusisha biashara ndogo na za kati), sawa na asilimia 38.2 ya mikopo yote, ikifuatiwa na shughuli za biashara asilimia 14, kilimo asilimia 10.4 na viwanda asilimia 9.8.

**Jedwali Na. 2.1: Mikopo Iliyotolewa na Benki za Biashara kwa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi (Shilingi Bilioni)**

| Shughuli | Kipindi Kinachoishia mwezi Desemba (Shilingi Bilioni) | | | | | | | Ukuaji (Asilimia) | | Mchango (Asilimia) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2022 | 2023 | 2022 | 2023 |
| Kilimo | 1,134.8 | 952.9 | 1,824.3 | 1,725.6 | 1,592.5 | 2,327.4 | 3,340.8 | 46.1 | 43.5 | 8.5 | 10.4 |
| Uchimbaji madini na mawe | 292.6 | 375.2 | 424.5 | 429.4 | 474.0 | 575.9 | 785.4 | 21.5 | 36.4 | 2.1 | 2.4 |
| Uzalishaji viwandani | 1,777.6 | 2,087.9 | 2,086.8 | 1,878.4 | 2,111.1 | 2,709.5 | 3,132.0 | 28.3 | 15.6 | 9.9 | 9.8 |
| Ujenzi | 837.2 | 643.3 | 1,129.9 | 1,072.3 | 998.4 | 1,200.6 | 1,483.1 | 20.3 | 23.5 | 4.4 | 4.6 |
| Uchukuzi na mawasiliano | 975.6 | 918.0 | 1,059.6 | 1,142.4 | 1,053.9 | 1,207.0 | 1,420.3 | 14.5 | 17.7 | 4.4 | 4.4 |
| Biashara | 3,306.9 | 3,228.9 | 3,379.5 | 3,054.9 | 3,657.3 | 4,556.4 | 4,473.4 | 24.6 | -1.8 | 16.6 | 14.0 |
| Mahoteli na migahawa | 595.0 | 587.3 | 555.0 | 549.5 | 542.7 | 511.3 | 534.0 | -5.8 | 4.4 | 1.9 | 1.7 |
| Umeme | 335.2 | 358.1 | 225.3 | 114.7 | 143.9 | 130.3 | 291.3 | -9.5 | 123.6 | 0.5 | 0.9 |
| Shughuli binafsi | 3,258.7 | 5,019.5 | 5,485.5 | 6,793.9 | 8,047.7 | 10,365.7 | 12,238.0 | 28.8 | 18.1 | 37.9 | 38.2 |
| Shughuli nyinginezo | 4,381.9 | 3,555.7 | 3,525.0 | 3,547.2 | 3,722.5 | 3,788.3 | 4,359.4 | 1.8 | 15.1 | 13.8 | 13.6 |
| **Jumla** | **16,895.4** | **17,726.8** | **19,695.4** | **20,308.3** | **22,344.1** | **27,372.5** | **32,057.6** | **22.5** | **17.1** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 2.2: Mchango wa Mikopo Iliyotolewa na Benki za Biashara katika baadhi ya Shughuli za Kiuchumi (Asilimia)**



**Amana katika Benki za Biashara**

34. Mwaka 2023, amana za benki za biashara zilifikia shilingi bilioni 36,501.1 kutoka shilingi bilioni 31,429.4 mwaka 2022, sawa na ukuaji wa asilimia 16.1. Ukuaji huo ulichangiwa na ongezeko la huduma za uwakala wa benki na matumizi ya mifumo ya kidigitali katika kutoa huduma za fedha. Katika kipindi hicho, amana za sekta binafsi zilifikia shilingi bilioni 35,345.0, sawa na asilimia 96.8 ya amana zote kutoka shilingi bilioni 30,724.9 mwaka 2022. Hadi Desemba 2023, uwiano wa amana za fedha za kigeni kwa amana zote ulifikia asilimia 25.6 kutoka asilimia 24.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Mwenendo wa Viwango vya Riba**

35. Mwaka 2023, wastani wa riba ya jumla katika soko la fedha baina ya mabenki ulifikia asilimia 5.37 ikilinganishwa na asilimia 4.53 mwaka 2022. Aidha, riba ya jumla ya dhamana za Serikali za muda mfupi ilifikia asilimia 7.32 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.64 mwaka 2022.


36. Mwaka 2023, Serikali kwa kushirikiana na wadau iliendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya biashara kwa lengo la kuhamasisha benki na taasisi za fedha kupunguza na kuweka viwango rafiki vya riba za mikopo na hivyo, kuwezesha wananchi wengi kupata na kufikia huduma rasmi za kifedha. Katika kipindi hicho, viwango vya riba za mikopo vilipungua kwa kasi ndogo ambapo wastani wa riba za jumla za mikopo ulikuwa asilimia 15.75 ikilinganishwa na asilimia 16.18 mwaka 2022. Viwango vya riba za mikopo ya mwaka mmoja vilipungua na kufikia wastani wa asilimia 16.53 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 16.79 mwaka 2022. Aidha, wastani wa riba za amana za muda maalum ulipungua hadi asilimia 7.07 mwaka 2023 kutoka asilimia 7.11 mwaka 2022. Kwa upande mwingine, wastani wa riba za amana za mwaka mmoja uliongezeka na kufikia asilimia 8.65 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 8.53 mwaka 2022. Kutokana na mwenendo huo, tofauti kati ya viwango vya riba za mikopo ya mwaka mmoja na riba za amana za mwaka mmoja ilipungua kufikia wastani wa asilimia 7.88 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 8.26 mwaka 2022

**Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania**

37. Mwaka 2023, thamani ya Shilingi dhidi ya sarafu za nchi washirika wakuu wa kibiashara iliendelea kuwa tulivu licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika uchumi wa dunia, hususan utekelezaji wa sera ya fedha katika nchi zilizoendelea uliolenga kupunguza ukwasi katika kukabiliana na mfumuko wa bei. Katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,395.7 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,314.5 mwaka 2022. Aidha, thamani ya shilingi ilishuka kwa asilimia 3.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 0.2 mwaka 2022. Vile vile, katika kipindi kilichoishia Desemba mwaka 2023, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi

2,516.0 ikilinganishwa na shilingi 2,320.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na kupungua kwa thamani ya shilingi kwa asilimia 8.4 Desemba 2023 ikilinganishwa na asilimia 0.56 Desemba 2022. Kupungua kwa thamani ya shilingi kulichangiwa na hatua zilizochukuliwa na nchi zilizoendelea katika kukabiliana na mfumuko wa bei ikiwemo utekelezaji wa sera ya fedha yenye lengo la kupunguza ujazi wa fedha. Utekelezaji wa sera hiyo ulisababisha kupanda kwa viwango vya riba ya dola ya Marekani kutoka asilimia 3.78 Novemba 2022 hadi asilimia 5.5 Agosti 2023 na hivyo, kuvutia uwekezaji katika masoko ya fedha ya Marekani na kusababisha upungufu wa dola katika mataifa mengine. Katika kuimarisha utulivu wa shilingi, Benki Kuu ya Tanzania ilichukua hatua mbalimbali zilizowezesha kuongeza fedha za kigeni katika soko la fedha za kigeni, ikiwemo kuuza dola pamoja na kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kupunguza ukwasi wa shilingi. Aidha, Serikali ilianzisha mkakakti wa kuimarisha sekta za uzalishaji na huduma ikiwemo kilimo, uvuvi, samaki, utalii, madini na nishati mwaka 2023 kwa lengo la kuongeza mauzo nje na mapato ya fedha za kigeni.

**Kielelezo Na. 2.3: Mwenendo wa Thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani (Soko la Jumla - IFEM)**




## MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA

### Huduma za Benki

38. Hadi Desemba 2023, idadi ya benki ilifikia 44 kutoka benki 45 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kupungua kwa idadi ya benki kulitokana na kuhamishwa kwa mali na madeni ya Yetu Microfinance Bank Plc kwenda NMB Bank Plc. Aidha, matawi ya benki yaliongezeka na kufikia 1,011 mwaka 2023 kutoka matawi 998 mwaka 2022. Hadi Desemba 2023, amana za wateja zilifikia shilingi bilioni 37,980.8 kutoka shilingi bilioni

32,526.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 16.8. Kwa upande mwingine, mikopo kwa wateja ilifikia shilingi bilioni 33,194.4 kutoka shilingi bilioni 27,309.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 21.6.

**Huduma za Mawakala wa Benki**

39. Mwaka 2023, benki 31 zilitoa huduma za benki kwa njia ya uwakala ikilinganishwa na benki 28 mwaka 2022. Aidha, idadi ya mawakala wa benki iliongezeka kwa asilimia 41.1 na kufikia mawakala 106,176 mwaka 2023 kutoka mawakala 75,238 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilichangiwa na hatua ya Benki Kuu ya Tanzania kuendelea kulegeza masharti ya usajili wa mawakala wa benki ikiwemo, kuondoa sharti la kutoa huduma za fedha kwa njia ya uwakala wa benki kwa kipindi cha miezi 18 ili kupata leseni ya kuwa wakala wa benki ambapo kwa sasa sharti ni kuwa na kitambulisho cha Taifa.

**Mwenendo wa Viashiria vya Sekta ya Benki**

40. Mwaka 2023, uwiano wa mtaji halisi na mtaji mkuu kwa mali hatarishi ulikuwa asilimia 17.7 na asilimia 18.4 ikilinganishwa na asilimia 18.0 na asilimia 18.9 mtawalia katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, uwiano wa ukwasi katika benki ulipungua hadi asilimia 28.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 29.4 mwaka 2022. Hii ilitokana na sekta ndogo ya benki kuendelea kuwa thabiti na kuongezeka kwa imani ya wananchi.

41. Mwaka 2023, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua na kufikia wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2022. Kupungua kwa mikopo chechefu kulitokana na hatua mbalimbali zilizoendelea kuchukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania zikiwemo: kuongeza ufuatiliaji wa utoaji mikopo na kuwaondoa wafanyakazi wa benki wasio waaminifu; kuzielekeza benki kutumia ripoti za mikopo kutoka kwa kampuni za kuchakata na kutunza kumbukumbu za mikopo; utekelezaji wa kanuni za kuwalinda walaji wa huduma za fedha za mwaka 2019 kwa kuhakikisha utunzaji wa haki na usawa kwa wakopaji; na kuzitaka benki na taasisi za fedha kuimarisha taratibu za utoaji na ufuatiliaji wa mikopo. Aidha, idadi ya taasisi zilizotumia kanzidata ya wakopaji iliongezeka na kufikia 181 mwaka 2023 ikilinganishwa na taasisi 166 mwaka 2022. Vile vile, idadi ya wakopaji waliosajiliwa kwenye Kanzidata ya Wakopaji iliongezeka na kufikia 8,134,863 ikilinganishwa na wakopaji 5,035,031 mwaka 2022.

**Maboresho katika Sekta ya Benki**

42. Mwaka 2023, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutoa kanuni na miongozo mbalimbali ya kusimamia benki na taasisi za fedha ili kuhakikisha sekta ya benki inabaki kuwa thabiti, imara na himilivu. Katika kipindi hicho, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa kanuni mbalimbali ikiwemo: kanuni za usimamizi wa biashara ya fedha za kigeni; kanuni za kutoa leseni ya benki na taasisi za fedha; kanuni za utawala bora wa benki na taasisi za fedha; kanuni za usimamizi wa benki za maendeleo; kanuni za mitaji ya benki na taasisi za fedha; kanuni za ukwasi wa benki na taasisi za fedha; kanuni za kuchukua hatua stahiki kwa benki

na taasisi za fedha; na kanuni za usimamizi wa mikopo ya karadha kwa benki na taasisi za fedha. Aidha, Benki Kuu ilitoa miongozo ya matumizi ya fedha za kigeni katika kufanya malipo ndani ya nchi pamoja na utekelezaji wa makubaliano ya pili na tatu kuhusu usimamizi wa benki na taasisi za fedha (Basel II na III).

**Huduma Ndogo za Fedha**

43. Mwaka 2023, Benki Kuu ilipokea maombi ya leseni 2,221 kutoka kwa watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili, ambapo watoa huduma 1,579 walipata leseni ikilinganishwa na maombi 1,558 na leseni 1,095 zilizotolewa mwaka 2022. Katika kipindi hicho, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ilipokea maombi ya leseni 1,215 ya watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la tatu ambapo leseni 884 zilitolewa ikilinganishwa na maombi 1,117 na leseni 759 zilizotolewa mwaka 2022. Aidha, maombi 49,026 ya watoa huduma za fedha wa daraja la nne yalipokelewa na vikundi 48,284 vilisajiliwa mwaka 2023 ikilinganishwa na maombi 37,282 na vikundi 34,127 vilivyosajiliwa mwaka 2022. Maombi yaliyokataliwa yalitokana na kutokidhi vigezo vya daraja husika kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo katika sekta ya huduma ndogo za fedha.

**Huduma Jumuishi za Fedha**

44. Kwa mujibu wa Taarifa ya Utafiti wa FinScope ya mwaka 2023, kiwango cha upatikanaji na matumizi ya huduma rasmi za kifedha na bidhaa kiliongezeka hadi asilimia 76 na asilimia 89 mwaka 2023 kutoka asilimia 65 na asilimia 86 mtawalia mwaka 2017. Hii ilitokana na kasi ya ukuaji wa sekta ya fedha uliochagizwa na ongezeko kubwa la matumizi ya teknolojia katika kuunda na kusambaza huduma na bidhaa za kifedha. Uwepo wa wigo mpana wa upatikanaji wa huduma na bidhaa rasmi za fedha uliwezesha watu binafsi na jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kuboresha maisha yao.

45. Mwaka 2023, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya fedha iliandaa Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha (2023 - 2028) unaolenga kuongeza kasi na kupanua wigo wa upatikanaji wa bidhaa na matumizi ya huduma rasmi za fedha hadi asilimia 95 na asilimia 85 ifikapo mwaka 2028 kutoka asilimia 89 na asilimia 76 mtawalia mwaka 2023. Katika kipindi hicho, Muundo wa Mawasiliano wa Masuala ya Huduma Jumuishi za Fedha uliandaliwa.

**Masoko ya Mitaji na Dhamana**

46. Mwaka 2023, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana - CMSA iliendelea kuchambua na kuidhinisha miamala ya uuzaji wa dhamana mbalimbali kwa lengo la kuongeza idadi ya bidhaa katika masoko ya mitaji. Katika kipindi hicho, bidhaa zilizoidhinishwa ni pamoja na:

i. Hatifungani yenye mguso na matokeo chanya kwa Jamii - NMB Jamii Bond yenye thamani ya shilingi trilioni moja ambapo Benki ya NMB ilipata idhini ya kutoa hatifungani hii kwa awamu 10 kwa lengo la kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa

biashara na miradi endelevu ya jamii ikiwemo, miradi inayomilikiwa na vijana. Katika awamu ya kwanza ya mauzo ya hatifungani hii, jumla ya shilingi bilioni 212.94 zilipatikana. Aidha, CMSA ilitoa idhini kwa benki ya NMB kuuza hatifungani hii katika fedha za kigeni, ambapo kiasi cha dola za Marekani milioni 73 kilipatikana ikilinganishwa na lengo la dola za Marekani milioni 10;

ii. Hatifungani ya kijani - CRDB Kijani Bond yenye thamani ya shilingi bilioni 780, sawa na dola za Marekani milioni 300 iliyolenga kupata fedha za kutekeleza biashara na miradi rafiki kwa mazingira ambayo itatolewa kwa awamu tano. Katika awamu ya kwanza jumla ya shilingi bilioni 171.83 zilipatikana;

iii. Hatifungani aina ya Sukuk iliyotolewa na Taasisi ya Fedha Imaan kwa ajili ya kupata fedha za kutekeleza biashara ndogo na za kati zilizokidhi misingi ya Shariah. Baada ya mauzo jumla ya shilingi bilioni 11.32 zilipatikana ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 5;

iv. Hatifungani kwa ajili ya kuendeleza sekta ya nyumba na makazi iliyotolewa na Kampuni ya *Tanzania Mortgage Refinance* ambapo jumla ya shilingi bilioni 11.28 zilipatikana;

v. Hatifungani ya Kijani ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Jiji la Tanga inayowezesha kupata fedha za kutekeleza shughuli za kuboresha miundombinu ya maji na utunzaji wa mazingira iliyoidhinishwa Desemba 2023. Aidha, mauzo yalifanyika Februari 2024 ambapo jumla ya shilingi bilioni 54.1 zilipatikana, sawa na asilimia 102 ya lengo la shilingi bilioni 53.12; na

vi. Mauzo ya Hisa Stahiki za kampuni ya TCCIA Investment Plc kwa wanahisa wake kwa lengo la kukuza uwekezaji wa kampuni katika dhamana mbalimbali za masoko ya mitaji. Mauzo ya hisa stahiki 72,957,660 za kampuni ya TCCIA Investment Plc yalifanyika kwa wanahisa kwa bei ya shilingi 145 kwa kila hisa katika uwiano wa hisa moja mpya kwa kila hisa moja aliyokuwanayo mwekezaji, ambapo jumla ya shilingi bilioni 10.58 zilipatikana.

47. Hadi Desemba 2023, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilitoa leseni 184 ikilinganishwa na leseni 166 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Leseni hizo zilitolewa kama ifuatavyo: Soko la Hisa la Dar es Salaam (1); Soko la Bidhaa Tanzania (1); Hifadhi Kuu ya Dhamana (1); kampuni za utendaji katika Soko la Hisa (18); Watendaji katika Soko la Bidhaa (5); Watendaji katika Soko la Hatifungani (8); Washauri Wateule (6); Washauri wa Uwekezaji (23); Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (10); Mameneja wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (12); Watunza Dhamana (7); na Wawakilishi wa Taasisi zinazotoa huduma katika masoko ya mitaji (92).

48. Hadi Desemba 2023, mtaji wa Soko la Hisa la Dar es Salaam - DSE kwa kampuni za ndani uliongezeka kwa asilimia 10.9 na kufikia shilingi trilioni 11.40 ikilinganishwa na shilingi trilioni 10.28 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa. Kampuni hizo ni pamoja na: CRDB Bank Plc, NMB Bank Plc, DSE Plc, National Investment Company Limited, Swissport Tanzania Plc, Twiga Cement Plc, Tanga Cement Plc, Tanzania Breweries Plc na Tanzania Cigarette Plc. Hata hivyo, mtaji wa jumla wa soko la hisa ulipungua kwa asilimia 6.9 na kufikia shilingi trilioni 14.6 ikilinganishwa na shilingi trilioni 15.68 katika kipindi kilichoishia Desemba 2022. Kupungua kwa mtaji wa jumla wa soko la hisa kulitokana na kushuka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam kutoka Soko la Hisa la Nairobi ambazo ni pamoja na National Media Group, Jubilee Holding Limited, Kenya Airways na KCB Group Plc.

49. Hadi Desemba 2023, fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni za ndani iliongezeka kwa asilimia 10.7 na kufikia alama 4,304.40 ikilinganishwa na alama 3,888.81 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kuongezeka kwa fahirisi kunaonesha ufanisi katika soko la hisa kwa kampuni za ndani, hususan kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam zinazotoa huduma katika sekta za viwanda na fedha. Kwa upande mwingine, fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni zote ilipungua kwa asilimia 7.0 na kufikia alama 1,750.63 mwaka 2023 ikilinganishwa na alama 1,881.99 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kupungua kwa fahirisi kulitokana na kushuka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam kutoka Soko la Hisa la Nairobi.

50. Mwaka 2023, mauzo ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 68.5 na kufikia shilingi bilioni 225.22 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 133.66 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 29.3 na kufikia shilingi trilioni 3.93 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi trilioni 3.04 katika kipindi hicho mwaka 2022. Aidha, mauzo ya hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 70.8 na kufikia shilingi bilioni 1.07 ikilinganishwa na shilingi bilioni 0.626 mwaka 2022. Ongezeko la mauzo ya hisa, hatifungani za Serikali na mauzo ya hatifungani za kampuni lilitokana na kuongezeka kwa wawekezaji kufuatia elimu iliyotolewa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine.

51. Hadi Desemba 2023, thamani ya uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja iliongezeka kwa asilimia 50.8 na kufikia shilingi trilioni 1.84 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.22 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Hii ilitokana na kuongezeka kwa

ushiriki wa wawekezaji kufuatia elimu inayotolewa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana pamoja na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa wawekezaji.

**Jedwali Na. 2.2: Thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja Mwaka 2022 - 2023**

| Meneja wa Mifuko | Jina la Mfuko | 31 Desemba 2022 | | 31 Desemba 2023 | | Ongezeko la Thamani | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Thamani ya Mfuko (Shilingi) | Bei ya Kipande (Shilingi) | Thamani ya Mfuko (Shilingi) | Bei ya Kipande (Shilingi) | Ongezeko la Thamani ya Mfuko (Asilimia) | Ongezeko la Bei ya Kipande (Asilimia) |
| UTT AMIS Plc | Mfuko wa Umoja | 302,291,686,824 | 877.0422 | 339,983,591,268 | 983.8384 | 12.5 | 12.2 |
| | Mfuko wa Wekeza Maisha | 6,658,727,935 | 741.6512 | 12,063,090,559 | 866.0778 | 81.2 | 16.8 |
| | Mfuko wa Watoto | 8,426,930,098 | 547.9748 | 14,560,377,763 | 634.5169 | 72.8 | 15.8 |
| | Mfuko wa Jikimu | 19,122,648,898 | 159.1157 | 22,994,371,528 | 170.5127 | 20.3 | 7.2 |
| | Mfuko wa Ukwasi | 559,272,074,566 | 342.5173 | 890,749,211,777 | 382.998 | 59.3 | 11.8 |
| | Mfuko wa Hatifungani | 322,543,871,717 | 114.7596 | 542,099,396,791 | 116.6001 | 68.1 | 1.6 |
| Watumishi Housing Investments | Mfuko wa Faida | * | * | 19,242,094,320 | 110.236 | | |
| **Thamani ya Jumla** | | **1,218,315,940,041** | | **1,841,692,134,009** | | **51.2** | |

**Chanzo:** Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja na Watumishi Housing Investments
*Mfuko wa Faida ulikuwa bado haujapata idhini ya kutoa huduma ya uwekezaji

### Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma

52. Mwaka 2022/23, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma - PSSSF ulisajili wanachama wapya 47,851 ikilinganishwa na wanachama 19,910 kulingana na taarifa ya takwimu zilizokaguliwa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwaka 2021/22. Aidha, wanachama wachangiaji wa Mfuko walifikia 729,346 mwaka 2022/23 kutoka wanachama 717,943 mwaka 2021/22. Katika kipindi hicho, Mfuko ulikusanya shilingi trilioni 1.67 kutokana na michango ya wanachama ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.52 mwaka 2021/22. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wanachama na kiwango cha mishahara kulikotokana na kupandishwa kwa madaraja na nyongeza kidato kwa watumishi wa umma. Aidha, Mfuko ulilipa mafao yenye thamani ya shilingi trilioni 1.56 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.69 zilizolipwa mwaka 2021/22, sawa na upungufu wa asilimia 7.7. Hii ilitokana na mabadiliko ya Kanuni ya Mafao iliyoanza kutumika Julai 2022 na kupungua kwa idadi ya wanachama wanaostahili kulipwa mafao mbalimbali.

53. Mwaka 2022/23, thamani ya uwekezaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ilifikia shilingi trilioni 7.90 kutoka shilingi trilioni 7.48 mwaka 2021/22. Aidha, mapato ya Mfuko yatokanayo na uwekezaji yaliongezeka kwa asilimia 16.7 na kufikia shilingi bilioni 685.44 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi bilioni

587.56 mwaka 2021/22. Kwa upande mwingine, thamani ya Mfuko ilikuwa shilingi bilioni 8,102.34 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi bilioni 7,415.7 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 9.3. Hii ilitokana na kupungua kwa gharama za uendeshaji na kuongezeka kwa uwekezaji na mapato yatokanayo na uwekezaji.

**Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii**

54. Mwaka 2022/23, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii - NSSF ilisajili wanachama wapya 243,895 ikilinganishwa na wanachama wapya 233,643 walioandikishwa mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 4.4. Katika kipindi hicho, wanachama wachangiaji wa Mfuko walifikia 1,189,222 kutoka wanachama 1,039,183 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 14.4. Ongezeko hilo lilichangiwa na ukuaji wa shughuli za sekta binafsi pamoja na uwekezaji. Mwaka 2022/23, Mfuko ulikuwa na wastaafu 28,820 ikilinganishwa na wastaafu 25,608 waliokuwepo mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 12.5. Aidha, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yaliongezeka kwa asilimia 12.0 na kufikia shillingi bilioni 738.61 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi bilioni 659.77 mwaka 2021/22. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa maombi ya fao la ukosefu wa ajira na idadi ya wastaafu.

55. Mwaka 2022/23, mapato halisi yatokanayo na uwekezaji wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii yaliongezeka kwa asilimia 20.5 na kufikia shilingi bilioni 380.63 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 315.77 mwaka 2021/22. Ongezeko hilo lilichangiwa na uwekezaji uliofanywa na Mfuko katika hatifungani za Serikali. Aidha, thamani ya vitega uchumi vya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 21.0 na kufikia shilingi trilioni 6.880 mwaka 2022/23 kutoka shilingi trilioni 5.687 mwaka 2021/22. Hii ilitokana na ongezeko la michango ya wanachama pamoja na uwekezaji uliofanywa na Mfuko katika hatifungani za Serikali.

56. Mwaka 2022/23, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulikusanya michango kutoka kwa wanachama kiasi cha shilingi bilioni 1,719.25 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,419.71 zilizokusanywa mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 21.1. Ongezeko hilo lilichangiwa na ukuaji wa shughuli za sekta binafsi, maboresho ya mifumo ya ukaguzi na matumizi ya TEHAMA. Kwa upande mwingine, thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 18.0 na kufikia shilingi trilioni 7.2 mwaka 2022/23 kutoka shilingi trilioni 6.1 mwaka 2021/22. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa thamani ya uwekezaji wa Mfuko na kuongezeka kwa michango ya wanachama.

**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi**

57. Mwaka 2022/23, idadi ya waajiri waliosajiliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ilifikia 30,853 kutoka waajiri 27,794 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 10.0. Katika kipindi hicho, idadi ya waajiri wanaochangia iliongezeka na kufikia waajiri 19,036

kutoka waajiri wachangiaji 17,309 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 10 ya waajiri wanaochangia Mfuko. Aidha, idadi ya waajiri wanaochangia katika Mfuko ni sawa na asilimia 61.7 ya waajiri waliosajiliwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na asilimia 62.2 mwaka 2021/23. Katika kuhakikisha waajiri wote wanajisajili na kuchangia, Mfuko uliendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kutimiza wajibu wao kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura 263. Vile vile, Mfuko uliendelea kufanya kaguzi pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa waajiri waliokiuka matakwa ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura 263. Kwa upande mwingine, idadi ya wafanyakazi wanaochangiwa kwenye Mfuko ilipungua kwa asilimia 25 hadi 1,159,792 mwaka 2022/23 kutoka wafanyakazi 1,546,150 mwaka 2021/22. Hii ilitokana na Mfuko kusajili zaidi waajiri wenye watumishi wachache ikilinganishwa na waajiri waliofunga biashara ambao walikuwa na watumishi wengi, hususan katika sekta ya ujenzi.

58. Mwaka 2022/23, mapato ya uwekezaji wa Mfuko yaliongezeka kwa asilimia 35 na kufikia shilingi bilioni 103.78 ikilinganishwa na shilingi bilioni 67.31 mwaka 2021/22. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji hasa katika hatifungani na amana zisizohamishika. Aidha, mapato yaliyotokana na shughuli nyingine za kiuchumi yalifikia shilingi milioni 114.36 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi milioni 106.91 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 7.0. Ongezeko hilo lilitokana na riba iliyopokelewa kutokana na malipo ya mkopo. Katika kipindi hicho, gharama za uendeshaji wa Mfuko ziliongezeka kwa asilimia 17 na kufikia shilingi bilioni 30.83 ikilinganishwa na shilingi bilioni 25.49 mwaka 2021/22. Ongezeko hilo lilitokana na upanuzi wa shughuli za Mfuko hasa katika uhamishaji wa Mfuko kwenda Dodoma.

59. Mwaka 2022/23, Mfuko ulilipa shilingi bilioni 17.91 ikiwa ni madai ya matibabu na fidia kwa wafanyakazi walioumia au kufariki wakiwa kazini ikilinganishwa na shilingi bilioni 12.9 zilizolipwa mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 28. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya madai ya fidia yaliyopokelewa na malipo ya madai yaliyopokelewa na kuchakatwa kipindi cha nyuma. Kwa upande mwingine, thamani halisi ya mali za Mfuko iliongezeka kwa asilimia 23.13 na kufikia shilingi bilioni 602.77 mwaka 2022/23 kutoka shilingi bilioni 545.1 mwaka 2021/22. Ongezeko hili, lilitokana na ongezeko la faida ya uwekezaji na ununuzi wa mali na vifaa vya Mfuko. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya mali ghafi za Mfuko ziliongezeka kufikia shilingi bilioni 677. 892 kutoka shilingi bilioni 559.39 sawa na ongezeko la asimilia 21.18.

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

60. Hadi Desemba 2023, idadi ya wanachama wachangiaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya - NHIF ilipungua kwa asilimia 8.0 na kufikia wanachama 1,246,046 kutoka wanachama 1,353,535 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kupungua kwa idadi ya wanachama wachangiaji kulitokana na maboresho yaliyofanyika katika usajili wa Toto

Afya pamoja na kuondolewa kwa makundi ya wananchi katika sekta isiyo rasmi kupitia Ushirika Afya. Aidha, idadi ya wanufaika iliongezeka kwa asilimia 3.3 na kufikia wanufaika 4,987,292 mwaka 2023 kutoka wanufaika 4,821,233 mwaka 2022. Hii ilichangiwa na ajira mpya na kuongezeka kwa idadi ya wanufaika wa vifurushi.

**Jedwali Na. 2.3: Wanachama Wachangiaji na Wanufaika wa Mfuko Mwaka 2018/19 - 2022/23**

| Mwaka | Idadi ya Wanachama wachangiaji | Idadi ya Wanufaika | Ongezeko wanachama wachangiaji (Asilimia) | Ongezeko Wanufaika (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| 2018/19 | 966,792 | 4,025,693 | - | - |
| 2019/20 | 1,055,555 | 4,403,581 | 9.2 | 9.4 |
| 2020/21 | 1,212,519 | 4,550,207 | 14.9 | 3.3 |
| 2021/22 | 1,353,535 | 4,821,233 | 11.6 | 6.0 |
| 2022/23 | 1,246,046 | 4,987,292 | -7.9 | 3.4 |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

61. Mwaka 2022/23, idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyosajiliwa na Mfuko viliongezeka kwa asilimia 3.1 na kufikia vituo 9,467 ikilinganishwa na vituo 9,178 vilivyosajiliwa mwaka 2021/22. Kati ya hivyo, vituo 6,852 (asilimia 72) vilikuwa vya Serikali; vituo 849 (asilimia 9) vya madhehebu ya dini na vituo 1,766 (asilimia 19) vya binafsi. Ongezeko la idadi ya vituo vilivyosajiliwa lilitokana na kurahisishwa kwa utaratibu wa kusajili vituo kwa kuwawezesha watoa huduma kuanzisha mchakato wa kujisajili kwa njia ya mtandao.

**Jedwali 2.4: Vituo Vilivyosajiliwa na Mfuko Mwaka 2018/19 - 2022/23**

| Ngazi ya Kituo | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zahanati | 5,753 | 6,485 | 6,252 | 6,582 | 6,896 | 4.8 |
| Vituo vya Afya | 766 | 853 | 832 | 912 | 999 | 9.5 |
| Hospitali | 298 | 346 | 381 | 417 | 449 | 7.7 |
| Maduka ya Dawa | 449 | 597 | 560 | 685 | 625 | -8.8 |
| ADDO | 200 | 461 | 179 | 207 | 129 | -37.7 |
| Polikliniki | - | - | - | - | 242 | 0.0 |
| Kliniki maalumu | 130 | 211 | 265 | 360 | 113 | -68.6 |
| Vituo vya Uchunguzi | 9 | 16 | 13 | 14 | 12 | -14.3 |
| Vituo vya Uokozi | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 100.0 |
| **Jumla** | **7,605** | **8,969** | **8,482** | **9,178** | **9,467** | **3.1** |

**Chanzo**: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

62. Mwaka 2022/23, Mfuko wa Taifa wa Bima ulilipa shilingi bilioni 752.1 kwa watoa huduma ikilinganishwa na shilingi bilioni 674.3 zilizolipwa mwaka 2021/22, sawa na

ongezeko la asilimia 11.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa malipo ya madai kwa wastaafu wanaolipwa na Mfuko pamoja na wenzi wao bila kuchangia, na kuongezeka kwa gharama za matibabu kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Katika kipindi hicho, mapato ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yalikuwa shilingi bilioni 697.15 ikilinganishwa na shilingi bilioni 624.5 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 11.6. Hii ilitokana na juhudi za Mfuko katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mifumo ya kielektroniki.

**Jedwali Na. 2.6: Mapato ya Mfuko wa Taifa wa Bima Mwaka 2018/19 - 2022/23**

| Vyanzo vya mapato | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Michango ya wanachama | 431,003.12 | 467,772.19 | 489,479.55 | 552,580.23 | 633,508.83 | 14.6 |
| Uwekezaji | 84,771.81 | 80,757.62 | 77,110.90 | 69,446.95 | 58,978.39 | -15.1 |
| Vyanzo vingine | 3,111.06 | 1,903.36 | 3,161.57 | 2,468.62 | 4,234.98 | 71.6 |
| Jumla | 518,885.99 | 550,433.17 | 569,752.03 | 624,495.80 | 696,722.20 | 11.6 |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

63. Mwaka 2022/23, rasilimali halisi za Mfuko zilifikia shilingi bilioni 987.0 kutoka shilingi bilioni 1,097.7 mwaka 2021/22, sawa na upungufu wa asilimia 10.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa malipo ya madai na kupungua kwa mapato yatokanayo na uwekezaji.

**Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa**

64. Mwaka 2022/23, idadi ya wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa - iCHF iliongezeka kwa asilimia 9.0 na kufikia wanachama 4,230,368 (kaya 872,013) kutoka wanachama 3,862,266 (kaya 863,195) mwaka 2021/22. Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyoendelea kutolewa kwa wananchi kuhusu huduma zinazotolewa na umuhimu wa kujiunga na Mfuko. Katika kipindi hicho, jumla ya vituo 6,755 vilitoa huduma kwa wanachama wa Mfuko ikilinganishwa na vituo 6,378 mwaka 2021/22. Kati ya hivyo, vituo vya umma vilikuwa 6,733; vituo vya taasisi za kidini vilikuwa 20 (vituo vya afya vitatu na zahanati 17); na zahanati mbili za watu binafsi. Vituo vinavyomilikuwa na Serikali vilijumuisha: zahanati 5,723; vituo vya afya 807; hospitali za Halmashauri 175; na hospitali za rufaa za mikoa 28. Aidha, shilingi milioni 3,755.8 zilikusanywa kutokana na michango ya wanachama ikilinganishwa na shilingi milioni 7,822.7 mwaka 2021/22 sawa na upungufu wa asilimia 51.9. Upungufu huo ulitokana na idadi ndogo ya wanachama waliohamasika kujiunga na Mfuko. Kwa upande mwingine, shilingi milioni 3,959.4 zililipwa kwa watoa huduma mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi milioni 8,301.5 mwaka 2021/22, sawa na upungufu wa asilimia 52.3. Hii ilitokana na idadi ndogo ya wanachama waliojiunga na Mfuko kulikosababisha kupungua kwa michango.

**Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania**

65. Mwaka 2023, kampuni za bima zilizosajiliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kufanya biashara ya bima nchini zilikuwa 39 ikilinganishwa na kampuni 35

mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na usajili wa kampuni mbili (2) za bima za kiimani (ZIC Takaful Insurance na First United Takaful), kampuni moja (1) ya bima za kawaida (CRDB Insurance Company) na kampuni moja (1) ya bima mtawanyo (East Africa Reinsurance Company). Katika kipindi hicho, kampuni za udalali wa bima zilifikia 113, mawakala wa bima 1,083, wakadiriaji hasara 56, benki wakala 29 na watakwimu wa bima watano (5) ikilinganishwa na kampuni za udalali wa bima 100, mawakala wa bima 1,019, wakadiriaji hasara 46, benki wakala 29 na watakwimu wa bima wanne (4) mwaka 2022.

66. Mwaka 2023, mauzo katika soko la bima yaliongezeka kwa asilimia 6.8 na kufikia shilingi bilioni 1,238.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,159.3 mwaka 2022. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za bima, ubunifu katika utoaji wa huduma za bima ikiwemo, matumizi ya TEHAMA na uwepo wa programu za uhamasishaji kwa umma. Katika kipindi hicho, mauzo ya bima za kawaida yalikuwa shilingi bilioni 974.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 895.1 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Hii ilitokana na ongezeko la mahitaji ya bima ya uhandisi katika miradi mikubwa ya ujenzi pamoja na bima ya vyombo vya moto. Aidha, mauzo ya bima za maisha yalikuwa shilingi bilioni 264.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 264.2 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 0.1. Ongezeko hilo lilichangiwa na ada ya bima za mikopo.

67. Mwaka 2023, mchango wa bima za kawaida katika mauzo ulikuwa kama ifuatavyo: bima za vyombo vya moto (asilimia 34.9); moto (asilimia 18.7); afya (asilimia 16.6); ajali (asilimia 6.3); usafiri wa maji (asilimia 4.0); usafiri wa anga (asilimia 5.4); mradi wa mafuta na gesi (asilimia 0.3), uhandisi (asilimia 5.3) na bima nyinginezo (asilimia 8.4). Aidha, bima za maisha zilichangiwa na biashara ya kikundi (asilimia 82.6) ikifuatiwa na mtu binafsi (asilimia 17.4).

68. Mwaka 2023, thamani ya mali katika soko la bima ilikuwa shilingi bilioni 1,870.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1697.0 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Ongezeko hilo lilichangiwa na uwekezaji kwenye amana ya muda ili kufidia madai ya muda mfupi. Aidha, uwekezaji wa kampuni za bima uliongezeka kwa asilimia 12.7 na kufikia shilingi bilioni 1,318.5 mwaka 2023 kutoka shilingi bilioni 1,169.7 mwaka 2022. Kwa upande mwingine, madeni ya kampuni za bima yaliongezeka kwa asilimia 10.2 na kufikia shilingi bilioni 1,128.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,006.5 mwaka 2022. Hii lilitokana na kuongezeka mahitaji ya fidia kwa wamiliki wa bima kwani lengo kuu la bima ni kutoa ahadi ya kulipa madeni. Tofauti kati ya mali na madeni ilikuwa shilingi bilioni 742.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 690.5 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.5

69. Mwaka 2023 jumla ya mapato yatokanayo na uwekezaji yalikuwa shilingi bilioni 100.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 89.3 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia

12.9. Kati ya mapato hayo, mapato ya uwekezaji katika bima za kawaida yalikuwa shilingi bilioni 65.9, bima za maisha shilingi bilioni 21.7 na bima mtawanyo shilingi bilioni 13.1. Aidha, mapato baada ya kodi yaliyotokana na bima za kawaida yalikuwa shilingi bilioni 77.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 85.5 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 9.3.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania**

70. Mwaka 2023, mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania - TADB uliongezeka na kufikia shilingi bilioni 346.67 kutoka shilingi bilioni 305.6 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 13.4. Katika kipindi hicho, amana za benki ziliongezeka kwa asilimia 33.6 na kufikia shilingi bilioni 606.94 kutoka shilingi bilioni 454.40 mwaka 2022. Aidha, thamani ya hisa za wanachama iliongezeka kwa asilimia 4.2. na kufikia shilingi bilioni 315.14 mwaka 2023 kutoka shilingi bilioni 302.31 mwaka 2022.

71. Mwaka 2023, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 161.13 ikilinganishwa na shilingi bilioni 161.70 zilizotolewa mwaka 2022. Aidha, Benki kupitia Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Wakulima Wadogo ilitoa dhamana kwa mikopo yenye thamani ya shilingi ya bilioni 77.28 ikilinganishwa na shilingi bilioni 48.47 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 59.4. Mikopo hiyo ilitolewa kwa wakulima 5,622, vikundi vya wakulima na ushirika vipatavyo 129, biashara ndogo na za kati 117 za uchakataji, biashara ya mazao, pamoja na miradi inayolenga uhifadhi ili kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna.

72. Mwaka 2023, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilipata faida ya shilingi bilioni 18.78 ikilinganishwa na faida ya shilingi bilioni 11.05 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 70.0. Hii ilichangiwa na juhudi za benki kuongeza ukopeshaji, kufuatilia urejeshwaji wa mikopo na kupunguza gharama za uendeshaji. Kwa upande mwingine, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua na kufikia asilimia 3.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.8 mwaka 2022. Kiwango hiki ni chini ya ukomo wa asilimia 5 uliowekwa na Benki Kuu ya Tanzania.

## Jedwali Na. 24: MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

| | Kipindi Kinachoishia Mwezi Desemba (Shilingi Bilioni) | | | | | | | Badiliko 2022 - 2023 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **Kiasi** | **Asilimia** |
| **Fedha ya msingi (M0)** | **6,954.4** | **6,992.9** | **7,466.4** | **7,169.3** | **8,407.3** | **9,736.3** | **10,099.8** | **363.5** | **3.7** |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **11,155.3** | **11,723.7** | **13,325.1** | **14,321.7** | **17,625.5** | **18,948.2** | **20,601.6** | **1,653.4** | **8.7** |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 7,194.6 | 7,316.7 | 7,955.1 | 8,711.0 | 9,462.8 | 11,430.7 | 13,400.1 | 1,969.5 | 17.2 |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **18,349.9** | **19,040.4** | **21,280.3** | **23,032.6** | **27,088.8** | **30,378.9** | **34,001.7** | **3,622.9** | **11.9** |
| Amana za fedha za kigeni | 6364.4 | 6783.1 | 7032.9 | 6,887.9 | 7,469.7 | 8,201.1 | 10,000.8 | 1,799.7 | 21.9 |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **24,714.3** | **25,823.5** | **28,313.1** | **29,920.6** | **34,558.0** | **38,580.0** | **44,002.6** | **5,422.6** | **14.1** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)** | **11596.1** | **10629.8** | **12034.5** | **10,722.5** | **13,966.0** | **9,437.5** | **11,302.4** | **1,864.9** | **19.8** |
| Rasilimali halisi katika fedha za kigeni Benki Kuu | 12,249.9 | 10,692.3 | 12,063.1 | 10,308.8 | 13,219.1 | 10,732.8 | 12,079.3 | 1,346.4 | 12.5 |
| Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye mabenki | -553.8 | -62.5 | -28.5 | 413.8 | 746.8 | -1,295.3 | -776.9 | 518.5 | -40.0 |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)** | **13,118.2** | **15,193.7** | **16,278.6** | **19,198.0** | **20,592.1** | **29,142.5** | **32,700.2** | **3,557.7** | **12.2** |
| Karadha Nchini | 24,977.2 | 26,249.3 | 28,103.3 | 26,139.6 | 30,030.5 | 37,557.3 | 43,411.5 | 5,854.2 | 15.6 |
| Madai halisi kwa serikali kuu | 3,275.7 | 4,481.6 | 3,893.9 | 5,831.3 | 7,686.4 | 10,184.8 | 11,353.9 | 1,169.1 | 11.5 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 16895.4 | 17726.8 | 19695.4 | 20,308.3 | 22,344.1 | 27,372.49 | 32,057.6 | 4,685.1 | 17.1 |
| Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara | 4,806.1 | 4,040.9 | 4,514.1 | 6767.7 | 7,089.0 | 8,076.2 | 11,445.2 | 3,369.0 | 41.7 |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | -7,052.9 | -7,014.7 | -7,310.7 | -6,941.6 | -9,438.4 | -8,414.8 | -10,711.3 | -2,296.6 | 27.3 |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali Na. 25: VIWANGO VYA UKUAJI WA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

| | Kipindi kinachoishia mwezi Desemba (Asilimia) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
| **Fedha ya msingi (M0)** | **1.5** | **0.6** | **6.8** | **-4.0** | **17.3** | 15.8 | **3.7** |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **10.6** | **5.1** | **13.7** | **7.5** | **23.1** | **7.5** | **8.7** |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 10.1 | 1.7 | 8.7 | 9.5 | 8.6 | 20.8 | 17.2 |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **10.4** | **3.8** | **11.8** | **8.2** | **17.6** | **12.1** | **11.9** |
| Amana za fedha za kigeni | 1.7 | 6.6 | 3.7 | -2.1 | 8.4 | 9.8 | 21.9 |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **8.0** | **4.5** | **9.6** | **5.7** | **15.5** | **11.6** | **14.1** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)** | **41.7** | **-8.3** | **13.2** | **-10.9** | **30.2** | **-32.4** | 19.8 |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)** | **-10.7** | **15.8** | **7.1** | **17.9** | **7.3** | **41.5** | 12.2 |
| Karadha Nchini | 5.1 | 5.1 | 7.1 | -7.0 | 14.9 | 25.1 | 15.6 |
| Madai halisi kwa serikali kuu | -23.5 | 36.8 | -13.1 | 49.8 | 31.8 | 32.5 | 11.5 |
| Mikopo kwa sekta Binafsi | 1.7 | 4.9 | 11.1 | 3.1 | 10.0 | 22.5 | 17.1 |
| Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara | 66.6 | -15.9 | 11.7 | 49.9 | - | 13.9 | 41.7 |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | 13.8 | -0.5 | 4.2 | -5.0 | 36.0 | -10.8 | 27.3 |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 26: MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI**

| | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shs/Dola mwisho wa mwaka | 2,242.21 | 2,291.29 | 2,299.97 | 2,309.8 | 2,307.4 | 2,320.2 | 2,516.0 |
| Badiliko la thamani ya shilingi (%) | 2.79 | 2.19 | 0.38 | 0.4 | -0.1 | 0.6 | 8.4 |
| Shs/Dola wastani wa mwaka | 2,240.76 | 2,275.41 | 2,299.79 | 2,305.6 | 2,309.2 | 2,314.5 | 2,395.7 |
| Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (%) | 2.4 | 1.5 | 1.1 | 0.3 | 0.2 | 0.2 | 3.5 |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 27: MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA**

| | Kipindi Kinachoishia mwezi Desemba (Shilingi bilioni) | | | | | | | Badiliko (Asilimia) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2022 | 2023 |
| **Amana za Sekta Binafsi** | | | | | | | | | |
| Amana za Hundi/Zinazaohamishika | 6,685.3 | 7,031.7 | 7,866.5 | 8,121.4 | 9,894.0 | 11,909.1 | 12,976.1 | 20.4 | 9.0 |
| Amana za Akiba na za Muda Maalum | 7,052.2 | 7,154.7 | 7,750.4 | 8,519.4 | 9,350.8 | 11,240.7 | 13,037.2 | 20.2 | 16.0 |
| Amana za fedha za kigeni | 6,087.1 | 6,376.3 | 6,160.6 | 6,427.1 | 7,146.0 | 7,575.1 | 9,331.7 | 6.0 | 23.2 |
| **Jumla** | **19,824.6** | **20,562.8** | **21,777.5** | **23,067.9** | **26,390.7** | **30,724.9** | **35,345.0** | 16.4 | 15.0 |
| Amana za Serikali | 560.6 | 358.5 | 981.3 | 652.9 | 422.5 | 704.4 | 1,156.05 | 66.7 | 64.1 |
| **Jumla za Amana zote** | **20,385.1** | **20,921.3** | **22,758.9** | **23,720.7** | **26,813.2** | **31,429.4** | **36,501.08** | **17.2** | **16.1** |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 28: VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA**

| Aina ya Riba | Wastani wa Mwaka (Asilimia) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
| Riba ya Benki kuu (Discount rate) | 16.00 | 7.00 | 7.00 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 5.00 |
| Riba katika soko la fedha kati ya benki za biashara kwa ujumla | 6.00 | 2.21 | 5.13 | 4.50 | 4.44 | 4.53 | 5.37 |
| Riba za dhamana za serikali kwa ujumla | 11.10 | 6.43 | 7.71 | 4.42 | 4.78 | 4.64 | 7.32 |
| Siku 35 | 5.54 | 2.51 | 3.47 | 2.37 | 2.60 | 2.25 | 4.20 |
| Siku 91 | 5.49 | 2.89 | 4.17 | 2.37 | 2.74 | 2.80 | 5.36 |
| Siku 182 | 10.01 | 4.13 | 5.07 | 2.88 | 3.20 | 3.47 | 6.37 |
| Siku 364 | 11.79 | 7.08 | 8.04 | 2.32 | 4.85 | 4.79 | 7.69 |
| **Riba za Hatifungani** | | | | | | | |
| Miaka miwili | 14.52 | 9.42 | 11.45 | 8.14 | 7.67 | 6.56 | 9.75 |
| Miaka mitano | 15.78 | 11.64 | 12.56 | 11.24 | 9.19 | 9.04 | 9.89 |
| Miaka saba | 16.31 | 12.62 | 13.09 | 11.48 | 10.09 | 9.58 | 9.71 |
| Miaka kumi | 16.79 | 14.39 | 15.04 | 12.51 | 11.59 | 10.63 | 11.35 |
| Miaka kumi na tano | 17.54 | 14.69 | 15.52 | 14.05 | 13.59 | 11.70 | 11.95 |
| Miaka ishirini | - | 17.70 | 17.35 | 15.79 | 16.06 | 12.22 | 12.96 |
| Miaka ishirini na tano | | | | | 16.09 | 12.76 | 13.46 |
| **Riba za Amana** | | | | | | | |
| Amana za akiba | 3.03 | 2.52 | 2.44 | 2.34 | 1.95 | 1.69 | 1.86 |
| Amana za muda maalum kwa ujumla | 10.04 | 8.24 | 7.25 | 6.70 | 6.85 | 7.11 | 7.07 |
| Mwaka mmoja | 11.66 | 8.78 | 8.80 | 8.28 | 8.32 | 8.53 | 8.65 |
| **Riba za Mikopo** | | | | | | | |
| Mikopo kwa ujumla | 17.77 | 17.43 | 16.97 | 16.66 | 16.59 | 16.18 | 15.76 |
| Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja | 18.30 | 18.25 | 16.69 | 15.73 | 16.43 | 16.79 | 16.53 |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

## SURA YA 3

## FEDHA ZA SERIKALI

**Utangulizi**

73. Bajeti ya mwaka 2023/24 iliandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26. Kwa kuzingatia hilo, bajeti ya mwaka 2023/24 ililenga katika kutekeleza vipaumbele mbalimbali vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 ikiwemo: kuendelea kukamilisha miradi ya kielelezo na ile ya kimkakati ikijumuisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115; kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara na uwekezaji; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu.

74. Shabaha za uchumi jumla na bajeti katika mwaka 2023/24 ni: Pato la Taifa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2023 kutoka ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 2022; mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 - 5.0 katika kipindi cha muda wa kati; mapato ya ndani kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa; mapato ya kodi kufikia asilimia 12.0 ya Pato la Taifa; nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; akiba ya fedha za kigeni kufikia kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

75. Katika mwaka 2023/24, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 44,388.1 kutoka vyanzo vya ndani na nje. Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) yalitarajiwa kuwa shilingi bilioni 31,381.0. Aidha, mapato ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 26,725.4 na yasiyo ya kodi kutoka wizara, idara zinazojitegemea, wakala na taasisi za serikali yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 3,511.7 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 1,143.9. Vile vile, misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo ilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 5,466.2 na mikopo ya kibiashara kutoka vyanzo vya ndani na nje ni shilingi bilioni 7,540.8. Kwa upande wa matumizi, shilingi bilioni 30,310.8 zilipangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu pamoja na kugharamia programu ya elimumsingi na sekondari bila ada na shilingi bilioni 14,077.2 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mwenendo wa Mapato**

**Mapato ya Ndani**

76. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 22,029.2, sawa na asilimia 94.9 ya lengo la kipindi hicho na ukuaji wa asilimia 11.0

ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, Kutofikiwa kwa lengo la makusanyo ya mapato ya ndani kumetokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na: baadhi ya walipakodi kutotoa risiti wakati wanapouza bidhaa/huduma zao; kuwepo kwa udanganyifu wa kuripoti mauzo kwa baadhi ya walipakodi; uwepo wa mianya ya upotevu wa mapato hasa maeneo ya mipakani; ufanisi mdogo wa mifumo inayotumika kukusanya ada na tozo za ardhi; na baadhi ya taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kutowasilisha michango stahiki kwa wakati.

**Jedwali Na. 3.1: Mwenendo wa Mapato ya Ndani (Shilingi Bilioni)**


| | Julai - Machi | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | | Ufanisi (%) | Ukuaji (%) |
| | Halisi | Makadirio | Halisi | | |
| **Mapato ya Ndani** | **19,840.3** | **23,211.2** | **22,029.2** | **94.9** | **11.0** |
| **Mapato Yanayokusanywa na TRA** | **17,260.3** | **19,940.5** | **19,431.2** | **97.4** | **12.6** |
| Kodi | 16,297.7 | 18,749.0 | 18,380.1 | 98.0 | 12.8 |
| Yasiyo ya Kodi | 962.6 | 1,191.5 | 1,051.1 | 88.2 | 9.2 |
| **Mapato Yasiyo ya Kodi** | **2,580.0** | **3,270.7** | **2,598.1** | **79.4** | **0.7** |
| Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali | 1,247.0 | 1,785.3 | 1,344.0 | 75.3 | 7.8 |
| Ofisi ya Msajili wa Hazina | 625.5 | 618.9 | 405.9 | 65.6 | -35.1 |
| Halmashauri | 707.4 | 866.5 | 848.1 | 97.9 | 19.9 |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

**Misaada na Mikopo Nafuu**

77. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo ilifikia shilingi bilioni 4,272.8, sawa na asilimia 107.8 ya lengo la kipindi hicho. Ufanisi kwa ujumla ulichangiwa na utekelezaji unaoridhisha wa miradi ya maendeleo na kuwasilisha ripoti za utekelezaji kwa washirika wa maendeleo kwa wakati kwa miradi inayoendelea.

**Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Misaada na Mikopo Nafuu (Julai 2023 - Machi 2024**




**Mikopo Yenye Masharti ya Kibiashara ya Ndani na Nje**

78. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 4,283.62 kutoka soko la ndani, sawa na asilimia 88.5 ya lengo la mwaka 2023/24. Kati ya kiasi kilichokopwa, shilingi bilioni 2,727.21 zilitumika kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zilizoiva na shilingi bilioni 1,556.41 zilitumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Katika kipindi hicho, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 1,564.5 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Kiasi kilichokopwa ni sawa na asilimia 74.5 ya shilingi bilioni 2,100.5 ambazo Serikali ilipanga kukopa katika mwaka 2023/24.

**Mwenendo wa Matumizi**

79. Mwaka 2023/24, Sera za Matumizi zililenga: kuendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo; kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kubana matumizi ikiwa ni pamoja na kuendesha vikao kwa njia ya mtandao na kupunguza matumizi ya karatasi; kuimarisha usimamizi wa mashirika, wakala na taasisi za Serikali ili yajiendeshe kwa ufanisi na kuipunguzia mzigo Serikali; kuimarisha usimamizi wa miradi kwa kufanya ukaguzi wa ufanisi kwa wakati ili kuokoa gharama za ziada zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi; na kufanya mapitio ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 ili kuufanya mfumo wa ununuzi wa umma kuwa wa kimkakati pamoja na kuziba mianya ya ubadhirifu kwa lengo la kupata thamani ya fedha katika matumizi ya Serikali.

80. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, ridhaa za matumizi zilizotolewa zilikuwa shilingi bilioni 31,938.0, sawa na asilimia 97.4 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya


kiasi hicho, shilingi bilioni 20,232.0 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 11,706.0 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, kiasi kilichotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kilijumuisha shilingi bilioni 7,535.9 za kugharamia malipo ya deni la Serikali ambapo malipo ya riba kwa madeni ya ndani na nje yalikuwa shilingi bilioni 2,847.5, sawa na asilimia 95.6 ya makadirio. Vile vile, malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje yalikuwa shilingi bilioni 4,688.4, sawa na asilimia 99.1 ya lengo. Matumizi ya kawaida pia yalijumuisha shilingi bilioni 7,722.0 kugharamia malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali, sawa na asilimia 94.6 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,355.7 zililipwa kwa watumishi wa Serikali Kuu, na shilingi bilioni 2,366.3 kwa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

81. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, shilingi bilioni 10,640.4 ya ridhaa za matumizi ya fedha za maendeleo zilitolewa, sawa na asilimia 95.8 ya makadirio. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 10,385.9 zilikuwa fedha za ndani na shilingi milioni 254.5 fedha za nje. Kutofikiwa kwa malengo ya utoaji wa fedha za matumizi ya kawaida na ya maendeleo kulitokana na kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo vya ndani na nje.

**Deni la Serikali**

82. Hadi Machi 2024, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 91,708.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 77,010.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 19.1. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 30,753.8 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 60,954.5. Aidha, ongezeko la deni lilitokana na Serikali kuendelea kupokea fedha za mikopo ya zamani na mipya kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji. Vile vile, ongezeko la deni lilichangiwa na kupanda kwa viwango vya kubadilisha fedha pamoja na kuongezeka kwa riba kwenye mikopo ya nje ambayo riba zake hutegemea mabadiliko ya hali ya soko (floating rates).

**Kielelezo Na. 3.2: Mwenendo wa Deni la Serikali Machi 2017 - 2024 (Shilingi Bilioni)**




**Deni la Nje**

83. Hadi Machi 2024, deni la Serikali la nje lilifikia dola za Marekani milioni 23,720.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 21,700.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 9.3. Ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo ya zamani na mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kupanda kwa viwango vya kubadilisha fedha na kuongezeka kwa riba kwenye mikopo ambayo riba zake hutegemea mabadiliko ya hali ya soko.

84. Hadi Machi 2024, mashirika ya fedha ya kimataifa yaliendelea kuongoza kwa kuchangia asilimia 63.7 ya deni lote la nje ikilinganishwa na asilimia 62.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Benki za biashara zilichangia asilimia 26.9 na washirika wa maendeleo walichangia asilimia 5.8 ya deni lote la nje. Aidha, kati ya deni lote la nje, mikopo yenye masharti nafuu ilichangia dola za Marekani milioni 15,972.5, sawa na asilimia 67.3, mikopo yenye masharti nafuu ya kati dola za Marekani milioni 1,488.6 (asilimia 6.3) na mikopo yenye masharti ya kibiashara ilichangia dola za Marekani milioni 6,259.6 (asilimia 26.4).

**Jedwali Na. 3.2: Deni la Nje kwa Wakopeshaji Mwaka 2022 - 2024 (Dola za Marekani Milioni)**


| Taasisi | Machi 2022 | Mchango (Asilimia) | Machi 2023 | Mchango (Asilimia) | Machi 2024 | Mchango (Asilimia) |
|---|---:|---:|---:|---:|---:|---:|
| Mashirika ya Fedha | 12,416.4 | 60.1 | 13,456.6 | 62.0 | 15,972.5 | 67.3 |
| Washirika wa Maendeleo | 2,255.4 | 10.9 | 2,267.0 | 10.5 | 1,379.1 | 5.8 |
| Benki za Kibiashara | 5,986.4 | 29.0 | 5,976.6 | 27.5 | 6,369.2 | 26.9 |
| **Jumla** | **20,658.2** | **100.0** | **21,700.2** | **100.0** | **23,720.8** | **100.0** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

### Deni la Ndani

85. Hadi Machi 2024, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 30,753.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 26,851.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 14.5. Aidha, mikopo ya hatifungani iliendelea kuwa sehemu kubwa ya deni la ndani, sawa na asilimia 63.9 ya deni lote la ndani. Vile vile, dhamana za Serikali za muda mfupi zilikuwa asilimia 8.8 na hatifungani maalum asilimia 13.2.

**Kielelezo Na. 3.3: Mwenendo wa Deni la Ndani Mwaka 2018 - 2024 (Shilingi Bilioni)**




86. Hadi Machi 2024, benki za biashara ziliongoza kwa kuhodhi asilimia 42.0 ya deni la ndani ikilinganishwa na asilimia 34.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, mifuko ya jamii ilihodhi asilimia 33.9 ikifuatiwa na watu binafsi asilimia 11.3 na kampuni za bima asilimia 7.6.

**Jedwali Na. 3.3: Deni la Ndani kwa Wakopeshaji Mwaka 2022 - 2024 (Shilingi Bilioni)**

| Taasisi | Machi 2022 | Mchango Asilimia | Machi 2023 | Mchango Asilimia | Machi 2024 | Mchango Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Benki za Biashara | 6,606.60 | 35.2 | 7,204.82 | 34.8 | 10,169.95 | 42.0 |
| Taasisi za Fedha | 187.9 | 1.0 | 211.72 | 1.0 | 686.44 | 2.8 |
| Mifuko ya Jamii | 7,429.40 | 39.6 | 7,961.12 | 38.5 | 8,211.84 | 33.9 |
| Kampuni za Bima | 1,425.30 | 7.6 | 1,494.73 | 7.2 | 1,844.75 | 7.6 |
| Taasisi za Kigeni | 1,051.80 | 5.6 | 1,006.93 | 4.9 | - | - |
| Mashirika Madogo | 686.6 | 3.7 | 1,162.49 | 5.6 | 593.79 | 2.4 |
| Watu binafsi | 1,386.80 | 7.4 | 1,660.20 | 8.0 | 2,733.60 | 11.3 |
| **Jumla** | **18,774.40** | **100.0** | **20,702.01** | **100.00** | **24,240.37** | **100.0** |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

### Tathmini ya Uhimilivu wa Deni

87. Matokeo ya Tathmini ya Uhimilivu wa Deni iliyofanyika Desemba 2023 yalionesha kuwa deni ni himilivu kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Tathmini hiyo hufanyika kwa kuzingatia vigezo vya uhimilivu ambavyo ni uwiano wa deni halisi kwa Pato

la Taifa, uwiano wa deni halisi kwa malipo ya nje na uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani na mapato yatokanayo na mauzo ya nje.

88. Viashiria vya deni vilionesha kuwa kwa mwaka 2023/24: thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 20.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 114.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180; ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato yatokanayo na mauzo ya nje ni asilimia 11.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15; na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ni asilimia 11.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 18. Aidha kwa upande wa viashiria vya deni lote (deni la nje na la ndani), thamani ya deni kwa Pato la Taifa ni asilimia 36.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55.

**Jedwali Na. 3.4: Tathmini ya Viashiria vya Deni la Taifa**

| **Viashiria vya Deni la Nje** | **2023/24** | **2024/25** | **2025/26** | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2033/34** | **Ukomo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni (PV)/Pato la Taifa | 20.1 | 20.1 | 20.1 | 20.1 | 18.1 | 17.6 | 15.8 | 40 |
| Deni (PV)/uuzaji wa bidhaa nje | 114.2 | 114.2 | 114.2 | 114.2 | 101.4 | 105.1 | 93.8 | 180 |
| Ulipaji wa deni la nje/Uuzaji wa bidhaa nje | 11.1 | 11.1 | 11.1 | 11.1 | 11.3 | 12.2 | 10.0 | 15 |
| Ulipaji wa deni /Mapato ya ndani | 11.6 | 11.6 | 11.6 | 11.6 | 12.0 | 12.2 | 10.0 | 18 |
| **Viashiria vya Deni la Nje na Ndani** | **2023/24** | **2024/25** | **2025/26** | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2033/34** | **Ukomo** |
| Deni (PV)/ Pato la Taifa | 36.4 | 36.4 | 36.4 | 36.4 | 36.4 | 33.0 | 30.3 | 55 |
| Deni (PV)/ Mapato ya ndani | 209.2 | 209.2 | 209.2 | 209.2 | 209.2 | 189.6 | 172.8 | - |
| Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani | 44.3 | 44.3 | 44.3 | 44.3 | 44.3 | 30.9 | 25.2 | - |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**Tathmini ya Uwezo wa Nchi Kukopa na Kulipa Madeni katika Masoko ya Kimataifa**

89. Machi 2024, Kampuni ya *Moody's Investors Services* ilifanya mapitio ya kwanza ya uchumi wa Tanzania ili kubaini uwezo wa nchi kukopesheka. Katika mapitio hayo, Tanzania ilipandishwa hadi daraja la B1 ikiwa ni mtazamo thabiti (Stable Outlook) kutoka daraja la B2 ikiwa ni mtazamo chanya (Positive Outlook) Machi 2023. Daraja la B1 linaashiria kuendelea kuimarika kwa uchumi wa nchi, hususan katika kipindi cha misukosuko ya kiuchumi iliyotokana na majanga mbalimbali kutoka nje ya nchi katika miaka ya hivi karibuni. Aidha, hii inaashiria uwezo wa nchi kuendelea kuhimili misukosuko ya kiuchumi kutoka nje (external shocks). Kwa upande mwingine, Kampuni ya *Fitch Ratings* ilifanya tathmini hiyo na kuchapisha matokeo Juni 2023, ambapo Tanzania iliwekwa katika daraja la B+ ikiwa na mtazamo thabiti (Stable Outlook). Matokeo hayo yaliendelea kubaki kama yalivyokuwa katika mapitio yaliyofanywa na *Fitch Ratings* Desemba 2023.

90. Kupandishwa kwa daraja kulichangiwa na ukuaji wa uchumi kuendelea kuwa imara na wenye uwezo wa kuhimili misukosuko mbalimbali ya kiuchumi ndani na nje ya nchi. Aidha, maboresho katika sekta ya umma yaliyochangia kuimarika kwa ufanisi katika utendaji kazi pamoja na kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Kukamilika kwa mapitio kunaiwezesha nchi kuendelea kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje unaochangia katika kuongeza ajira, fedha za kigeni, teknolojia pamoja na kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa gharama nafuu kutoka masoko ya fedha ya kimataifa.

## Jedwali Na. 29: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

Shilingi Milioni

| | 2020/21 Halisi | 2021/22 Halisi | 2022/23 Halisi | 2023/24 Bajeti | 2023/24 Matokeo hadi Machi | 2023/24 Matarajio hadi Juni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri)** | **20,594,735.2** | **24,395,566.1** | **26,277,887.1** | **31,381,011.7** | **22,029,246.2** | **30,503,027.3** |
| MAPATO YA NDANI | 19,837,680.3 | 23,506,098.2 | 25,256,847.8 | 30,237,128.5 | 21,181,101.4 | 29,416,338.1 |
| 1. Mapato yatokanayo na Kodi | 17,624,454.4 | 20,931,261.6 | 21,411,398.9 | 25,489,767.2 | 18,380,058.7 | 25,081,930.9 |
| Ushuru wa Forodha na Excise Duty | 4,042,533.8 | 4,367,465.7 | 4,583,909.9 | 5,370,423.4 | 4,014,622.1 | 5,462,829.5 |
| Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) | 5,217,889.3 | 6,297,722.6 | 7,066,881.5 | 8,371,344.5 | 5,638,916.0 | 7,843,740.6 |
| Bidhaa toka nje | 2,584,453.5 | 3,344,798.5 | 3,639,577.6 | 3,967,439.7 | 2,785,767.7 | 3,952,209.4 |
| Bidhaa za ndani | 2,633,435.8 | 2,952,924.1 | 3,427,304.0 | 4,403,904.8 | 2,853,148.3 | 3,891,531.2 |
| Kodi ya Mapato | 6,015,898.2 | 7,549,185.9 | 7,760,301.5 | 9,007,599.2 | 6,674,802.2 | 8,899,736.2 |
| Kodi nyingine | 2,570,987.9 | 3,712,545.6 | 3,073,133.2 | 3,846,062.3 | 2,798,775.4 | 3,781,700.6 |
| Marejesho (Refunds Accounts) | (222,854.8) | (995,658.2) | (1,072,827.2) | (1,105,662.1) | (747,057.0) | (906,076.0) |
| 2. Mapato yasiyotokana na Kodi | 2,213,225.8 | 2,574,836.6 | 3,845,448.9 | 4,747,361.3 | 2,801,042.7 | 4,334,407.2 |
| 3. Mapato ya Halmashauri | 757,055.0 | 889,467.9 | 1,021,039.3 | 1,143,883.3 | 848,144.9 | 1,086,689.1 |
| **B. JUMLA YA MATUMIZI** | **26,585,306.7** | **31,815,747.3** | **36,157,462.0** | **38,082,059.3** | **27,064,371.6** | **37,204,074.8** |
| 1. Matumizi ya Kawaida | 14,883,722.6 | 15,998,691.7 | 20,475,131.8 | 24,004,839.3 | 15,519,025.0 | 23,872,263.7 |
| 2. Matumizi ya Maendeleo | 11,701,584.2 | 15,817,055.6 | 15,682,330.2 | 14,077,220.0 | 11,545,346.6 | 13,331,811.1 |
| Fedha za ndani | 9,251,759.3 | 12,386,668.7 | 13,970,706.2 | 10,795,139.1 | 8,916,135.1 | 10,049,730.3 |
| Fedha za nje | 2,449,824.8 | 3,430,387.0 | 1,711,623.9 | 3,282,080.9 | 2,629,211.5 | 3,282,080.9 |
| **C. NAKISI/SALIO (A-B)** | **(5,990,571.5)** | **(7,420,181.2)** | **(9,879,574.8)** | **(6,701,047.5)** | **(5,035,125.3)** | **(6,701,047.5)** |
| **D. KUZIBA NAKISI** | **5,990,571.5** | **7,420,181.2** | **8,167,950.9** | **6,701,047.5** | **5,035,125.3** | **6,701,047.5** |
| 1. Fedha kutoka nje | 3,354,230.2 | 3,818,767.9 | 3,681,040.7 | 4,802,731.9 | 3,936,864.4 | 4,802,731.9 |
| Ruzuku | 527,487.8 | 622,525.4 | 506,327.7 | 981,199.1 | 379,963.7 | 981,199.1 |
| Basket support | 175,363.7 | 85,966.8 | 90,052.5 | 130,122.8 | 73,663.1 | 130,122.8 |
| Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL | 287,345.5 | 1,298,502.6 | 1,851,237.4 | 2,127,770.5 | 1,663,008.8 | 2,127,770.5 |
| Mikopo ya miradi | 1,669,866.4 | 2,818,336.6 | 1,115,243.7 | 2,227,122.3 | 2,156,145.5 | 2,227,122.3 |
| Mikopo ya masharti ya kibiashara | 3,121,190.2 | 1,809,493.7 | 3,011,725.4 | 2,100,464.0 | 1,596,602.5 | 2,100,464.0 |
| Kulipia madeni ya nje (Amortization Foreign) | (2,427,023.4) | (2,816,057.3) | (2,893,546.0) | (2,763,946.8) | (1,932,519.3) | (2,763,946.8) |
| 2. Fedha za Ndani | 2,636,341.3 | 3,601,413.3 | 4,486,910.2 | 1,898,315.6 | 1,098,260.9 | 1,898,315.6 |
| Mikopo isiyo ya mabenki | 1,550,288.0 | 1,003,509.3 | 2,171,460.3 | 209,642.4 | 1,815,899.1 | 209,642.4 |
| Mikopo ya mabenki | 1,808,932.4 | 1,846,493.2 | 2,426,063.1 | 1,688,673.2 | (807,482.9) | 1,688,673.2 |
| Mikopo ya ndani (Rollover) | 3,262,551.9 | 3,044,431.8 | 3,513,913.7 | 3,542,060.7 | 2,446,885.1 | 3,542,060.7 |
| Marekebisho (Adjustment to Cash) | (715,561.1) | 753,597.9 | (97,656.8) | - | 98,568.0 | 8,723.3 |
| Kulipia madeni ya ndani (amortization) | (3,262,551.9) | (3,044,431.8) | (3,513,913.7) | (3,542,060.7) | (2,446,885.1) | (3,542,060.7) |
| Expenditure float | (7,318.0) | (2,187.1) | (12,956.4) | - | (8,723.3) | (8,723.3) |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**Kielelezo Na. 3.4: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI (Shilingi Milioni)**



## Jedwali Na. 30: MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI

**Shilingi Milioni**

| Fungu | Maelezo | Halisi 2022/2023 | | | Bajeti iliyoidhinishwa 2023/2024 | | | Makadirio 2024/2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
| **701** | **Huduma za Kawaida** | **11,809,729.6** | **5,523,214.2** | **17,332,943.9** | **9,407,214.0** | **6,846,846.7** | **16,254,060.7** | **12,217,855.7** | **6,525,488.7** | **18,743,344.4** |
| 70111 | Utawala na Shughuli za Bunge (CS) | 1,875,069.2 | 1,854,370.0 | 3,729,439.1 | 1,838,291.5 | 4,207,186.1 | 6,045,477.6 | 2,583,277.7 | 3,228,315.9 | 5,811,593.6 |
| **70112** | **Fedha na Masuala ya Kodi (CS)** | **6,195,793.1** | **2,398,948.5** | **8,594,741.5** | **3,130,441.0** | **897,802.7** | **4,028,243.7** | **1,637,074.5** | **1,064,473.4** | **2,701,547.9** |
| 70113 | Mambo ya Nje (CS) | 150,525.3 | 34,990.0 | 185,515.3 | 128,334.1 | 39,786.1 | 168,120.2 | 186,874.4 | 60,746.0 | 247,620.4 |
| 70121 | Misaada ya Kiuchumi kutoka Nje (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70122 | Misaada ya Kiuchumi kupitia Mashirika ya Kimataifa(CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70131 | Huduma za Umma (CS) | 393,493.3 | 27,237.7 | 420,731.0 | 258,296.6 | 98,867.4 | 357,164.0 | 534,610.5 | 101,723.3 | 636,333.8 |
| 70132 | Huduma za Mipango na Takwimu (CS) | 1,708,377.9 | 480,307.6 | 2,188,685.6 | 2,293,129.1 | 1,090,776.0 | 3,383,905.1 | 3,802,339.4 | 1,400,931.5 | 5,203,270.9 |
| 70133 | Huduma nyingine za Kawaida (CS) | 168,694.1 | 55,109.3 | 223,803.4 | 61,403.1 | 67,337.3 | 128,740.4 | 174,204.5 | 147,942.5 | 322,147.0 |
| 70140 | Utafiti wa Msingi (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70150 | Utafiti na Maendeleo Huduma za Umma (CS) | 1,673.2 | 1,030.4 | 2,703.6 | 4,429.7 | 5,782.8 | 10,212.5 | 8,264.7 | 2,507.2 | 10,771.9 |
| 70160 | Huduma za Umma zisizotajwa hapo Juu (CS) | 676,973.9 | 525,032.0 | 1,202,005.9 | 632,666.0 | 358,280.6 | 990,946.6 | 1,415,349.5 | 409,610.0 | 1,824,959.4 |
| 70170 | Deni la Taifa (CS) | 10,807.5 | 622.3 | 11,429.8 | 13,978.1 | 3,181.0 | 17,159.1 | 21,024.0 | 2,322.3 | 23,346.2 |
| 70180 | Uhamishaji Fedha Ndani ya Serikali (CS) | 628,322.2 | 145,566.4 | 773,888.6 | 1,046,244.9 | 77,846.7 | 1,124,091.5 | 1,854,836.6 | 106,916.7 | 1,961,753.3 |
| **702** | **Ulinzi** | **358,655.2** | **17,436.4** | **376,091.6** | **2,156,098.8** | **53,334.9** | **2,209,433.7** | **3,064,405.3** | **50,260.3** | **3,114,665.6** |
| 70210 | Huduma za Ulinzi wa Kijeshi (CS) | 357,960.5 | 16,792.6 | 374,753.1 | 2,155,387.5 | 50,071.6 | 2,205,459.0 | 3,063,162.6 | 46,775.7 | 3,109,938.4 |
| 70220 | Huduma za Ulinzi wa Kiraia (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70230 | Misaada ya Nje ya Ulinzi (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70240 | Utafiti na Maendeleo ya Ulinzi (CS) | 694.7 | 643.8 | 1,338.5 | 711.3 | 3,263.4 | 3,974.6 | 1,242.7 | 3,484.5 | 4,727.2 |
| 70250 | Huduma za Ulinzi zisizotajwa hapo Juu (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| **703** | **Usalama wa Raia** | **955,888.9** | **647,112.6** | **1,603,001.6** | **1,278,566.6** | **1,377,087.0** | **2,655,653.6** | **5,169,393.5** | **1,671,377.4** | **6,840,770.9** |
| 70310 | Huduma za Ulinzi wa Kijeshi (CS) | 317,075.4 | 66,364.2 | 383,439.6 | 425,568.0 | 137,475.9 | 563,043.9 | 3,931,113.5 | 117,808.2 | 4,048,921.7 |
| 70320 | Huduma za Ulinzi wa Kiraia (CS) | 35,602.6 | 124,152.3 | 159,755.0 | 42,716.8 | 202,899.8 | 245,616.6 | 74,631.3 | 168,753.9 | 243,385.2 |
| 70330 | Mahakama (CS) | 433,857.0 | 413,015.6 | 846,872.6 | 619,274.8 | 884,319.7 | 1,503,594.5 | 860,192.8 | 1,235,701.9 | 2,095,894.7 |
| 70340 | Magereza (CS) | 103,920.2 | 16,636.9 | 120,557.1 | 140,746.4 | 78,136.0 | 218,882.4 | 244,338.1 | 65,616.2 | 309,954.2 |
| 70350 | Huduma za utafiti na Maendeleo Usalama wa Raia (CS) | 13.2 | 5,411.2 | 5,424.4 | 34.7 | 6,100.0 | 6,134.7 | 232.9 | 6,105.0 | 6,337.9 |
| 70360 | Huduma Usalama wa Raia zisizotajwa hapo juu (CS) | 65,420.5 | 21,532.3 | 86,952.9 | 50,226.0 | 68,155.5 | 118,381.5 | 58,884.9 | 77,392.2 | 136,277.1 |
| **704** | **Shughuli za Kiuchumi** | **1,195,473.2** | **3,967,555.8** | **5,163,029.0** | **1,290,129.3** | **4,459,935.4** | **5,750,064.7** | **1,697,374.3** | **5,432,268.0** | **7,129,642.3** |
| 70411 | Shughuli za Kiuchumi na Biashara (CS) | 160,690.1 | 308,257.2 | 468,947.3 | 231,251.9 | 649,905.8 | 881,157.6 | 352,873.0 | 254,459.7 | 607,332.7 |
| 70412 | Masuala ya Kazi (CS) | 16,999.8 | 3,531.9 | 20,531.7 | 35,422.5 | 12,395.6 | 47,818.2 | 45,562.9 | 6,787.6 | 52,350.4 |
| 70421 | Kilimo (CS) | 273,767.6 | 1,007,320.6 | 1,281,088.2 | 265,210.1 | 1,360,669.1 | 1,625,879.2 | 394,391.9 | 1,131,208.4 | 1,525,600.3 |
| 70422 | Misitu (CS) | 45,920.3 | 883,534.0 | 929,454.3 | 41,267.3 | 1,183,161.7 | 1,224,428.9 | 76,912.4 | 1,988,489.9 | 2,065,402.3 |
| 70423 | Uvuvi na Uwindaji (CS) | 146,782.6 | 484,899.4 | 631,681.9 | 155,354.7 | 565,446.7 | 720,801.4 | 72,091.0 | 393,126.4 | 465,217.3 |
| 70431 | Makaa ya Mawe na Nishati nyingine (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70432 | Petroli na Gesi Asilia (CS) | 15,365.1 | 23,208.5 | 38,573.6 | 18,558.4 | 26,877.3 | 45,435.8 | 28,796.5 | 60,303.4 | 89,099.8 |
| 70433 | Nishati ya Nyukilia (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70434 | Nishati nyingine (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70435 | Umeme (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70436 | Nishati isiyo ya umeme (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70441 | Uchimbaji Madini yasiyo Nishati (CS) | 41,405.8 | 43,635.2 | 85,040.9 | 33,804.5 | 36,278.6 | 70,083.1 | 50,132.4 | 28,602.0 | 78,734.4 |
| 70442 | Uzalishaji Viwandani (CS) | 16,732.6 | 11,895.1 | 28,627.7 | 15,808.6 | 9,779.3 | 25,587.9 | 37,794.5 | 11,772.2 | 49,566.7 |
| 70443 | Ujenzi (CS) | 18,801.8 | 12,188.7 | 30,990.5 | 20,968.6 | 28,222.0 | 49,190.7 | 33,954.8 | 21,671.2 | 55,626.0 |
| 70451 | Usafiri wa Barabara (CS) | 31,172.2 | 6,916.8 | 38,089.0 | 102,420.5 | 22,089.4 | 124,509.9 | 72,694.3 | 11,074.3 | 83,768.7 |
| 70452 | Usafiri wa Majini (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70453 | Usafiri wa Reli (CS) | 101,698.5 | 8,588.5 | 110,287.1 | 96,483.0 | 13,115.6 | 109,598.6 | 130,743.2 | 32,139.8 | 162,883.0 |
| 70454 | Usafiri wa Anga (CS) | 73,391.1 | 6,038.8 | 79,429.9 | 2,102.6 | 4,810.2 | 6,912.8 | 3,026.3 | 5,032.7 | 8,059.0 |
| 70455 | Usafirishaji kwa njia ya Bomba na njia nyingine za usafiri (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70460 | Mawasiliano (CS) | 64,126.4 | 471,198.3 | 535,324.7 | 105,800.0 | 187,043.0 | 292,843.0 | 125,831.8 | 204,864.5 | 330,696.3 |
| 70471 | Huduma za Biashara na Utunzaji Mizigo (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |

**Jedwali Na. 30 Linaendelea**

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 70472 | Hoteli na Migahawa (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70473 | Utalii (CS) | 10,956.6 | 152,566.3 | 163,522.8 | 12,577.4 | 203,455.9 | 216,033.3 | 43,574.7 | 497,992.4 | 541,567.1 |
| 70474 | Miradi ya Maendeleo (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70481 | Utafiti katika shughuli za Kiuchumi, Biashara na Kazi (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70482 | Utafiti na Maendeleo ya Kilimo, Misitu, Uvuvi na Uwindaji (CS) | 3,029.2 | 66.3 | 3,095.5 | 1,584.2 | 542.8 | 2,127.0 | 2,152.7 | 527.0 | 2,679.7 |
| 70483 | Utafiti na Maendeleo ya Mafuta na Nishati (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70484 | Utafiti na Maendeleo ya Uchimbaji Madini, Uzalishaji Viwandani na Ujenzi (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70485 | Utafiti na Maendeleo ya Usafiri (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70486 | Utafiti na Maendeleo ya Mawasiliano (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70487 | Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Vingine (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70490 | Shughuli nyingine za Kiuchumi zisizotajwa hapo juu (CS) | 174,633.7 | 543,710.1 | 718,343.8 | 151,514.9 | 156,142.5 | 307,657.4 | 226,842.0 | 784,216.7 | 1,011,058.6 |
| **705** | **Hifadhi ya Mazingira** | **55,912.4** | **8,036.0** | **63,948.4** | **35,621.6** | **36,555.1** | **72,176.7** | **66,539.5** | **41,297.9** | **107,837.4** |
| 70510 | Hifadhi ya Taka (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70520 | Hifadhi ya Maji Taka (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70530 | Kupunguza Uharibifu wa Mazingira (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70540 | Hifadhi ya Viumbehai na Mazingira (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70550 | Utafiti na Maendeleo ya Hifadhi ya Mazingira (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70560 | Huduma nyingine za Hifadhi ya Mazingira zisizotajwa hapo juu (CS) | 55,912.4 | 8,036.0 | 63,948.4 | 35,621.6 | 36,555.1 | 72,176.7 | 66,539.5 | 41,297.9 | 107,837.4 |
| **706** | **Nyumba na Huduma za Jamii** | **947,542.7** | **233,867.6** | **1,181,410.3** | **490,202.4** | **313,027.8** | **803,230.1** | **515,266.5** | **381,608.0** | **896,874.5** |
| 70610 | Maendeleo ya Nyumba (CS) | 400,792.7 | 40,161.6 | 440,954.3 | 274,844.8 | 12,690.3 | 287,535.1 | 271,413.7 | 148,777.2 | 420,190.9 |
| 70620 | Maendeleo ya Jamii (CS) | 70,447.9 | 101,150.9 | 171,598.8 | 109,983.6 | 109,093.1 | 219,076.7 | 110,981.9 | 125,316.9 | 236,298.8 |
| 70630 | Usambazaji Maji (CS) | 42,873.2 | 69,549.6 | 112,422.8 | 82,523.0 | 165,783.7 | 248,306.7 | 83,738.4 | 88,079.1 | 171,817.5 |
| 70640 | Taa za Barabarani (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70650 | Utafiti wa Nyumba na Maendeleo ya Jamii (CS) | 136.7 | 6.7 | 143.4 | 737.8 | 890.1 | 1,627.9 | 2,049.9 | 1,840.5 | 3,890.4 |
| 70660 | Nyumba na Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu (CS) | 433,292.2 | 22,998.8 | 456,291.0 | 22,113.0 | 24,570.6 | 46,683.7 | 47,082.5 | 17,594.4 | 64,676.9 |
| **707** | **Afya** | **1,215,954.2** | **354,454.9** | **1,570,409.1** | **1,466,237.3** | **561,989.6** | **2,028,227.0** | **2,109,919.7** | **755,161.0** | **2,865,080.7** |
| 70711 | Madawa (IS) | 562.9 | 0.0 | 562.9 | 1,137.8 | 0.0 | 1,137.8 | 3,433.7 | 0.0 | 3,433.7 |
| 70712 | Bidhaa nyingine za madawa (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70713 | uduma za Tiba na Vifaa vya Tiba (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70721 | Huduma za Tiba za Jumla (IS) | 82,189.9 | 1,222.0 | 83,412.0 | 54,214.6 | 82,845.4 | 137,060.0 | 43,782.3 | 37,682.5 | 81,464.8 |
| 70722 | Huduma Maalumu za Tibas (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70723 | Huduma za Meno (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70724 | Huduma za Wakunga Wasaidizi (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70731 | Huduma za Hospitali (IS) | 43,739.7 | 14,682.3 | 58,422.0 | 29,235.7 | 84,144.9 | 113,380.6 | 31,342.0 | 35,872.1 | 67,214.0 |
| 70732 | Huduma Maalumu za Hospitali (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70733 | Huduma za Vifaa vya Kujifungulia (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70734 | Huduma za Wakunga na Wakunga wa Jadi (IS) | 8,997.8 | 0.0 | 8,997.8 | 1,047.7 | 0.0 | 1,047.7 | 2,210.0 | 0.0 | 2,210.0 |
| 70740 | Huduma za Afya kwa Umma (IS) | 667,460.9 | 106,913.7 | 774,374.6 | 633,146.0 | 244,345.1 | 877,491.2 | 990,561.6 | 520,146.0 | 1,510,707.6 |
| 70750 | Utafiti na Maendeleo ya Huduma za Afya (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70760 | Huduma za Afya zisizotajwa hapo juu (CS) | 413,003.0 | 231,636.9 | 644,639.9 | 747,455.4 | 150,654.2 | 898,109.6 | 1,038,590.1 | 161,460.4 | 1,200,050.5 |
| **708** | **Burudani, Utamaduni na Dini** | **9,090.9** | **10,767.8** | **19,858.7** | **12,405.9** | **10,193.1** | **22,599.0** | **18,341.1** | **30,921.5** | **49,262.6** |
| 70810 | Huduma za Burudani na Michezo (IS) | 2,496.9 | 9,456.3 | 11,953.2 | 4,076.1 | 7,884.0 | 11,960.1 | 5,495.1 | 6,060.5 | 11,555.6 |
| 70820 | Huduma za Utamaduni (IS) | 6,087.0 | 1,288.6 | 7,375.6 | 7,213.8 | 1,676.3 | 8,890.1 | 11,730.0 | 23,656.2 | 35,386.2 |
| 70830 | Huduma za Utangazaji na Uchapishaji (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70840 | Dini na Huduma nyingine za Kijamii (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70850 | Utafiti na Maendeleo katika Burudani, Utamaduni na Dini (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70860 | Huduma nyingine za Burudani, Utamaduni na Dini zisizotajwa hapo juu (CS) | 507.0 | 22.9 | 529.9 | 1,116.0 | 632.8 | 1,748.8 | 1,116.0 | 1,204.8 | 2,320.8 |
| **709** | **Elimu** | **3,903,604.7** | **2,392,191.6** | **6,295,796.3** | **6,663,668.0** | **1,509,125.3** | **8,172,793.3** | **8,471,108.1** | **981,468.9** | **9,452,576.9** |
| 70911 | Elimu ya Awali (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70912 | Elimu ya Msingi (IS) | 2,254,071.7 | 1,553,211.7 | 3,807,283.4 | 4,943,620.7 | 408,158.1 | 5,351,778.8 | 6,188,339.3 | 204,141.3 | 6,392,480.6 |
| 70921 | Elimu ya Sekondari (Kidato cha I - IV) (IS) | 1,130,460.2 | 567,451.9 | 1,697,912.1 | 1,165,462.3 | 527,366.3 | 1,692,828.5 | 1,470,032.3 | 398,845.3 | 1,868,877.6 |
| 70922 | Elimu ya Sekondari (Kidato cha V - VI) (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70930 | Elimu baada ya Sekondari isiyo ya Chuo Kikuu (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70941 | Daraja la Awali Elimu ya Chuo Kikuu (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70942 | Daraja linalofuata Elimu ya Chuo Kikuu (IS) | 23,772.6 | 172,200.1 | 195,972.7 | 29,387.9 | 312,287.5 | 341,675.4 | 46,533.8 | 75,998.2 | 122,532.0 |
| 70950 | Elimu isiyopambanuliwa (IS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70960 | Huduma za Ziada kwa Elimu (IS) | 495,300.1 | 99,327.9 | 594,628.0 | 525,197.1 | 261,313.4 | 786,510.6 | 766,202.6 | 302,484.1 | 1,068,686.7 |
| 70970 | Utafiti na Maendeleo ya Elimu (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70980 | Huduma za Elimu zisizotajwa hapo juu (CS) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| **710** | **Kinga ya Jamii** | **52,670.0** | **25,202.6** | **77,872.6** | **64,580.0** | **46,993.9** | **111,573.9** | **71,127.4** | **74,505.1** | **145,632.5** |
| 71011 | Ugonjwa | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71012 | Ulemavu | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71020 | Wazee | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71030 | Waathirika | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71040 | Familia na Watoto | 38,420.9 | 15,682.3 | 54,103.2 | 34,071.8 | 40,100.8 | 74,172.6 | 52,924.7 | 69,632.1 | 122,556.8 |
| 71050 | Ukosefu wa Ajira | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71060 | Nyumba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71070 | Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71080 | Utafiti na Maendeleo ya Kinga ya Jamii | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71090 | Huduma za Kinga ya Jamii zisizotajwa hapo juu | 14,249.0 | 9,520.3 | 23,769.4 | 30,508.2 | 6,893.1 | 37,401.3 | 18,202.7 | 4,873.0 | 23,075.7 |
| **7** | **Jumla** | **20,504,521.8** | **13,179,839.6** | **33,684,361.4** | **22,864,723.8** | **15,215,088.7** | **38,079,812.6** | **33,401,331.0** | **15,944,356.8** | **49,345,687.8** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
CS: Collective Services IS: Individual Services

# SURA YA 4

## SEKTA YA NJE

**Bidhaa Zilizouzwa Nje**

91. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 7,696.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,223.8 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia, hususan kahawa na tumbaku na bidhaa zisizo asilia ikiwemo, dhahabu, mbogamboga, maua na mbegu za mafuta. Aidha, mauzo ya bidhaa zisizo asilia yalichangia asilimia 82.1 ya mauzo yote nje ya nchi, bidhaa asilia zilichangia asilimia 12.4 na bidhaa zisizorekodiwa asilimia 5.5.

**Bidhaa Asilia**

92. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 953.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 766.5 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 24.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya mazao ya tumbaku, kahawa na chai sambamba na kuongezeka kwa mahitaji nje ya nchi pamoja na kuendelea kuimarika kwa uzalishaji wa ndani. Mchango wa thamani ya mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi uliongezeka hadi asilimia 12.4 mwaka 2023 kutoka asilimia 10.6 mwaka 2022.

**Korosho**

93. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya korosho nje ilipungua hadi dola za Marekani milioni 206.4 kutoka dola za Marekani milioni 226.9 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 9.0. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha korosho kilichouzwa nje kutoka tani 234,000 mwaka 2022 hadi tani 219,602 mwaka 2023. Aidha, wastani wa bei ya korosho ulipungua kwa asilimia 3.1 na kufikia dola za Marekani 940 kwa tani mwaka 2023 kutoka wastani wa dola za Marekani 970 kwa tani mwaka 2022.

**Kahawa**

94. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya kahawa nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 41.1 hadi dola za Marekani milioni 227.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 161.2 mwaka 2022. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha kahawa kilichouzwa nje hadi tani 84,400 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 55,200 mwaka 2022. Aidha, wastani wa bei ya kuuza kahawa ulipungua kwa asilimia 7.5 na kufikia dola za Marekani 2,700.8 kwa tani mwaka 2023 kutoka wastani wa dola za Marekani 2,919.6 kwa tani mwaka 2022.

**Pamba**

95. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya pamba nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 101.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 103.4 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 1.4. Hii ilitokana na kupungua kwa bei ya kuuza pamba na kufikia

wastani wa dola za Marekani 1,463.4 kwa tani mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 2,113.2 kwa tani mwaka 2022. Kiasi cha pamba kilichouzwa nje kiliongezeka kwa asilimia 42.3 kufikia tani 69,600 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 48,900 mwaka 2022.

**Katani**

96. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya katani nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 20.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 24.3 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 16.2. Hii ilichangiwa na kupungua kwa kiasi cha katani kilichouzwa nje kwa asilimia 16.2 na kufikia tani 12,500 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 14,900 zilizouzwa mwaka 2022. Aidha, wastani wa bei ya kuuza katani ulikuwa dola za Marekani 1,628.9 kwa tani mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 1,629.1 kwa tani mwaka 2022.

**Chai**

97. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya chai nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 31.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 30.0 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha chai kilichouzwa nje ya nchi na kufikia tani 22,200 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 21,100 mwaka 2022. Aidha, wastani wa bei ya kuuza chai ulipungua kwa asilimia 1.2 na kufikia dola za Marekani 1,403.6 kwa tani mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 1,420.3 kwa tani mwaka 2022.

**Tumbaku**

98. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya tumbaku nje ilikuwa dola za Marekani milioni 340.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 178.5 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 90.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya tumbaku na kufikia tani 82,000 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 49,300 mwaka 2022. Aidha, wastani wa bei ya kuuza tumbaku uliongezeka kwa asilimia 14.5 na kufikia dola za Marekani 4,150.8 kwa tani mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani 3,624.1 kwa tani mwaka 2022.

**Bidhaa Zisizo Asilia**

99. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 6,321.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,058.4 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya madini na bidhaa nyingine ikiwemo, mbogamboga, maua na mbegu za mafuta.

**Madini**

100. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 3,551.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,395.3 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 4.6. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu nje ya nchi. Thamani ya mauzo ya dhahabu nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 7.9 na kufikia

dola za Marekani milioni 3,058.9 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,835.1 mwaka 2022. Aidha, mauzo ya madini yalichangia asilimia 56.2 ya mauzo yote ya bidhaa zisizo asilia mwaka 2023. Vile vile, mauzo ya dhahabu nje ya nchi yalichangia asilimia 86.1 katika mauzo ya madini nje ya nchi mwaka 2023.

**Bidhaa za Viwandani**

101. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 1,363.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,419.2 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 3.9. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo ya bidhaa, hususan chuma, nguo na bidhaa za karatasi. Katika kipindi hicho, mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi yalichangia asilimia 21.6 ya mauzo yote ya bidhaa zisizo asilia.

**Samaki na Mazao ya Samaki**

102. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya samaki na mazao yake nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 164 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 168.2 mwaka 2022. Hii ilitokana na kupungua kwa bei ya kuuza samaki na mazao ya samaki.

**Mbogamboga na Maua**

103. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya mbogamboga na maua nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 417.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 289.6 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 44.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya mbogamboga na matunda nje ya nchi kulikosababishwa na kuongezeka kwa uhitaji wa bidhaa hizi katika soko la nje.

**Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje**


104. Mwaka 2023, thamani ya bidhaa nyinginezo zilizouzwa nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 690.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 654.9 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 5.4. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya mbegu za mafuta na kufikia dola za Marekani milioni 306.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 172.4 mwaka 2022. Bidhaa zinazojumuishwa katika kundi hili ni pamoja na mbegu za mafuta, kakao, ngozi, maharage, bidhaa za mbao na nafaka, hususan mahindi na mchele. Sehemu kubwa ya bidhaa hizo iliuzwa nchi jirani ikiwemo Kenya, Uganda na Rwanda.

## Jedwali Na. 4.1: Bidhaa Zilizouzwa Nje Mwaka 2019 - 2023

| **Bidhaa** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa Asilia (US$ milioni)** | | | | | | |
| **Kahawa** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 152.2 | 145.2 | 155.2 | 161.2 | 227.9 | 41.4 |
| Kiasi ('000 tani) | 76.2 | 64.0 | 68.0 | 55.2 | 84.4 | 52.9 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,996.5 | 2,268.9 | 2,284.4 | 2,919.6 | 2,700.8 | -7.5 |
| **Pamba** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 91.8 | 87.5 | 81.3 | 103.4 | 101.9 | -1.4 |
| Kiasi ('000 tani) | 79.0 | 72.6 | 48.8 | 48.9 | 69.6 | 42.3 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,162.2 | 1,206.4 | 1,665.0 | 2,113.2 | 1,463.4 | -30.7 |
| **Katani** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 19.3 | 17.6 | 20.2 | 24.3 | 20.4 | -16.2 |
| Kiasi ('000 tani) | 12.2 | 11.2 | 12.6 | 14.9 | 12.5 | -16.2 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,581.7 | 1,566.2 | 1,600.0 | 1,629.1 | 1,628.9 | 0.0 |
| **Chai** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 45.7 | 32.4 | 32.9 | 30.0 | 31.1 | 3.7 |
| Kiasi ('000 tani) | 31.7 | 24.1 | 24.2 | 21.1 | 22.2 | 4.9 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,444.2 | 1,345.5 | 1,356.5 | 1,420.3 | 1,403.6 | -1.2 |
| **Tumbaku** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 146.5 | 148.7 | 127.5 | 178.5 | 340.4 | 90.7 |
| Kiasi ('000 tani) | 42.6 | 42.6 | 37.7 | 49.3 | 82.0 | 66.5 |
| Bei (US$ kwa tani) | 3,440.9 | 3,494.2 | 3,381.5 | 3,624.1 | 4,150.8 | 14.5 |
| **Korosho** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 353.1 | 359.6 | 159.0 | 226.9 | 206.4 | -9.0 |
| Kiasi ('000 tani) | 295.6 | 320.9 | 154.4 | 234.0 | 219.6 | -6.1 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,194.6 | 1,120.6 | 1,030.3 | 970.0 | 939.9 | -3.1 |
| **Karafuu** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 9.1 | 17.1 | 51.8 | 42.1 | 25.1 | -40.3 |
| Kiasi ('000 tani) | 1.8 | 3.6 | 7.0 | 5.9 | 4.7 | -20.9 |
| Bei (US$ kwa tani) | 5,047.8 | 4,770.0 | 7,347.6 | 7,104.0 | 5,356.9 | -24.6 |
| **Jumla (Bidhaa Asilia)** | **817.7** | **808.1** | **627.9** | **766.5** | **953.3** | **24.4** |
| **Bidhaa Zisizo Asilia (US$ millioni)** | | | | | | |
| **Madini** | 2,332.7 | 3,375.0 | 3,116.4 | 3,395.3 | 3,551.4 | 4.6 |
| Dhahabu | 2,215.1 | 2,957.5 | 2,737.1 | 2,835.1 | 3,058.9 | 7.9 |
| Almasi | 81.3 | 20.2 | 8.5 | 62.7 | 23.6 | -62.4 |
| Madini mengine | 36.3 | 397.2 | 370.8 | 497.4 | 469.0 | -5.7 |
| **Bidhaa za Viwandani** | **845.8** | **902.7** | **1,200.0** | **1,419.2** | **1,363.3** | **-3.9** |
| Nyuzi za Pamba | 5.2 | 6.9 | 3.6 | 1.9 | 0.5 | -75.2 |
| Kahawa iliyozalishwa | 1.4 | 5.2 | 16.3 | 21.8 | 4.5 | -79.2 |
| Tumbaku iliyozalishwa | 24.5 | 18.3 | 32.0 | 34.5 | 37.9 | 9.8 |
| Mazao ya Katani | 23.4 | 23.2 | 33.6 | 35.4 | 31.4 | -11.1 |
| Mazao mengine ya Viwandani | 791.3 | 849.1 | 1,114.5 | 1,325.6 | 1,289.0 | -2.8 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | 168.0 | 139.6 | 164.3 | 168.2 | 164.0 | -2.5 |
| Mazao ya Mboga na Maua | 209.6 | 274.1 | 378.6 | 289.6 | 417.2 | 44.1 |
| Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports) | 242.8 | 87.7 | 90.2 | 131.2 | 135.2 | 3.1 |
| Bidhaa nyinginezo | 387.1 | 474.2 | 813.5 | 654.9 | 690.5 | 5.4 |
| Jumla (Bidhaa zisizo Asilia) | 4,186.0 | 5,253.3 | 5,763.0 | 6,058.4 | 6,321.6 | 4.3 |
| Bidhaa zisizo rekodiwa | 387.8 | 315.3 | 370.1 | 404.2 | 426.9 | 5.6 |
| **Jumla Kuu (Bidhaa Zote)** | **5,377.6** | **6,371.7** | **6,756.2** | **7,223.8** | **7,696.6** | **6.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 4.1: Mchanganuo wa Bidhaa Zilizouzwa Nje**




**Mapato ya Huduma**

105. Mwaka 2023, mapato yatokanayo na biashara ya huduma yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 6,285.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,762.0 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 32.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato yaliyotokana na huduma za utalii pamoja na usafirishaji. Mapato yatokanayo na huduma za safari za utalii yaliongezeka kwa asilimia 33.5 na kufikia dola za Marekani milioni 3,373.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,527.8 mwaka 2022. Aidha, idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka kwa asilimia 24.3 na kufikia watalii 1,808,205 mwaka 2023 ikilinganishwa na watalii 1,454,920 mwaka 2022. Vile vile, mapato yatokanayo na huduma ya usafirishaji yalikuwa dola za Marekani milioni 2,426.0 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,872.0 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 29.6. Mapato ya huduma yalichangia asilimia 45.0 ya thamani ya mapato yote ya bidhaa na huduma kutoka nje.

**Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi**

106. Mwaka 2023, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ilipungua hadi dola za Marekani milioni 13,728.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 14,208.7 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 3.4. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi na thamani ya mafuta ya petroli yaliyoagizwa kutoka nje ya nchi pamoja na kuendelea kuimarika kwa uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi ikiwemo, bidhaa za kati kama vile mbolea na bidhaa za matumizi ya kawaida.

**Bidhaa za Kukuza Mitaji**

107. Mwaka 2023, thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoingizwa nchini ilikuwa dola za Marekani milioni 5,592.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,167.5 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama ya vyombo vya usafiri, mitambo, na vifaa vya ujenzi sambamba na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini baada ya changamoto zilizotokana na UVIKO - 19.

**Bidhaa za Kati**

108. Mwaka 2023, thamani ya bidhaa za kati zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 4,466.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,102.1 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 12.5. Hii ilitokana na kupungua kwa thamani na kiasi cha mafuta ya petroli yaliyoagizwa kutoka nje ya nchi pamoja na kupungua kwa thamani ya mbolea iliyoagizwa kufuatia kushuka kwa bei katika soko la dunia. Katika kipindi hicho, thamani ya uagizaji wa mafuta ya petroli ilipungua kwa asilimia 16.0 na kuchangia asilimia 21.6 ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

**Bidhaa za Matumizi ya Kawaida**

109. Mwaka 2023, thamani ya bidhaa za matumizi ya kawaida zilizoagizwa kutoka nje ilikuwa dola za Marekani milioni 3,669.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,939.1 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 6.8. Hii ilitokana na kuendelea kuimarika kwa uzalishaji wa ndani wa bidhaa nyingine, hususan bidhaa za chuma, saruji, rangi za majengo na bidhaa za plastiki. Aidha, uagizaji wa bidhaa za vyakula kutoka nje uliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 885.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 735.5, sawa na ongezeko la asilimia 20.4. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uagizaji wa ngano kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya nchi.

**Malipo ya Huduma**


110. Mwaka 2023, malipo ya huduma yalikuwa dola za Marekani milioni 2,329.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,465.4 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 5.5. Hii ilitokana na kupungua kwa gharama za huduma za usafirishaji sambamba na kushuka kwa gharama za uagizaji bidhaa nje ya nchi.


**Jedwali Na. 4.2: Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje Mwaka 2019 - 2023 (Dola za Marekani Milioni)**

| Bidhaa | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa za Kukuza Mitaji** | **3,521.2** | **3,138.8** | **3,836.0** | **5,167.5** | **5,592.9** | **8.2** |
| Vifaa vya Usafirishaji | 989.3 | 738.1 | 970.4 | 1,420.4 | 1,571.4 | 10.6 |
| Majengo na Ujenzi | 996.2 | 925.5 | 1,159.0 | 1,455.1 | 1,486.4 | 2.1 |
| Mitambo | 1,535.7 | 1,475.3 | 1,706.6 | 2,291.9 | 2,535.2 | 10.6 |
| **Bidhaa za Kati** | **2,666.9** | **2,229.8** | **3,250.5** | **5,102.1** | **4,466.3** | **-12.5** |
| Uagizaji Mafuta | 1,785.8 | 1,282.7 | 2,084.4 | 3,532.6 | 2,967.0 | -16.0 |
| Mbolea | 129.3 | 187.7 | 189.4 | 500.9 | 414.0 | -17.3 |
| Malighafi za Viwanda | 751.7 | 759.4 | 976.7 | 1,068.6 | 1,085.2 | 1.6 |
| **Bidhaa za Matumizi ya Kawaida** | **2,427.1** | **2,463.1** | **2,916.9** | **3,939.1** | **3,669.7** | **-6.8** |
| Bidhaa za Vyakula | 431.9 | 420.4 | 500.9 | 735.5 | 885.5 | 20.4 |
| Bidhaa Nyingine | 1,995.1 | 2,042.7 | 2,415.9 | 3,203.6 | 2,784.2 | -13.1 |
| **Jumla (FoB)** | **8,615.2** | **7,831.7** | **10,003.4** | **14,208.7** | **13,728.9** | **-3.4** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 4.2: Mchanganuo wa Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje**








## Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali

111. Mwaka 2023, mahusiano ya kibiashara kati ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani ikiwemo, jumuiya za kikanda na kimataifa yaliendelea kuimarika licha ya kuwepo kwa misukosuko katika uchumi wa dunia kufuatia vita baina ya Urusi na Ukraine. Katika kipindi hicho, bidhaa za Tanzania ziliuzwa zaidi katika nchi ya India ambayo ilichangia asilimia 21.4 ya mauzo yote, ikifuatiwa na Afrika Kusini (asilimia 15.4) pamoja na Umoja wa Falme

za Kiarabu (asilimia 9.4). Aidha, mazao ya nafaka (mahindi na mchele) na mbogamboga yaliuzwa zaidi nchi ya Kenya na mbegu za mafuta, tumbaku, kahawa na korosho ziliuzwa katika nchi ya China, India na Umoja wa Falme za Kiarabu. Vile vile, dhahabu iliuzwa katika nchi za Afrika Kusini, India, Umoja wa Falme za Kiarabu na Uswisi ambapo asilimia 97 ya dhahabu yote iliuzwa katika nchi hizo mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 4.3: Mchanganuo wa Masoko ya Bidhaa za Tanzania kwenda Nje ya Nchi Mwaka 2023 (Asilimia)**




112. Thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC ilipungua kwa asilimia 16.5 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,180.8 mwaka 2023, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,414.9 mwaka 2022. Hii ilichangiwa na kupungua kwa mauzo ya bidhaa katika nchi za Kenya na Uganda. Aidha, bidhaa zilizouzwa zaidi ni pamoja na mchele, mahindi, vyuma na mbolea.

113. Mwaka 2023, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ilikuwa dola za Marekani milioni 1,667.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,416.7 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 17.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo katika nchi za Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia. Aidha, bidhaa zilizouzwa zaidi ni pamoja na dhahabu, bidhaa za nguo, bidhaa za vioo, mbolea na bidhaa nyingine za viwandani.

114. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya bidhaa katika soko la Jumuiya ya Ulaya na Uswisi ilikuwa dola za Marekani milioni 1,125.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 961.7 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 17.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo hususan dhahabu katika nchi ya Uswisi.

115. Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia ilikuwa dola za Marekani milioni 3,370.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,129.4 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo katika nchi za China, India na Umoja wa Falme za Kiarabu.


**Jedwali Na. 4.3: Mauzo ya Bidhaa Kwenda Nchi Mbalimbali Mwaka 2019 - 2023**

| JUMUIYA/ NCHI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI | 741.5 | 1,490.5 | 893.5 | 955.6 | 1,120.0 | 17.2 |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 7.5 | 11.2 | 11.7 | 6.2 | 5.8 | -5.3 |
| **JUMLA- BARA LA ULAYA** | **749.0** | **1,501.7** | **905.2** | **961.7** | **1,125.9** | **17.1** |
| **AFRIKA** | | | | | | |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | |
| Afrika ya Kusini | 971.6 | 1161.6 | 916.7 | 929.6 | 1123.5 | 20.9 |
| Zambia | 63.6 | 54.1 | 68.6 | 80.0 | 98.6 | 23.3 |
| Swaziland | 5.9 | 0.1 | 0.1 | 0.3 | 0.4 | 61.6 |
| Zimbabwe | 18.8 | 21.1 | 14.8 | 15.5 | 38.9 | 151.5 |
| Msumbiji | 32.6 | 21.0 | 15.5 | 35.2 | 17.7 | -49.7 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 164.1 | 144.2 | 207.2 | 280.5 | 312.8 | 11.5 |
| Nchi nyingine za SADC | 69.7 | 51.4 | 73.7 | 75.6 | 75.6 | 0.0 |
| **JUMLA-SADC** | **1,326.3** | **1,453.5** | **1,296.7** | **1,416.7** | **1,667.5** | **17.7** |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | |
| Burundi | 87.9 | 177.7 | 163.3 | 212.8 | 172.3 | -19.0 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 164.1 | 144.2 | 207.2 | 280.5 | 312.8 | 11.5 |
| Kenya | 269.9 | 230.2 | 397.2 | 381.7 | 176.5 | -53.7 |
| Rwanda | 190.9 | 205.3 | 277.8 | 262.5 | 188.2 | -28.3 |
| Uganda | 123.7 | 191.2 | 314.0 | 264.2 | 311.7 | 18.0 |
| Sudan ya Kusini | 2.0 | 3.4 | 8.9 | 13.1 | 19.2 | 46.7 |
| **JUMLA-EAC** | **838.5** | **952.0** | **1,368.5** | **1,414.9** | **1,180.8** | **-16.5** |
| Nchi nyingine za Afrika | 64.5 | 36.4 | 57.3 | 94.0 | 163.8 | 74.2 |
| **JUMLA-AFRIKA** | **2,065.3** | **2,297.8** | **2,515.2** | **2,645.0** | **2,667.0** | **2.1** |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | |
| Marekani | 52.4 | 47.0 | 39.1 | 74.6 | 97.8 | 31.2 |
| Canada | 3.7 | 3.2 | 3.7 | 6.1 | 4.1 | -32.1 |
| Nchi nyingine za bara la Amerika | 8.5 | 2.7 | 1.8 | 2.7 | 4.4 | 61.2 |
| **JUMLA - BARA LA AMERIKA** | **64.6** | **52.8** | **44.5** | **83.4** | **106.4** | **27.5** |
| **BARA LA ASIA** | | | | | | |
| China | 233.7 | 238.9 | 273.1 | 293.7 | 427.9 | 45.7 |
| India | 867.8 | 528.7 | 1,008.7 | 1,178.6 | 1,554.0 | 31.9 |
| Japan | 64.2 | 55.8 | 67.5 | 89.0 | 67.9 | -23.7 |
| Falme za Kiarabu | 395.1 | 754.9 | 1,051.8 | 763.0 | 686.4 | -10.0 |
| Honkong | 49.6 | 128.3 | 61.3 | 177.0 | 45.9 | -74.0 |
| Singapore | 7.6 | 43.7 | 139.2 | 183.0 | 142.0 | -22.4 |
| Nchi nyingine za Asia | 493.0 | 453.8 | 319.6 | 445.2 | 446.3 | 0.2 |
| **JUMLA-ASIA** | **2,110.9** | **2,204.1** | **2,921.2** | **3,129.4** | **3,370.5** | **7.7** |
| Nchi nyinginezo | 387.8 | 315.3 | 370.1 | 404.2 | 426.9 | 5.6 |
| **JUMLA KUU** | **5,377.6** | **6,371.7** | **6,756.2** | **7,223.8** | **7,696.6** | **6.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

116. Mwaka 2023, Tanzania iliagiza kwa wingi bidhaa kutoka nchi ya China (asilimia 27.5), India (asilimia 12.9), Umoja wa Falme za Kiarabu (asilimia 9.4) na Saudi Arabia (asilimia 6.1). Aidha, bidhaa zilizoagizwa kwa kiasi kikubwa zilijumuisha: mitambo, matrekta na bidhaa za kielektroniki kutoka China; mafuta ya petroli na mbolea kutoka Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu; na magari na vyuma kutoka Japani, India na Afrika Kusini.

**Kielelezo Na. 4.4: Mchanganuo wa Uagizaji wa Bidhaa Nchini Mwaka 2023 (Asilimia)**




117. Mwaka 2023, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikuwa dola za Marekani milioni 523.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 578.0 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 9.4. Aidha, bidhaa zilizoagizwa kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 786.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 779.2 mwaka 2022. Aidha, urari wa biashara ya bidhaa baina ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 657.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 836.9 mwaka 2022, sawa na upungufu wa ziada kwa asilimia 21.5. Vile vile, mwaka 2023 urari wa biashara ya bidhaa baina ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 941.4 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 637.3 mwaka 2022, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 47.7.

118. Mwaka 2023, thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za Bara la Asia ilikuwa dola za Marekani milioni 10,987.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 11,315.9 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 2.9. Hii ilitokana na kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan mafuta ya petroli na mbolea. Vile vile, thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka Jumuiya ya Ulaya na Uswisi ilipungua kwa asilimia 19.0 na kufikia dola za Marekani milioni 1,452.0 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani

milioni 1,792.3 mwaka 2022. Hii ilitokana na kupungua kwa bei katika soko la dunia kulikosababisha kupungua kwa gharama za uagizaji.

**Jedwali Na. 4.4: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nchi Mbalimbali Duniani Mwaka 2019 - 2023 (Dola za Marekani Milioni)**

| **JUMUIYA/ NCHI** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI | 1,269.9 | 1,264.9 | 1,126.1 | 1,792.3 | 1,452.0 | -19.0 |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 222.6 | 230.0 | 244.1 | 193.0 | 447.4 | 131.8 |
| **JUMLA - BARA LA ULAYA** | **1,492.5** | **1,494.9** | **1,370.2** | **1,985.4** | **1,899.4** | **-4.3** |
| **AFRIKA** | | | | | | |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | |
| Afrika ya Kusini | 437.6 | 344.7 | 432.1 | 548.9 | 555.5 | 1.2 |
| Zambia | 47.3 | 49.4 | 70.5 | 91.0 | 113.1 | 24.3 |
| Swaziland | 48.8 | 26.4 | 39.6 | 43.7 | 37.8 | -13.7 |
| Zimbabwe | 0.9 | 4.7 | 9.9 | 8.1 | 9.8 | 21.0 |
| Msumbiji | 8.4 | 2.3 | 4.6 | 22.6 | 3.4 | -85.0 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 1.3 | 2.1 | 2.6 | 3.1 | 2.9 | -5.9 |
| Nchi nyingine za SADC | 49.4 | 38.6 | 57.4 | 61.8 | 63.7 | 3.0 |
| **JUMLA-SADC** | **593.7** | **468.2** | **616.6** | **779.2** | **786.1** | **0.9** |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | |
| Burundi | 0.3 | 0.3 | 0.6 | 2.6 | 3.1 | 18.7 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 1.3 | 2.1 | 2.6 | 3.1 | 2.9 | -5.9 |
| Kenya | 266.5 | 253.5 | 413.0 | 426.6 | 408.9 | -4.2 |
| Rwanda | 1.5 | 2.1 | 2.2 | 3.1 | 1.4 | -55.2 |
| Uganda | 58.6 | 77.4 | 109.6 | 142.6 | 107.3 | -24.7 |
| Sudani ya Kusini | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 15.1 |
| **JUMLA-EAC** | **328.2** | **335.3** | **528.0** | **578.0** | **523.6** | **-9.4** |
| Nchi nyingine za Afrika | 56.2 | 62.9 | 70.1 | 251.4 | 204.4 | -18.7 |
| **JUMLA-AFRIKA** | **976.8** | **864.3** | **1,212.2** | **1,605.6** | **1,511.2** | **-5.9** |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | |
| Marekani | 325.0 | 239.8 | 260.4 | 335.1 | 378.3 | 12.9 |
| Canada | 47.5 | 30.9 | 45.4 | 56.9 | 81.8 | 43.8 |
| Nchi nyingine za bara la Amerika | 71.5 | 60.6 | 79.2 | 176.1 | 113.9 | -35.3 |
| **JUMLA - BARA LA AMERIKA** | **444.0** | **331.2** | **385.0** | **568.2** | **574.0** | **1.0** |
| **BARA LA ASIA** | | | | | | |
| China | 2,004.0 | 2,116.8 | 2,700.0 | 3,946.3 | 4,158.7 | 5.4 |
| India | 1,272.1 | 1,091.2 | 1,209.1 | 1,960.6 | 1,949.0 | -0.6 |
| Japani | 409.7 | 345.6 | 465.5 | 521.6 | 649.5 | 24.5 |
| Umoja wa Falme za Kiarabu | 954.8 | 821.2 | 1,378.6 | 2,492.3 | 1,417.9 | -43.1 |
| Honkong | 47.7 | 47.8 | 53.1 | 83.9 | 77.7 | -7.3 |
| Singapuri | 66.9 | 31.6 | 82.2 | 107.9 | 156.5 | 45.0 |
| Nchi nyingine za Asia | 1,430.6 | 1,275.6 | 1,901.9 | 2,203.3 | 2,578.1 | 17.0 |
| **JUMLA-ASIA** | **6,185.8** | **5,729.8** | **7,790.4** | **11,315.9** | **10,987.4** | **-2.9** |
| Nchi nyinginezo | 76.6 | 48.2 | 92.0 | 179.4 | 145.5 | -18.9 |
| **JUMLA KUU (CIF)** | **9,175.7** | **8,468.4** | **10,849.9** | **15,654.5** | **15,117.5** | **-3.4** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Mizania ya Malipo na Nchi za Nje**

**Urari wa Malipo Yote**

119. Mwaka 2023, urari wa malipo yote ya nje ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 52.3 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 988.4 mwaka 2022. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa**

120. Urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 6,032.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 6,984.9 mwaka 2022. Hii ilitokana na kupungua kwa gharama ya uagizaji bidhaa kutoka nje, hususan mafuta ya petrol na mbolea kulikotokana na kushuka kwa bei katika soko la dunia.

**Urari wa Biashara ya Huduma**

121. Mwaka 2023, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 3,956.1 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 2,296.6 mwaka 2022, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 72.3. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii kutokana na kuimarika kwa sekta hiyo pamoja na kuongezeka kwa mapato ya huduma za usafirishaji.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma**

122. Urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,076.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 4,688.3 mwaka 2022. Hii ilichangiwa na kupungua kwa nakisi katika urari wa biashara ya huduma.

**Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi**

123. Urari wa mapato ya vitega uchumi ambao unajumuisha kiasi cha malipo yatokanayo na ajira kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,505.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,393.2 mwaka 2022, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 8.1. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa malipo ya riba.

**Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida**

124. Mwaka 2023, urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha unaofanywa na sekta binafsi, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 646.0 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 599.3 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa fedha kutoka kwa watanzania wanaoishi nje ya nchi (remittances) na mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo.

**Urari wa Malipo ya Kawaida**

125. Mwaka 2023, urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za

Marekani milioni 2,935.9 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 5,482.2 mwaka 2022. Kupungua kwa nakisi kulitokana na kuongezeka zaidi kwa mapato ya huduma, mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi sambamba na kupungua kwa gharama za uagizaji bidhaa.

**Urari wa Uhamisho wa Mitaji**

126. Urari wa uhamisho wa mitaji unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa mashirika ya fedha ya kimataifa na nchi wahisani ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 229.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 407.3 mwaka 2022, sawa na upungufu wa ziada kwa asilimia 46.7. Hii ilitokana na kupungua kwa misaada iliyokuwa ikitolewa kwa ajili ya miradi.

**Urari wa Rasilimali Fedha**

127. Mwaka 2023, urari wa malipo katika rasilimali fedha unaojumuisha uwekezaji wa moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,894.6 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 4,127.5 mwaka 2022. kupungua kwa ziada kulitokana na kuongezeka kwa amana nje ya nchi.

**Akiba ya Fedha za Kigeni**

128. Hadi Desemba 2023, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,450.1 kutoka dola za Marekani milioni 5,177.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kiasi hicho kilitosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.5 ambayo ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua 4.0. Aidha, kiwango hicho ni sawa na lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la miezi isiyopungua 4.5.

**Jedwali Na. 31: THAMANI YA BIASHARA YA BIDHAA BAINA YA TANZANIA NA NCHI NYINGINE**

**Shilingi Milioni**

| **Aina ya Bidhaa** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zilizouzwa Nje | 10,064,249 | 11,378,808 | 13,882,712 | 14,384,874 | 15,637,519 | 17,299,166 |
| Bidhaa Halisi | 8,307,170 | 10,824,002 | 13,673,643 | 14,178,681 | 15,337,701 | 16,979,274 |
| Zilizouzwa Tena | 422,733 | 554,806 | 209,069 | 206,192 | 299,818 | 319,891 |
| Zilizoagizwa | 18,789,124 | 20,939,079 | 19,631,818 | 24,862,261 | 36,239,349 | 36,294,408 |
| **Jumla** | **28,853,373** | **32,317,886** | **33,514,530** | **39,247,135** | **51,876,868** | 53,593,574 |
| Urari | -8,724,875 | -9,560,271 | -5,749,106 | -10,477,387 | -20,601,830 | -18,995,243 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 32: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE**

| Bidhaa | Kiasi (Tani '000) | | | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | |
| Kahawa | 76.2 | 64.0 | 68.0 | 55.2 | 84.4 | 52.9 |
| Pamba | 79.0 | 72.6 | 48.8 | 48.9 | 69.6 | 42.4 |
| Katani | 12.2 | 11.2 | 12.6 | 14.9 | 12.5 | -16.0 |
| Chai | 31.7 | 24.1 | 24.2 | 21.1 | 22.2 | 5.2 |
| Tumbaku | 42.6 | 42.6 | 37.7 | 49.3 | 82.0 | 66.4 |
| Korosho | 295.6 | 320.9 | 154.4 | 234.0 | 219.6 | -6.2 |
| Karafuu | 1.8 | 3.6 | 7.0 | 5.9 | 4.7 | -20.5 |
| Almasi (Carat) | 592,252.00 | 154,331.10 | 808,844.00 | 374,131.50 | 201,923.0 | -46.0 |
| Dhahabu( gms) | 66,078,000 | 66,871,114.90 | 59,392,496.20 | 64,091,782.50 | 79,706,632.9 | 24.4 |

* 1 Carat = 200 milligrams

| | Thamani (Shilingi Milioni) | | | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | |
| Kahawa | 348,112.54 | 333,113.2 | 356,556.7 | 371,288.2 | 545,332.34 | 46.9 |
| Pamba | 210,056.61 | 200,796.8 | 186,843.6 | 238,317.4 | 247,137.66 | 3.7 |
| Katani | 44,081.28 | 40,269.9 | 46,358.2 | 56,062.1 | 48,334.66 | -13.8 |
| Chai | 104,577.54 | 74,356.4 | 75,550.0 | 69,123.6 | 73,611.95 | 6.5 |
| Tumbaku | 335,250.34 | 341,132.9 | 292,867.2 | 411,542.2 | 828,228.22 | 101.2 |
| Korosho | 808,346.69 | 824,866.3 | 365,039.7 | 523,030.8 | 509,196.47 | -2.6 |
| Karafuu | 20,911.00 | 39,110.1 | 119,004.7 | 97,083.7 | 61,214.78 | -36.9 |
| Almasi (Carat) | 185,948.16 | 46,311.5 | 19,546.0 | 144,513.5 | 57,346.70 | -60.3 |
| Dhahabu( gms) | 5,068,720.85 | 6,786,265.3 | 6,289,142.0 | 6,530,001.3 | 7,301,343.78 | 11.8 |


**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali Na. 33: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE


| **Bidhaa** | **Kiasi (000" Tani)** | | | | | **Badiliko (Asilimia)** | **Thamani (Milioni US$)** | | | | | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2022/23** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2022/23** |
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | | | | | | |
| Kahawa | 76.2 | 64.0 | 68.0 | 55.2 | 84.4 | 52.9 | 152.2 | 145.2 | 155.2 | 161.2 | 227.9 | 41.4 |
| Pamba | 79.0 | 72.6 | 48.8 | 48.9 | 69.6 | 42.4 | 91.8 | 87.5 | 81.3 | 103.4 | 101.9 | -1.4 |
| Katani | 12.2 | 11.2 | 12.6 | 14.9 | 12.5 | -16.0 | 19.3 | 17.6 | 20.2 | 24.3 | 20.4 | -16.2 |
| Chai | 31.7 | 24.1 | 24.2 | 21.1 | 22.2 | 5.1 | 45.7 | 32.4 | 32.9 | 30.0 | 31.1 | 3.7 |
| Tumbaku | 42.6 | 42.6 | 37.7 | 49.3 | 82.0 | 66.4 | 146.5 | 148.7 | 127.5 | 178.5 | 340.5 | 90.7 |
| Korosho | 295.6 | 320.9 | 154.4 | 234.0 | 219.6 | -6.2 | 353.1 | 359.6 | 159.0 | 226.9 | 206.4 | -9.0 |
| Karafuu | 1.8 | 3.6 | 7.0 | 5.9 | 4.7 | -20.5 | 9.1 | 17.1 | 51.8 | 42.1 | 25.1 | -40.3 |
| **Jumla** | | | | | | | **817.7** | **808.1** | **627.9** | **766.5** | **953.3** | **24.4** |
| **Bidhaa zisizo asilia** | | | | | | | | | | | | |
| Madini | | | | | | | 2,332.7 | 3,375.0 | 3,116.4 | 3,395.3 | 3,551.4 | 4.6 |
| Bidhaa za Viwanda | | | | | | | 845.8 | 902.7 | 1,200.0 | 1,419.2 | 1,363.3 | -3.9 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | | | | | | | 168.0 | 139.6 | 164.3 | 168.2 | 164.0 | -2.5 |
| Mazao ya Mboga na Maua | | | | | | | 209.6 | 274.1 | 378.6 | 289.6 | 417.2 | 44.1 |
| Bidhaa zilizouzwa tena | | | | | | | 242.8 | 87.7 | 90.2 | 131.2 | 135.2 | 3.1 |
| Bidhaa nyinginezo | | | | | | | 387.1 | 474.2 | 813.5 | 654.9 | 690.5 | 5.4 |
| **Jumla** | | | | | | | **4,186.0** | **5,253.3** | **5,763.0** | **6,058.4** | **6,321.6** | **4.3** |
| Bidhaa Zisizorekodiwa | | | | | | | 373.8 | 310.4 | 365.4 | 399.0 | 421.6 | 5.7 |
| **Jumla Kuu** | | | | | | | **5,377.5** | **6,371.7** | **6,756.2** | **7,223.8** | **7,696.6** | **6.5** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 4.5: THAMANI YA BIDHAA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI MWAKA 2017 - 2023**



**Kielelezo Na. 4.6: MCHANGO WA BIDHAA KATIKA MAUZO NJE YA NCHI MWAKA 2023**



## Jedwali Na. 34: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

| **Bidhaa** | **Shilingi/Tani*** | | | | | | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2022-2023** |
| Kahawa | 5,818,259 | 4,585,610 | 5,178,939 | 5,217,177 | 6,692,686 | 6,429,800 | -3.9 |
| Pamba | 3,099,625 | 2,690,875 | 2,753,527 | 3,806,866 | 4,846,836 | 3,530,423 | -27.2 |
| Katani | 3,910,417 | 3,901,618 | 3,575,866 | 3,657,568 | 3,734,604 | 3,841,269 | 2.9 |
| Chai | 3,841,673 | 3,292,541 | 3,070,579 | 3,101,340 | 3,254,080 | 3,302,729 | 1.5 |
| Tumbaku | 8,444,280 | 9,143,243 | 7,975,654 | 7,727,540 | 8,312,638 | 10,053,861 | 20.9 |
| Korosho | 3,733,995 | 2,759,651 | 2,570,147 | 2,351,759 | 2,224,266 | 2,309,110 | 3.8 |
| Karafuu | 6,840,000 | 16,005,679 | 10,868,651 | 16,801,625 | 16,293,998 | 12,996,777 | -20.2 |
| Almasi (kwa carat) | 205,594 | 313,503 | 298,578 | 409,930 | 469,384 | 282,534 | -39.8 |
| Dhahabu (gramu) | 56,522 | 62,185 | 100,976 | 105,355 | 101,403 | 91,210 | -10.1 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania
*Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

**Jedwali Na. 35: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI**

| Bidhaa | US$/Tani* | | | | | | Badiliko 2022-2023 (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | |
| Kahawa | 2,584 | 2,017 | 2,269 | 2,602 | 2,902 | 2,701 | -6.9 |
| Pamba | 1,371 | 1,147 | 1,206 | 1,678 | 2,113 | 1,463 | -30.7 |
| Katani | 1,733 | 2,109 | 1,566 | 1,614 | 1,629 | 1,629 | 0.0 |
| Chai | 1,706 | 1,446 | 1,346 | 1,301 | 1,420 | 1,404 | -1.2 |
| Tumbaku | 3,744 | 3,441 | 3,494 | 3,538 | 3,624 | 4,150 | 14.5 |
| Korosho | 1,674 | 1,193 | 1,121 | 1,123 | 970 | 940 | -3.1 |
| Karafuu | 3,000 | 7,000 | 4,770 | 5,493 | 7,104 | 5,357 | -24.6 |
| Almasi (kwa carat) | 200 | 138 | 131 | 180 | 205 | 117 | -43.1 |
| Dhahabu (kwa gramu) | 25 | 27 | 44 | 46 | 44 | 38 | -13.2 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania
*Isipokuwa kwa almasi na dhahabu


## Jedwali Na. 36: MIZANIA YA MALIPO MWAKA 2019 - 2023

**Dola za Marekani Milioni**

| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022r | 2023p |
|---|---|---|---|---|---|
| **Urari wa Biashara ya Bidhaa** | **-3,237.6** | **-1,460.0** | **-3,247.1** | **-6,984.9** | **-6,032.3** |
| Zilizouzwa nje (fob) | 5,377.6 | 6,371.7 | 6,756.2 | 7,223.8 | 7,696.6 |
| Zilizonunuliwa toka nje (fob)* | 8,615.2 | 7,831.7 | 10,003.4 | 14,208.7 | 13,728.9 |
| **Urari wa Huduma** | **2,492.5** | **864.7** | **1,510.7** | **2,296.6** | **3,956.1** |
| Mapato | 4,281.0 | 2,183.8 | 3,117.7 | 4,762.0 | 6,285.9 |
| Malipo | 1,788.4 | 1,319.0 | 1,607.0 | 2,465.4 | 2,329.8 |
| **Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi** | **-1,013.7** | **-1,264.5** | **-1,191.6** | **-1,393.2** | **-1,505.7** |
| Yaliyoingia | 212.4 | 111.2 | 102.5 | 183.9 | 189.8 |
| Yaliyotoka | 1,226.2 | 1,375.7 | 1,294.2 | 1,577.1 | 1,695.5 |
| **Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida** | **418.5** | **401.2** | **553.7** | **599.3** | **646.0** |
| Iliyoingia | 474.9 | 453.9 | 640.1 | 716.5 | 791.9 |
| Serikalini | 103.5 | 141.2 | 104.7 | 76.4 | 111.8 |
| Sekta nyingine | 371.4 | 312.7 | 535.4 | 640.2 | 680.0 |
| Iliyotoka | 56.4 | 52.7 | 86.4 | 117.2 | 145.9 |
| **Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali** | **-1,340.2** | **-1,458.5** | **-2,374.3** | **-5,482.2** | **-2,935.9** |
| **Urari wa Uhamisho wa Mitaji** | **481.2** | **344.3** | **390.2** | **407.3** | **229.6** |
| Iliyoingia | 481.2 | 344.3 | 390.2 | 407.3 | 229.6 |
| Iliyotoka | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| **Urari katika uwekezaji** | **2,518.8** | **898.8** | **3,341.5** | **4,127.5** | **2,894.6** |
| Uwekezaji katika miradi | -1,217.2 | -943.8 | -1,190.5 | -1,437.6 | -1,627.0 |
| Uwekezaji katika hisa | 37.8 | -3.6 | -7.9 | 24.6 | 13.9 |
| Uwekezaji aina nyingine | 1,263.7 | -41.3 | 2,158.9 | 2,665.3 | 1,253.6 |
| Makosa na Masahihisho | -1,072.7 | -549.5 | 494.7 | -53.5 | -811.2 |
| **Urari wa Malipo yote** | **587.0** | **-764.9** | **1,852.1** | **-988.4** | **52.3** |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania
P takwimu za awali
r – Takwimu zimeboreshwa

**Kielelezo Na. 4.7: MWENENDO WA URARI KATIKA MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE MWAKA 2017 - 2023**



# SURA YA 5

## HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

### HALI YA UCHUMI WA DUNIA

**Ukuaji wa Uchumi**

129. Kulingana na taarifa ya mwenendo wa uchumi wa dunia ya Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF toleo la Aprili 2024, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo: kuendelea kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi, hususan wa bidhaa za petroli na chakula kufuatia vita kati ya Ukraine na Urusi; kuongezeka kwa gharama za kukopa katika masoko ya fedha kulikoathiri zaidi nchi zinazoendelea; utekelezaji wa sera ya kupunguza ujazi wa fedha kwa kuongeza viwango vya riba ili kukabiliana na mfumuko wa bei; athari za muda mrefu za janga la UVIKO - 19; athari za mabadiliko ya tabianchi; na kuongezeka kwa mgawanyiko wa kiuchumi kikanda (geoeconomic fragmentation). Pamoja na changamoto zilizojitokeza, uchumi wa dunia uliendelea kuwa himilivu mwaka 2023 na kukua kwa kiwango cha juu zaidi ya malengo yaliyowekwa ya asilimia 2.8 kulingana na taarifa ya IMF ya Aprili 2023. Hii ilitokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi tofauti na ilivyotarajiwa, hususan kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali na ya kaya kwa nchi zilizoendelea na zinazoendelea yaliyochachua shughuli za kiuchumi.

130. Kasi ya ukuaji wa Pato la nchi zilizoendelea ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2022. Kushuka kwa ukuaji kulichangiwa zaidi na athari za utekelezaji wa sera ya kupunguza ujazi wa fedha pamoja na gharama kubwa za nishati. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2022. Vile vile, kasi ya ukuaji wa Pato la nchi za Asia zinazoendelea ikijumuisha China na India iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.4 mwaka 2022. Kuongezeka kwa ukuaji kulitokana na kupungua kwa changamoto zilizoukumba uchumi wa dunia ikiwemo UVIKO - 19 na vita pamoja na kuimarika kwa biashara ya kimataifa.

131. Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulishuka na kufikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2022. Kushuka kwa ukuaji kulichangiwa na utekelezaji wa sera ya kupunguza ujazi wa fedha kwenye uchumi wa Marekani ili kukabiliana na mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea na hivyo, kusababisha uhaba wa fedha za kigeni katika nchi zinazoendelea, hususan dola ya Marekani, kushuka kwa thamani ya fedha dhidi ya dola ya Marekani, kuongezeka kwa gharama za mikopo katika masoko ya fedha ya kikanda na

kimataifa na kupungua kwa mauzo ya bidhaa kutoka nchi za Afrika kufuatia kupungua kwa uhitaji kutoka nchi washirika wakuu wa kibiashara. Aidha, uchumi kwa nchi za Afrika ulipungua kutokana na athari za muda mrefu za janga la UVIKO - 19 pamoja na uwiano hasi wa bei za bidhaa zinazouzwa na kununuliwa nje ya bara la Afrika.

**Jedwali Na. 5.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia Mwaka 2019 - 2023**

| Kundi/Mwaka | Ukuaji Halisi (Asilimia) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
| Dunia | 2.8 | -2.7 | 6.5 | 3.5 | 3.2 |
| Nchi Zilizoendelea | 1.8 | -3.9 | 5.7 | 2.6 | 1.6 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | 3.6 | 1.8 | 7.0 | 4.1 | 4.3 |
| Nchi za Asia Zinazoendelea | 5.2 | -0.5 | 7.7 | 4.4 | 5.6 |
| Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara | 3.2 | -1.6 | 4.7 | 4.0 | 3.4 |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF-WEO), Aprili 2024

132. Mwaka 2023, ukuaji wa Pato la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa wastani wa asilimia 3.8 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2022. Kupungua kwa ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa mfumuko wa bei, kuongezeka kwa gharama za ukopaji katika masoko ya fedha ya kimataifa, kupungua kwa misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na athari za vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine. Aidha, ukuaji wa Pato la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliongezeka kufikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2022.

**Jedwali Na. 5.2: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Kikanda Mwaka 2019 - 2023**

| Nchi/Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ukuaji wa Nchi za SADC** | | | | | |
| Angola | -0.7 | -5.6 | 1.2 | 3.0 | 0.5 |
| Afrika Kusini | 0.3 | -6 | 4.7 | 1.9 | 0.6 |
| Botswana | 3 | -8.7 | 11.9 | 5.8 | 3.2 |
| Comoros | 1.8 | -0.2 | 2.0 | 2.6 | 3.0 |
| DRC | 4.5 | 1.7 | 6.0 | 8.8 | 6.1 |
| Eswatin | 2.7 | -1.6 | 10.7 | 0.5 | 5.1* |
| Lesotho | -3.1 | -5.3 | 1.7 | 1.6 | 1.9 |
| Madagascar | 4.4 | -7.1 | 5.7 | 4.0 | 3.8 |
| Malawi | 5.4 | 0.9 | 4.6 | 0.8 | 1.6 |
| Mauritius | 2.9 | -14.5 | 3.4 | 8.9 | 6.9 |
| Msumbiji | 2.3 | -1.2 | 2.4 | 4.4 | 6.0 |
| Namibia | -0.8 | -8.1 | 3.5 | 4.6 | 3.2 |
| Seychelles | 5.5 | -11.7 | 0.6 | 15 | 3.7 |
| Tanzania | 6.9 | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1* |
| Zambia | 1.4 | -2.8 | 6.2 | 5.2 | 4.3 |
| Zimbabwe | 6.3 | -7.8 | 8.4 | 6.5 | 5.3 |
| **Wastani** | **2.7** | **-4.6** | **4.9** | **4.9** | **3.8** |
| **Ukuaji wa Nchi za EAC** | | | | | |
| Burundi | 1.8 | 0.3 | 3.1 | 1.8 | 2.7 |
| Kenya | 5.1 | -0.3 | 7.6 | 4.8 | 5.5 |
| Rwanda | 9.5 | -3.4 | 10.9 | 8.2 | 6.9 |
| Sudan Kusini | 0.9 | -6.5 | 5.3 | -5.2 | -0.1 |
| Tanzania | 6.9 | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1* |
| Uganda | 7.6 | -1.1 | 5.5 | 6.3 | 4.8 |
| DRC | 4.5 | 1.7 | 6.0 | 8.8 | 6.1 |
| **Wastani** | **5.2** | **-0.7** | **6.2** | **4.2** | **4.4** |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF-WEO), Aprili 2024

* Makadirio ya IMF yalikuwa ukuaji wa asilimia 5.0 lakini takwimu rasmi kutoka NBS ni asilimia 5.1

### Mwenendo wa Bei

133. Mwaka 2023, mfumuko wa bei wa dunia ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 6.8 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa na huduma duniani kulitokana na kuimarika kwa bei ya bidhaa, hususan nishati. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea ulifikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2022. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Ulaya ulikuwa wa wastani wa asilimia 19.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 27.8 mwaka 2022 kutokana na kuimarika kwa mnyororo wa ugavi pamoja na ufanisi wa utekelezaji wa sera ya kupunguza ujazi wa fedha. Hata hivyo, kiwango hicho bado kipo juu kutokana na uwepo wa gharama kubwa za nishati na ongezeko la mahitaji kufuatia kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zilizofungua fursa za ajira. Vile vile, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia

ulifikia wastani wa asilimia 2.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2022.

134. Mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulifikia wastani wa asilimia 16.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 14.5 mwaka 2022. Ongezeko la mfumuko wa bei lilitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupungua kwa ugavi wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya kikanda, kuongezeka kwa wastani wa bei za mafuta na mbolea kwa baadhi ya nchi hizo, pamoja na kasi ya kushuka kwa thamani ya sarafu kuliko ilivyotarajiwa. Nchi zilizokuwa na mfumuko wa bei wa juu ni pamoja na Zimbabwe (asilimia 667.4), Sudani ya Kusini (asilimia 40.2), Ghana (asilimia 37.5), Malawi (asilimia 30.3) na Ethiopia (asilimia 30.2). Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa wastani wa asilimia 50.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 21.4 mwaka 2022. Vile vile, mfumuko wa bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa wastani wa asilimia 16.9 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.3 mwaka 2022. Miongoni mwa nchi za EAC, Sudan ya Kusini ilikuwa na kiwango kikubwa cha mfumuko wa bei cha asilimia 40.2 na Tanzania ilikuwa na kiwango cha chini zaidi cha mfumuko wa bei cha asilimia 3.8.

**Jedwali Na. 5.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za SADC na EAC Mwaka 2019 - 2023**

| Nchi | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mfumuko wa Bei (Asilimia) wa Nchi za SADC** | | | | | |
| Angola | 17.1 | 22.3 | 25.8 | 21.4 | 13.6 |
| Afrika Kusini | 4.1 | 3.3 | 4.6 | 6.9 | 5.9 |
| Botswana | 2.7 | 1.9 | 6.7 | 12.2 | 5.1 |
| Comoros | 3.7 | 0.8 | 0.0 | 12.4 | 8.5 |
| DRC | 4.7 | 11.4 | 9.0 | 9.3 | 19.9 |
| Eswatin | 2.6 | 3.9 | 3.7 | 4.8 | 4.9 |
| Lesotho | 5.2 | 5.0 | 6.0 | 8.3 | 6.3 |
| Madagascar | 5.6 | 4.2 | 5.8 | 8.2 | 9.9 |
| Malawi | 9.4 | 8.6 | 9.3 | 20.8 | 30.3 |
| Mauritius | 0.5 | 2.5 | 4.0 | 10.8 | 7.0 |
| Msumbiji | 2.8 | 3.1 | 5.7 | 9.8 | 6.1 |
| Namibia | 3.7 | 2.2 | 3.6 | 6.1 | 5.9 |
| Seychelles | 1.8 | 1.2 | 9.8 | 2.6 | -1 |
| Tanzania | 3.4 | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8* |
| Zambia | 9.2 | 15.7 | 22 | 11 | 11 |
| Zimbabwe | 255.3 | 557.2 | 98.5 | 193.4 | 667.4 |
| **Wastani** | **20.7** | **40.4** | **13.6** | **21.4** | **50.3** |
| **Mfumuko wa Bei (Asilimia) wa Nchi za EAC** | | | | | |
| Tanzania | 3.4 | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8* |
| Uganda | 2.1 | 2.8 | 2.2 | 7.2 | 5.4 |
| Kenya | 5.2 | 5.3 | 6.1 | 7.6 | 7.7 |
| Rwanda | 2.4 | 7.7 | 0.8 | 13.9 | 14 |
| Burundi | -0.7 | 7.3 | 8.3 | 18.9 | 27 |
| Sudani ya Kusini | 49.3 | 24 | 30.2 | -3.2 | 40.2 |
| DRC | 4.7 | 11.4 | 9 | 9.3 | 19.9 |
| **Wastani** | **9.5** | **8.8** | **8.6** | **8.3** | **16.9** |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO Aprili 2024
* Makadirio ya IMF yalikuwa mfumuko wa bei wa asilimia 4.0 lakini takwimu rasmi kutoka NBS ni asilimia 3.8

**Mwenendo wa Biashara Duniani**

135. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mwenendo wa Biashara Duniani ya Shirika la Biashara Duniani - WTO toleo la Aprili 2024, ukuaji wa shughuli za biashara duniani ulipungua na kufikia asilimia 1.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.0 mwaka 2022. Kupungua kwa ukuaji wa biashara kulitokana na mfumuko wa bei, kuongezeka kwa riba, kupanda kwa thamani ya dola ya Marekani pamoja na misukosuko ya kisiasa na kiuchumi kulikosababisha kushuka kwa mahitaji ya bidhaa za viwandani, hususan bidhaa za nguo na mavazi, chuma na mitambo ya mawasiliano.

136. Licha ya bara la Ulaya kuwa na mchango mkubwa kwenye shughuli za biashara duniani mwaka 2023, uuzaji wa bidhaa nje ya Bara la Ulaya ulishuka na kufikia asilimia 2.6 na uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya bara hilo ulipungua kwa asilimia 4.7. Hii ilichangiwa zaidi na mabadiliko ya bei ya bidhaa, hususan katika masoko ya gesi asilia. Aidha, uuzaji wa bidhaa nje ya Bara la Afrika uliongezeka na kufikia asilimia 3.1 mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 2.4 mwaka 2022. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa, hususan mafuta kwa nchi zinazozalisha mafuta. Vile vile, uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya Bara la Afrika ulipungua na kufikia ukuaji wa asilimia 2.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.8 mwaka 2022. Hii ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa kulikosababishwa na kushuka kwa kipato na upungufu wa fedha za kigeni.

**Jedwali Na. 5.4: Mwenendo wa Shughuli za Biashara Duniani Mwaka 2020 - 2023**

| **Kundi/Mwaka** | **Ukuaji Halisi (Asilimia)** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
| **Dunia** | -5.0 | 9.6 | 3.0 | -1.2 |
| **Uuzaji wa bidhaa nje** | | | | |
| Bara la Ulaya | -7.7 | 8.1 | 3.7 | -2.6 |
| Bara la Asia | 0.6 | 13.1 | 0.4 | 0.1 |
| Afrika | -7.2 | 4.2 | -2.4 | 3.1 |
| **Uagizaji wa bidhaa kutoka nje** | | | | |
| Bara la Ulaya | -7.2 | 8.8 | 6.0 | -4.7 |
| Bara la Asia | -1.0 | 10.5 | -0.7 | -0.6 |
| Bara la Afrika | -15.5 | 7.4 | 8.8 | -2.4 |

**Chanzo:** Shirika la Biashara Duniani - WTO, Aprili 2024

**Ushirikiano wa Uchumi Kimataifa**

137. Mwaka 2023, Tanzania iliendelea kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya ushirikiano wa kiuchumi kwenye jumuiya za kimataifa kupitia Umoja wa Mataifa, taasisi na mashirika ya uchumi, fedha na biashara ya kimataifa na majukwaa mengine ya kimataifa. Katika kipindi hicho, Tanzania ilishiriki Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi - COP28 uliofanyika Dubai - Umoja wa Falme za Kiarabu. Katika mkutano huo, nchi wanachama ziliridhia utaratibu wa uendeshaji wa mfuko wa kukabiliana na upotevu na uharibifu utokanao na mabadiliko ya tabianchi pamoja na uundwaji wa bodi ya ushauri ya mfuko huo. Kwa mujibu wa makubaliano yaliyofanyika, Benki ya Dunia itausimamia mfuko kwa kipindi cha miaka mitano (5), Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia majanga itakuwa Sekretarieti ya Bodi ya Ushauri. Aidha, nchi wanachama zilikubaliana kuhusu lengo la dunia la kuhimili mabadiliko ya tabianchi (global goal on adaptation) pamoja na mwongozo wake. Vile vile, nchi wanachama zilijadili tathmini ya kwanza ya utekelezaji wa makubaliano ya Paris na kupitisha maamuzi ya kuanza tathmini ya pili. Kwa mujibu wa

tathmini hiyo, nchi zinapaswa kupunguza gesi joto kwa kiasi cha asilimia 43 ifikapo mwaka 2030 ili kudhibiti joto la dunia kupanda kwa zaidi ya nyuzi joto 1.5°C.

138. Mwaka 2023, sanjari na Mkutano wa COP28, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wanawake wa Afrika (African Women Clean Cooking Support Programme - AWCCSP). Mpango huo unalenga kusaidia wanawake barani Afrika, hususan wanaoishi vijijini kupunguza matumizi ya nishati zinazozalisha hewa ukaa yenye athari hasi kwa mazingira na afya.

139. Mwaka 2023, Tanzania ilishiriki kwenye Mkutano wa Baraza la Wasafiri na Utalii Duniani - WTTC uliofanyika Kigali, Rwanda. Mkutano ulijadili kuhusu mchango wa bara la Afrika katika kukuza sekta ya utalii duniani, matumizi ya teknolojia ya habari na ubunifu katika kuimarisha sekta hiyo, athari za mabadiliko ya tabianchi kwa sekta hiyo, na umuhimu wa mafunzo ya kujenga uwezo wa jamii. Kwa upande mwingine, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 45 wa Kamati ya Urithi wa Dunia ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni uliofanyika Riyadh, Saudi Arabia. Katika mkutano huo, nchi wanachama zilijadili kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Urithi wa Dunia wa mwaka 1972 (Convention Concerning the Protection of the World Cultural and Natural Heritage, 1972) na matumizi ya hazina ya urithi wa dunia. Aidha, Mkutano ulijadili hali ya uhifadhi wa maeneo yaliyomo kwenye orodha ya urithi wa dunia ikiwemo, Pori Tengefu la Selous, Bonde la Ngorongoro na Mji Mkongwe wa Zanzibar.

140. Mwaka 2023, Tanzania ilishiriki katika Kikao cha 78 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika New York, Marekani. Kupitia Kikao hicho, Tanzania iliainisha mafanikio yake katika utekelezaji wa Agenda 2030 ya Umoja wa Mataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na kusisitiza umuhimu wa jumuiya ya kimataifa kuongeza ufadhili ili kufikiwa kwa malengo hayo. Aidha, Tanzania iliwasilisha taarifa ya pili ya mapitio ya hiari ya nchi katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Jukwaa la Ngazi ya Juu la Siasa la Umoja wa Mataifa jijini New York, Marekani. Kwa upande mwingine, Tanzania ilialikwa na kushiriki kwenye Mkutano Mkuu wa Nchi zinazounda umoja wa BRICS (Brazil, Russia, India, China, South Africa) uliofanyika Johannesburg, Afrika Kusini. Mkutano huo ulijadili jinsi ya kuimarisha ushirikiano kati ya nchi za BRICS na nchi za Afrika pamoja na nchi nyingine zinazoendelea, hususan kwenye maeneo ya uchumi, maendeleo na amani.

141. Mwaka 2023, Tanzania ilisaini Mkataba wa Ubia baina ya Jumuiya ya Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (Organisation of African, Caribbean and Pacific States) na Umoja wa Ulaya. Mkataba huo utatumika kama nyenzo ya kisera na kisheria ya kuratibu uhusiano wa kiuchumi kati ya pande hizo mbili kwa kipindi cha miaka 20 ijayo.

**Ushirikiano wa Kiuchumi Barani Afrika**

142. Mwaka 2023, Tanzania iliendelea kushiriki katika majadiliano na utekelezaji wa itifaki na makubaliano ya Eneo Huru la Biashara Barani Afrika - AfCFTA. Katika kuhakikisha Tanzania inatumia ipasavyo soko AfCFTA, iliamua kuwa sehemu ya Mpango wa Majaribio wa Utekelezaji wa AfCFTA (Guided Trade Initiative) ulioanzishwa mwaka 2022. Kupitia Mpango huo, kampuni 11 za Tanzania zilipewa vyeti vya uasili wa bidhaa vya AfCFTA kwa ajili ya kuuza bidhaa kwenye nchi wanachama. Aidha, bidhaa zilizouzwa kwa wingi kupitia Mpango huo ni katani, kahawa, tumbaku, viungo na karanga. Bidhaa hizo ziliuzwa katika nchi za Algeria, Nigeria, Misri, Morocco na Ghana. Kwa upande mwingine, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa kongamano la pili la AfCFTA kuhusu wanawake na vijana katika biashara barani Afrika lililofanyika jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo lilikuwa na lengo la kujadili changamoto zinazowakabili wanawake na vijana katika ufanyaji biashara barani Afrika na kuweka mikakati ya pamoja ya kuzitatua.

143. Mwaka 2023, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika kuhusu Mtaji wa Watu uliofanyika jijini Dar es Salaam. Katika mkutano huo, nchi washiriki ziliridhia Azimio la Dar es Salaam kuhusu Mtaji wa Watu (Dar es Salaam Human Capital Declaration 2023) linalolenga kuchagiza ongezeko la uwekezaji katika kukuza maarifa, ujuzi na kuboresha afya ya watu, hususan vijana. Katika kipindi hicho, Tanzania na Algeria zilifanya mkutano wa kwanza wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano. Kupitia Mkutano huo, Tanzania na Algeria zilisaini hati sita (6) za makubaliano ya ushirikiano katika sekta za nishati, elimu, biashara na utunzaji na uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu.

**Ushirikiano wa Kiuchumi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**

144. Mwaka 2023, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 43 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika jijini Luanda, Jamhuri ya Angola. Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulimteua Mheshimiwa João Manuel Gonçalves Lourenço, Rais wa Jamhuri ya Angola kuwa Mwenyekiti Mpya wa SADC. Aidha, Mkutano huo ulimteua Mheshimiwa Hakainde Hichilema, Rais wa Jamhuri ya Zambia kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya SADC. Katika kipindi hicho, Tanzania ilishiriki Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika jijini Luanda, Jamhuri ya Angola. Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulionyesha wasiwasi wa kuzorota kwa hali ya kibinadamu na usalama mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hii ilitokana na ukiukwaji wa Makubaliano ya Kusitisha Mapigano na kuripotiwa kwa mashambulizi na uvamizi wa ardhi uliofanywa na kikundi cha waasi wa M23. Aidha, Mkutano huo ulitoa maelekezo ya kupeleka Misheni ya Ulinzi wa Amani ya SADC (SAMIDRC) kurejesha amani na usalama katika nchi hiyo.

145. Mwaka 2023, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa Fedha na Uwekezaji na Kamati ya Tathmini ya Uchumi uliofanyika jijini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Katika Mkutano huo pamoja na mambo mengine, Mawaziri walijadili uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo wa SADC (Regional Development Fund) ambao unalenga kuweka mfumo wa ugharamiaji wa maendeleo ya kiuchumi na ukuaji endelevu kupitia maendeleo ya miundombinu, viwanda, kijamii pamoja na kuimarisha utangamano na mageuzi ya kiuchumi. Katika kipindi hicho, Mkutano huo ulijadili Mwelekeo wa Itifaki ya Fedha na Uwekezaji ya SADC unaolenga kuwezesha ushirikiano wa kifedha na uwekezaji ili kukidhi mahitaji mapya ya ukuaji wa viwanda na maendeleo ya kikanda katika siku zijazo. Aidha, Mkutano huo ulijadili na kuridhia taarifa za Tathmini za Kiuchumi za Nchi Wanachama (Peer Review Reports) ambazo ni Lesotho, Madagascar na Malawi. Tathmini ya Kiuchumi ya nchi ya Lesotho ilifanywa na Tanzania, Tathmini ya nchi ya Madagascar ilifanywa na Mauritius na Tathmini ya nchi ya Malawi ilifanywa na Zambia.

**Ushirikiano wa Kiuchumi Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

146. Mwaka 2023, Tanzania iliendelea kushiriki katika utekelezaji wa hatua za mtangamano wa Afrika Mashariki na itifaki zake pamoja na maeneo ya ushirikiano. Katika kipindi hicho, Tanzania ilishiriki Mkutano wa 23 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika jijini Arusha ambao uliridhia ombi la Jamhuri ya Shirikisho la Somalia kujiunga na Jumuiya. Kujiunga kwa Somalia kunaifanya Jumuiya kuwa na Nchi Wanachama nane (8) na kumeongeza takriban watu milioni 18 katika soko la Afrika Mashariki.

147. Mwaka 2023, Tanzania na nchi nyingine wanachama ziliendelea kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inayolenga kukuza biashara, kuongeza ufanisi katika uzalishaji, kukuza uwekezaji baina ya nchi wanachama na kuendeleza viwanda. Katika kipindi hicho, Jumuiya ilianza utaratibu wa kutoa vyeti vya uasili wa bidhaa za kielektroniki. Utaratibu huo utawezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kupokea vyeti kutoka mamlaka za mapato za nchi wanachama kutokana na kuunganishwa kwa mifumo ya kiforodha kupitia utaratibu wa Himaya Moja ya Forodha ya Afrika Mashariki. Aidha, Jumuiya ilianzisha programu-tumizi ya simu ya kutoa taarifa za vikwazo vya biashara visivyo vya kiforodha (NTB Reporting - EAC) iliyounganishwa na mifumo mingine ya utoaji taarifa za vikwazo. Hatua hii ni sehemu ya jitihada za kuboresha na kurahisisha ufanyaji biashara na kutatua migogoro ya kibiashara ndani ya Jumuiya.

148. Mwaka 2023, Tanzania na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliendelea kutumia Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani kwa lengo la kuharakisha usafirishaji wa mizigo na abiria ndani ya Jumuiya. Katika kipindi hicho, Serikali ilipata mkopo wa masharti nafuu wa dola za Marekani milioni 12 kutoka Benki ya

Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa Kituo cha Manyovu/Mugina kilichopo mpakani mwa Tanzania na Burundi.

149. Mwaka 2023, Nchi Wanachama wa Jumuiya zilipitisha Sera ya Kanda Maalumu za Kiuchumi ya Afrika Mashariki kupitia Mkutano wa 43 wa Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Bujumbura, Burundi. Utekelezaji wa Sera hiyo utawezesha nchi wanachama kuanzisha au kuendeleza kanda na maeneo maalumu ya kiuchumi na hivyo, kuimarisha ukuaji wa viwanda na mauzo ya nje. Aidha, Tanzania ilianza utekelezaji wa Mpango wa Eneo Moja la Mtandao la Afrika Mashariki (East Africa One Area Network) unaolenga kupunguza gharama za mawasiliano kwa njia ya simu za mkononi kwa nchi wanachama.

# SURA YA 6

## RASILIMALI WATU

### Idadi ya Watu

150. Mwaka 2023, idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa 63,670,531 ikilinganishwa na watu 61,741,120 iliyotokana na Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Aidha, Tanzania Bara ilikuwa na watu 61,718,700, sawa na asilimia 96.9 ya watu wote na Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu 1,951,831 (asilimia 3.1). Vile vile, wanawake walikadiriwa kuwa 32,644,994, sawa na asilimia 51.3 ya watu wote na wanaume walikuwa 31,025,537. Makadirio ya mwaka 2023 ni maoteo ya mwenendo wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa kutumia mbinu ya kipeo (exponential method).

### Mgawanyiko wa Watu Kimkoa

151. Mwaka 2023, Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na idadi kubwa ya watu wapatao 5,604,582, sawa na asilimia 9.1 ya watu wote Tanzania Bara ikifuatiwa na Mkoa wa Mwanza uliokuwa na watu 3,809,881, sawa na asilimia 6.2. Aidha, idadi kubwa ya watu katika Mkoa wa Dar es Salaam ilichangiwa na upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii na fursa za kiuchumi zilizovutia watu kuhamia kutoka mikoa mingine. Vile vile, Mkoa wa Njombe ulikuwa na idadi ndogo ya watu wapatao 925,816, sawa na asilimia 1.5 ya watu wote Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na idadi kubwa ya watu wapatao 927,681, sawa na asilimia 47.5 ya watu wote Tanzania Zanzibar. Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na idadi ndogo ya watu wapatao 203,646, sawa na asilimia 10.4 ya watu wote Tanzania Zanzibar.

152. Mwaka 2023, msongamano wa watu Tanzania ulikuwa wastani wa watu 72 kwa kila kilometa ya mraba ikilinganishwa na wastani wa watu 70 mwaka 2022. Aidha, msongamano wa watu Tanzania Bara ulikuwa wastani wa watu 70 kwa kila kilometa ya mraba ikilinganishwa na wastani wa watu 68 mwaka 2022. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 4,023 kwa kila kilometa ya mraba, ikifuatiwa na Mkoa wa Mwanza uliokuwa na wastani wa watu 402 kwa kila kilometa ya mraba. Vile vile, Mkoa wa Lindi ulikuwa na msongamano mdogo wa wastani wa watu 19 kwa kila kilometa ya mraba, ikifuatiwa na Mkoa wa Katavi uliokuwa na wastani wa watu 26 kwa kila kilometa ya mraba. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 4,033 kwa kila kilometa ya mraba, ikifuatiwa na Mkoa wa Kusini Pemba uliokuwa na wastani wa watu 840 kwa kila kilometa ya mraba. Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na msongamano mdogo wa wastani wa watu 238 kwa kila kilometa ya mraba.

153. Mwaka 2023, wastani wa idadi ya watu kwa kaya kwa Tanzania na Tanzania Bara ulibaki kuwa watu 4.3 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Aidha, Mkoa wa Simiyu uliongoza

kwa kuwa na wastani mkubwa wa idadi ya watu kwa kaya wa wastani wa watu 6.7 kwa kaya na Mkoa wa Mtwara ulikuwa na wastani mdogo wa watu 3.3 kwa kaya. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, wastani wa idadi ya watu kwa kaya ulibaki kuwa watu 5.0 mwaka 2023 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Mkoa wa Kusini Pemba uliongoza kwa kuwa na wastani mkubwa wa idadi ya watu kwa kaya wa 5.7 na Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na wastani mdogo wa 4.2.

**Jedwali 6.1: Idadi ya Watu na Wastani wa Idadi ya Watu kwa Kaya Mwaka 2023**

| Mkoa | Idadi ya Watu | | | Uwiano Kijinsi | Msongamano wa Watu | Idadi ya Kaya | Wastani wa Idadi ya Watu kwa Kaya |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Wanaume | Wanawake | | | | |
| **Tanzania** | **63,670,531** | **31,025,537** | **32,644,994** | **95** | **72** | **14,755,355** | **4.3** |
| **Tanzania Bara** | **61,718,700** | **30,078,239** | **31,640,461** | **95** | **70** | **14,362,463** | **4.3** |
| Dodoma | 3,177,174 | 1,559,510 | 1,617,664 | 96 | 77 | 780,305 | 4.1 |
| Arusha | 2,419,445 | 1,158,452 | 1,260,993 | 92 | 64 | 631,680 | 3.8 |
| Kilimanjaro | 1,936,220 | 942,141 | 994,079 | 95 | 146 | 517,713 | 3.7 |
| Tanga | 2,697,944 | 1,317,238 | 1,380,706 | 95 | 101 | 655,522 | 4.1 |
| Morogoro | 3,298,632 | 1,630,313 | 1,668,319 | 98 | 47 | 856,242 | 3.9 |
| Pwani | 2,076,480 | 1,024,387 | 1,052,093 | 97 | 64 | 556,736 | 3.7 |
| Dar es Salaam | 5,604,582 | 2,704,320 | 2,900,262 | 93 | 4,023 | 1,613,654 | 3.5 |
| Lindi | 1,241,992 | 603,785 | 638,207 | 95 | 19 | 361,183 | 3.4 |
| Mtwara | 1,710,148 | 808,451 | 901,697 | 90 | 102 | 515,774 | 3.3 |
| Ruvuma | 1,927,924 | 940,132 | 987,792 | 95 | 30 | 486,803 | 4.0 |
| Iringa | 1,233,733 | 595,199 | 638,534 | 93 | 35 | 332,955 | 3.7 |
| Mbeya | 2,416,550 | 1,162,427 | 1,254,123 | 93 | 64 | 649,673 | 3.7 |
| Singida | 2,068,494 | 1,026,618 | 1,041,876 | 99 | 42 | 407,769 | 5.1 |
| Tabora | 3,468,780 | 1,702,926 | 1,765,854 | 96 | 46 | 612,268 | 5.7 |
| Rukwa | 1,579,858 | 764,430 | 815,428 | 94 | 69 | 338,451 | 4.7 |
| Kigoma | 2,533,738 | 1,222,087 | 1,311,651 | 93 | 68 | 491,280 | 5.2 |
| Shinyanga | 2,298,016 | 1,132,854 | 1,165,162 | 97 | 122 | 434,087 | 5.3 |
| Kagera | 3,093,648 | 1,511,501 | 1,582,147 | 96 | 122 | 726,931 | 4.3 |
| Mwanza | 3,809,881 | 1,857,847 | 1,952,034 | 95 | 402 | 773,979 | 4.9 |
| Mara | 2,444,607 | 1,176,176 | 1,268,431 | 93 | 112 | 485,294 | 5.0 |
| Manyara | 1,938,948 | 980,396 | 958,552 | 102 | 44 | 413,370 | 4.7 |
| Njombe | 925,816 | 437,612 | 488,204 | 90 | 43 | 256,439 | 3.6 |
| Katavi | 1,178,923 | 583,824 | 595,099 | 98 | 26 | 220,845 | 5.3 |
| Simiyu | 2,198,807 | 1,065,432 | 1,133,375 | 94 | 87 | 326,625 | 6.7 |
| Geita | 3,053,478 | 1,504,464 | 1,549,014 | 97 | 152 | 576,260 | 5.3 |
| Songwe | 1,384,882 | 665,717 | 719,165 | 93 | 61 | 340,625 | 4.1 |
| **Tanzania Zanzibar** | **1,951,831** | **947,298** | **1,004,533** | **94** | **793** | **392,892** | **5.0** |
| Kaskazini Unguja | 263,634 | 129,640 | 133,994 | 97 | 561 | 56,161 | 4.7 |
| Kusini Unguja | 203,646 | 102,456 | 101,190 | 101 | 238 | 48,876 | 4.2 |
| Mjini Magharibi | 927,681 | 444,831 | 482,850 | 92 | 4,033 | 189,115 | 4.9 |
| Kaskazini Pemba | 278,042 | 134,985 | 143,057 | 94 | 484 | 49,637 | 5.6 |
| Kusini Pemba | 278,828 | 135,386 | 143,442 | 94 | 840 | 49,103 | 5.7 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Mgawanyo wa Watu kwa Umri**


154. Mwaka 2023, kulikuwa na watoto 9,470,626 wenye umri chini ya miaka mitano sawa na asilimia 15.3 ya watu wote Tanzania Bara. Watu wenye umri wa miaka 5 hadi 14 walikuwa 16,731,608, sawa na asilimia 27.1. Aidha, idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 35 ilikuwa 21,378,933, sawa na asilimia 34.6 ya watu wote. Idadi ya nguvukazi ambao ni watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 ilikuwa 33,222,424 (asilimia 53.8). Idadi ya watu wenye umri wa miaka 65 na zaidi ilikuwa 2,294,042 (asilimia 3.7). Vile vile, idadi ya umri tegemezi ambao ni watu wenye umri wa miaka 65 na zaidi na wenye umri chini ya miaka 15 ilikuwa 28,496,276, sawa na asilimia 46.1 ya watu wote. Kwa kuzingatia kiwango hiki kikubwa cha umri tegemezi na kasi ya ongezeko la idadi ya watu, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuongeza fedha katika bajeti ili kukidhi mahitaji ya kugharamia huduma za jamii. Mahitaji ya kugharamia huduma za jamii kupitia bajeti ya Serikali yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 10,124.0 mwaka 2020/21 sawa na asilimia 6.7 ya Pato la Taifa hadi shilingi bilioni 12,652.75 mwaka 2022/23, sawa na asilimia 7.1 ya Pato la Taifa.

**Jedwali Na. 6.2: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri na Jinsi Mwaka 2023**


| **Umri** | **Jinsi** | | **Jumla** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| | **Wanawake** | **Wanaume** | | |
| 0 - 4 | 4,737,416 | 4,733,210 | 9,470,626 | 15.3 |
| 5 - 14 | 8,361,377 | 8,370,231 | 16,731,608 | 27.1 |
| 15 - 35 | 11,156,288 | 10,222,645 | 21,378,933 | 34.6 |
| 36 - 64 | 6,107,360 | 5,736,131 | 11,843,491 | 19.2 |
| 65+ | 1,278,020 | 1,016,022 | 2,294,042 | 3.7 |
| **Jumla** | **31,640,461** | **30,078,239** | **61,718,700** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo Na. 6.1: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri Mwaka 2023**




**Kielelezo Na. 6.2: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri na Jinsi Mwaka 2023**



**Nguvu Kazi na Ajira**

155. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Taifa ya Ukuzaji Ujuzi kwa vijana kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira. Katika kipindi hicho, vijana 10,220 walipata mafunzo ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira ili waweze kuajiriwa na kujiajiri ikilinganishwa na vijana 21,586 waliopata mafunzo mwaka 2022. Kati ya hao, vijana 4,273 walipata mafunzo ya uanagenzi (ufundi stadi vyuoni, uchumi wa buluu, unenepeshaji wa mifugo na Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora - BBT), wafanyakazi 1,593 wa sekta ndogo ya utalii na ukarimu pamoja na wafanyabiashara wadogo na wa kati walipata mafunzo ya kukuza ujuzi na wahitimu 4,354 walipata mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi.

156. Mwaka 2023, Serikali kupitia Kitengo cha Huduma za Ajira ilisajili watafutakazi 17,107 (wanaume 8,902 na wanawake 8,205) na kuwapatia ushauri nasaha kuhusu uchaguzi wa kazi ikilinganishwa na watafutakazi 10,540 waliosajiliwa na kupatiwa huduma ya ushauri nasaha mwaka 2022, sawa na ongezeka la asilimia 62.3. Katika kipindi hicho, watu 10,847 (wanaume 6,025 na wanawake 4,822) walipata mafunzo ya kushindania fursa za ajira ikilinganishwa na watafutakazi 5,161 (wanaume 2,816 na wanawake 2,345) waliopata mafunzo husika mwaka 2022. Aidha, mafunzo hayo yalitolewa kwa ajili ya kuwajengea uwezo watafutakazi kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi pamoja na kujenga maadili ya kazi yanayohitajika na waajiri mbalimbali. Vile vile, vijana 311 (wanaume 180 na wanawake 131) waliunganishwa na fursa za kazi kwa waajiri mbalimbali nchini ikilinganishwa na vijana 909 waliounganishwa na kazi mwaka 2022. Katika kipindi hicho, vijana 2,895 (wanaume 1,564 na wanawake 1,331) wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo waliunganishwa kwa waajiri kufanya mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa kipindi cha miezi 12 ili kupata uzoefu wa kazi pamoja na kujenga stadi muhimu za kuongeza tija na ufanisi kazini ikilinganishwa na vijana 3,231 mwaka 2022. Mwaka 2023, Kitengo cha Huduma za Ajira kiliunganisha Watanzania 2,529 (wanaume 416 na wanawake 2,113) kwenye fursa za kazi nje ya nchi.

## Jedwali Na. 37: IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA MWAKA 2017 - 2023

| **Mkoa** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 2,419,941 | 2,492,989 | 2,568,514 | 2,647,410 | 2,729,668 | 3,085,625 | 3,177,174 |
| Arusha | 1,948,219 | 1,999,907 | 2,051,852 | 2,104,074 | 2,156,511 | 2,356,255 | 2,419,445 |
| Kilimanjaro | 1,823,151 | 1,864,329 | 1,906,978 | 1,951,252 | 1,996,952 | 1,861,934 | 1,936,220 |
| Tanga | 2,284,712 | 2,337,053 | 2,391,791 | 2,449,235 | 2,509,439 | 2,615,597 | 2,697,944 |
| Morogoro | 2,531,268 | 2,596,287 | 2,662,468 | 2,730,058 | 2,799,260 | 3,197,104 | 3,298,632 |
| Pwani | 1,236,481 | 1,265,504 | 1,295,267 | 1,325,852 | 1,357,271 | 2,024,947 | 2,076,480 |
| Dar es Salaam | 5,017,294 | 5,147,070 | 5,275,315 | 5,401,814 | 5,526,638 | 5,383,728 | 5,604,582 |
| Lindi | 963,465 | 983,738 | 1,004,439 | 1,025,800 | 1,047,783 | 1,194,028 | 1,241,992 |
| Mtwara | 1,397,723 | 1,424,083 | 1,451,078 | 1,478,874 | 1,507,426 | 1,634,947 | 1,710,148 |
| Ruvuma | 1,543,869 | 1,579,811 | 1,616,991 | 1,655,443 | 1,695,057 | 1,848,794 | 1,927,924 |
| Iringa | 1,068,695 | 1,095,172 | 1,122,131 | 1,149,481 | 1,177,327 | 1,192,728 | 1,233,733 |
| Mbeya | 2,006,072 | 2,070,412 | 2,136,614 | 2,204,543 | 2,274,236 | 2,343,754 | 2,416,550 |
| Singida | 1,569,304 | 1,612,854 | 1,658,086 | 1,705,182 | 1,754,370 | 2,008,058 | 2,068,494 |
| Tabora | 2,769,093 | 2,870,522 | 2,974,427 | 3,081,263 | 3,191,194 | 3,391,679 | 3,468,780 |
| Rukwa | 1,160,568 | 1,195,550 | 1,231,959 | 1,270,049 | 1,310,007 | 1,540,519 | 1,579,858 |
| Kigoma | 2,528,708 | 2,616,200 | 2,706,831 | 2,800,919 | 2,898,568 | 2,470,967 | 2,533,738 |
| Shinyanga | 1,816,316 | 1,874,709 | 1,933,768 | 1,993,589 | 2,054,229 | 2,241,299 | 2,298,016 |
| Kagera | 2,919,942 | 3,022,037 | 3,127,908 | 3,238,347 | 3,353,241 | 2,989,299 | 3,093,648 |
| Mwanza | 3,393,620 | 3,532,378 | 3,676,300 | 3,826,573 | 3,983,793 | 3,699,872 | 3,809,881 |
| Mara | 2,123,683 | 2,209,143 | 2,298,317 | 2,391,845 | 2,490,155 | 2,372,015 | 2,444,607 |
| Manyara | 1,692,667 | 1,750,864 | 1,810,929 | 1,873,105 | 1,937,450 | 1,892,502 | 1,938,948 |
| Njombe | 786,347 | 803,299 | 820,355 | 837,557 | 854,932 | 889,946 | 925,816 |
| Katavi | 706,472 | 738,237 | 771,287 | 805,887 | 842,200 | 1,152,958 | 1,178,923 |
| Simiyu | 1,998,224 | 2,094,798 | 2,196,449 | 2,304,228 | 2,418,495 | 2,140,497 | 2,198,807 |
| Geita | 2,148,409 | 2,239,949 | 2,335,134 | 2,434,800 | 2,539,114 | 2,977,608 | 3,053,478 |
| Songwe | 1,166,094 | 1,202,419 | 1,239,970 | 1,278,850 | 1,319,064 | 1,344,687 | 1,384,882 |
| **Tanzania Bara** | **51,020,337** | **52,619,314** | **54,265,158** | **55,966,030** | **57,724,380** | **59,851,347** | **61,718,700** |
| Kaskazini Unguja | 216,697 | 222,066 | 227,317 | 232,480 | 237,505 | 257290 | 263,634 |
| Kusini Unguja | 131,162 | 133,767 | 136,235 | 138,589 | 140,821 | 195873 | 203,646 |
| Mjini Magharibi | 683,833 | 700,791 | 717,468 | 733,914 | 750,033 | 893169 | 927,681 |
| Kaskazini Pemba | 260,884 | 271,594 | 282,716 | 294,267 | 306,173 | 272091 | 278,042 |
| Kusini Pemba | 241,715 | 251,631 | 261,853 | 272,348 | 283,076 | 271350 | 278,828 |
| **Zanzibar** | **1,534,291** | **1,579,849** | **1,625,589** | **1,671,598** | **1,717,608** | **1,889,773** | **1,951,831** |
| **Tanzania** | **52,554,628** | **54,199,163** | **55,890,747** | **57,637,628** | **59,441,988** | **61,741,120** | **63,670,531** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu



## Sehemu ya Pili

# Maendeleo ya Sekta Mbalimbali

# SURA YA 7

# KILIMO NA USHIRIKA

## UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO

### Mazao ya Chakula

157. Mwaka 2023, uzalishaji wa mazao makuu ya chakula uliongezeka kwa asilimia 19.0 na kufikia tani 20,402,014 ikilinganishwa na tani 17,148,290 mwaka 2022. Kati ya hizo, tani 11,448,757 zilikuwa za mazao ya nafaka na tani 8,953,258 mazao yasiyo ya nafaka. Ongezeko la uzalishaji lilichangiwa na: kuwepo kwa mvua za kutosha katika maeneo mengi ya uzalishaji; kuimarika kwa huduma za ugani na upatikanaji wa vitendea kazi; matumizi ya teknolojia na pembejeo bora za kilimo ikiwemo mbegu na mbolea; na kuimarika kwa usimamizi wa upotevu mazao kabla na baada ya kuvuna. Katika kipindi hicho, mahitaji ya chakula yalikuwa tani 16,390,404 ikilinganishwa na tani 15,053,034 mwaka 2022 na hivyo kuwa na ziada ya chakula ya kiasi cha tani 4,011,611. Kulingana na mahitaji ya chakula, nchi ilikuwa na kiwango cha utoshelevu wa chakula wa asilimia 124.5

**Jedwali Na 7.1: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Chakula (Tani '000') Mwaka 2019 - 2023**

| Aina ya Zao | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mazao ya Nafaka** | | | | | | |
| Mahindi | 5,652 | 6,711 | 7,039 | 6,417 | 8,011 | 24.8 |
| Mchele | 2,063 | 3,038 | 2,687 | 1,708 | 2,332 | 36.5 |
| Ngano | 63 | 77 | 70 | 62 | 87 | 40.3 |
| Mtama/Uwele/Ulezi | 1,117 | 1043 | 1,077 | 1,046 | 1,019 | -2.6 |
| **Mazao yasiyo Nafaka** | | | | | | |
| Muhogo | 2,728 | 2,427 | 2,486 | 2,411 | 2,575 | 6.8 |
| Maharage/Mikunde | 1,888 | 1895 | 2,235 | 2,499 | 2803 | 12.2 |
| Ndizi | 1,135 | 1,358 | 1,442 | 1,290 | 1,224 | -5.1 |
| Viazi (Vitamu na mviringo) | 1,644 | 1,646 | 1,626 | 1,715 | 2351 | 37.1 |
| **Jumla** | **16,290** | **18,195** | **18,665** | **17,148** | **20,402** | **19.0** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

### Miundombinu ya Hifadhi ya Chakula

158. Mwaka 2023, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA ilijenga vihenge nane (8) katika mkoa wa Manyara vyenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 15,000 za nafaka ikilinganishwa na vihenge 12 vyenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 20,000 vilivyojengwa katika mikoa ya Rukwa na Katavi mwaka 2022. Aidha, ghala nne (4) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 25,000 za nafaka zilijengwa na NFRA katika mikoa ya Manyara, Rukwa na Katavi. Ujenzi wa vihenge na ghala uliongeza uwezo wa

Wakala wa kuhifadhi nafaka na kufikia tani 341,000 mwaka 2023 kutoka tani 321,000 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 12.5.

159. Hadi Desemba 2023, ghala zilizojengwa na kukamilika kupitia Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu - TANIPAC zilifikia ghala 12 zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 19,500 kutoka ghala sita (6) zilizojengwa na kukamilika katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ghala hizo zilijengwa katika Halmashauri zifuatazo: Chemba - Dodoma yenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,500; Bukombe - Geita (tani 1,500); Nanyumbu - Mtwara (tani 1,500); Buchosa - Mwanza (tani 1,500); Itilima - Simiyu (tani 1,500); Nzega - Tabora (tani 1,000); Namtumbo - Mtwara (tani 1,500); Babati - Manyara (tani 2,000); Gairo - Morogoro (tani 1,500); Kasulu - Kigoma (tani 2,000); Kibondo - Kigoma (tani 2,000); na Kiteto - Manyara (tani 2,000). Lengo la Mradi ni kujenga miundombinu wezeshi kwa ajili ya kudhibiti sumukuvu pamoja na kuimarisha teknolojia ya kabla na baada ya kuvuna.

**Mazao ya Biashara**

160. Mwaka 2023, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ulifikia tani 1,267,160 ikilinganishwa na tani 973,436 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 30.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la tumbaku, pamba, pareto na korosho kulikochangiwa na utoaji wa huduma bora za kilimo na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa mpango wa ruzuku.

**Jedwali Na. 7.2: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (Tani) Mwaka 2019 - 2023**

| Zao | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Pamba | 348,910 | 348,958 | 122,836 | 144,792 | 282,163 | 94.8 |
| Kahawa | 68,147 | 60,651 | 73,027 | 66,837 | 62,917 | -5.9 |
| Chai | 37,193 | 28,715 | 27,510 | 24,825 | 23,775 | -4.2 |
| Pareto | 2,014 | 2,510 | 2,412 | 2,694 | 4,239 | 57.3 |
| Tumbaku | 70,824 | 37,546 | 58,508 | 70,699 | 122,859 | 73.7 |
| Korosho | 225,053 | 232,681 | 210,786 | 240,158 | 254,425 | 5.9 |
| Mkonge | 33,271 | 36,379 | 36,170 | 44,151 | 56,733 | 28.5 |
| Sukari | 359,219 | 311,358 | 367,718 | 379,280 | 460,049 | 21.3 |
| **Jumla** | **1,144,631** | **1,058,798** | **898,967** | **973,436** | **1,267,160** | **30.2** |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

**Mazao ya Bustani**

161. Mwaka 2023, uzalishaji wa mazao ya bustani unaojumuisha maua, matunda, viungo na mboga ulikuwa tani 8,438,273.98 ikilinganishwa na tani 7,723,116 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.3. Hii ilitokana na kuendelea kuimarika kwa huduma za ugani,

matumizi bora ya pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora na mbolea ya ruzuku pamoja na matumizi ya teknolojia bora za kilimo, hususan kitalu nyumba na umwagiliaji kwa njia ya matone.

**Jedwali Na 7.3: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani) Mwaka 2019 - 2023**

| Zao | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Matunda | 4,576,948 | 5,582,117 | 5,199,312 | 5,407,284 | 6,530,302 | 20.8 |
| Mboga | 1,926,927 | 1,852,676 | 2,011,684 | 2,212,852 | 1,777,878.49 | -19.7 |
| Maua | 13,240 | 1,710 | 1,338 | 1,351 | 576.9 | -57.3 |
| Viungo | 80,748 | 123,507 | 92,389 | 101,628 | 129,516.59 | 27.4 |
| **Jumla** | **6,597,863** | **7,560,010** | **7,304,723** | **7,723,116** | **8,438,273.9** | **9.3** |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

**Mazao ya Mbegu za Mafuta**

162. Mwaka 2023, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta yanayojumuisha alizeti, ufuta, soya, chikichi na karanga uliongezeka kwa asilimia 36.7 na kufikia tani 2,061,217.47 ikilinganishwa na tani 1,507,565 zilizozalishwa mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa mpango wa ruzuku na hali nzuri ya hewa.

**Jedwali Na 7.4: Uzalishaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta (Tani) Mwaka 2019 - 2023**

| Zao | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Alizeti | 561,297 | 649,437.30 | 478,900 | 425,653.1 | 1,132,298.34 | 166.0 |
| Karanga | 376,520 | 631,465.30 | 895,219 | 936,799 | 586,216.09 | -37.4 |
| Ufuta | 227,821 | 228,919.80 | 236,162 | 79,170 | 266,994 | 237.2 |
| Chikichi | 42,176 | 42,386.90 | 58,791 | 60,790 | 62,125.00 | 2.2 |
| Soya | 22,953 | 31,460 | 44,106 | 5,152 | 13,584.04 | 163.7 |
| **Jumla** | **1,230,767** | **1,583,669** | **1,713,178** | **1,507,565** | **2,061,217.47** | **36.7** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo.

**Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo**

163. Mwaka 2023, upatikanaji wa mbegu bora uliongezeka kwa asilimia 8.3 na kufikia tani 58,746.5 ikilinganishwa na tani 54,221.8 mwaka 2022. Kati ya mbegu hizo, tani 47,848.5 zilizalishwa nchini ikilinganishwa na tani 44,461.8 zilizozalishwa nchini mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.6. Ongezeko hilo lilichangiwa na uwepo wa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wa mbegu nchini. Aidha, tani 10,898.0 za mbegu ziliingizwa kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na tani 10,031 zilizoingizwa kutoka nje ya nchi mwaka 2022. Kwa mbegu zilizozalishwa nchini, tani 3,549 zilizalishwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo - ASA ikilinganishwa na tani 3,173 zilizozalishwa na ASA mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.8.

164. Mwaka 2022/23, upatikanaji wa mbolea ulikuwa tani 1,007,678 ikilinganishwa na tani 560,551 mwaka 2021/22. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa ndani ulikuwa tani 84,696 ikilinganishwa na tani 62,724 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 35.0. Aidha, uagizaji wa mbolea ulikuwa tani 824,085 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na tani 379,927 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 116.9. Ongezeko la uzalishaji na uagizaji wa mbolea lilitokana na Serikali kutoa ruzuku ya mbolea iliyoongeza motisha kwa wazalishaji wa ndani kuongeza kiwango cha uzalishaji na kwa wafanyabiashara kuagiza mbolea kutoka nje.

**Jedwali Na. 7.5: Upatikanaji wa Mbolea Nchini (Tani) Mwaka 2018/19 - 2022/23**

| **Mwaka** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** |
|---|---|---|---|---|---|
| Makadirio ya Mahitaji | 514,138 | 586,604 | 718,051 | 698,260 | 667,730 |
| **Upatikanaji** | | | | | |
| Bakaa | - | 168,397 | 219,206 | 117,900 | 98,897 |
| Uzalishaji Ndani ya Nchi | 28,318 | 33,873 | 42,695 | 62,724 | 84,696 |
| Kiasi Kilichoingizwa Ndani ya Nchi | 514,725 | 524,972 | 504,122 | 379,927 | 824,085 |
| **Jumla ya Upatikanaji** | **543,043** | **727,242** | **766,023** | **560,551** | **1,007,678** |
| Kiasi Kilichouzwa Nje ya Nchi | 96,370 | 145,367 | 171,254 | 98,055 | 128,774 |
| Matumizi ya Ndani ya Nchi | 364,968 | 457,855 | 476,870 | 363,599 | 580,628 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania

165. Mwaka 2022/23, wastani wa bei ya mbolea ya kukuzia - UREA katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 688 kwa tani ikilinganishwa na dola za Marekani 744 kwa tani mwaka 2021/22, sawa na upungufu wa asilimia 7.5. Aidha, wastani wa bei ya mbolea ya kupandia - DAP katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 800 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na dola za Marekani 713 kwa tani mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 12.2. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa athari ya vita kati ya Ukraine na Urusi iliyochangia kushuka kwa uzalishaji wa mbolea. Ukraine na Urusi ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa mbolea ya kupandia duniani.

166. Mwaka 2023, jumla ya mikopo 42 yenye thamani ya shilingi milioni 1,371.40 ilitolewa na Mfuko wa Pembejeo za kilimo - AGITF ikilinganishwa na mikopo 56 yenye thamani ya shilingi milioni 2,048.40 iliyotolewa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 33.1. Hii ilitokana na kupungua kwa utolewaji wa baadhi ya mikopo kutokana na wakopaji kutokidhi vigezo vya kukopa. Mikopo iliyotolewa ilijumuisha: ununuzi wa matrekta yenye thamani ya shilingi milioni 577.0; ununuzi wa mtambo wa kuvunia (shilingi milioni 74.0); ujenzi wa miundombinu ya ufugaji (shilingi milioni 123.0), ujenzi wa ghala (shilingi milioni 60.0); ununuzi wa mashine za kuongeza thamani (shilingi milioni 86.9); ununuzi wa pembejeo za kilimo (shilingi milioni 60.0); ununuzi wa treka la mkono (shilingi milioni 12.5); shughuli za shamba (shilingi milioni 243.0); shughuli za umwagiliaji (shilingi

milioni 70.0); ukarabati wa matrekta (shilingi milioni 5.0); na shughuli za kilimo katika Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (shilingi milioni 60.0). Aidha, shilingi milioni 1,625.30 zilirejeshwa ikiwa ni asilimia 22.9 ya lengo la marejesho ya shilingi milioni 7,082.43 mwaka 2023 ikilinganishwa na marejesho ya shilingi milioni 3,210.69 sawa na asilimia 53.2 ya lengo la shilingi milioni 6,031.14 mwaka 2022. Kupungua kwa kiwango cha urejeshaji kulitokana na wakopaji wengi kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati kutokana na kuwepo kwa changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuathri uzalishaji.

**Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao**

167. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kuimarisha mifumo ya uuzaji na ununuzi wa mazao ya kilimo ikiwemo Soko la Bidhaa - TMX, Stakabadhi za Ghala, Minada na Kilimo cha Mkataba. Mfumo wa minada ulitumika katika uuzaji wa kahawa na kakao. Kwa upande wa mazao ya korosho na mbaazi, mfumo wa stakabadhi za ghala uliendelea kutumika. Aidha, mfumo wa Soko la Bidhaa ulitumika katika uuzaji wa kahawa na kakao na mazao ya mahindi, mpunga na mchele yaliuzwa kupitia mfumo wa soko huria. Kwa upande mwingine, Mfumo wa Kilimo cha Mkataba ulitumika kwa mazao ya chai, tumbaku, alizeti, pamba na kahawa. Matumizi ya mifumo hiyo ya masoko yalichangia kuimarika kwa bei ya baadhi ya mazao ya kilimo katika soko la ndani.

168. Mwaka 2023, wastani wa bei ya kahawa aina ya robusta katika soko la ndani ulikuwa shilingi 2,965 kwa kilogramu ikilinganishwa na shilingi 1,850 kwa kilogramu mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 60.3. Aidha, wastani wa bei ya mahindi uliongezeka kwa asilimia 26.4 na kufikia shilingi 105,200 kwa gunia la kilo 100 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 83,200 kwa gunia la kilo 100 mwaka 2022. Vile vile, bei ya mchele iliongezeka kutoka wastani wa shilingi 216,800 kwa gunia la kilo 100 mwaka 2022 hadi wastani wa shilingi 275,440 kwa gunia la kilo 100 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 27.0. Hali kadhalika, bei ya maharage iliongezeka kutoka wastani wa shilingi 215,100 kwa gunia la kilo 100 mwaka 2022 hadi wastani wa shilingi 276,930 kwa gunia la kilo 100 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 28.7. Pamoja na ongezeko la bei katika mazao hayo, wastani wa ongezeko la bei ulikuwa mdogo ikilinganishwa na ongezeko la bei mwaka 2022 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 7.6**. Kwa upande mwingine, wastani wa bei ya pamba ulipungua kwa asilimia 36.1 na kufikia shilingi 1,150 kwa kilogramu mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,800 kwa kilogramu mwaka 2022. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa wastani wa bei ya pamba kwenye soko la dunia kulikosababishwa na ongezeko la uzalishaji wa zao la hilo katika nchi nyingine baada ya kipindi cha UVIKO - 19.

**Jedwali Na. 7.6: Wastani wa Bei za Jumla za Mazao Makuu ya Chakula (Shilingi/Gunia la Kilo 100) Mwaka 2019 - 2023**

| Zao | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko 2022-2021 (Asilimia) | Badiliko 2023- 2022 (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 64,400 | 63,200 | 47,800 | 83,200 | 105,200 | 74.1 | 26.4 |
| Mchele | 169,200 | 159,500 | 142,800 | 216,800 | 275,440 | 51.8 | 27.0 |
| Mtama | 86,400 | 107,600 | 99,200 | 123,600 | 139,910 | 24.6 | 13.2 |
| Ulezi | 132,900 | 129,500 | 151,800 | 169,500 | 141,000 | 11.7 | -16.8 |
| Ngano | 124,300 | 123,400 | 124,900 | 182,100 | 191,930 | 45.8 | 5.4 |
| Maharage | 169,000 | 197,400 | 176,100 | 215,100 | 276,930 | 22.1 | 28.7 |
| Viazi mviringo | 72,800 | 75,600 | 68,000 | 82,000 | 97,710 | 20.6 | 19.2 |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

**Jedwali Na. 7.7: Mwenendo wa Wastani wa Bei za Mazao ya Asili ya Biashara (Shilingi/Kilogramu) Mwaka 2020 - 2023**

| Zao | Aina/Daraja | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | Arabica | 4,500 | 6,500 | 8,428 | 5,978 | **-29.1** |
| | Robusta | 1,300 | 1,400 | 2,646 | 2,965 | **12.1** |
| Pamba | Pamba mbegu | 900 | 1,400 | 1,800 | 1,150 | **-36.1** |
| Korosho | *Standard grade* | 2,229 | 2,150 | 1,860 | 1,720 | **-7.5** |
| | *Under grade* | 1,642 | 1,595 | 1,331 | 1,200 | **-9.8** |
| Tumbaku* | Mvuke (VFC) | 1.55 | 1.79 | 1.79 | 2.34 | **19.6** |
| | Moshi (DFC) | 1.25 | 1.51 | 1.51 | 1.69 | **11.9** |
| Chai | Majani mabichi | 314 | 314 | 366 | 366 | **0.0** |
| | Majani Makavu* | 1.49 | 1.62 | 1.55 | 1.24 | **-20.0** |
| Mkonge | Singa (*Fibres*) | 3,300 | 3,500 | 3,626 | 3,483 | **-3.9** |
| Pareto | Maua makavu | 2,500 | 3,200 | 3,200 | 3,500 | **9.4** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo
***** (Dola za Marekani /Kilogramu)

### Huduma za Ugani

169. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya kilimo kwa wakulima kupitia mfumo wa M-Kilimo na Kituo cha Huduma kwa Wateja (Kilimo Call Center). Katika kipindi hicho, maafisa ugani 9,985 na wakulima 3,610,543 walikuwa wamesajiliwa katika mfumo wa M-Kilimo ikilinganishwa na maafisa ugani 9,985 na wakulima 7,269,103 waliosajiliwa mwaka 2022. Kupungua kwa idadi ya wakulima waliosajiliwa kulitokana na zoezi la uhuishaji wa takwimu liliofanyika katika mfumo huo. Aidha, maswali/hoja za wakulima zilikuwa 116,865 mwaka 2023 ikilinganishwa na maswali/hoja 75,697 mwaka 2022. Vile vile, jumla ya simu 11,355 zilipokelewa na kuhudumiwa katika Kituo cha Huduma kwa Wateja.

170. Mwaka 2023, Serikali ilitoa mafunzo rejea kwa wataalam 497 kuhusu matumizi ya vifaa vya kupima afya ya udongo; utunzaji wa vitendea kazi vya maafisa ugani vilivyogawiwa na Serikali; matumizi ya mifumo ya kidigitali katika kutoa huduma za ugani; uendeshaji wa mashamba darasa na usimamizi wa Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata. Wataalamu hao walihusisha wakuu wa idara za kilimo, mifugo na uvuvi ngazi ya halmashauri (184); Makatibu Tawala Wasaidizi Idara ya Uchumi na Uzalishaji (26); maafisa kilimo ngazi ya mkoa (26) na maafisa kilimo ngazi ya halmashauri (184).

171. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kuhakikisha huduma za ugani zinawafikia wakulima kwa wakati. Katika kipindi hicho, Serikali ilinunua na kusambaza seti ya vifaa ambata 143 ikijumuisha kompyuta 143, vishikwambi 143, *lamination machine* 143 na printa 143 kwa ajili ya kuwezesha zoezi la upimaji na utunzaji wa kumbukumbu za afya ya udongo katika Halmashauri 141 kwenye mikoa 25. Aidha, Serikali ilinunua vishikwambi 805 na kusambaza kwa maafisa ugani wa mikoa ya Dar es salaam, Tanga na Pwani pamoja na visanduku vya ugani 1,000 vilivyosambazwa katika mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa, na Ruvuma.

**Utafiti katika Uzalishaji wa Mazao**

172. Mwaka 2023, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo - TARI iligundua aina mpya tano (5) za mbegu bora za zabibu kwa ajili ya matumizi ya wakulima ikilinganishwa na aina kumi (10) za mbegu bora za mazao mbalimbali zilizogunduliwa mwaka 2022. Mbegu hizo ni TARIZAB1, TARIZAB2, TARIZAB3, TARIZAB4 na TARIZAB5. Sifa za mbegu hizo ni pamoja na kutoa mavuno kwa wingi (tani 7.5 - 27.5/hekta), kutoshambuliwa na wadudu na uwezo wa kuhifadhiwa kwa muda mrefu bila kuharibika (siku 14 - 21) baada ya kuvunwa ikilinganishwa na aina nyingine ambayo huharibika siku saba (7) baada ya kuvunwa. Aidha, aina 20 za mbegu zilizoonekana kufanya vizuri ziliwasilishwa Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania - TOSCI kwa ajili ya majaribio na kuidhinishwa kwa matumizi katika mchanganuo ufuatao: mbegu za maharage aina tatu (3), choroko aina nne (4), korosho aina 10 na biringanya aina tatu (3).

173. Mwaka 2023, TARI ilizalisha jumla ya tani 1,131.36 za mbegu bora za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta ikilinganishwa na tani 259.9 zilizozalishwa mwaka 2022. Kati ya hizo, tani 17.5 zilikuwa za mbegu mama, tani 189.0 mbegu za awali, tani 508.3 mbegu za msingi na tani 416.5 mbegu zilizothibitishwa. Aidha, miche/vikonyo 6,316,095 vilizalishwa mwaka 2023 ikilinganishwa na miche/vikonyo 1,482,016 vilivyozalishwa mwaka 2022. Ongezeko la mbegu na miche/vikonyo lilitokana na ongezeko la mahitaji ya miche/vikonyo pamoja na Serikali kuongeza bajeti kwenye utafiti katika kipindi husika.

174. Mwaka 2023, TARI ilikusanya aina 312 za mbegu za asili za mpunga. Kati ya hizo, aina 54 za mbegu zilisafishwa na kuendelea kuzalishwa kwa ajili ya masoko maalumu na kutunzwa kwa ajili ya utafiti. Aidha, mbegu bora za bamia (pusa sawani), nyanya (Tanya na Tengeru) na ngano (Lumbesa, Mbayuwayu, Chiriku na Sifa) zilisafishwa.

**Mafunzo ya Kilimo**

175. Mwaka 2023, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo 14 vya mafunzo ya kilimo ngazi ya astashahada na stashahada iliongezeka kwa asilimia 8.3 na kufikia 3,372 ikilinganishwa na wanafunzi 3,115 waliodahiliwa mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na ujenzi wa majengo mapya na ukarabati wa majengo katika vyuo hivyo. Katika kipindi hicho, wakufunzi tisa (9) walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ngazi ya shahada ya uzamili na shahada ya kwanza ikilinganishwa na wakufunzi 14 waliopatiwa mafunzo hayo mwaka 2022. Lengo la mafunzo hayo ni kuwaongezea maarifa na ujuzi wakufunzi hao ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kufundisha kwa ufanisi.

**Umwagiliaji**

176. Mwaka 2023, eneo la umwagiliaji lilikuwa hekta 727,280.6, kama ilivyokuwa mwaka 2022 kutokana na kutokamilika kwa ujenzi wa skimu za umwagiliaji. Aidha, skimu mpya za umwagiliaji zilizoanza kujengwa zilifikia 22 (Skimu la bonde la Eyasi - Arusha, Lyamalagwa - Tabora, Magurukenda - Mwanza, Sukuma - Mwanza, Kongogo-Dodoma, Ulyanyama-Tabora, Membe Scheme - Dodoma, Mahiga Mwanza, Msesule - Mbeya, Rudewa - Morogoro, Rabour - Mara, Mkombozi I, II, III, IV - Iringa, Makwale - Mbeya, Ibanda - Geita , Ilemba - Rukwa , Mandaka Mnono - Kilimanjaro, Kasoli - Simiyu, Luiche - Kigoma, Kalupale - Tabora, Katunguru - Mwanza, Tlawi - Manyara, na Msingi - Singida) kati ya 25 zilizopangwa mwaka 2023. Kwa wastani ujenzi wa skimu hizo umefikia asilimia 40. Vile vile, jumla ya skimu 19 kati ya 30 zilianza kukarabatiwa ikilinganishwa na skimu 17 kati ya 30 zilizopangwa kukarabatiwa mwaka 2022.

177. Mwaka 2023, vyama vya umwagiliaji vilivyosajiliwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji viliongezeka kwa asilimia 53.9 na kufikia 631 kutoka vyama 410 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa uhamasishaji na utoaji wa mafunzo kuhusu umuhimu wa kujisajili katika vyama vya umwagiliaji.

**MIFUGO**

**Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake**

178. Mwaka 2023, idadi ya mifugo nchini ikijumuisha ng’ombe, mbuzi, kuku, nguruwe na kondoo ilikadiriwa kufikia milioni 181.9 ikilinganishwa na mifugo milioni 173.9 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 4.6. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali na wadau katika kuendelea kuimarisha afya za mifugo kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo: kujenga majosho pamoja na kutoa ruzuku, hususan kwenye dawa za kuogeshea

mifugo; kuongeza uzalishaji na usambazaji wa chanjo; kuimarisha elimu ya uzalishaji wa malisho kwa wafugaji kupitia mashamba darasa ya malisho na uhamasishaji wa utengaji wa maeneo ya malisho; utoaji wa elimu ya ufugaji wa kibiashara; na uboreshaji wa mbari za mifugo.

**Jedwali Na. 7.8: Idadi ya Mifugo Mwaka 2019 - 2023 (Milioni)**

| **Aina ya Mifugo** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ng'ombe | 32.2 | 33.9 | 35.3 | 36.6 | 37.9 | 3.6 |
| Mbuzi | 20 | 24.5 | 25.6 | 26.6 | 27.6 | 3.8 |
| Kondoo | 5.5 | 8.5 | 8.8 | 9.1 | 9.4 | 3.3 |
| Nguruwe | 2.0 | 3.2 | 3.4 | 3.7 | 3.9 | 5.4 |
| Kuku | 79.1 | 87.7 | 92.8 | 97.9 | 103.1 | 5.3 |
| **Jumla** | **138.8** | **157.8** | **165.9** | **173.9** | **181.9** | **4.6** |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

179. Mwaka 2023, uzalishaji wa nyama ulikuwa tani 803,264.3 ikilinganishwa na tani 769,966.5 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Aidha, mayai milioni 5,500.0 yalizalishwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mayai milioni 4,949.8 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Vile vile, uzalishaji wa maziwa uliongezeka kwa asilimia 5.1 na kufikia lita milioni 3,600 mwaka 2023 ikilinganishwa na lita milioni 3,426 mwaka 2022. Ongezeko la uzalishaji wa mazao ya mifugo lilitokana na: jitihada za Serikali katika kutoa elimu ya ufugaji bora wa kibiashara; kuimarika kwa upatikanaji wa mbegu bora za ng'ombe wa maziwa katika mashamba ya Serikali; na kufutwa kwa tozo ya uingizaji wa ng'ombe wazazi kutoka nje ya nchi.

180. Mwaka 2023, lita milioni 77.9 za maziwa zilisindikwa ikilinganishwa na lita milioni 77.6 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa viwanda vya maziwa kutoka viwanda 111 mwaka 2022 hadi viwanda 152 mwaka 2023 pamoja na kuongezeka kwa vituo vya kukusanyia maziwa kutoka 238 mwaka 2022 hadi vituo 246 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 7.9: Uzalishaji wa Mazao ya Mifugo Mwaka 2019 - 2023**

| Aina ya Zao | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Uzalishaji Maziwa (Lita 000")** | | | | | |
| Ng'ombe wa Asili | 1,874,923 | 2,101,789 | 2,170,461 | 2,287,887 | 2,400,000 |
| Ng'ombe wa Kisasa | 803,538 | 900,766 | 930,923 | 1,138,331 | 1,200,000 |
| **Jumla** | **2,678,461** | **3,002,555** | **3,101,384** | **3,426,218** | **3,600,000** |
| **Uzalishaji Nyama (Tani)** | | | | | |
| Ng'ombe | 506,798 | 486,736 | 508,355 | 526,351 | 544,983.8 |
| Mbuzi na kondoo | 110,563 | 95,964 | 102,137 | 107,791 | 113,781.8 |
| Nguruwe | 23,140 | 38,377 | 41,468 | 44,420 | 47,583.1 |
| Kuku | 41,000 | 80,601 | 86,206 | 91,404 | 96,915.6 |
| **Jumla** | **681,501** | **701,678** | **738,166** | **769,966** | **803,264.3** |
| **Uzalishaji Mayai ('000')** | | | | | |
| Mayai | 3,575,621 | 4,051,179 | 4,510,345 | 4,949,772 | 5,500,000 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

181. Mwaka 2023, tani 53,508 za vipande vya ngozi zilizalishwa ikilinganishwa na tani 53,256 zilizozalishwa mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na wafugaji kuendelea kupata elimu ya ufugaji wa kisasa na kibiashara kwa ajili ya soko la ndani na nje pamoja na mafunzo yaliyotolewa kwa wachunaji na wapanga madaraja ya ngozi.

**Jedwali Na. 7.10: Uzalishaji wa Ngozi Mwaka 2019 - 2023 (Tani)**

| Mwaka | Ngozi za Ng'ombe | Ngozi za Mbuzi na Kondoo | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2019 | 14,449 | 24,503 | 38,952 |
| 2020 | 14,510 | 24,648 | 39,158 |
| 2021 | 20,340 | 30,773 | 51,113 |
| 2022 | 21,180 | 32,076 | 53,256 |
| 2023 | 21,168 | 32,340 | 53,508 |

**Chanzo**: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Biashara ya Mifugo na Mazao yake**

182. Mwaka 2023, ng'ombe 2,957,724, mbuzi 2,554,266 na kondoo 273,982 wenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 3,478.4 waliuzwa katika soko la ndani ikilinganishwa na ng'ombe 2,194,937, mbuzi 1,879,623, na kondoo 201,610 wenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 1,741.0 mwaka 2022, sawa na ongezeko la thamani kwa asilimia 99.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mifugo katika viwanda vya kuchakata na kusindika nyama pamoja na kuimarishwa kwa miundombinu ya minada ya mifugo.

183. Mwaka 2023, idadi ya mifugo hai iliyouzwa nje ya nchi ilikuwa ng'ombe 20,536, mbuzi na kondoo 37,157 wenye thamani ya shilingi bilioni 44.4 ikilinganishwa na ng'ombe 23,356, mbuzi na kondoo 39,951 wenye thamani ya shilingi bilioni 62.4 mwaka 2022, sawa na upungufu wa thamani wa asilimia 28.8. Kupungua kwa thamani na kiwango cha mauzo ya mifugo hai nje ya nchi kulitokana na ongezeko la uzalishaji kwa viwanda vya ndani vya

kuchakata na kusindika nyama kwa ajili ya kuuza nje ya nchi pamoja na Serikali kuongeza jitihada za kutafuta masoko mapya ya nyama nje ya nchi ikiwemo Hong Kong, Vietnam, Kuwait, Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu (Dubai), Oman, Jordan, Bahrain, Kenya na Comoro.

**Jedwali Na. 7.11: Mwenendo wa Biashara ya Mifugo na Mazao ya Mifugo Mwaka 2019 - 2023**

| **Soko la ndani** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Ng'ombe** | **Kondoo** | **Mbuzi** | **Punda** | **Jumla** | **Thamani (Shilingi Bilioni)** |
| 2019 | 1,427,212 | 122,390 | 1,062,324 | * | 2,611,926 | 947.4 |
| 2020 | 1,023,200 | 205,161 | 987,867 | * | 2,216,228 | 865 |
| 2021 | 1,843,904 | 360,745 | 2,081,233 | 191,656 | 4,477,538 | 1,531 |
| 2022 | 2,194,937 | 201,610 | 1,879,623 | * | 4,276,170 | 1,741 |
| 2023 | 2,957,724 | 273,982 | 2,554,266 | * | 5,785,972 | 3,478 |
| **Soko la nje** | | | | | | |
| **Mwaka** | **Ng'ombe** | **Kondoo na Mbuzi** | | | **Jumla** | **Thamani (Shilingi Bilioni)** |
| 2019 | 11,670 | 44,79 | | | 56,460 | 22.9 |
| 2020 | 3,574 | 49,18 | | | 52,758 | 1.9 |
| 2021 | 24,014 | 106,09 | | | 130,113 | 46.6 |
| 2022 | 23,356 | 39,952 | | | 63,307 | 62.4 |
| 2023 | 20,536 | 37,157 | | | 57,693 | 44.4 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi
*Haikuuzwa

184. Mwaka 2023, mauzo ya nyama nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 41.1 na kufikia tani 14,701.2 zenye thamani ya shilingi bilioni 220.52 (dola za Marekani milioni 86.31) ikilinganishwa na tani 10,416.0 za nyama zenye thamani ya shilingi bilioni 98.9 (dola za Marekani milioni 42.5) mwaka 2022. Kati ya mauzo hayo, nyama ya ng'ombe ilikuwa tani 467.01, nyama ya mbuzi tani 10,263.4, nyama ya kondoo tani 3,767.2, nyama ya kuku tani 25.7, nyama ya nguruwe tani 5.5 na tani 172.5 za nyama nyingine. Kuongezeka kwa mauzo ya nyama nje ya nchi kulitokana na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji pamoja na kuimarika kwa masoko ya nyama katika nchi za Hong Kong, Vietnam, Kuwait, Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu (Dubai), Oman, Jordan, Bahrain, Kenya na Comoro.

185. Mwaka 2023, tani 4,933 za vipande vya ngozi ziliuzwa nje ya nchi katika nchi za Nigeria, Ghana, Togo na Pakistan ikilinganishwa na tani 7,472 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, mauzo ya vipande vya ngozi yalikuwa na thamani ya shilingi bilioni 6.11

ikilinganishwa na shilingi bilioni 10.05 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 39.2. Hii ilisababishwa na baadhi ya wafanyabiashara kusitisha usafirishaji wa ngozi kwenda Nigeria kutokana na uchaguzi mkuu katika nchi hiyo ambayo inachukua zaidi ya asilimia 90 ya ngozi zinazouzwa nje ya nchi.

**Jedwali Na. 7.12: Uuzaji wa Ngozi Nje ya Nchi (Tani) Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Ngozi za Ng'ombe | Ngozi za Mbuzi na Kondoo | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2019 | 2,951 | 166 | 3,117 |
| 2020 | 3,020 | 161 | 3,181 |
| 2021 | 7,251 | 120 | 7,371 |
| 2022 | 6,691 | 781 | 7,472 |
| 2023 | 4,511 | 422 | 4,933 |

**Chanzo**: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Uzalishaji wa Chanjo za Mifugo**

186. Mwaka 2023, Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania - TVLA ulizalisha na kusambaza dozi milioni 67.46 za chanjo katika Halmashauri zote nchini ikilinganishwa na dozi milioni 66.59 zilizozalishwa na kusambazwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 1.3. Kati ya chanjo hizo, dozi 64,211,230 zilikuwa dhidi ya ugonjwa wa mdondo, dozi 437,550 (kimeta), dozi 137,110 (chambavu), dozi 2,124,220 (mapafu ya ng'ombe), dozi 2,350 (ugonjwa wa kutupa mimba), dozi 179,630 (mapafu ya mbuzi), na dozi 366,500 (kimeta na chambavu). Ongezeko la uzalishaji wa chanjo lilitokana na ununuzi wa mashine na vifaa vya kisasa vya kuzalisha chanjo katika Taasisi ya Chanjo Tanzania - TVI na kuongezeka kwa mahitaji ya chanjo kufuatia juhudi za Serikali katika kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa kuchanja mifugo.

**Uzalishaji wa Malisho na Utengenezaji wa Vyakula vya Mifugo**

187. Mwaka 2023, mbegu bora za malisho zenye uzito wa kilogramu 22,691.65 zilizalishwa katika mashamba ya Serikali ikilinganishwa na kilogramu 4,481.9 zilizozalishwa mwaka 2022. Aidha, marobota 130,132 ya hei yalizalishwa katika mashamba ya Serikali mwaka 2023 ikilinganishwa na marobota 51,181 yaliyozalishwa mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha malisho na mbegu za malisho katika mashamba mawili (2) kwa kuweka mashine na zana muhimu. Kwa upande mwingine, marobota 118,077 ya hei yalizalishwa katika mashamba binafsi mwaka 2023 ikilinganishwa na marobota 60,000 yaliyozalishwa mwaka 2022.

188. Mwaka 2023, viwanda vya kuzalisha vyakula vya mifugo viliongezeka na kufikia 221 kutoka viwanda 199 mwaka 2022, sawa na ongezeko la viwanda vipya 22. Viwanda hivyo vilisajiliwa katika mikoa nane (8) kama ifuatavyo: Arusha viwanda vinne (4), Kilimanjaro (3), Dar es Salaam (4), Iringa (3), Pwani (3), Morogoro (2), Shinyanga (2), na

Mbeya (1). Kufuatia ongezeko la viwanda hivyo, jumla ya tani 1,580,000 za vyakula vya mifugo zilizalishwa na sekta binafsi mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 1,380,000 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.5. Aidha, Serikali ilikagua na kusajili maeneo 221 ya kuzalisha vyakula vya mifugo, maeneo 364 ya kuuzia vyakula vya mifugo na maeneo 73 ya kuhifadhi vyakula vya mifugo mwaka 2023 ikilinganishwa na maeneo 198 ya kuzalisha vyakula vya mifugo, maeneo 321 ya kuuzia vyakula vya mifugo na maeneo 60 ya kuhifadhi vyakula vya mifugo mwaka 2022. Ongezeko la maeneo yaliyokaguliwa lilitokana na juhudi za Serikali za kuhakikisha upatikanaji wa vyakula vya mifugo vyenye ubora na viwango stahiki pamoja na utoaji wa mafunzo kwa wakaguzi 212 kuhusu mfumo wa utoaji wa Vibali vya Kielektroniki - MIMIS.

**Mafunzo ya Mifugo**

189. Mwaka 2023, Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo ulidahili wanafunzi 4,452 katika ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na wanafunzi 4,136 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.6. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga jumla ya kumbi nne (4) za mihadhara katika kampasi za Mpwapwa (ukumbi mmoja), Mabuki (2) na Morogoro (1) pamoja na ujenzi wa jumla ya hosteli mbili (2) katika kampasi za Mpwapwa (1) na Morogoro (1). Katika kipindi hicho, Wakala ilitoa mafunzo kwa wafugaji 3,254 kuhusu mbinu bora za uzalishaji wa mifugo na malisho ikilinganishwa na wafugaji 2,816 waliopatiwa mafunzo mwaka 2022.

**Utafiti wa Mifugo**

190. Mwaka 2023, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania - TALIRI ilifanya tafiti 87 kuhusu uboreshaji wa mbari za mifugo, uendelezaji wa malisho, uzalishaji wa mbegu bora za malisho na ushiriki wa wanawake na vijana katika shughuli za ufugaji ikilinganishwa na tafiti 70 zilizofanyika mwaka 2022. Tafiti hizo ziliwezesha uzalishaji na usambazaji wa ng’ombe chotara wa nyama na maziwa 191 na mbuzi chotara 77 katika Halmashauri za Bahi, Mpwapwa, Kongwa, Morogoro, Muheza, Tanga Jiji, Mbeya Jiji, Mkuranga, Dodoma Jiji, Kisarawe, Ilala, Arumeru na Longido ikilinganishwa na ng’ombe chotara 109 na mbuzi chotara 221 waliozalishwa mwaka 2022.

191. Mwaka 2023, kilogramu 5,298 za mbegu bora za malisho zilizalishwa na kusambazwa na TALIRI ikilinganishwa na kilogramu 4,000.1 za mbegu zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 32.4. Ongezeko hilo lilitokana na uboreshaji wa mitambo na ununuzi wa vifaa shamba. Mbegu hizo zilisambazwa katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Kilimanjaro, Shinyanga, Dodoma, Tanga, Simiyu, Mara, Mwanza, Morogoro, Manyara na Arusha.

**Huduma za Ugani katika Mifugo**

192. Mwaka 2023, Serikali ilitoa mafunzo rejea ya ufugaji bora kwa maafisa ugani 515 wa sekta ya umma na sekta binafsi ikilinganishwa na maafisa ugani 580 mwaka 2022. Kati ya hao, maafisa ugani 28 walitoka sekta binafsi na maafisa 487 walitoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kipindi hicho, Serikali ilisajili jumla ya maafisa ugani 3,201 na wafugaji 752 kwenye mfumo wa M-Kilimo ikilinganishwa na maafisa ugani 3,018 na wafugaji 2,149 mwaka 2022. Aidha, Serikali iliendelea kuboresha utoaji wa huduma za ugani kwa kugawa pikipiki 948 kwa maafisa ugani katika mikoa 26 ikilinganishwa na pikipiki 300 mwaka 2022.

**UVUVI**

**Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi**

193. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kusimamia na kudhibiti rasilimali za uvuvi kulikowezesha kukamatwa kwa vifaa na zana mbalimbali zilizotumika katika uvuvi haramu (**Jedwali Na. 7.12**). Katika kudhibiti uvuvi haramu, samaki wachanga waliokamatwa walikuwa kilogramu 8,112, kaa wachanga kilogramu 47, kambamiti kilogramu 100 na mabondo kilogramu 11. Katika kipindi hicho, watuhumiwa 1,070 wa uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira walikamatwa na kulipa faini ya shilingi milioni 560.5 ikilinganishwa na watuhumiwa 1,552 na faini ya shilingi milioni 531.1 mwaka 2022.

**Jedwali Na. 7.13: Vifaa na Zana Zilizokamatwa katika Uvuvi Haramu**

| Na. | Zana Zilizokamatwa | Mwaka | |
|---|---|---|---|
| | | **2022** | **2023** |
| 1. | Nyavu za makila | 2,988 | 176 |
| 2. | Kokoro | 2,268 | 416 |
| 3. | Nyavu za timba | 11,284 | 3,842 |
| 4. | Nyavu za dagaa | 443 | 10 |
| 5. | Vyandarua | 42 | 0 |
| 6. | Pikipiki | 0 | 4 |
| 7. | Magari | 0 | 1 |
| 8. | Kamba za kokoro (mita) | 290,133 | 362,509 |
| 9. | Nyavu za gonga | 1 | 0 |
| 10. | Boti | 60 | 17 |
| 11. | Mitumbwi | 380 | 432 |
| 12. | Injini za boti | 70 | 80 |
| 13. | Kasia | 02 | 02 |
| 14. | Kipe | 1 | 0 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Ukuzaji Viumbe Maji**

194. Mwaka 2023, kulikuwa na wakuzaji viumbe maji 34,057 ikilinganishwa na wakuzaji viumbe maji 31,998 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.4. Aidha, mabwawa ya kufugia samaki yaliongezeka kwa asilimia 4.7 na kufikia 32,878 mwaka 2023 kutoka mabwawa 31,407 mwaka 2022. Vile vile, vizimba vya kuzalishia samaki katika maziwa na malambo viliongezeka kwa asilimia 27.3 na kufikia vizimba 993 ikilinganishwa na vizimba 780 mwaka 2022. Kati ya hivyo, vizimba 911 vilikuwa katika Ziwa Victoria, vizimba vitatu (3) Ziwa Tanganyika na vizimba 79 katika malambo mbalimbali.

195. Mwaka 2023, vifaranga vya samaki 35,967,180 vilizalishwa ikilinganishwa na vifaranga 29,295,638 vilivyozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 22.8. Kati ya hivyo, vifaranga 4,069,172 vilizalishwa na taasisi za umma na vifaranga 31,898,008 vilizalishwa na vituo vya sekta binafsi. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya vifaranga na uwekezaji wa wadau wa ukuzaji viumbe maji. Katika kipindi hicho, tani 4,337.9 za chakula cha samaki zilitumika ikilinganishwa na tani 2,156.1 mwaka 2022. Kati ya hizo, tani 1,325.2 zilizalishwa nchini na tani 3,012.7 ziliagizwa kutoka nje ya nchi. Kwa upande mwingine, wananchi 8,788 walipata mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji wa samaki na udhibiti wa magonjwa mwaka 2023 ikilinganishwa na wananchi 7,884 mwaka 2022.

**Jedwali Na. 7.14: Idadi ya Wakuzaji Viumbe Maji, Mabwawa, Vizimba na Vifaranga Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Idadi ya Wakuzaji Viumbe Maji | Idadi ya Mabwawa ya Samaki | Idadi ya Vizimba | Idadi ya Vifaranga |
|---|---:|---:|---:|---:|
| 2019 | 26,474 | 26,445 | 408 | 21,173,226 |
| 2020 | 28,009 | 27,979 | 431 | 21,676,187 |
| 2021 | 30,064 | 30,032 | 473 | 27,120,320 |
| 2022 | 31,998 | 31,407 | 780 | 29,295,638 |
| 2023 | 34,057 | 32,878 | 993 | 35,967,180 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

196. Mwaka 2023, uzalishaji wa samaki (sato na kambale) ulikuwa tani 29,106.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 235 ikilinganishwa na tani 25,286.5 zenye thamani ya shilingi bilioni 177.0 mwaka 2022, sawa na ongezeko la uzalishaji la asilimia 15.1. Aidha, uzalishaji wa mwani ulikuwa tani 4,379.1 zenye thamani ya shilingi bilioni 4.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 3,514.8 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.7 mwaka 2022, sawa na ongezeko la uzalishaji la asilimia 24.6. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa jitihada za Serikali katika kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za ukuzaji viumbe maji pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

**Jedwali Na. 7.15: Mwenendo wa Ukuzaji Viumbe Maji Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Samaki (Sato na Kambale) (Tani) | Samaki Maji Chumvi - Mwatiko (Tani) | Mwani (Tani) | Kambamiti (Tani) | Kambakoche (Tani) | Kaa (Kilogramu) | Uzalishaji wa Majongoo Bahari (Kilogramu) | Lulu (Vipande) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2019 | 18,073.6 | - | 1,449.0 | 336 | - | - | - | 550 |
| 2020 | 18,716.6 | - | 1,410.0 | 73.6 | - | - | - | 164 |
| 2021 | 20,258.0 | - | 2,438.0 | 97 | - | 410 | 115 | 360 |
| 2022 | 25,286.5 | 6 | 3,514.8 | 74.85 | 30 | 1,144 | 370 | 164 |
| 2023 | 29,106.6 | - | 4,379.1 | - | 30 | 600 | 860 | 550 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Uvunaji wa Samaki**

197. Mwaka 2023, uvunaji wa samaki uliongezeka kwa asilimia 1.8 na kufikia tani 479,976.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 3,359.8 ikilinganishwa na tani 471,512 zenye thamani ya bilioni 3,159.1 mwaka 2022. Kati ya hizo, tani 415,879.6 zilivunwa katika maji baridi na tani 64,097.0 zilivunwa katika maji chumvi. Ongezeko la uvunaji wa samaki lilitokana na kuimarika kwa usimamizi na udhibiti wa vitendo vya uvuvi haramu.

**Jedwali Na. 7.16: Mwenendo wa Uvunaji wa Samaki (Tani) Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Maji baridi | Maji chumvi | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2019 | 409,333 | 60,977 | 470,309 |
| 2020 | 409,828 | 63,764 | 473,592 |
| 2021 | 414,104 | 62,914 | 477,018 |
| 2022 | 404,639 | 66,873 | 471,512 |
| 2023 | 415,880 | 64,097 | 479,977 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

198. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa kufanya kaguzi 7,023 ikilinganishwa na kaguzi 7,321 zilizofanyika mwaka 2022. Kaguzi hizo zilifanyika katika viwanda 38 vikubwa na vya kati vya kuchakata samaki, mialo 124, masoko manne (4), ghala 90 na vyombo vya kusafirisha mazao ya uvuvi 1,904. Aidha, vibali 4,901 vilitolewa kwa wafanyabiashara wa ndani kwa ajili ya uuzaji wa tani 39,452 za mazao ya uvuvi katika masoko ya ndani ikilinganishwa na vibali 5,194 vilivyotolewa kwa uuzaji wa tani 45,725.3 mwaka 2022. Vile vile, vyeti vya afya 9,672 vilitolewa kwa wafanyabiashara kwa ajili ya uuzaji wa tani 42,592.0 za mazao ya uvuvi nje ya nchi ikilinganishwa na vyeti 4,260.0 vilivyotolewa kwa uuzaji wa tani 37,235.9 mwaka 2022.

199. Mwaka 2023, Maabara ya Taifa ya Uvuvi iliendelea kufanya uchunguzi wa kimaabara wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa ajili ya kulinda afya za walaji

katika soko la ndani na nje. Katika kipindi hicho, sampuli 2,725 zilifanyiwa uchunguzi ikilinganishwa na sampuli 4,023 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 32.3. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa uchakataji wa samaki viwandani na kupungua kwa wafanyabiashara wadogo wa kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi katika soko la ndani na nje. Kati ya sampuli zilizofanyiwa uchunguzi, sampuli 2,544, sawa na asilimia 93.4 zilikidhi viwango vya ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi kitaifa na kimataifa ikilinganishwa na asilimia 87.6 ya sampuli mwaka 2022.

**Mwenendo wa Uuzaji na Uagizaji wa Mazao ya Uvuvi Nje ya Nchi**

200. Mwaka 2023, tani 42,371.41 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 166,024 wenye thamani ya shilingi bilioni 509.91 waliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 37,235.9 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 208,744 wenye thamani ya shilingi bilioni 457.04 mwaka 2022. Ongezeko la mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi lilitokana na jitihada za Serikali kuendelea kudhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi. Mwaka 2023, mapato ya mrabaha yaliyotokana na mauzo ya mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo nje ya nchi yalikuwa shilingi bilioni 16.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 16.6 mwaka 2022. Mauzo hayo yalijumuisha tani 433.6 za mabondo zenye thamani ya shilingi bilioni 145.25 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 447.5 za mabondo zenye thamani ya shilingi bilioni 147.7 mwaka 2022. Aidha, mauzo ya mabondo nje ya nchi yaliwezesha upatikanaji wa mapato ya mrabaha yenye thamani ya shilingi bilioni 3.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 2.8 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 21.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei ya mabondo na kuendelea kuimarika kwa soko katika nchi ya China na Hong Kong.

201. Mwaka 2023, uagizaji wa samaki kutoka nje ya nchi uliongezeka kwa asilimia 14.5 na kufikia tani 9.5 zenye thamani ya shilingi milioni 269.8 ikilinganishwa na tani 8.3 zenye thamani ya shilingi milioni 268.4 mwaka 2022. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya samaki nchini, hususan katika hoteli za kitalii na kupungua kwa uvunaji wa samaki wa maji chumvi kulikosababishwa na ukosefu wa zana bora za uvuvi na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, mapato ya mrabaha yaliyotokana na uagizaji wa samaki kutoka nje ya nchi yalikuwa shilingi milioni 45.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi milioni 47.0 mwaka 2022.

**Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi**

202. Hadi Desemba 2023, kulikuwa na viwanda vikubwa vya samaki 21 na viwanda vidogo 29 ikilinganishwa na viwanda vikubwa 19 na vidogo 29 mwaka 2022. Viwanda vilivyoongezeka ni Lakestar na Aquaperch vilivyopo mkoani Mwanza. Aidha, kulikuwa na viwanda vya kati vitano (5) vya kutengeneza nyavu, kutengeneza boti vitatu (3), viwanda vya mabondo 17 na ghala 70 za kuhifadhia mazao ya uvuvi.

203. Mwaka 2023, Serikali kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu - MPRU iliendelea kusimamia shughuli za uhifadhi kwenye maeneo ya bahari ili kuvutia utalii na uwekezaji wa hoteli za kiikolojia. Katika kipindi hicho, wageni 42,696 walitembelea maeneo ya hifadhi za bahari ikilinganishwa na wageni 38,168 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.9. Aidha, mapato ya kiasi cha shilingi milioni 2,013.6 yalikusanywa kutokana na wageni waliotembelea maeneo ya hifadhi za bahari mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi milioni 1,504.7 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 33.8. Ongezeko la wageni na mapato lilitokana na mikakati ya Serikali ya kuongeza idadi ya watalii, hususan kupitia programu maalum ya *Tanzania the Royal Tour*, uhamasishaji wa utalii wa ndani, uwepo wa amani na utulivu nchini pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali za bahari ikiwemo matumbawe, nyasi bahari, samaki na wanyama wa baharini ambazo huvutia watalii wa ndani na nje ya nchi.

**Mafunzo ya Uvuvi**

204. Mwaka 2023, Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi - FETA ulidahili wanafunzi 1,222 ikilinganishwa na wanafunzi 1,227 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, wavuvi na wakuzaji viumbe maji 15,799 walipatiwa mafunzo rejea ikilinganishwa na wavuvi na wakuzaji viumbe maji 19,722 waliopatiwa mafunzo mwaka 2022. Mafunzo hayo yalihusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi, mbinu bora za ufugaji samaki, uanzishaji na uendeshaji wa vyama vya ushirika na udhibiti wa magonjwa. Aidha, wadau wa uvuvi 80,617 walipata elimu kuhusu sekta ya uvuvi pamoja na teknolojia mbalimbali wakati wa maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Siku ya Chakula Duniani na Siku ya Mvuvi Duniani ikilinganishwa na wadau 60,504 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 33.2. Vile vile, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu iliratibu mafunzo kwa vitendo - *BBT LIFE* kwa vijana 300 mwaka 2023 ikilinganishwa na vijana 200 mwaka 2022.

**MAENDELEO YA USHIRIKA**

205. Mwaka 2023, Idadi ya Vyama vya Ushirika ilikuwa 7,349 ikilinganishwa na Vyama 7,300 mwaka 2022. Kati ya hivyo, Vyama vya Masoko ya Mazao vilikuwa 4,279, Vyama vya Akiba na Mikopo 2,042, vyama vya aina nyingine 979 na Vyama Vikuu 49. Aidha, wanachama wa vyama ya ushirika waliongezeka na kufikia 8,400,304 mwaka 2023 kutoka wanachama 8,358,326 mwaka 2022. Vile vile, viwanda vya kuchakata mazao vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika vilikuwa 328 mwaka 2023 ikilinganishwa na viwanda 205 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 60. Ongezeko la wanachama na viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika lilitokana na uhamasishaji wa wadau kuhusu mafanikio ya ushirika kupitia vipindi na makala katika vyombo vya habari.

206. Mwaka 2023, Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliendelea kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa kuongeza ufanisi, uwazi na kuboresha utendaji.

Katika kipindi hicho, mafunzo ya awali na rejea yalitolewa kwa maafisa 104 na watendaji 1,243 wa Vyama vya Msingi na Vyama Vikuu. Aidha, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika - COASCO lilikagua hesabu za Vyama vya Ushirika 3,911 mwaka 2023 ikilinganishwa na Vyama 6,005 mwaka 2022. Kati ya hivyo, Vyama 479, sawa na asilimia 12.3 vilipata hati safi, vyama 2,475 (asilimia 63.3) vilipata hati yenye mashaka, vyama 830 (asilimia 21.2) vilipata hati chafu na vyama 127 (asilimia 3.3) vilipata hati isiyo na maoni.

## Jedwali Na. 38: UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI

| Msimu[1] | Miwa | | | | Sukari | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wakulima | | Jumla (000 Tani) | Bei[2] (Sh./Tani) | Iliyozalishwa Tani | iliyotumika[3] Jumla Tani | Kilo kwa kila mtu[4] |
| | Umma (000 Tani) | Binafsi (000 Tani) | | | | | |
| 2005/06 | 1,545 | 956 | 2,501 | 22,383 | 263,317 | 343,292 | 12.0 |
| 2006/07 | 1,430 | 611 | 2,041 | 29,000 | 192,095 | 366,708 | 12.0 |
| 2007/08 | 1,967 | 799 | 2,766 | 32,767 | 265,434 | 382,518 | 13.0 |
| 2008/09 | 2,056 | 693 | 2,749 | 32,771 | 279,850 | 396,113 | 13.4 |
| 2009/10 | 1,972 | 598 | 2,570 | 42,046 | 263,461 | 398,070 | 13.7 |
| 2010/11 | 2,357 | 661 | 3,018 | 43,865 | 304,135 | 410,259 | 12.0 |
| 2011/12 | 2,036 | 680 | 2,716 | 48,833 | 262,879 | 439,307 | 12.0 |
| 2012/13 | 2,242 | 711 | 2,953 | 52,167 | 296,698 | 468,000 | 12.0 |
| 2013/14 | 2,198 | 602 | 2,800 | 50,500 | 294,300 | 434,782 | 12.0 |
| 2014/15 | 2,466 | 697 | 3,163 | 51,333 | 304,007 | 511,680 | 12.0 |
| 2015/16 | 2,270 | 569 | 2,839 | 59,707 | 293,075 | 525,784 | 12.0 |
| 2016/17 | 2,504 | 557 | 3,061 | 72,667 | 324,930 | 456,000 | 12.8 |
| 2017/18 | 2,550 | 626 | 3,175 | 72,667 | 303,752 | 515,004 | 13.5 |
| 2018/19 | 2,792 | 797 | 3,589 | 72,667 | 359,219 | 524,772 | 13.5 |
| 2019/20 | 2,659 | 728 | 3,387 | 77,333 | 311,358 | 372,787 | 12.8 |
| 2020/21 | 2,985 | 1,092 | 4,014 | 79,000 | 367,718 | - | 12.0 |
| 2021/22 | 2,697 | 1,060 | 3,757 | 77,500 | 379,281 | 379,281 | 12.0 |
| 2022/23 | 3,396 | 1,046 | 4,442 | 78,375 | 460,049 | 460,049 | 12.0 |
| **Badiliko 2021/22-2022/23 (Asilimia)** | **25.91** | **-1.28** | **18.24** | **1.13** | **21.30** | **21.30** | **0.00** |

**Chanzo:** Bodi ya Sukari Tanzania

1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni
2 Bei ya Mimea ni ile iliyo na asilimia 10 za Sucrose
3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar
4 Ni kwa Tanzania bara
* Sukari yote huzalishwa na wakulima/mashirika binafsi
- sukari yote iliyozalishwa imetumika Tanzania Bara

## Jedwali Na. 39: PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

| Msimu [1] | Pamba yenye mbegu | | | | | Pamba iliyoondolewa mbegu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uzalishaji (Tani) | | | Bei ya wastani (Shilingi/kilogramu) | | Kiasi (Tani) | | | Mauzo nchini | | |
| | | | | | | | | | Kiasi (tani) | Bei ya wastani (Shilingi/tani) | |
| | AR | BR | Jumla | AR | BR | AR | BR | Jumla | Jumla [2] | AR | BR |
| 2005/06 | 376,591 | - | 376,591 | 220 | .. | 126,228 | .. | 126,228 | .. | .. | .. |
| 2006/07 | 130,585 | - | 130,585 | 350 | .. | 43,770 | .. | 43,770 | .. | .. | .. |
| 2007/08 | 200,662 | - | 200,662 | 450 | .. | 70,773 | .. | 70,773 | 37,488 | .. | .. |
| 2008/09 | 368,697 | - | 368,697 | 480 | .. | 123,582 | .. | 123,582 | 66,554 | .. | .. |
| 2009/10 | 267,644 | - | 267,644 | 480 | .. | 54,851 | .. | 54,851 | .. | .. | .. |
| 2010/11 | 163,518 | - | 163,518 | 900 | .. | 54,809 | .. | 54,809 | .. | .. | .. |
| 2011/12 | 225,938 | - | 225,938 | 1,000 | .. | 75,731 | .. | 75,731 | .. | .. | .. |
| 2012/13 | 351,156 | - | 351,156 | 660 | .. | 117,702 | .. | 117,702 | .. | .. | .. |
| 2013/14 | 245,815 | - | 245,815 | 700 | - | 82,394 | .. | 82,394 | .. | .. | .. |
| 2014/15 | 202,312 | - | 202,312 | 750 | - | 67,812 | .. | 67,812 | | | .. |
| 2015/16 | 149,765 | - | 149,765 | 800 | - | 50,199 | .. | 50,199 | 525,784 | 12 | .. |
| 2016/17 | 132,934 | - | 132,934 | 1,000 | - | 42,203 | .. | 42,203 | - | - | - |
| 2017/18 | 222,790 | - | 222,790 | 1,100 | - | 80,575 | .. | 80,575 | 39,244 | 3,667 | .. |
| 2018/19 | 348,901 | - | 348,901 | 1,200 | - | 129,408 | .. | 129,408 | 51,942 | 3,123 | |
| 2019/20 | 348,958 | - | 348,958 | 1,200 | | 128,660 | .. | 128,660 | 25,162 | 3,781 | .. |
| 2020/21 | 122,836 | - | 122,836 | 900 | - | 46,923 | .. | 46,923 | 9,479 | 2,924 | .. |
| 2021/22 | 144,792 | | 144,792 | 1,800 | - | 67,178 | .. | 67,178 | 14,779 | 2,761 | |
| 2022/23 | 282,163 | | 282,163 | 1,150 | - | 108,633 | .. | 108,633 | 11,950 | 1,952 | |
| **Badiliko (Asilimia) 2021/22-2022/23** | | | **94.9** | **-36.1** | | **61.7** | | **61.7** | **-19.1** | **-29.3** | |

**Chanzo:** Bodi ya Mauzo ya Pamba

[1]Msimu ni kati ya Juni na Mei

Takwimu hazikupatikana

Pamba ya Tanzania hainunuliwi wala kuuzwa katika madaraja kwa sasa

**Jedwali Na. 40: ENEO LILILOPANDWA CHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA**

| Msimu [1] | Eneo lililopandwa (Hekta) | | | Majani Mabichi yaliyopatikana (Tani) | | | | | | Bei kwa Mkulima (Shs/Kilo) | Mauzo Nchini[2] (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Kiumilikaji: mashamba | | | Kikanda: mashamba | | | | |
| | Makubwa | Madogo | Jumla | Makubwa | Madogo | Jumla | Kaskazini | Kusini | Jumla | | |
| 2005/06 | 11,310 | 10,977 | 22,287 | 91,337 | 31,881 | 123,218 | 29,046 | 94,172 | 123,218 | 93 | 3,881 |
| 2006/07 | 11,271 | 11,956 | 23,227 | 109,632 | 49,024 | 158,656 | 39,673 | 118,983 | 158,656 | 100 | 4,737 |
| 2007/08 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 97,310 | 51,160 | 148,470 | 33,456 | 115,015 | 148,471 | 111 | 4,253 |
| 2008/09 | 11,271 | 11,449 | 22,722 | 100,644 | 41,167 | 141,811 | 31,677 | 110,134 | 141,811 | 118 | 4,464 |
| 2009/10 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 106,021 | 44,716 | 150,737 | 33,309 | 117,428 | 150,737 | 124 | 5,084 |
| 2010/11 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 95,511 | 47,616 | 143,127 | 112,368 | 30,759 | 143,127 | 152 | 6,065 |
| 2011/12 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 88,582 | 52,359 | 140,941 | 27,009 | 113,932 | 140,941 | 200 | 4,839 |
| 2012/13 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 113,628 | 54,872 | 168,500 | 30,997 | 137,503 | 168,500 | 206 | 5,498 |
| 2013/14 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 101,489 | 47,001 | 148,490 | 27,935 | 120,555 | 148,490 | 225 | 5,672 |
| 2014/15 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 100,018 | 52,467 | 152,485 | 23,283 | 129,202 | 152,485 | 176 | 6,302 |
| 2015/16 | 11,272 | 11,449 | 22,721 | 96,759 | 44,605 | 141,364 | 25,413 | 115,915 | 141,328 | 230 | 10,257 |
| 2016/17 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 78,929 | 41,495 | 120,424 | 20,592 | 99,832 | 120,424 | 285 | 4,648 |
| 2017/18 | 11,322 | 11,705 | 23,028 | 97,428 | 55,620 | 153,048 | 31,599 | 121,449 | 153,048 | 299 | 5,434 |
| 2018/19 | 11,322 | 11,705 | 23,027 | 104,203 | 61,081 | 165,284 | 36,506 | 128,778 | 165,284 | 312 | 3,926 |
| 2019/20 | 12,445 | 11,030 | 23,475 | 76,028 | 53,188 | 129,216 | 22,930 | 106,286 | 129,216 | 312 | 27,128 |
| 2020/21 | 12,445 | 11,361 | 23,806 | 72,138 | 51,655 | 123,793 | 25,178 | 98,614 | 123,792 | 312 | 28,875 |
| 2021/22 | 12,445 | 11,361 | 23,806 | 73,030 | 54,203 | 127,233 | 25,872 | 101,361 | 127,233 | 314 | 4,312 |
| 2022/23 | 12,445 | 11,361 | 23,806 | 58,729 | 45,209 | 103,938 | 16,735 | 87,203 | 103,938 | 366 | 3,414 |
| **Badiliko 2022/23-2021/22 (Asilimia)** | **0.0** | **0.0** | **0.0** | **-19.6** | **-16.6** | **-18.3** | **-35.3** | **-14.0** | **-18.3** | **16.6** | **-20.8** |

**Chanzo:** Bodi ya Chai Tanzania
1Msimu ni kati ya Julai na Juni
2 Chai iliyotengenezwa

## Jedwali Na. 41: KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

| Msimu[1] | Iliyonunuliwa (Tani) | | | | Bei (Shilingi/Kilogramu) | | | Mauzo nchini[+] | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Arabica | | Robusta | Jumla | Arabica | | Robusta | Kiasi | Thamani |
| | Laini | Ngumu | | | Laini | Ngumu | Maganda | (Tani) | (Shs '000) |
| 2005/06 | 24,116 | 1,362 | 8,856 | 34,334 | 1,200.0 | 420.0 | 270.0 | 33,300.0 | 793,042.5 |
| 2006/07 | 33,345 | 2,417 | 19,076 | 54,838 | 2,840.0 | 1,796.0 | 1,616.0 | 548.4 | 129,867.5 |
| 2007/08 | 26,330 | 1,588 | 15,606 | 43,524 | 2,995.0 | 1,875.0 | 1,734.0 | 43,523.0 | 89,099.3 |
| 2008/09 | 37,207 | 1,727 | 29,643 | 68,577 | 2,887.0 | 2,172.0 | 1,836.0 | 68,577.0 | 165,615.6 |
| 2009/10 | 22,217 | 915 | 11,467 | 34,599 | 3,988.0 | 2,475.0 | 1,563.0 | 34,599.0 | 108,741.1 |
| 2010/11 | 30,309 | 2,013 | 24,348 | 56,670 | 4,500.0 | 1,300.0 | 1,200.0 | 56,670.0 | 264,143.6 |
| 2011/12 | 20,775 | 941 | 11,590 | 33,306 | 8,144.4 | 5,436.4 | 3,276.9 | 33,306.0 | 212,292.6 |
| 2012/13 | 33,204 | 1,655 | 36,150 | 71,009 | 4,850.0 | 3,600.0 | 3,200.0 | 71,009.0 | 281,781.8 |
| 2013/14 | 28,212 | 1,115 | 18,875 | 48,202 | 4,314.0 | 3,272.9 | 3,074.6 | 48,202.0 | 183,708.9 |
| 2014/15 | 26,335 | 810 | 18,788 | 45,933 | 5,848.0 | 4,515.0 | 3,848.5 | - | - |
| 2015/16 | 21,517 | 460 | 17,526 | 39,503 | 7,249.6 | 5,943.4 | 4,092.9 | 39,503.0 | 105,760.8 |
| 2016/17 | 27,023 | 681 | 19,989 | 47,693 | 7,636.0 | 6,164.0 | 4,347.0 | 47,693.0 | 129,428.7 |
| 2017/18 | 36,551 | 633 | 11,897 | 43,193 | 2,980.0 | 2,980.0 | 2,980.0 | 43,193.3 | 116,587.3 |
| 2018/19 | 30,664 | 2,068 | 27,927 | 66,546 | 2,210.0 | 2,210.0 | 2,210.0 | 66,546.2 | 123,185.6 |
| 2019/20 | 31,380 | 883 | 27,056 | 59,318 | 5,472.0 | 3,815.0 | 3,180.0 | 59,318.0 | 261,088.6 |
| 2020/21 | 28,783 | 2,576 | 41,668 | 73,027 | 6,665.0 | 3,749.0 | 3,065.0 | 73,027.0 | 329,205.8 |
| 2021/22 | 37,414 | 1,776 | 27,353 | 66,523 | 8,783.4 | 4,535.0 | 4,093.8 | 66,543.0 | 469,647.0 |
| 2022/23 | 28,422 | 878 | 31,109 | 60,409 | 5,978 0 | 4,234 | 2,965 | 60,409.3 | 393,329.3 |
| **Badiliko (Asilimia) 2021/22-2022/23** | **(24.0)** | **(50.6)** | **13.7** | **(9.2)** | **(31.9)** | **(6.6)** | **(27.6)** | **(9.2)** | **(16.3)** |

**Chanzo:** Bodi ya Kahawa Tanzania
+Kahawa iliyosafishwa
1Msimu ni kati ya Julai na Juni
-Takwimu hazikupatikana

## Jedwali Na. 42: ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA

| Msimu[1] | Eneo (Hekta) | | | Katani iliyopatikana | | Mauzo nchini+ | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uliokomaa | Usiokomaa | Jumla | Kiasi (Tani) | Bei kwa Mkulima (shilingi/tani) | Kiasi (tani) | Thamani (Shilingi milioni) |
| 2009/10 | 30,556 | 11,849 | 42,405 | 24,092 | 1,200,000 | 12,761 | 10,375 |
| 2010/11 | 31,117 | 12,169 | 43,286 | 25,090 | 1,300,000 | 11,617 | 13,154 |
| 2011/12 | 32,601 | 14,302 | 46,902 | 36,600 | 1,500,000 | 11,511 | 14,390 |
| 2012/13 | 33,649 | 11,994 | 45,643 | 34,874 | 1,600,000 | 11,466 | 16,823 |
| 2013/14 | 35,266 | 11,044 | 46,310 | 37,805 | 1,724,864 | 9,160 | – |
| 2014/15 | 35,946 | 12,494 | 48,440 | 38,872 | 2,071,446 | 8,972 | 17,513 |
| 2015/16 | 34,723 | 13,231 | 47,954 | 41,795 | 2,700,000 | 9,075 | 20,342 |
| 2016/17 | 41,661 | 12,850 | 54,511 | 36,533 | 2,700,000 | 9,559 | 21,541 |
| 2017/18 | 40,635 | 14,389 | 55,024 | 43,280 | 3,000,000 | 12,111 | 30,803 |
| 2018/19 | 43,406 | 18,031 | 61,436 | 33,271 | 3,300,000 | 14,646 | 43,907 |
| 2019/20 | 41,757 | 17,044 | 58,801 | 35,341 | 3,500,000 | 12,646 | 38,323 |
| 2020/21 | 41,685 | 16,898 | 59,053 | 39,343 | 3,500,000 | 13,440 | 39,545 |
| 2021/22 | 45,505 | 21,687 | 67,192 | 48,359 | 3,626,139 | 12,428 | 45,065 |
| 2022/23 | 47,774 | 24,575 | 72,349 | 48,623 | 3,482,613 | 9,289 | 32,351 |
| **Badiliko (Asilimia) 2021/22-2022/23** | **5.0** | **13.3** | **7.7** | **0.5** | **(4.0)** | **(25.3)** | **(28.2)** |

**Chanzo:** Bodi ya Katani

Katani aina ya Line fibre, Tow na Flume Tow

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

## Jedwali Na. 43: MAUA YA PARETO YALIYONUNULIWA NA MAUZO YA BIDHAA ZA PARETO NCHINI

| Msimu[1] | Maua yaliyonunuliwa (Tani) | | | | Mauzo Nchini: Kiasi (Tani) | | | Mauzo Nchini: Thamani (Sh.'000) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kaskazini | Kusini | Jumla | Bei[2] (Shilingi/ Kilogramu) | Utomvu | Poda | Dawa | Utomvu | Poda | Dawa |
| 2009/10 | - | 1,780.0 | 1,780.0 | 1,500 | 57.0 | 69.0 | 1,035.0 | 37,361.0 | 1,473.0 | 248.0 |
| 2010/11 | - | 1,786.8 | 1,786.8 | 1,500 | 57.2 | 69.3 | 69.3 | 37,503.7 | 1,478.6 | 246.9 |
| 2011/12 | 0 | 5,700.0 | 5,700.0 | 1,700 | 82.0 | - | 750.0 | - | 204.0 | 360,919.0 |
| 2012/13 | 0 | 6,100.0 | 6,100.0 | 2,400 | 84.0 | - | 2,000.0 | - | - | 462,000.0 |
| 2013/14 | 34 | 2,691.8 | 2,726.2 | 2,000 | 90.0 | 60.0 | 830.0 | 6,900,000.0 | 160,500.0 | 233,000.0 |
| 2014/15 | 31 | 2,255.0 | 2,286.0 | 2,500 | 76.0 | 30.0 | 430.0 | 133.6 | 116,048.0 | 235,612.7 |
| 2015/16 | 25 | 1,987.0 | 2,012.4 | 2,100 | 59.9 | 6.0 | 480.0 | 9,450,000.0 | 30,240.0 | 282,240.0 |
| 2016/17 | 39 | 2,111.8 | 2,151.0 | 2,050 | 53.2 | 162.0 | 727.0 | 6,782,016.0 | 651,810.0 | 436,232.0 |
| 2017/18 | 43 | 2,355.9 | 2,400.0 | 2,500 | 16.0 | 204.0 | 700.0 | 13,932,947.0 | 869,418.1 | 390,864.0 |
| 2018/19 | 68 | 2,050.0 | 2,118.0 | 3,200 | - | - | - | 144,487.0 | 844,213.9 | 409,299.4 |
| 2019/20 | 69 | 2,441.0 | 2,510.0 | 2,500 | 60.0 | 83.0 | 137.8 | 13,600,000.0 | 420,000.0 | 353,000.0 |
| 2020/21r | 33 | 2,379.0 | 2,412.0 | 2,500 | 75.0 | 109.0 | 945.0 | 16,097,877.0 | 488,807.0 | 523,494.0 |
| 2021/22 | 50 | 2,644.0 | 2,694.0 | 3,200 | 67.0 | 156.0 | 810.0 | 12,419,041.0 | 701,605.0 | 514,409.0 |
| 2022/23* | 48 | 4,191 | 4,239 | 3,500 | 87.0 | 762 | 144 | 16,239,000.0 | 4,191,000.0 | 237,000.0 |
| **Badiliko (Asilimia) 2021/22-2022/23** | **-4.0** | **58.5** | **57.3** | **9.4** | **29.9** | **…** | **-82.2** | **30.8** | **…** | **-53.9** |

**Chanzo:** Bodi ya Pareto Tanzania
1Msimu ni kati ya Julai na Juni
2Bei ni kwa maua ya daraja la tano
-Takwimu hazikupatikana
*Takwimu hizi hadi December 2023, Msimu bado unaendelea
r Takwimu zimeboreshwa
… Ongezeko ni zaidi ya asilimia 100

## Jedwali Na. 44: UZALISHAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI MWAKA 2010 - 2023

| Mwaka | Maji Baridi | | | | Maji Chumvi | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya Vyombo | Idadi ya Wavuvi | Uzito (tani) | Thamani '000 (Shilingi) | Idadi ya Vyombo | Idadi ya Wavuvi | Uzito (tani) | Thamani '000 (Shilingi) | Idadi ya Vyombo | Idadi ya Wavuvi | Uzito (tani) | Thamani '000 (Shilingi) |
| 2010 | 141,206 | 47,635 | 294,474 | 684,844,020 | 36,321 | 7,664 | 52,683 | 89,639,934 | 177,527 | 55,299 | 347,157 | 774,483,954 |
| 2011 | 141,206 | 47,635 | 290,474 | 1,031,883,681 | 36,321 | 7,664 | 50,592 | 166,954,953 | 177,527 | 55,299 | 341,066 | 1,198,838,634 |
| 2012 | 146,420 | 49,321 | 314,944 | 1,129,349,925 | 36,321 | 7,664 | 50,079 | 177,781,799 | 182,741 | 56,985 | 365,023 | 1,307,131,724 |
| 2013 | 147,020 | 49,721 | 315,008 | 1,248,903,393 | 36,321 | 7,664 | 52,846 | 195,529,127 | 183,431 | 57,385 | 367,854 | 1,444,432,520 |
| 2014 | 147,479 | 49,627 | 314,062 | 1,287,248,813 | 36,321 | 7,664 | 51,912 | 207,649,600 | 183,800 | 57,291 | 365,974 | 1,503,574,790 |
| 2015 | 147,479 | 49,627 | 309,922 | 1,270,856,680 | 36,321 | 7,664 | 52,723 | 210,892,897 | - | 57,291 | 362,645 | 1,481,749,577 |
| 2016 | 149,018 | 49,688 | 308,772 | 1,274,485,404 | 54,511 | 9,650 | 53,823 | 211,891,899 | 203,529 | 59,338 | 362,595 | 1,486,377,303 |
| 2017 | 149,018 | 49,688 | 309,922 | 1,270,856,680 | 54,511 | 9,650 | 52,723 | 210,892,897 | 203,529 | 59,338 | 362,645 | 1,481,749,577 |
| 2018 | 149,018 | 49,688 | 323,121 | 1,495,678,680 | 53,035 | 9,242 | 53,232 | 248,262,840 | 202,053 | 58,930 | 376,353 | 1,743,941,520 |
| 2019 | 149,018 | 49,688 | 365,104 | 1,715,988,903 | 53,035 | 9,242 | 105,205 | 494,464,498 | 202,053 | 58,930 | 470,309 | 2,210,453,400 |
| 2020 | 149,504 | 50,116 | 409,828 | 2,049,141,547 | 53,035 | 9,242 | 63,764 | 318,819,664 | 202,539 | 59,358 | 473,592 | 2,367,961,211 |
| 2021 | 141,769 | 48,749 | 414,105 | 2,418,489,585 | 53,035 | 9,242 | 62,914 | 357,308,946 | 194,804 | 57,991 | 477,019 | 2,775,798,531 |
| 2022 | 144,728 | 49,206 | 404,639 | 2,711,082,104 | 53,035 | 9,242 | 66,873 | 448,051,914 | 197,763 | 58,448 | 471,513 | 3,159,134,018 |
| 2023 | 144,728 | 49,206 | 415,880 | 2,911,157,222 | 53,035 | 9,242 | 64,097 | 448,679,086 | 197,763 | 58,448 | 479,977 | 3,359,836,308 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Jedwali Na. 45: MWENENDO WA UUZAJI WA SAMAKI NJE YA NCHI**

| Mwaka | Uzito (Mt) | Samaki wa mapambo | Thamani katika dola za Marekani | Thamani katika Shilingi | Ushuru |
|---|---|---|---|---|---|
| 2011 | 37,996.4 | 61,215 | 152,973,356.8 | 233,714,590,010.8 | 6,153,278,023.3 |
| 2012 | 41,394.3 | 45,550 | 163,299,365.5 | 254,901,017,111.3 | 6,819,926,007.1 |
| 2013 | 38,573.6 | 44,260 | 147,659,778.6 | 234,884,628,955.9 | 6,117,769,193.7 |
| 2014 | 43,354.4 | 42,100 | 188,101,262.0 | 314,489,903,877.1 | 7,490,632,355.2 |
| 2015 | 41,059.5 | 87,630 | 259,286,762.2 | 547,228,222,095.5 | 13,097,411,199.2 |
| 2016 | 39,691.5 | 65,841 | 257,257,100.5 | 526,985,019,569.3 | 14,302,761,906.9 |
| 2017 | 36,063.2 | 101,110 | 182,450,277.8 | 406,568,122,271.5 | 10,446,850,538.6 |
| 2018 | 44,939.8 | 63,978 | 239,680,014.6 | 546,993,779,393.0 | 13,520,367,822.3 |
| 2019 | 45,775.2 | 136,915 | 158,657,945.6 | 376,763,802,642.9 | 25,567,600,872.6 |
| 2020 | 40,478.0 | 128,316 | 169,111,837.1 | 386,369,197,733.3 | 21,678,640,820.1 |
| 2021 | 42,302.0 | 181,268 | 176,083,787.0 | 414,232,629,494.0 | 18,436,276,859.0 |
| 2022 | 37,235.9 | 208,744 | 199,810,553.9 | 457,047,515,491.1 | 16,557,211,745.0 |
| 2023 | 42,371.4 | 166,024 | 213,383,805.1 | 509,909,916,964.8 | 16,214,093,691.8 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Jedwali Na. 46: MAUZO YA SANGARA NJE YA NCHI MWAKA 2008 - 2023**

| Mwaka | Uzito (Tani) | Thamani (USD) | Thamani (Shilingi) | Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|
| 2010 | 27,229 | 139,666,995 | 194,012,069,314 | 4,509,670,994 |
| 2011 | 25,426 | 127,601,694 | 197,899,741,508 | 4,299,987,312 |
| 2012 | 28,951 | 141,189,162 | 220,149,518,646 | 4,967,311,025 |
| 2013 | 33,733 | 124,551,585 | 197,578,220,799 | 5,085,642,906 |
| 2014 | 24,473 | 665,856,773 | 1,131,575,531,076 | 4,569,314,170 |
| 2015 | 23,001 | 250,279,107 | 528,534,413,019 | 11,251,591,352 |
| 2016 | 26,045 | 177,338,054 | 345,417,803,263 | 6,964,514,349 |
| 2017 | 26,680 | 168,554,019 | 376,572,501,425 | 7,057,407,121 |
| 2018 | 32,167 | 179,522,959 | 409,654,290,065 | 9,689,153,198 |
| 2019 | 32,609 | 176,894,903 | 400,195,293,574 | 17,622,314,163 |
| 2020 | 24,173 | 132,369,802 | 302,303,225,916 | 13,627,647,551 |
| 2021 | 21,846 | 143,135,053 | 337,103,408,189 | 9,704,591,513 |
| 2022 | 21,647 | 162,165,160 | 375,439,047,154 | 8,917,297,123 |
| 2023 | 20,192 | 132,207,272 | 316,336,648,585 | 7,783,579,857 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

# SURA YA 8

# MISITU, WANYAMAPORI NA UTALII

## Misitu na Nyuki

207. Mwaka 2023, uzalishaji wa asali ulikuwa tani 33,276 ikilinganishwa na tani 31,695 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Kati ya kiasi hicho, tani 1,199.8 za asali zenye thamani ya shilingi milioni 11,998.2 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 1,562.9 zenye thamani ya shilingi milioni 15,629.3 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2022. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa nta ulikuwa tani 1,913 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 1,907 mwaka 2022. Aidha, tani 479.2 za nta zenye thamani ya shilingi milioni 4,792.3 ziliuzwa nje ya nchi mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 793.5 zenye thamani ya shilingi milioni 11,903.5 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2022. Kupungua kwa mauzo nje kulitokana na: kuyumba kwa soko la asali na nta nje ya nchi; kujitoa kwa nchi ya Uingereza katika Umoja wa Ulaya hali iliyosababisha kubadilika kwa taratibu za uagizaji wa asali na mazao ya nyuki ikiwemo wafanyabiashara waliokuwa na soko katika nchi hiyo kuanza upya taratibu za kusajili ili kuuza mazao hayo; na kuongezeka kwa ushindani katika masoko ya nje ya nchi. Asali na nta iliyozalishwa nchini iliuzwa zaidi katika nchi za Marekani, Ujerumani, Japan, Poland, Ireland na New Zealand.

**Jedwali Na. 8.1: Mauzo ya Mazao ya Nyuki Nje ya Nchi Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Asali | | Nta | |
|---|---|---|---|---|
| | Uzito (Tani) | Thamani (Shilingi) | Uzito (Tani) | Thamani (Shilingi) |
| 2019 | 607.6 | 4,860,834,400 | 179.3 | 1,437,865,600 |
| 2020 | 2,032.4 | 13,413,721,200 | 251.0 | 3,865,400,000 |
| 2021 | 1,988.0 | 19,878,220,000 | 393.0 | 6,489,999,500 |
| 2022 | 1,562.9 | 15,629,295,500 | 793.5 | 11,903,470,950 |
| 2023 | 1,199.8 | 11,998,150,000 | 479.2 | 4,792,300,000 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

## Upandaji wa Miti

208. Mwaka 2023, miche ya miti 35,381,994 ilioteshwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ikilinganishwa na miche 30,705,653 iliyooteshwa mwaka 2022. Miche hiyo ilipandwa katika maeneo yaliyovunwa yenye hekta 4,508.2, maeneo yaliyorudishiwa miti (hekta 2,071.1) na maeneo ambayo miti haikuota vizuri (hekta 2,384.3) ikilinganishwa na hekta 3,219.0, hekta 5,538.0 na hekta 3,496.0 mtawalia mwaka 2022.

**Jedwali Na. 8.2: Uendelezaji wa Mashamba ya Miti Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Idadi ya miche iliyooteshwa | Eneo la mashamba mapya | Mashamba yaliyorudishiwa miti | Eneo lililopandwa miche baada ya miti kuvunwa | Eneo lililorudishiwa miche katika maeneo yasiyoota vizuri | Eneo la mashamba ya miti lililosafishwa | Eneo la mashamba ya miti lililopogolewa | Eneo la mashamba ya miti ambalo miti ilipunguziwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Hekta | | | | | | |
| 2019 | 21,824,600 | 4,438 | 615 | 1,893 | 251 | 18,101 | 6,244 | 1,293 |
| 2020 | 20,689,369 | 56,500 | 4,543 | 3,583 | 3,303 | 37,469 | 9,647 | 3,317 |
| 2021 | 31,295,703 | 30,000 | 4,498 | 3,328 | 2076 | 41,527 | 10,860 | 4,685 |
| 2022 | 30,705,653 | 0 | 5,538 | 3,219 | 3,496 | 38,357 | 9,869 | 3,197 |
| 2023 | 35,381,994 | 0 | 2,071.10 | 4,508.20 | 2,384.30 | 27,681.30 | 7,155.50 | 2,690.60 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

209. Mwaka 2023, jumla ya miche 14,089,944 ilipandwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo misitu ya asili, vyanzo vya maji, makazi na maeneo yaliyoharibiwa kutokana na shughuli za binadamu ikilinganishwa na miche 12,473,083 iliyopandwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 13.0. Ongezeko hilo lilitokana na kampeni na programu za upandaji miti zilizofanyika katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, mipango 57 ya usimamizi wa hifadhi za misitu iliandaliwa na mipaka ya hifadhi ya misitu yenye urefu wa kilometa 1,713.2 ilisafishwa na kuwekwa maboya/vigingi 870 na mabango 973 mwaka 2023 ikilinganishwa mipango 42, kilometa 3,444, maboya/vigingi 1,295 na mabango 872 yaliyowekwa mwaka 2022. Vile vile, Wakala wa Huduma za Misitu uliwezesha upandaji miti kwa jamii kwa kugawa miche 14,089,994, viriba kilogramu 180 na mbegu kilogramu 25.1 mwaka 2023 ikilinganishwa na miche 11,052,876, viriba kilogramu 293 na mbegu kilogramu 30 zilizotolewa mwaka 2022.

210. Mwaka 2023, Wakala wa Huduma za Misitu ulikamata na kutaifisha magunia 42,272 ya mkaa, nguzo 2,139, mbao zenye mita za ujazo 4,022.9, kuni zenye mita za ujazo 392, na magogo yenye mita za ujazo 521.8. Aidha, pikipiki 2,287, baiskeli 4,187, magari 281, majahazi 16 na pikipiki 38 za miguu mitatu za kubebea mizigo zilizotumika katika uharibifu wa misitu zilishikiliwa na kutozwa faini.

**Mauzo ya Bidhaa za Misitu Nje ya Nchi**

211. Mwaka 2023, mauzo ya bidhaa za misitu nje ya nchi yalikuwa shilingi bilioni 2,044.3. Sehemu kubwa ya mapato hayo ilitokana na uuzaji wa zao la unga wa miwati na bidhaa za miwati. Mauzo kutokana na zao la unga wa miwati yalikuwa shilingi bilioni 1,690.82, sawa na asilimia 83 ya mauzo yote. Aidha, bidhaa za miwati zilichangia shilingi bilioni 160.12 na bidhaa nyinginezo zilichangia shilingi bilioni 193, sawa na mchango wa asilimia 8 na asilimia 9 mtawalia.

**Wanyamapori**

212. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa kufanya doria 433,572 ikilinganishwa na doria 623,807 zilizofanyika mwaka 2022. Kati ya doria hizo, Shirika la Hifadhi za Taifa lilifanya doria 75,879, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro doria 86,068, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori doria 270,795 na Kikosi cha Taifa cha Kupambana na Ujangili doria 830. Doria hizo ziliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 5,421 wa makosa ya ujangili wa wanyamapori na misitu ikilinganishwa na watuhumiwa 11,140 waliokamatwa mwaka 2022. Aidha, nyara mbalimbali zilikamatwa katika doria zilizofanyika kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 8.3.**

**Jedwali Na 8.3: Nyara Zilizokamatwa katika Doria Mwaka 2022 - 2023**

| **Aina ya Nyara** | **Mwaka** | |
|---|---:|---:|
| | **2022** | **2023** |
| Meno ya tembo | 222 | 208 |
| Vipande vya Meno ya Tembo | 544 | 390 |
| Nyamapori (Kilogramu) | 1,023 | 1,986 |
| Nyama kavu (Vipande) | 170 | 299 |
| Kobe hai | 406 | 63 |
| Ngozi (Vipande) | 4 | 9 |
| Magamba ya kakakuona | 436 | 123 |
| Chatu | 1 | 3 |
| Silaha | 315 | 408 |
| Risasi | 1,427 | 2,807 |
| Mitego | 19,263 | 17,211 |
| Magari | 7 | 34 |
| Pikipiki | 21 | 81 |
| Mifugo | 30,030 | 40,752 |
| Meno ya kiboko | - | 6 |
| Kucha za simba | - | 11 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

213. Mwaka 2023, mapato yatokanayo na sekta ndogo ya wanyamapori yalikuwa shilingi bilioni 634.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 500.5 kwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 26.7. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi mbalimbali za utangazaji wa vivutio vya utalii ikiwemo Programu Maalum ya *Tanzania - The Royal Tour* pamoja na uboreshaji wa miundombinu katika maeneo ya hifadhi.

**Jedwali Na. 8.4: Mapato ya Sekta Ndogo ya Wanyamapori Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Shirika la Hifadhi za Taifa | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 2019 | 292,539,502,030.0 | 147,043,375,161.0 | 20,864,030,536.0 | 460,446,909,746.0 |
| 2020 | 85,614,710,442.0 | 47,862,177,819.0 | 20,913,213,013.0 | 154,390,103,294.0 |
| 2021 | 127,028,556,252.0 | 63,852,180,870.0 | 60,651,257,787.0 | 251,531,996,930.0 |
| 2022 | 293,079,503,086.0 | 144,354,627,647.0 | 63,030,304,315.3 | 500,464,435,048.3 |
| 2023 | 379,790,063,492.1 | 195,748,756,367.0 | 58,730,532,598.2 | 634,269,352,457.2 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Uwindaji wa Kitalii**

214. Mwaka 2023, idadi ya watalii wa nje waliotembelea maeneo ya uwindaji ilikuwa ni 191,475 ikilinganishwa na watalii 141,157 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 35.6. Aidha, mapato yaliyotokana na uwindaji wa kitalii yalikuwa shilingi bilioni 58.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 63.1 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 7.0. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa idadi ya wawindaji wa kitalii na watazamaji ambao ndio wanaochochea upatikanaji mkubwa wa mapato **(Jedwali 8.5)**. Aidha, watalii wa picha walikuwa 190,378 mwaka 2023 ikilinganishwa na watalii 139,967 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 36.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kushamiri kwa utalii wa picha.

**Jedwali Na. 8.5: Idadi ya Wawindaji wa Kitalii na Mapato Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | | | Mapato (Shilingi milioni) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wawindaji | Watazamaji | Watalii wa picha | Jumla | |
| 2019 | 519 | 483 | - | 1,002 | 20,864.0 |
| 2020 | 251 | 185 | - | 436 | 15,590.6 |
| 2021 | 548 | 101,382 | - | 101,930 | 35,726.0 |
| 2022 | 687 | 503 | 139,967 | 141,157 | 63,030.3 |
| 2023 | 599 | 498 | 190,378 | 191,475 | 58,730.5 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Utalii**

215. Mwaka 2023, watalii 1,808,205 walitembelea nchini ikilinganishwa na watalii 1,454,920 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 24.3. Ongezeko hilo lilitokana na; utangazaji wa utalii, hususan kupitia Programu ya Tanzania - *The Royal Tour*; kuimarika kwa miundombinu ya utalii ikiwemo barabara na viwanja vya ndege; na utekelezaji wa mkakati wa kuongeza wigo wa mazao ya utalii ikiwemo utalii wa meli na fukwe. Kati ya hao, watalii 888,506 walitembelea Hifadhi za Taifa na watalii 919,699 walitembelea maeneo mengine ya vivutio vya utalii nchini. Kwa upande mwingine, watalii wa ndani

walikuwa 1,985,707 mwaka 2023 ikilinganishwa na watalii 2,363,260 mwaka 2022. Kati ya hao, watalii 902,176 walitembelea Hifadhi za Taifa mwaka 2023 ikilinganishwa na watalii 787,742 mwaka 2022.

216. Mwaka 2023, watalii 843,473 walitembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ikilinganishwa na watalii 645,275 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 30.7. Kati ya hao, watalii 515,961 walitoka nje ya nchi na watalii 327,512 walikuwa wa ndani.

**Jedwali Na. 8.6: Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Mwaka 2019 - 2023**

| **Mwezi** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 108,027 | 132,684 | 79,116 | 94,441 | 146,877 |
| Februari | 122,929 | 137,204 | 79,730 | 101,042 | 144,019 |
| Machi | 108,323 | 66,581 | 72,285 | 93,889 | 118,186 |
| Aprili | 95,212 | 7,105 | 43,966 | 79,405 | 96,852 |
| Mei | 80,172 | 5,529 | 42,173 | 89,271 | 106,497 |
| Juni | 121,173 | 9,671 | 57,689 | 117,349 | 146,896 |
| Julai | 156,664 | 17,136 | 81,307 | 166,736 | 185,929 |
| Agosti | 155,734 | 24,863 | 87,397 | 158,049 | 186,030 |
| Septemba | 143,690 | 29,566 | 80,733 | 134,231 | 168,708 |
| Oktoba | 133,014 | 41,740 | 92,345 | 141,517 | 171,573 |
| Novemba | 124,917 | 61,183 | 92,939 | 123,351 | 152,162 |
| Desemba | 160,296 | 87,605 | 113,012 | 155,639 | 182,630 |
| **Jumla** | **1,510,151** | **620,867** | **922,692** | **1,454,920** | **1,808,205** |

**Chanzo:** Idara ya Uhamiaji na Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 8.7: Idadi ya Watalii Waliotembelea Hifadhi za Taifa na Mapato ya Utalii Mwaka 2019 - 2023**

| **Mwaka** | **Idadi ya Watalii** | | **Jumla** | **Mapato (Shilingi Milioni)** |
|---|---|---|---|---|
| | **Nje** | **Ndani** | | |
| 2019 | 763,276 | 494,676 | 1,257,952 | 292,539.5 |
| 2020 | 218,310 | 288,867 | 507,177 | 85,614.7 |
| 2021 | 317,654 | 518,480 | 836,134 | 127,028.6 |
| 2022 | 697,264 | 787,742 | 1,485,006 | 293,079.5 |
| 2023 | 888,506 | 902,176 | 1,790,682 | 379, 790.1 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

217. Mwaka 2023, watalii 250,808 walitembelea Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia ikilinganishwa na watalii 210,987 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 18.87. Kati ya hao, watalii wa ndani walikuwa 219,727 na watalii wa nje walikuwa 31,081 mwaka 2023 ikilinganishwa na watalii wa ndani 184,187, na watalii wa nje 26,800 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na watalii waliotembelea Hifadhi za Misitu ya

Mazingira Asilia yalikuwa shilingi milioni 1,984.21 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 1,214.77 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 63.3. Ongezeko la utalii katika Hifadhi za Mazingira Asilia lilitokana na utangazaji wa utalii, hususan kupitia Programu ya *Tanzania - The Royal Tour*, kuongezeka kwa doria katika misitu kwa ajili ya kuzuia ukataji wa miti na kuboreshwa kwa miundombinu katika maeneo ya Hifadhi za Misitu.

**Jedwali Na. 8.8: Mwenendo wa Watalii Waliotembelea Vivutio vilivyopo katika Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia na Mashamba ya Miti Mwaka 2023**

| Mwezi | Idadi ya Watali | | | Mapato | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ndani | Nje | Jumla | Ndani | Nje | Jumla |
| Januari | 16,037 | 3,229 | 19,266 | 44,739,000 | 75,582,000 | 120,321,000 |
| Februari | 14,765 | 2,565 | 17,330 | 47,464,300 | 193,505,200 | 240,969,500 |
| Machi | 12,278 | 1,709 | 13,987 | 37,826,100 | 42,605,460 | 80,431,560 |
| Aprili | 9,789 | 846 | 10,635 | 34,575,400 | 17,344,000 | 51,919,400 |
| Mei | 13,426 | 884 | 14,310 | 40,159,135 | 23,384,440 | 63,543,575 |
| Juni | 19,823 | 2,503 | 22,326 | 65,689,110 | 90,034,110 | 155,723,220 |
| Julai | 18,364 | 4,281 | 22,645 | 62,224,500 | 530,971,200 | 593,195,700 |
| Agosti | 22,022 | 4,006 | 26,028 | 62,409,200 | 94,789,500 | 157,198,700 |
| Septemba | 29,233 | 4,414 | 33,647 | 70,508,400 | 72,925,500 | 143,433,900 |
| Oktoba | 24,218 | 3,369 | 27,587 | 79,941,000 | 71,537,800 | 151,478,800 |
| Novemba | 14,203 | 793 | 14,996 | 41,749,000 | 22,413,500 | 64,162,500 |
| Desemba | 25,569 | 2,482 | 28,051 | 93,819,500 | 68,013,000 | 161,832,500 |
| **Jumla** | **219,727** | **31,081** | **250,808** | **681,104,645** | **1,303,105,710** | **1,984,210,355** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Malikale**

218. Mwaka 2023, wageni 147,275 walitembelea vivutio vya malikale ikilinganishwa na wageni 127,463 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 15.5. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu katika vivutio vya Malikale. Aidha, mapato yaliyotokana na wageni waliotembelea vivutio vya malikale yalikuwa shilingi milioni 237.09 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi milioni 1,102.94 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 78.5. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya watafiti wa malikale, hususan kutoka nje ya nchi.

**Jedwali Na. 8.9: Wageni Waliotembelea Vivutio vya Malikale na Mapato Mwaka 2021 - 2023**

| Kituo | 2021 | | 2022 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Wageni** | **Mapato** | **Wageni** | **Mapato** | **Wageni** | **Mapato** |
| Magomeni | 1,163 | 1,423,000 | 531 | 1,601,668 | 688 | 1,069,522 |
| Kaole | 24,765 | 13,086,080 | 33,805 | 64,370,196 | 39,481 | 75,895,283 |
| Isimila | 8,517 | 21,720,385 | 10,104 | 29,627,384 | 3,890 | 3,845,142 |
| Mji Mkongwe | 15,678 | 12,937,020 | 17,920 | 51,056,832 | 21,940 | 37,489,242 |
| Kalenga | 6,693 | 10,174,020 | 4,972 | 8,154,194 | 4,494 | 6,527,284 |
| Kilwa | 5,947 | 29,066,000 | 5,729 | 48,862,750 | 6,902 | 12,649,553 |
| Olduvai | 6,272 | 178,585,353.6 | 12,388 | 799,696,715 | 27,535 | 18,412,626 |
| Mbozi | 4,058 | 7,972,160 | 4,800 | 11,697,726 | 3,953 | 6,686,300 |
| Amboni | 13,666 | 27,971,627 | 17,044 | 34,148,326 | 15,522 | 25,368,567 |
| Tongoni | 164 | 295,641 | 193 | 464,164 | 657 | 1,003,257 |
| Ujiji | 4,194 | 9,296,750 | 4,664 | 14,338,354 | 4,531 | 10,437,353 |
| Kwihara | 181 | 249,800 | 271 | 300,000 | 1,013 | 1,343,103 |
| Kolo | 3,578 | 12,588,890 | 5,191 | 23,223,430 | 6,900 | 21,677,337 |
| Caravan Serai | 4,446 | 7,534,000 | 5,554 | 10,388,796 | 5,738 | 9,702,250 |
| Kunduchi | 1,228 | 1,030,000 | 4,297 | 5,008,416 | 4031 | 4,981,032 |
| **Jumla** | **94,278** | **155,345,373** | **127,463** | **1,102,938,951** | **147,275** | **237,087,851** |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii

**Makumbusho ya Taifa**

219. Mwaka 2023, wageni 490,526 walitembelea Makumbusho ya Taifa ikilinganishwa na wageni 1,096,120 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 55.2. Kati ya hao, wageni wa ndani walikuwa 473,761 na wageni wa nje walikuwa 16,765. Upungufu huo ulitokana na kutofanyika kwa Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania, Siku ya *Zinjanthropus* duniani, KijijiSoko na Siku ya Makumbusho duniani. Aidha, kutofanyika kwa matamasha/matukio hayo kulitokana na upungufu wa mapato ya ndani kutoka makadario ya shilingi milioni 305.98 yaliyopangwa kwa kipindi cha Oktoba - Desemba, 2023 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya shilingi milioni 257.32 sawa na upungufu wa asilimia 15.90. Vile vile, mapato yaliyotokana na viingilio vya wageni katika vituo vya Makumbusho ya Taifa yalikuwa shilingi milioni 425.47 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi milioni 687.60 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 38.1.

**Jedwali Na. 8.10: Idadi ya Watalii na Mapato katika Vivutio vya Makumbusho ya Taifa Mwaka 2022 - 2023**

| Na. | Kituo | 2022 | | | | 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Watalii | | | Mapato (Shilingi) | Idadi ya Watalii | | | Mapato (Shilingi) |
| | | Nje | Ndani | Jumla | | Nje | Ndani | Jumla | |
| 1 | Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni | 6,701 | 47,818 | 54,519 | 335,667,101 | 8,802 | 202,040 | 210,842 | 271,096,91 |
| 2 | Kijiji cha Makumbusho | 2,575 | 1,009,757 | 1,012,332 | 218,480,300 | 4,489 | 148,209 | 152,698 | 208,770,300 |
| 3 | Makumbusho ya Azimio la Arusha | 112 | 4,971 | 5,083 | 13,582,500 | 400 | 23,233 | 23,633 | 22,932,000 |
| 4 | Makumbusho ya Elimu Viumbe | 1,903 | 8,494 | 10,397 | 49,574,090 | 2,875 | 45,139 | 48,014 | 87433275 |
| 5 | Makumbusho ya Mwl. Nyerere | 31 | 7,446 | 7,477 | 57,268,300 | 91 | 18,485 | 18,576 | 67,058,800 |
| 6 | Makumbusho ya Vita ya Majimaji | 42 | 3,340 | 3,382 | 7,686,100 | 78 | 27,714 | 27,792 | 30,847,300 |
| 7 | Makumbusho ya Dkt. Rashid Kawawa | 17 | 848 | 865 | 2,328,400 | 14 | 3,693 | 3,707 | 3,432,800 |
| 8 | Mji wa Kihistoria Mikindani | 2 | 2,063 | 2,065 | 3,017,000 | 16 | 5,248 | 5,264 | 4,997,000 |
| | **Jumla** | **11,383** | **1,084,737** | **1,096,120** | **687,603,791** | **16,765** | **473,761** | **490,526** | **425,471,475** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Jedwali Na. 47: WATALII WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA KATIKA MWAKA 2010 - 2023**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | Jumla | Mapato (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|
| | Nje | Ndani | | |
| 2010 | 540,440 | 333,294 | 873,734 | 113,856,861,145 |
| 2011 | 586,869 | 360,928 | 947,797 | 119,549,704,203 |
| 2012 | 537,675 | 364,217 | 901,892 | 137,545,109,618 |
| 2013 | 530,142 | 427,208 | 957,350 | 150,861,426,031 |
| 2014 | 535,140 | 417,220 | 952,360 | 152,977,487,000 |
| 2015 | 432,124 | 526,110 | 958,234 | 149,957,485,000 |
| 2016 | 439,119 | 518,457 | 957,576 | 175,089,696,000 |
| 2017 | 386,529 | 595,811 | 982,340 | 207,587,218,000 |
| 2018 | 726,003 | 442,543 | 1,168,546 | 214,486,751,736 |
| 2019 | 763,276 | 494,676 | 1,257,952 | 292,539,502,030 |
| 2020 | 218,310 | 288,867 | 507,177 | 85,614,710,442 |
| 2021 | 317,654 | 518,480 | 836,134 | 127,028,556,252 |
| 2022 | 697,264 | 787,742 | 1,485,006 | 293,079,503,086 |
| 2023 | 888,506 | 902,176 | 1,790,682 | 379,790,063,492 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Jedwali Na. 48: MAUZO YA BIDHAA ZA MISITU KATIKA MASOKO YA NCHI ZA NJE KWA MWAKA 2023**

| Bidhaa | Idadi | Kipimo | Thamani (USD) | Thamani (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|
| Bamboo | 1 | Score | 2.0 | 4,820 |
| baobab | 61052.5 | Kg | 32,617 | 78,605,765 |
| Baobab Oil | 820 | Kg | 8,195 | 19,749,251 |
| Barks | 12172 | Kg | 8,140 | 19,617,400 |
| Baskets/Mats | 3002.29 | Kg | 72,026 | 173,582,901 |
| Beds | 70 | pcs | 258 | 621,780 |
| Briquete | 1,502,499.80 | Kg | 1,029,855 | 2,481,951,273 |
| Cane chairs | 4 | pcs | 1,613 | 3,887,330 |
| Carvings | 16153.59 | Kg | 1,056,920 | 2,547,177,778 |
| Chairs & Stools | 12 | pcs | 190 | 457,900 |
| Charcoal dust | 30 | Bags | 20 | 48,200 |
| Clarinets | 8.92 | M3 | 62,083 | 149,620,753 |
| Clarinets Sets | 7.12 | M3 | 57,304 | 138,101,869 |
| Cup Boards | 74.6 | pcs | 425 | 1,024,250 |
| Door Shutters | 9 | M3 | 100 | 241,000 |
| Fibre | 50 | Kg | 3 | 7,230 |
| Fibre and Raffia | 20925 | Kg | 41,610 | 100,280,100 |
| Firewood | 625 | M3 | 38,547 | 92,897,788 |
| Furniture | 20905.66 | pcs | 15,278 | 36,819,980 |
| Grasses | 22 | Kg | 0 | 24 |
| Gums | 227025 | Kg | 517,852 | 1,248,022,115 |
| Logs | 1357.03 | M3 | 2,299,561 | 5,541,940,853 |
| Marine board | 11427.47 | pcs | 3,064,004 | 7,384,249,640 |
| MDF Laminated Board | 8533.82 | Tons | 2,770,745 | 6,677,495,185 |
| MDF Plain Board | 1433.23 | Tons | 467,307 | 1,126,209,870 |
| Medicinal Plants (Leaves, Flowers, Roots) | 667.52 | Kg | 32,021 | 77,171,261 |
| Ornamental Plants | 29,390.07 | pcs | 142,134 | 342,542,458 |
| Other wooden small items | 164970.2 | pcs | 255,279 | 615,223,137 |
| Pallet | 163.09 | pcs | 26,464 | 63,777,927 |
| Palm Fruit | 25000 | Tons | 10,000 | 24,100,000 |
| Particle Board Flower | 20 | Tons | 34 | 81,940 |
| Plywood | 27,815.30 | pcs | 7,548,703 | 18,192,374,110 |
| Poles | 584.15 | pcs | 39,085 | 94,194,850 |
| Resin | 1334113.3 | Kg | 1,129,829 | 2,722,886,781 |
| Sandalwood | 5056.26 | Kg | 2,435,038 | 5,868,441,580 |
| Sandalwood spent dust | 44000 | Kg | 43,120 | 103,919,200 |
| Sawn Timber | 193,784.01 | M3 | 31,512,839 | 75,945,941,243 |
| sleepers | 1597.07 | M3 | 1,067,026 | 2,571,532,033 |
| Tree Seedlings | 1 | Number | 4 | 9,640 |
| Veneer | 184,128.91 | pcs | 23,480,037 | 56,586,889,315 |
| Wattle extract | 318005 | Tons | 457,515 | 1,102,611,150 |
| Wattle Extract Powder | 1365028 | Kg | 701,586,750 | 1,690,824,067,090 |
| Wattle Extract Solid | 140020 | Kg | 66,441,510 | 160,124,039,100 |
| Window Frames | 4 | M3 | 8 | 19,280 |
| Withies | 80874 | Bundle | 86,350 | 208,103,500 |
| Wood oil | 783.74 | Kg | 368,000 | 886,880,000 |
| Wooden Office/Dinning Table | 22.53 | pcs | 1,555 | 3,747,550 |
| Wooden small items | 234597.68 | pcs | 54,909 | 132,330,280 |
| **Jumla** | | | **848,262,865** | **2,044,313,498,480** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Jedwali Na. 49: MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII 2016 - 2023**

| Maelezo | Kipimo | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022r | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Watalii | Idadi | 1,284,279 | 1,327,143 | 1,505,702 | 1,527,230 | 620,867 | 922,692 | 1,454,920 | 1,808,205 |
| Watalii wa hotelini | Idadi | 1,155,851 | 1,163,752 | 1,404,672 | 1,353,279 | 563,779 | 848,936 | 1,365,861 | 1,710,333 |
| Mapato | Dola za Marekani Milioni | 2,132 | 2,200 | 2,433 | 2,604 | 715 | 1,248 | 2,528 | 3,374 |
| Wastani wa siku za kukaa watalii hotelini | Siku | 10 | 9 | 10 | 13 | 10 | 10 | 9 | 10 |
| Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa siku (Dola za Marekani) | *Package Tour* | 351 | 410 | 331 | 379 | 312 | 364 | 377 | 419 |
| | *Non Package Tour* | 145 | 136 | 135 | 216 | 115 | 141 | 166 | 178 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

r- Takwimu zimeboreshwa

**Jedwali Na. 50: WATALII WALIOTEMBELEA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO**

| Mwaka | Wageni kutoka Nje | Watanzania | Jumla |
|---|---:|---:|---:|
| 2010 | 281,513 | 242,133 | 523,646 |
| 2011 | 281,513 | 307,086 | 588,599 |
| 2012 | 310,537 | 254,730 | 565,267 |
| 2013 | 350,970 | 296,763 | 647,733 |
| 2014 | 332,469 | 278,221 | 610,690 |
| 2015 | 289,061 | 278,922 | 567,983 |
| 2016 | 284,794 | 265,845 | 550,639 |
| 2017 | 391,030 | 249,428 | 640,458 |
| 2018 | 410,574 | 268,880 | 679,454 |
| 2019 | 445,283 | 279,255 | 724,538 |
| 2020 | 122,228 | 125,953 | 248,181 |
| 2021 | 160,877 | 165,235 | 326,112 |
| 2022 | 388,853 | 256,422 | 645,275 |
| 2023 | 515,961 | 327, 512 | 843,473 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

# SURA YA 9

# MADINI

**Leseni za Utafutaji na Uchimbaji wa Madini**

220. Mwaka 2023, maombi 18,438 ya leseni yalipokelewa na kuidhinishwa ikilinganishwa na maombi 19,071 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 3.3. Upungufu huo ulitokana na maombi mengi yaliyopokelewa kukosa vigezo vya kupewa leseni kwa mujibu wa mwongozo wa utoaji wa leseni. Aidha, jumla ya leseni 11,251 zilitolewa mwaka 2023 ikilinganishwa na leseni 7,960 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 41.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uelewa kuhusu Sheria ya Madini Sura 123 pamoja na kuimarika kwa mfumo wa utoaji wa leseni kufuatia jitihada zilizofanyika kuongeza vitendea kazi, kuboresha mfumo wenyewe na kutolewa kwa mafunzo kwa watumiaji wa mfumo. Kati ya leseni zilizotolewa, leseni 398 zilikuwa za utafutaji wa madini, leseni moja ya uchimbaji mkubwa, leseni 14 za uchimbaji wa kati, leseni 8,079 za uchimbaji mdogo, leseni 63 za uchenjuaji wa madini, leseni moja ya usafishaji wa madini, leseni 797 za biashara ya madini (dealers) na leseni 1,898 za biashara ndogo ya madini (brokers).

**Vibali vya Uuzaji wa Madini**

221. Mwaka 2023, vibali 11,258 vya kuuza madini nje ya nchi vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,478.42 vilitolewa ikilinganishwa na vibali 10,318 vilivyokuwa na thamani ya dola milioni 3,240.35 vilivyotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la vibali kwa asilimia 9.1. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya madini ya vito na makaa ya mawe nje ya nchi.

**Dhahabu**

222. Mwaka 2023, jumla ya kilogramu 54,760.32 za dhahabu zilizalishwa ikilinganishwa na kilogramu 56,942.98 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa uzalishaji kwa asilimia 3.8. Hii ilitokana na kusitishwa kwa shughuli za uzalishaji kulikochangiwa na migodi mingi ya wachimbaji wadogo kufikia kina kirefu. Aidha, kupungua kwa uzalishaji kulitokana na kiwango kikubwa cha mvua za El Nino zilizojaza maji kwenye machimbo na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji.

223. Mwaka 2023, jumla ya kilogramu 62,781.75 za dhahabu zilipata vibali vya kusafirishwa nje ya nchi ikilinganishwa na kilogramu 62,632.0 zilizopata vibali mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 0.2. Aidha, thamani ya dhahabu iliyopata vibali vya kuuzwa nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 6.0 na kufikia dola za Marekani milioni 3,021.62 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,850.35 mwaka 2022. Hii ilitokana na kupanda kwa wastani wa bei ya dhahabu katika soko la dunia na kufikia

dola za Marekeni 1,940.5 kwa wakia mwaka 2023 ikilinganishwa na dola 1,800.1 kwa wakia mwaka 2022.

**Almasi**

224. Mwaka 2023, uzalishaji wa madini ya almasi ulikuwa karati 132,636.40 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 18.5 ikilinganishwa na karati 442,016.26 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 118.01 mwaka 2022. Kupungua kwa uzalishaji wa almasi kulitokana na kusitishwa kwa uzalishaji katika mgodi wa almasi wa Williamson Diamonds Limited kwa kipindi cha Novemba 2022 hadi Julai 2023 baada ya kupasuka kwa bwawa la kuhifadhi tope laini. Mgodi huo ndio unaozalisha almasi kwa wingi nchini.

**Vito vya Thamani**

225. Mwaka 2023, uzalishaji wa madini ya vito ghafi (isipokuwa tanzanite na almasi) ulikuwa kilogramu 55,954,779.72 ikilinganishwa na kilogramu 12,752,079.67 zilizozalishwa mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na mahitaji makubwa ya madini ya quartz na feldpar katika viwanda vya maruramu na rangi nchini na nje ya nchi hususan China.

**Tanzanite**

226. Mwaka 2023, madini ya Tanzanite ghafi na magonga yaliyozalishwa yalikuwa kilogramu 122,664.92 ikilinganishwa na kilogramu 90,186.90 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 36.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji kwenye Kitalu C kilichopo ndani ya Eneo Tengefu la Mirerani kufutuatia kupatikana kwa mwamba wenye ubora mzuri. Aidha, karati 34,904.33 za madini ya Tanzanite yenye thamani ya wastani wa dola za Marekani milioni 4.52 yalikatwa na kusanifiwa mwaka 2023 ikilinganishwa na karati 57,864.28 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 19.15 mwaka 2022, sawa na upungufu wa karati kwa asilimia 39.7. Kwa upande mwingine, wastani wa bei ya tanzanite ghafi katika soko la dunia ilikuwa dola za Marekani 1,376.58 kwa kilogramu mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani 682.67 kwa kilogramu mwaka 2022.

**Makaa ya Mawe**

227. Mwaka 2023, tani 3,256,481.06 za makaa ya mawe yenye thamani ya shilingi trilioni 1.01 zilizalishwa ikilinganishwa na tani 2,511,419.40 zenye thamani ya shilingi bilioni 878.86 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la uzalishaji kwa asilimia 29.7. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya makaa ya mawe ndani na nje ya nchi.

**Madini ya Jasi**

228. Mwaka 2023, tani 549,835.74 za madini ya jasi zilizalishwa ikilinganishwa na tani 604,407.91 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 9.0. Hii ilitokana na

kupungua kwa mahitaji ya madini ya jasi katika baadhi ya viwanda vya saruji nchini. Katika kipindi hicho, tani 10,485.56 za madini ya jasi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 1.80 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 8,300 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 0.94 zilizouzwa nje mwaka 2022. Aidha, vibali 55 vya kusafirisha madini ya jasi nje ya nchi vilitolewa mwaka 2023 ikilinganishwa na vibali 35 vilivyotolewa mwaka 2022. Ongezeko la vibali na mauzo nje lilitokana na kupatikana kwa masoko mapya ya madini ya jasi katika nchi ya Malawi.

**Madini ya ujenzi**

229. Mwaka 2023, madini ya ujenzi yaliyozalishwa yalikuwa tani milioni 33.81 zenye thamani ya shilingi bilioni 543.99 ikilinganishwa na tani milioni 37.50 zenye thamani ya shilingi bilioni 639.88 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa uzalishaji kwa asilimia 9.8. Hii ilitokana na kupungua kwa mahitaji kufuatia kufikia hatua za mwisho kwa mradi wa ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere pamoja na mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa kwa kipande cha kwanza na cha pili.

**Madini Mengine**

230. Mwaka 2023, uzalishaji wa madini ya fedha ulikuwa kilogramu 14,481.35 ikilinganishwa na kilogramu 13,602.43 zilizozalishwa mwaka 2022. Aidha, madini ya fedha yaliyopata vibali vya mauzo nje ya nchi yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 0.89 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 0.63 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 41.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wastani wa bei ya madini ya fedha katika soko la dunia kutoka dola za Marekani 21.75 kwa wakia mwaka 2022 hadi dola za Marekani 23.39 kwa wakia mwaka 2023. Vile vile, uzalishaji wa madini ya lithium ulikuwa tani 2,060.72 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 731.90 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 181.56. Kwa upande mwingine, vibali 18 vya mauzo ya madini ya lithium nje ya nchi vyenye thamani ya shilingi milioni 2,656.13 vilitolewa ikilinganishwa na vibali viwili vyenye thamani ya shilingi milioni 766.13 vilivyotolewa mwaka 2022. Kuongezeka kwa uzalishaji na idadi ya vibali vilivyotolewa kulichangiwa na mahitaji mkubwa ya madini ya lithium nje ya nchi, hususan kwenye viwanda vya utengenezaji wa betri za magari ya umeme kwa ajili ya kupunguza hewa ya ukaa.

**Masoko ya Madini**

231. Mwaka 2023, masoko ya madini yaliendelea kubaki 42 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Aidha, vituo vya ununuzi wa madini vilikuwa 98 ikilinganishwa vituo 86 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.0. Kwa upande mwingine, ukusanyaji wa maduhuli katika masoko ulikuwa shilingi bilioni 176.57 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 167.85 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Kati ya makusanyo hayo, shilingi bilioni 144.26 zilitokana na mrabaha, shilingi bilioni 25.01 ada ya ukaguzi na shilingi bilioni 7.3 tozo ya huduma. Kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli kulitokana

na Serikali kuendelea kuimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye masoko ya madini na vituo vya ununuzi wa madini.

232. Mwaka 2023, tani 17.25 za dhahabu zenye thamani ya shilingi trilioni 2.34 ziliuzwa katika masoko ya madini nchini ikilinganishwa na tani 18.68 zenye thamani ya shilingi trilioni 2.19 zilizouzwa mwaka 2022. Aidha, karati 13,311.73 za madini ya almasi zenye thamani ya shilingi bilioni 3.96 ziliuzwa katika masoko hayo mwaka 2023 ikilinganishwa na karati 23,913.19 zenye thamani ya shilingi bilioni 12.37 zilizouzwa mwaka 2022.

## Jedwali Na. 51: UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA

| Madini | Kipimo | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Almasi | karati | 381,302.06 | 416,749.51 | 147,190.95 | 62,545 | 442,016.26 | 132,636.40 |
| Dhahabu | Kg | 39,304.07 | 48,408.09 | 55,805.33 | 59,638 | 56,942.98 | 54,760.32 |
| Tanzanite (ghafi) | Kg | - | - | 51,542.47 | 177,145.50 | 14,487.48 | 32,870.63 |
| Tanzanite (iliyokatwa na kusanifiwa) | karati | - | - | 118,772.95 | 120,458 | 57,864.28 | 34,904.33 |
| Madini mengine ya Vito (ghafi) | Kg | 284,321.19 | 1,929,714.44 | 23,564,524.64 | 7,197,217 | 12,752,079.67 | 55,954,779.72 |
| Chumvi | Tani | 226,756.69 | 99,510.11 | 83,974.32 | 112,995 | 181,818.07 | 159,020.49 |
| Phosphate | Tani | - | - | 28,376.22 | 24,493 | 26,596.79 | 31,745.08 |
| Mawe ya chokaa | 000 Tani | 5,805.17 | 5,526.59 | 6,788.35 | 8,506 | 7,741 | 10,128.67 |
| Bati | Tani | 8.04 | 24.32 | 47 | 211 | 538.17 | 420.81 |
| Jasi | Tani | 269,752.66 | 256,529.11 | 443,926.34 | 598,053 | 604,407.91 | 549,835.74 |
| Makaa ya mawe | Tani | 627,651.64 | 712,136.37 | 689,958.96 | 976,319 | 2,511,419.40 | 3,256,481.06 |
| Pozolana | Tani | 157,405.56 | 263,063.59 | 160,077.81 | 216,934 | 226,038.26 | 351,988.16 |
| Kaolin | Tani | 153,505.58 | 15,342.55 | 98,453.67 | 100,950 | 46,973.44 | 75,246.95 |
| Fedha | Kg | 10,262.28 | 12,607.07 | 13,186.58 | 9,324 | 13,602.43 | 14,481.35 |
| Shaba | Pound | - | - | 3,761,086.19 | 3,352,630 | 6,827,930.74 | 5,285,443.13 |
| Chuma | Tani | - | - | 28,431.17 | 78,190 | 51,071.14 | 67,626.44 |
| Bauxite | Tani | 10,795.71 | - | 25,995.00 | 38,142 | 40,920.98 | 61,353.23 |
| Madini ya ujenzi | 000 Tani | 10,374.49 | 20,188.47 | 31,891.75 | 32,304 | 37,498.03 | 33,807.05 |
| Madini mengine ya viwandani | 000 Tani | - | - | 2,160.57 | 1,037 | 1,458.38 | 1,745.02 |
| Madini mengine ya metali | 000 Tani | - | - | - | - | 93.41 | 63.55 |
| Makinikia ya shaba | Tani | - | - | 33,377.08 | - | 2,013.26 | 5,926.27 |
| Mbale za shaba (Copper ore) | Tani | - | - | 1,204.84 | - | 6,623.58 | 6,307.01 |

**Chanzo:** Wizara ya Madini
-Takwimu hazikupatikana
Carat = 0.205 gm

**Jedwali Na. 52: THAMANI YA MADINI YALIYOTOLEWA VIBALI KWA AJILI YA KUUZWA NJE YA NCHI**

| Aina ya Madini | | Kiasi | | | Thamani ('000 "US$) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kipimo | 2021 | 2022 | 2023 | 2021 | 2022 | 2023 |
| Almasi (Rough) | 000 Karati | 47,337 | 326 | 194 | 8,473 | 65,903 | 31,474 |
| Dhahabu | 000 Gramu | 42,902 | 62,512 | 62,781 | 2,831,840 | 2,850,345 | 3,021,627 |
| Vito (ghafi) | 000 Gramu | 4,463,669 | 15,017,635 | 98,891,510 | 16,501 | 19,415 | 28,456 |
| Vito (vilivyokatwa na kusanifiwa) | Karati | 166,728 | 93,351 | 101,153 | 7,425 | 2,480 | 2,622 |
| Chumvi | Tani | 21,095 | 22,225 | 34,350 | 2,360 | 2,375 | 3,509 |
| Phosphate | Tani | 15,632 | 40,710 | 9,934 | 3,442 | 6,944 | 3,646 |
| Bati | Tani | 155 | 564 | 440 | 4,603 | 12,505 | 7,061 |
| Jasi | Tani | 9,129 | 8,300 | 10,486 | 936 | 941 | 1,802 |
| Kinywe | Tani | 2,887 | 7,271 | 13,475 | 1,264 | 2,909 | 5,394 |
| Mawe ya chokaa | Tani | - | 194,980 | 249,396 | 1,944 | 1,806 | 6,344 |
| Fedha | 000 Gramu | 10,532 | 802 | 1214 | 9,284 | 629 | 886 |
| Shaba | 000 Lb | 4081 | 6993 | 4,156 | 4,293 | 3,879 | 2,273 |
| Makinikia ya shaba | Tani | 16,679 | 26,591 | 25,688 | 121,871 | 189,648 | 179.044 |
| Makinikia ya dhahabu | Tani | - | 2,730 | 2,554 | - | 8,993 | - |
| Bauxite | Tani | 12,570 | 14,790 | 14,430 | 630 | 758 | 795 |
| Makaa ya mawe | Tani | 346,779 | 848,434 | 1,601,850 | 11,838 | 43,806 | 158,575 |
| Madini ujenzi | Tani | 57,469 | 66,667 | 46,544 | 1,070 | 2,410 | 3,105 |
| Madini ya metali | Tani | 6,965 | 32,113 | 34,462 | 6,411 | 21,500 | 30,948 |
| Madini ya viwandani | Tani | 595,765 | 1,141,651 | 1,948,848 | 23,341,059 | 57,165,093 | 441,053,717 |
| **Jumla** | | | | | **23,353,707** | **57,438,522** | **441,256,822** |

**Chanzo:** Wizara ya Madini

## SURA YA 10

## VIWANDA NA BIASHARA

### Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani

233. Mwaka 2023, thamani ya bidhaa zilizozalishwa viwandani ilifikia shilingi bilioni 26,438.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 25,034.5 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa baadhi ya bidhaa uliongezeka ikiwemo, dawa za pareto (asilimia 87.9), konyagi (asilimia 38.0), nyavu za uvuvi (asilimia 31.0), unga wa ngano (asilimia 22.6) na rangi asilimia (17.8). Aidha, uzalishaji wa tabaka za mbao ulipungua kwa asilimia 29.7, nguo (asilimia 18.0), kamba za katani (asilimia 17.5), bati (asilimia 8.0) na biskuti na tambi (asilimia 7.2). Kwa upande mwingine, gharama za uzalishaji bidhaa viwandani ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 1.9 na kufikia shilingi bilioni 11,790.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11,574.6 mwaka 2022. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei za malighafi zinazotumika katika uzalishaji viwandani zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

**Jedwali Na. 10.1: Uzalishaji wa Baadhi ya Bidhaa Viwandani Mwaka 2019 - 2023**

| Aina ya Bidhaa | Kipimo | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Biskuti na tambi | Tani | 18,113 | 22,430 | 30,154 | 29,653 | 27,509 | -7.2 |
| Unga wa ngano | Tani | 680,393 | 767,476 | 737,652 | 684,708 | 839,266 | 22.6 |
| Konyagi | 000 Lita | 32,366 | 33,287 | 22,066 | 22,489 | 31,024 | 38.0 |
| Bia | 000 Lita | 391,299 | 385,851 | 380,464 | 456,035 | 498,611 | 9.3 |
| Chibuku | 000 Lita | 20,350 | 21,712 | 22,256 | 24,366 | 23,757 | -2.5 |
| Sigara | Milioni | 8,369 | 7,320 | 7,021 | 12,201 | 11,868 | -2.7 |
| Nguo | 000 $M^2$ | 45,415 | 53,067 | 65,365 | 48,504 | 39,774 | -18.0 |
| Kamba za katani | Tani | 9,287 | 8,187 | 8,583 | 6,171 | 5,093 | -17.5 |
| Nyavu za uvuvi | Tani | 254 | 261 | 273 | 461 | 604 | 31.0 |
| Tabaka za mbao | $M^3$ | 42,563 | 34,237 | 29,867 | 25,305 | 17,788 | -29.7 |
| Dawa za pareto | Tani | 145 | 154 | 152 | 173 | 325 | 87.9 |
| Rangi | 000 Lita | 58,024 | 48,261 | 62,785 | 64,028 | 75,423 | 17.8 |
| Saruji | 000 Tani | 6,514 | 6,496 | 6,531 | 7,598 | 7,673 | 1.0 |
| Chuma | Tani | 272,531 | 277,785 | 293,797 | 311,781 | 343,575 | 10.2 |
| Bati | Tani | 100,963 | 107,836 | 119,844 | 129,038 | 118,767 | -8.0 |
| Betri | Milioni | 120 | 132 | - | - | - | |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
-Takwimu hazikupatikana

### Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

234. Mwaka 2023, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo - SIDO lilitoa mafunzo mbalimbali kwa wajasiriamali 22,139 ikilinganishwa na wajasiriamali 19,188 waliopata mafunzo mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Ongezeko hilo lilitokana na

mwitikio wa wananchi kupata mafunzo ikiwemo, kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Mafunzo hayo yalihusu: usindikaji wa mafuta ya kula na vyakula vya mifugo; utengenezaji wa bidhaa za ngozi, chaki na vibuyu; ubanguaji korosho na uhifadhi na usindikaji vyakula; mbinu za uzalishaji mali na biashara; utunzaji wa vitabu vya hesabu; na uongozi wa vikundi/vyama.

235. Mwaka 2023, SIDO kupitia Vituo vya Uendelezaji Teknolojia - TDCs ilitengeneza na kusambaza mashine 878 ikilinganishwa na mashine 743 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 18.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mashine za uchakataji wa mazao ya kilimo, mifugo, madini, misitu na uvuvi pamoja na kusimikwa kwa mitambo ya kisasa ya uzalishaji wa mashine. Aidha, katika kuwaendeleza wajasiriamali wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya, wajasiriamali nane (8) walipata mafunzo ya kukuza vipaji vyao mwaka 2023 ikilinganishwa na wajasiriamali 17 waliopata mafunzo hayo mwaka 2022. Vile vile, wajasiriamali 29,640 walipatiwa ushauri wa kiufundi na biashara mwaka 2023 ikilinganishwa na wajasiriamali 23,465 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 26.3. Hii ilitokana na mwitikio mkubwa wa wananchi kuanzisha miradi ili kujiongezea kipato na kukabiliana na changamoto za ajira.

236. Mwaka 2023, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali - NEDF ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.4 kwa wajasiriamali 2,038 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.5 zilizotolewa kwa wajasiriamali 2,785 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 16.9 wa mikopo iliyotolewa. Aidha, mikopo iliyotolewa iliwezesha upatikanaji wa fursa za ajira 4,532 mwaka 2023 ikilinganishwa na fursa za ajira 7,771 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 41.7. Kwa upande mwingine, hali ya marejesho ya mkopo iliendelea kuimarika na kufikia asilimia 92.1 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 91.6 mwaka 2022.

237. Mwaka 2023, Chuo cha Elimu ya Biashara - CBE kilitoa mafunzo ya kozi 33 za muda mfupi zinazohusu elimu ya biashara katika fani mbalimbali kwa washiriki 305 ikilinganishwa na kozi 16 za muda mfupi kwa washiriki 675 mwaka 2022. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kozi za muda mfupi katika nyanja za biashara.

238. Mwaka 2023, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO lilifanya tafiti saba (7) ikilinganishwa na tafiti tatu (3) zilizofanyika mwaka 2022. Tafiti hizo zilijumuisha: uibuaji wa fursa za uwekezaji kupitia *industrial mapping*; matumizi ya vumbi la makaa ya mawe kutengeneza mkaa mbadala; matumizi ya mkaa mbadala; kuinua vipaji na kuendeleza ubunifu; uandaaji wa ramani za viwanda vya nguo, ngozi na katani; matumizi bora ya nishati; na malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea.

239. Mwaka 2023, TIRDO ilitoa huduma za kitaalamu kuhusu mazingira, matumizi bora ya nishati na upimaji kwa viwanda 18 ikilinganishwa na viwanda 11 mwaka 2022, sawa na

ongezeko la asilimia 63.6. Aidha, TIRDO ilipima sampuli 188 za maabara mwaka 2023 ikilinganishwa na sampuli 75 mwaka 2022. Ongezeko la huduma za kitaalamu na sampuli zilizopimwa lilitokana na kuboreshwa kwa huduma za maabara na uhamasishaji kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

240. Mwaka 2023, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - CAMARTEC kiliboresha, kuzalisha na kununua aina 338 za zana za kilimo na teknolojia vijijini ikilinganishwa na aina 204 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 65.7. Mchanganuo wa zana za kilimo na teknolojia ni kama ifuatavyo: mashine 18 za kufanya usanifu wa teknolojia za kilimo, kupanda na kupura mazao; mashine 129 katika Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi, mashine 49 katika kiwanda darasa cha kubangua korosho; na vifaa 142 vya kuzimia moto.

241. Mwaka 2023, CAMARTEC ilifanya kaguzi na majaribio ya aina 82 za zana za kilimo zilizozalishwa nje ya nchi ikilinganishwa na kaguzi na majaribio ya aina 76 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.9. Aidha, CAMARTEC ilitoa mafunzo kuhusu ubanguaji korosho, matumizi ya mashine za kufyatua tofali na kuchakata malisho ya mifugo kwa vijana 63 ikilinganishwa na vijana 68 mwaka 2022.

242. Mwaka 2023, Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania - TEMDO ilisanifu teknolojia tisa (9) zilizowezesha utengenezaji wa mitambo minne (4) ya kuchakata mbegu za alizeti, majokofu mawili (2) ya kisasa na tenki moja la kisasa la kutunza na kusafirisha mafuta ikilinganishwa na teknolojia 12 zilizosanifiwa na kutengeneza mashine nne (4) mwaka 2022. Aidha, TEMDO ilitoa mafunzo kwa wahitimu 63 kutoka vyuo vya awali (VETA), vyuo vya kati na vyuo vikuu ili kuwajengea uwezo kwa vitendo kupitia teknolojia mbalimbali kwenye sekta za viwanda, afya, kilimo na mifugo ikilinganishwa na wahitimu 50 mwaka 2022.

243. Mwaka 2023, Serikali kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania - TanTrade iliratibu programu 17 za mafunzo kwa wafanyabiashara 2,150 ikilinganishwa na programu 10 kwa wafanyabiashara 307 mwaka 2022. Mafunzo hayo yalijumuisha: usimamizi na uendeshaji wa biashara; utafutaji wa masoko ndani na nje ya nchi; na jinsi ya kutumia fursa za biashara katika Soko Huru la Afrika.

**Usajili wa Biashara na Viwanda**

244. Mwaka 2023, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni - BRELA ilisajili kampuni 15,397 ikilinganishwa na kampuni 13,756 zilizosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.9. Aidha, majina ya biashara 29,448 yalisajiliwa mwaka 2023 ikilinganishwa na majina ya biashara 25,507 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 15.5. Vile vile, leseni 18,448 za biashara daraja “A” zilitolewa mwaka 2023 ikilinganishwa na leseni 14,263 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 29.3. Ongezeko hilo lilitokana na

kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya biashara ikiwemo, matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa leseni, utoaji wa mafunzo kwa maafisa biashara na elimu kwa umma. Kwa upande mwingine, BRELA ilitoa leseni 253 za viwanda mwaka 2023 ikilinganishwa na leseni 165 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 53.3.

245. Mwaka 2023, alama 3,829 za biashara na huduma zilisajiliwa na BRELA ikilinganishwa na alama 3,607 za biashara na huduma zilizosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Hii ilitokana na kuimarika kwa mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Aidha, BRELA ilipokea na kufanyia kazi maombi 538 ya kuwekea ulinzi uvumbuzi wa sayansi na teknolojia mwaka 2023 ikilinganishwa na maombi 497 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Kati ya hayo, maombi 76 yalikuwa ya ndani na maombi 462 yalipitia Shirika la Kanda la Afrika linalosimamia Haki Miliki za Kitaaluma - ARIPO.

**Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa**

246. Mwaka 2023, kampuni 3,500 zilishiriki katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ikilinganishwa na kampuni 3,425 mwaka 2022. Kati ya hizo, kampuni 3,233 zilikuwa za ndani na kampuni 267 kutoka nje ya nchi. Aidha, nchi 19 zilishiriki katika maonesho mwaka 2023 ikilinganishwa na nchi 23 mwaka 2022. Vile vile, mikataba ya kibiashara isiyofungani yenye thamani ya shilingi bilioni 16.98 ilisainiwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 176 iliyosainiwa mwaka 2022. Ajira za muda mfupi takribani 11,869 zilipatikana katika maonesho ya mwaka 2023 ikilinganishwa na ajira 11,852 mwaka 2022.

247. Mwaka 2023, wadau 164 kutoka viwanda vidogo, vya kati na vikubwa pamoja na Wizara na Taasisi za Serikali walishiriki katika Maonesho ya Nane ya bidhaa za viwanda yaliyofanyika Dar es Salaam ikilinganishwa na wadau 502 walioshiriki mwaka 2022. Upungufu huo ulitokana na mwitikio mdogo wa wadau wa viwanda kushiriki katika Maonesho.

**Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo**

248. Mwaka 2023, Shirika la Viwango Tanzania - TBS liliandaa viwango 627 vya ubora ikilinganishwa na viwango 537 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 16.8. Ongezeko hilo lilitokana na mwitikio mkubwa wa wazalishaji na watumiaji wa bidhaa katika kuzingatia ubora na usalama wa bidhaa. Katika kipindi hicho, sampuli 28,791 zilipimwa ikilinganishwa na sampuli 32,817 zilizopimwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 12.3. Upungufu huo ulitokana na bidhaa nyingi kukaguliwa na mawakala walioko nje ya nchi kupitia mfumo wa kukagua bidhaa kabla ya usafirishaji - PVoC. Aidha, vifaa 10,564 vilifanyiwa uhakiki/ugezi mwaka 2023 ikilinganishwa na vifaa 9,473 mwaka 2022, sawa na

ongezeko la asilimia 11.5. Ongezeko hilo lilitokana na maabara nyingi za afya kupata vyeti vya umahiri na kuhitaji uhakiki/ugezi.

249. Mwaka 2023, Shirika la Viwango Tanzania lilitoa leseni 733 za ubora ikilinganishwa na leseni 836 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 12.3. Kati ya hizo, leseni 366 zilitolewa kwa wazalishaji wakubwa na wa kati, na leseni 367 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo. Aidha, mafunzo ya aina 73 ya udhibiti ubora yalitolewa kwa washiriki 2,194 ikilinganishwa na mafunzo 68 yaliyotolewa kwa washiriki 2,890 mwaka 2022.

250. Mwaka 2023, Shirika la Viwango Tanzania lilisajili bidhaa 1,623 za chakula na vipodozi ikilinganishwa na bidhaa 1,827 zilizosajiliwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 11.2. Hii ilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa kulikosababisha maombi machache ya usajili. Kati ya hizo, bidhaa 1,278 zilikuwa za chakula na bidhaa za vipodozi 345. Aidha, vibali 9,775 vya maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi vilitolewa mwaka 2023 ikilinganishwa na vibali 8,915 vilivyotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.6. Ongezeko hilo lilitokana na mwitikio wa wahusika wa majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa kuzingatia ubora na usalama wa bidhaa. Kati ya hivyo, vibali 8,082 vilikuwa vya maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vibali 1,693 vya bidhaa za vipodozi.

251. Mwaka 2023, Shirika la Viwango Tanzania lilikagua magari 48,075 yaliyotumika ikilinganishwa na magari 43,982 yaliyokaguliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.3. Kati ya hayo, magari 46,927 yalikidhi viwango vya ubora na kuruhusiwa kutumika nchini na magari 1,148 hayakukidhi viwango. Aidha, bidhaa 37,826 kutoka nje ya nchi zilikaguliwa kupitia mawakala wa Shirika kabla ya kuingizwa nchini ikilinganishwa na bidhaa 33,707 zilizokaguliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 12.2. Kati ya hizo, bidhaa 357 hazikukidhi viwango vya ubora na wateja waliomiliki bidhaa hizo walipatiwa Non-Conformity Certificates ili kuzuiwa kuingiza bidhaa hizo nchini. Vile vile, Shirika lilifanya ukaguzi wa bidhaa 62,796 kupitia mfumo wa ukaguzi bidhaa baada ya kuwasili nchini ikilinganishwa na bidhaa 80,138 mwaka 2022. Kati ya bidhaa zilizokaguliwa, bidhaa 2,624 hazikukidhi viwango vya ubora.

252. Mwaka 2023, Wakala wa Vipimo - WMA ilihakiki vipimo 971,541 ikilinganishwa na vipimo 862,024 vilivyohakikiwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 12.7. Ongezeko hilo lilitokana na utoaji wa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu matumizi ya vipimo sahihi. Aidha, Wakala ilifanya kaguzi za kushtukiza 5,445 za vipimo vinavyotumika kwenye biashara, afya, usalama na mazingira ikilinganishwa na kaguzi 5,123 zilizokaguliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vitendea kazi vilivyorahisisha kufikia maeneo mengi zaidi. Vile vile, aina mpya 214 za vipimo

kutoka ndani na nje ya nchi zilipimwa mwaka 2023 ikilinganishwa na aina 130 zilizopimwa mwaka 2022. Kati ya hizo, aina 153 za vipimo ziliidhinishwa na aina 61 hazikuidhinishwa.

253. Mwaka 2023, Wakala ilitoa leseni na vibali 447 kwa mafundi wanaojihusisha na uundaji, usimikaji na urekebishaji wa vipimo ikilinganishwa na leseni na vibali 412 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.5. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutolewa kwa elimu kwa wadau mbalimbali wa vipimo kuhusu umuhimu wa kuwa na vibali na leseni. Aidha, Wakala iliendelea kusimamia matumizi sahihi ya vipimo wakati wa upakuaji na upokeaji wa mafuta ya kupikia na petroli yaliyoingizwa nchini. Katika kipindi hicho, meli 147 zenye ujazo wa lita milioni 8,547.52 zilihakikiwa ikilinganishwa na meli 143 zenye ujazo wa lita milioni 8,291.3 mwaka 2022.

**Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia**

254. Mwaka 2023, Tume ya Ushindani - FCC iliidhinisha maombi ya muungano wa kampuni 54 ikilinganishwa na maombi 97 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 44.3. Maombi hayo yalitoka katika sekta za kilimo, uzalishaji, fedha, afya, mawasiliano, madini, biashara na nishati. Aidha, mikataba 48 ya walaji kutoka sekta ya fedha ilisajiliwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mikataba 60 iliyosajiliwa mwaka 2022.

255. Mwaka 2023, Tume ya Ushindani ilikagua makasha 6,909 ya kusafirishia mizigo ikilinganishwa na makasha 11,718 yaliyokaguliwa mwaka 2022. Kati ya hayo, makasha 390 yenye thamani ya shilingi bilioni 17.1 yalibainika kuwa na bidhaa bandia. Bidhaa hizo zilikuwa ni zana za kilimo, vilainishi vya magari, vipuri vya magari na pikipiki, vifaa vya matumizi ya nyumbani, vifaa vya ujenzi, shajala pamoja na vifaa vya kielektroniki.

**Shirika la Maendeleo la Taifa**

256. Mwaka 2023, Shirika la Maendeleo la Taifa - NDC kupitia Mradi wa mashamba ya mpira ya Kihuhwi (Muheza) na Kalunga (Kilombero) lilizalisha tani 95.3 ikilinganishwa na tani 80.3 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 18.7. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa kwa usimamizi na kuanzishwa kwa mfumo wa malipo taslimu uliovutia wagemaji wengi na hivyo kuongeza uzalishaji. Aidha, kiwanda cha viuadudu kilizalisha lita 65,202 za viuadudu kwa ajili ya kuua viluilui vya aina mbalimbali za mbu, hususan wanaoeneza malaria mwaka 2023 ikilinganishwa na lita 15,504 zilizozalishwa mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na maboresho yaliyofanyika katika mitambo ya uzalishaji. Vile vile, uzalishaji huo ulifanikisha mauzo ya shilingi milioni 963.79 mwaka 2023. Kati ya mauzo hayo, mauzo nje katika nchi za Kenya na Msumbiji yalikuwa shilingi milioni 208.74 na mauzo ya ndani ya nchi yalikuwa shilingi milioni 755.05 ikilinganishwa na mauzo ndani ya shilingi milioni 405.88 mwaka 2022.

257. Mwaka 2023, Shirika la Maendeleo la Taifa kupitia kiwanda cha kuunganisha magari cha GF Assemblers Ltd liliunganisha magari 1,120 ikilinganishwa na magari 595 yaliyounganishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 88.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya magari. Kiwanda kinaunganisha magari aina tatu (3) ambayo ni FAW Trucks, SAIC vehicle na Fulland vehicle. Katika kipindi hicho, Shirika kupitia kiwanda cha mashine na vipuri - KMTC kilizalisha mashine 33 na kukamilisha kazi za vipuri vya mashine 25.

**Jedwali Na. 53: MATUMIZI YA SARUJI NCHINI**

| Mwaka | Kutoka Nje | Uuzaji nje | Uzalishaji wa Ndani | Matumizi Tani | Badiliko ( Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2010 | 566,828 | 189,321 | 2,312,055 | 2,689,562 | 12.1 |
| 2011 | 768,343 | 217,944 | 2,408,765 | 2,959,164 | 10.0 |
| 2012 | 1,013,986 | 145,793 | 2,557,798 | 3,425,991 | 15.8 |
| 2013 | 1,218,453 | 154,481 | 2,369,819 | 3,433,791 | 0.2 |
| 2014 | 1,428,995 | 142,001 | 2,795,687 | 4,082,681 | 18.9 |
| 2015r | 896,872 | 129,083 | 3,140,160 | 4,404,187 | 7.9 |
| 2016 | 513,307 | 253,506 | 4,047,712 | 4,307,513 | -2.2 |
| 2017 | 188,599 | 226,588 | 4,397,684 | 4,359,696 | 1.2 |
| 2018 | 341,179 | 196,449 | 4,540,309 | 4,685,039 | 7.5 |
| 2019 | 448,579 | 410,607 | 5,290,878 | 5,328,850 | 13.7 |
| 2020 | 716,929 | 493,867 | 5,605,626 | 5,828,688 | 9.4 |
| 2021 | 690,474 | 441,828 | 6,614,359 | 6,863,004 | 17.7 |
| 2022 | 566,826 | 632,726 | 7,598,073 | 7,532,173 | 9.8 |
| 2023* | 809,199 | 531,699 | 7,673,016 | 7,950,515 | 5.6 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa Takwimu na TRA
* Takwimu za awali
r – Takwimu zimeboreshwa kuondoa clinker ambayo sio final product bali intermidiate

**Jedwali Na. 54: UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI**

| Aina ya Bidhaa | Kipimo | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021r | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) 2022/23 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Biskuti & tambi | Tani | 15,890 | 16,451 | 16,911 | 18,113 | 22,430 | 30,154 | 29,653 | 27,509 | -7.2 |
| Unga wa ngano | Tani | 498,940 | 606,432 | 662,967 | 680,393 | 767,476 | 737,652 | 684,708 | 839,266 | 22.6 |
| Konyagi | 000 Lita | 28,754 | 25,555 | 29,335 | 32,366 | 33,287 | 22,066 | 22,489 | 31,024 | 38.0 |
| Bia | 000 Lita | 383,251 | 396,864 | 412,555 | 391,299 | 385,851 | 380,464 | 456,035 | 498,611 | 9.3 |
| Chibuku | 000 Lita | 26,513 | 22,624 | 20,819 | 20,350 | 21,712 | 22,256 | 24,366 | 23,757 | -2.5 |
| Sigara | Milioni | 8,091 | 7,412 | 7,921 | 8,369 | 7,320 | 7,021 | 12,201 | 11,868 | -2.7 |
| Nguo | 000 $M^2$ | 76,436 | 52,052 | 52,613 | 45,415 | 53,067 | 65,365 | 48,504 | 39,774 | -18.0 |
| Kamba za katani | Tani | 9,216 | 8,188 | 8,148 | 9,287 | 8,187 | 8,583 | 6,171 | 5,093 | -17.5 |
| Nyavu za uvuvi | Tani | 312 | 196 | 228 | 254 | 261 | 273 | 461 | 604 | 31.0 |
| Tabaka za mbao | $M^2$ | 34,983 | 37,302 | 37,849 | 42,563 | 34,237 | 29,867 | 25,305 | 17,788 | -29.7 |
| Dawa za pareto | Tani | 126 | 134 | 139 | 145 | 154 | 152 | 173 | 325 | 87.9 |
| Rangi | 000 Lita | 35,096 | 40,146 | 47,928 | 58,024 | 48,261 | 62,785 | 64,028 | 75,423 | 17.8 |
| Saruji | 000 Tani | 4,047 | 4,397 | 4,540 | 5,290 | 5,605 | 6,614 | 7,598 | 7,673 | 1.0 |
| Chuma* | Tani | 65,686 | 231,591 | 275,267 | 266,314 | 277,785 | 293,797 | 311,781 | 343,575 | 10.2 |
| Bati | Tani | 91,421 | 84,541 | 84,132 | 100,963 | 107,836 | 119,844 | 129,038 | 118,767 | -8.0 |
| Betri | Milioni | 69 | 122 | 115 | 120 | 132 | - | - | - | - |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara
-Hakuna uzalishaji
* Takwimu za uzalishaji wa chuma kuanzia mwaka 2008 - 2018 zimerekebishwa
r takwimu zimeboreshwa

**Jedwali Na. 55: VIWANDA: IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA**

| ISIC Rev.4 | Shughuli | Walioajiriwa | | | Wengine | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021* | 2022* | 2023* | 2021* | 2022* | 2023* | 2021* | 2022* | 2023* |
| 10 | Vyakula | 110,456 | 113,772 | 128,606 | 17,154 | 17,128 | 25,189 | 127,610 | 130,900 | 153,795 |
| 11 | Vinywaji | 10,406 | 10,718 | 37,026 | 68 | 68 | 7,758 | 10,474 | 10,786 | 44,784 |
| 12 | Tumbaku na Sigara | 7,637 | 7,866 | 7,501 | 5 | 5 | 2,104 | 7,642 | 7,871 | 9,605 |
| 13,14 | Ufumaji na Ushonaji | 55,262 | 56,921 | 43,938 | 16,902 | 16,876 | 2,455 | 72,164 | 73,797 | 46,393 |
| 15 | Ngozi Bidhaa za Ngozi | 2,331 | 2,401 | 7,116 | 253 | 301 | 782 | 2,584 | 2,702 | 7,898 |
| 16 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 12,319 | 12,689 | 8,474 | 1,765 | 1,762 | 1,555 | 14,084 | 14,451 | 10,029 |
| 17, 18 | Karatasi, Uchapishaji | 8,202 | 8,448 | 10,752 | 161 | 161 | 468 | 8,363 | 8,609 | 11,220 |
| 20, 21 | Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu | 10,940 | 11,268 | 19,982 | 181 | 221 | 3,317 | 11,121 | 11,489 | 23,299 |
| 22 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 6,449 | 6,643 | 11,279 | 45 | 63 | 1,149 | 6,494 | 6,706 | 12,428 |
| 23 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 13,004 | 13,394 | 14,407 | 1,032 | 1,030 | 2,852 | 14,036 | 14,424 | 17,259 |
| 19, 24-33 | Nyinginezo | 57,297 | 59,017 | 35,548 | 13,746 | 13,725 | 2,290 | 71,043 | 72,742 | 37,838 |
| | **Jumla** | **294,303** | **303,137** | **324,629** | **51,312** | **51,340** | **49,919** | **345,615** | **354,477** | **374,548** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013, 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

- Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## Jedwali Na. 56: VIWANDA: GHARAMA ZA KAZI

| ISIC Rev.4 | Shughuli | Mishahara (TShs. Milioni) | | | Malipo Mengine (TShs. Milioni) | | | Jumla (TShs. Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021* | 2022* | 2023* | 2021* | 2022* | 2023* | 2021* | 2022* | 2023* |
| 10 | Vyakula | 580,251 | 638,276 | 708,073 | 106,232 | 116,855 | 107,197 | 686,483 | 755,131 | 815,270 |
| 11 | Vinywaji | 355,612 | 391,173 | 433,949 | 151,136 | 166,249 | 152,508 | 506,748 | 557,422 | 586,457 |
| 12 | Tumbaku na Sigara | 158,405 | 174,246 | 193,300 | 44,301 | 48,731 | 44,703 | 202,706 | 222,977 | 238,003 |
| 13,14 | Ufumaji na Ushonaji | 176,504 | 194,154 | 215,385 | 93,162 | 102,478 | 94,008 | 269,666 | 296,632 | 309,393 |
| 15 | Ngozi Bidhaa za Ngozi | 10,030 | 11,033 | 12,239 | 1,014 | 1,115 | 1,022 | 11,044 | 12,148 | 13,261 |
| 16 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 46,691 | 51,360 | 56,976 | 6,611 | 7,272 | 6,672 | 53,302 | 58,632 | 63,648 |
| 17, 18 | Karatasi, Uchapishaji | 84,844 | 93,328 | 103,534 | 18,812 | 20,693 | 18,983 | 103,656 | 114,021 | 122,517 |
| 20, 21 | Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu | 115,182 | 126,700 | 140,556 | 18,000 | 19,800 | 18,164 | 133,182 | 146,500 | 58,720 |
| 22 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 59,191 | 65,110 | 72,230 | 8,704 | 9,574 | 8,782 | 67,895 | 74,684 | 81,012 |
| 23 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 155,922 | 171,514 | 190,269 | 47,259 | 51,985 | 47,688 | 203,181 | 223,499 | 237,957 |
| 19, 24-33 | Nyinginezo | 257,222 | 282,944 | 313,884 | 53,529 | 58,882 | 54,015 | 310,751 | 341,826 | 367,899 |
| | **Jumla** | **1,999,854** | **2,199,838** | **2,440,395** | **548,760** | **603,634** | **553,742** | **2,548,614** | **2,803,472** | **2,994,137** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani
Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

**Jedwali Na. 57:VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO**

| ISIC Rev.4 | Shughuli | PATO (TShs. Milioni) | | | GHARAMA (TShs. Milioni) | | | Thamani iliyoongezeka (Value added) (TShs. Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2021*** | **2022*** | **2023*** | **2021*** | **2022*** | **2023*** | **2021*** | **2022*** | **2023*** |
| 10 | Vyakula | 8,804,671 | 9,685,138 | 10,228,274 | 4,046,478 | 4,451,126 | 4,534,228 | 4,758,193 | 5,234,012 | 5,694,046 |
| 11 | Vinywaji | 3,631,031 | 3,994,134 | 4,218,122 | 1,087,259 | 1,195,985 | 1,218,315 | 2,543,772 | 2,798,149 | 2,999,807 |
| 12 | Tumbaku na Sigara | 1,364,477 | 1,500,925 | 1,585,095 | 342,445 | 376,689 | 383,722 | 1,022,032 | 1,124,236 | 1,201,373 |
| 13,14 | Ufumaji na Ushonaji | 1,065,473 | 1,172,020 | 1,237,746 | 487,762 | 536,538 | 546,555 | 577,711 | 635,482 | 691,191 |
| 15 | Ngozi Bidhaa za Ngozi | 119,585 | 131,543 | 138,920 | 81,180 | 89,298 | 90,965 | 38,405 | 42,245 | 47,955 |
| 16 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 323,716 | 356,088 | 376,057 | 107,382 | 118,120 | 120,325 | 216,334 | 237,968 | 255,732 |
| 17, 18 | Karatasi, Uchapishaji | 585,215 | 643,736 | 679,837 | 362,366 | 398,603 | 406,045 | 222,849 | 245,133 | 273,792 |
| 20, 21 | Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu | 1,281,796 | 1,409,976 | 1,489,048 | 802,088 | 882,297 | 898,770 | 479,708 | 527,679 | 590,278 |
| 22 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 1,316,648 | 1,448,313 | 1,529,533 | 851,345 | 936,479 | 953,963 | 465,303 | 511,834 | 575,570 |
| 23 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 1,681,231 | 1,849,354 | 1,953,064 | 853,214 | 938,535 | 956,057 | 828,017 | 910,819 | 997,007 |
| 19, 24-33 | Nyinginezo | 2,584,830 | 2,843,313 | 3,002,764 | 1,500,865 | 1,650,951 | 1,681,774 | 1,083,965 | 1,192,361 | 1,320,990 |
| | **Jumla** | **22,758,673** | **25,034,540** | **26,438,460** | **10,522,384** | **11,574,622** | **11,790,719** | **12,236,289** | **13,459,918** | **14,647,741** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani
Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## Jedwali Na. 58: VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA

| Jina la Mkoa | Idadi ya Wafanyakazi | | | Idadi ya waajiriwa | | | Mishahara (TShs.Milioni) | | | Thamani Iliyoongezeka (TShs. Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2021* | 2022* | 2023* | 2021* | 2022* | 2023* | 2021* | 2022* | 2023* | 2021* | 2022* | 2023* |
| Dodoma | 3,740 | 3,836 | 4,053 | 3,184 | 3,280 | 3,512 | 25,025 | 27,527 | 30,537 | 153,120 | 168,432 | 183,296 |
| Arusha | 29,333 | 30,085 | 31,789 | 24,978 | 25,728 | 27,552 | 84,967 | 93,464 | 103,684 | 519,888 | 571,877 | 622,345 |
| Kilimanjaro | 22,025 | 22,590 | 23,870 | 18,756 | 19,319 | 20,689 | 107,624 | 118,386 | 131,332 | 658,512 | 724,363 | 788,285 |
| Tanga | 16,627 | 17,053 | 18,019 | 14,159 | 14,584 | 15,618 | 134,114 | 147,525 | 163,657 | 820,593 | 902,652 | 982,310 |
| Morogoro | 52,104 | 53,440 | 56,466 | 44,367 | 45,699 | 48,939 | 56,898 | 62,588 | 69,432 | 348,128 | 382,941 | 416,735 |
| Pwani | 16,218 | 16,634 | 17,576 | 13,811 | 14,226 | 15,235 | 80,724 | 88,796 | 98,507 | 493,915 | 543,307 | 591,254 |
| Dar es Salaam | 111,517 | 114,376 | 120,853 | 94,959 | 97,809 | 104,744 | 1,148,323 | 1,263,154 | 1,401,282 | 7,026,113 | 7,728,724 | 8,410,776 |
| Lindi | 1,663 | 1,706 | 1,802 | 1,418 | 1,461 | 1,565 | 510 | 561 | 622 | 3,126 | 3,439 | 3,741 |
| Mtwara | 4,822 | 4,946 | 5,225 | 4,106 | 4,229 | 4,529 | 19,043 | 20,947 | 23,238 | 116,511 | 128,162 | 139,472 |
| Ruvuma | 3,111 | 3,191 | 3,372 | 2,649 | 2,729 | 2,923 | 3,839 | 4,223 | 4,684 | 23,498 | 25,848 | 28,129 |
| Iringa | 8,292 | 8,505 | 8,987 | 7,061 | 7,273 | 7,788 | 45,425 | 49,967 | 55,431 | 277,932 | 305,725 | 332,705 |
| Mbeya | 9,931 | 10,186 | 10,763 | 8,456 | 8,710 | 9,327 | 92,415 | 101,656 | 112,773 | 565,447 | 621,992 | 676,882 |
| Singida | 3,842 | 3,941 | 4,164 | 3,273 | 3,371 | 3,610 | 3,324 | 3,656 | 4,056 | 20,332 | 22,365 | 24,339 |
| Tabora | 1,225 | 1,256 | 1,327 | 1,041 | 1,072 | 1,148 | 18,330 | 20,163 | 22,368 | 112,154 | 123,369 | 134,256 |
| Rukwa | 2,560 | 2,626 | 2,774 | 2,179 | 2,244 | 2,403 | 10,588 | 11,647 | 12,922 | 64,781 | 71,259 | 77,548 |
| Kigoma | 3,115 | 3,195 | 3,376 | 2,653 | 2,733 | 2,927 | 1,784 | 1,962 | 2,176 | 10,919 | 12,011 | 13,071 |
| Shinyanga | 4,582 | 4,698 | 4,964 | 3,902 | 4,019 | 4,304 | 18,207 | 20,028 | 22,218 | 111,397 | 122,537 | 133,351 |
| Kagera | 5,969 | 6,122 | 6,469 | 5,083 | 5,236 | 5,607 | 8,478 | 9,326 | 10,344 | 51,868 | 57,055 | 62,091 |
| Mwanza | 18,279 | 18,748 | 19,810 | 15,565 | 16,032 | 17,168 | 106,448 | 117,093 | 129,898 | 651,314 | 716,445 | 779,671 |
| Mara | 5,856 | 6,006 | 6,345 | 4,987 | 5,137 | 5,501 | 9,302 | 10,232 | 11,351 | 56,906 | 62,597 | 68,121 |
| Manyara | 8,519 | 8,736 | 9,230 | 7,253 | 7,471 | 8,000 | 4,428 | 4,871 | 5,404 | 27,099 | 29,809 | 32,440 |
| Njombe | 4,559 | 4,676 | 4,940 | 3,883 | 4,000 | 4,284 | 8,452 | 9,297 | 10,314 | 51,717 | 56,889 | 61,909 |
| Katavi | 2,362 | 2,423 | 2,560 | 2,012 | 2,072 | 2,219 | 1,818 | 2,000 | 2,219 | 11,123 | 12,235 | 13,315 |
| Simiyu | 2,904 | 2,978 | 3,147 | 2,473 | 2,546 | 2,725 | 6,787 | 7,466 | 8,283 | 41,536 | 45,690 | 49,722 |
| Geita | 997 | 1,023 | 1,081 | 849 | 874 | 938 | 334 | 369 | 409 | 2,043 | 2,247 | 2,445 |
| Songwe | 1,463 | 1,501 | 1,586 | 1,246 | 1,283 | 1,374 | 2,667 | 2,934 | 3,254 | 16,317 | 17,948 | 19,532 |
| **Jumla** | **345,615** | **354,477** | **374,548** | **294,303** | **303,137** | **324,629** | **1,999,854** | **2,199,838** | **2,440,395** | **12,236,289** | **13,459,918** | **14,647,741** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani
Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

# SURA YA 11

## UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

### UJENZI

**Mtandao wa Barabara Nchini**

258. Mwaka 2023, mtandao wa barabara nchini ulifikia kilometa 181,655.49 ikilinganishwa na kilometa 181,190.06 mwaka 2022. Kati ya kilometa hizo, mtandao unaosimamiwa na Wakala wa Barabara nchini - TANROADS ni kilometa 37,225.72 na mtandao unaosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini - TARURA ni kilometa 144,429.77.

259. Mwaka 2023, mtandao wa barabara zinazosimamiwa na TANROADS ulifikia kilometa 37,225.72 kutoka kilometa 36,760.29 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kufunguliwa kwa barabara mpya, kukasimishwa kwa barabara za wilaya na kupandishwa hadhi kwa baadhi ya barabara za wilaya na kuwa barabara za mikoa. Aidha, mtandao wa barabara unaosimamiwa na TANROADS unajumuisha kilometa 12,336 za barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani na kilometa 24,889.72 za barabara za mikoa zinazounganisha miji mikuu ya mikoa na wilaya.

260. Hadi Desemba 2023, barabara kuu na za mikoa zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilizofanyiwa tathmini zilikuwa na urefu wa kilometa 34,150.76, ikilinganishwa na kilometa 35,269.38 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 3.2. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya sehemu katika barabara kuwepo katika hatua za ujenzi. Kati ya barabara zilizofanyiwa tathmini, kilometa 3,219.43 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 17,945.45 katika hali ya wastani na kilometa 12,985.88 katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 3,806.47, kilometa 18,818.76 na kilometa 12,644.15 mtawalia mwaka 2022. Barabara zenye hali nzuri ziliongezeka kutokana na matengenezo yanayoendelea kufanyika.

261. Hadi Desemba 2023, barabara kuu zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilizofanyiwa tathmini zilikuwa na urefu wa kilometa 10,750.72 ikilinganishwa na kilometa 11,158.23 zilizofanyiwa tathmini mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 3.7. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya sehemu za barabara kuwa katika hatua za matengenezo na ujenzi. Kati ya kilometa zilizofanyiwa tathmini, kilometa 1,345.44 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 3,377.99 hali ya wastani na kilometa 6,027.29 hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 1,619.15 zilizokuwa katika hali mbaya, kilometa 3,372.89 hali ya wastani na kilometa 6,166.19 hali nzuri mwaka 2022.

262. Mwaka 2023, kilometa 23,400.04 za barabara za mikoa zinazounganisha mikoa na wilaya zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilifanyiwa tathmini ikilinganishwa na kilometa 24,111.15 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 2.9. Upungufu huo

ulitokana na baadhi ya sehemu ya barabara kuwa katika hatua za matengenezo na ujenzi. Kati ya barabara hizo, kilometa 1,873.99 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 14,567.46 hali ya wastani na kilometa 6,958.59 zilikuwa na hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 2,187.32 zilizokuwa katika hali mbaya, kilometa 15,445.87 hali ya wastani na kilometa 6,477.96 hali nzuri mwaka 2022. Kuongezeka kwa barabara zenye hali nzuri kulitokana na uwepo wa hali ya hewa nzuri katika kipindi ambacho tathmini ya barabara hizo ikifanyika.

**Jedwali Na. 11.1: Hali ya Mtandao wa Barabara Zilizofanyiwa Tathmini Mwaka 2023**

| Aina ya Barabara | Nzuri | | Wastani | | Mbaya | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kilometa | % | Kilometa | % | Kilometa | % | Kilometa |
| Barabara kuu lami | 5,372.41 | 61.7 | 2,121.48 | 24.4 | 1,216.10 | 14 | 8,709.99 |
| Barabara kuu changarawe/udongo | 654.88 | 32.1 | 1,256.51 | 61.6 | 129.34 | 6.3 | 2,040.73 |
| **Jumla ndogo** | **6,027.29** | 56.1 | **3,377.99** | 31.4 | **1,345.44** | 12.5 | **10,750.72** |
| Barabara za mikoa lami | 944.78 | 46.5 | 665.59 | 32.8 | 421.89 | 20.8 | 2,032.26 |
| Barabara za mikoa changarawe/udongo | 6,013.82 | 28.1 | 13,901.87 | 65.1 | 1,452.10 | 6.8 | 21,367.78 |
| **Jumla ndogo** | **6,958.59** | 29.7 | **14,567.46** | 62.3 | **1,873.99** | **8.0** | **23,400.04** |
| **Jumla Kuu** | **12,985.88** | **38.0** | **17,945.45** | **52.5** | **3,219.43** | **9.4** | **34,150.76** |

**Chanzo:** Wizara ya Ujenzi

263. Mwaka 2023, mtandao wa barabara unaosimamiwa na TARURA ulikuwa na jumla ya kilometa 144,429.77 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Kati ya hizo, kilometa 41,125.41 zilikuwa katika hali nzuri, kilometa 50,632.74 hali ya wastani na kilometa 52,671.62 hali mbaya. Hadi Desemba 2023, mtandao wa barabara za wilaya zenye kiwango cha lami ulifikia kilometa 3,224.12, changarawe kilometa 41,107.52 na udongo kilometa 100,098.13 ikilinganishwa na kilometa 2,847.48 za lami, kilometa 35,476.59 za changarawe na kilometa 106,105.71 za udongo mwaka 2022.

**Jedwali Na. 11.2: Hali ya Mtandao wa Barabara za Vijijini na Mijini Mwaka 2023**

| Aina ya Barabara | Hali ya Barabara (Kilometa) | | | Jumla (Kilometa) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Nzuri** | **Wastani** | **Mbaya** | | |
| Barabara za lami | 2,659.98 | 434.28 | 129.87 | 3,224.12 | 2.2 |
| Barabara za changarawe | 21,597.58 | 15,499.08 | 4,010.85 | 41,107.52 | 28.5 |
| Barabara za udongo | 16,867.85 | 34,699.38 | 48,530.90 | 100,098.13 | 69.3 |
| **Jumla** | **41,125.41** | **50,632.74** | **52,671.62** | **144,429.77** | **100** |
| Asilimia | 28.5 | 35.0 | 36.5 | 100 | |

**Chanzo:** Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini

264. Mwaka 2023, TARURA ulijenga, ilikarabati na kutengeneza barabara za wilaya zenye urefu wa kilometa 42,153.35 ikilinganishwa na kilometa 39,705.94 zilizojengwa na kukarabatiwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.16. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi,ukarabati na matengenezo ya barabara ikiwepo ujenzi wa barabara za lami awamu ya pili Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma na barabara za teknolojia mbadala. Aidha, barabara zenye urefu wa kilometa 431.45 zilijengwa kwa kiwango cha lami, kilometa 9,651.97 zilijengwa kwa kiwango cha changarawe na kilometa 32,069.93 zilifanyiwa ukarabati maalum, ukarabati wa kawaida na matengenezo ya maeneo korofi. Mwaka 2023, Wakala ilijenga madaraja 2,741, makalavati 3,308, mitaro mikubwa ya maji ya mvua yenye mita za mraba 102,891.69 na kukarabati madaraja 31 ikilinganishwa na madaraja 652, makalavati 1,121, mitaro ya maji yenye urefu wa kilometa 2,415 na madaraja 251 yalikarabatiwa kwa mwaka 2022.

**Barabara, Madaraja, Vivuko na Magari**

265. Mwaka 2023, Wakala wa Barabara Tanzania - TANROADS ulitengeneza barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa kilometa 36,549.17 ikilinganishwa na kilometa 30,558.29 zilizofanyiwa matengenezo mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 19.6. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa barabara zenye hali mbaya zilizokasimishwa kutoka TARURA kwenda TANROADS. Aidha, madaraja 3,271 yalifanyiwa matengenezo ikilinganishwa na madaraja 2,917 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Serikali kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara na madaraja.

266. Mwaka 2023, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania - TEMESA uliendelea kusimamia vivuko 32 ikilinganishwa na vivuko 34 mwaka 2022. Upungufu huo ulitokana na vivuko viwili (2) vya MV Ilagala na MV Mwanza I kusimamishwa kutoa huduma kutokana na uchakavu mkubwa usiorekebishika. Aidha, katika kipindi hicho, abiria 29,775,113, magari 794,514 na mizigo yenye uzito wa tani 307.18 ilivushwa kwa kutumia vivuko ikilinganishwa na abiria 33,598,960, magari 1,011,791 na mizigo yenye uzito wa tani 538.47 mwaka 2022. Kupungua kwa idadi ya abiria, magari na mizigo iliyosafirishwa kulitokana na baadhi ya vivuko kuwa kwenye matengenezo makubwa ikiwemo, MV Ujenzi, MV Mara, MV Magogoni, MV Kilindoni na MV Kitunda.

267. Mwaka 2023, TEMESA ilitengeneza magari 27,964 kwa nyakati tofauti ikilinganishwa na magari 27,067 yaliyotengenezwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Ongezeko hilo lilitokana na maboresho yaliyofanyika katika karakana za TEMESA, ununuzi wa vitendea kazi stahiki na mafunzo ya kuwajengea uwezo mafundi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia. Maboresho hayo yalisaidia kupunguza vibali vya kuruhusu magari ya Serikali kutengenezwa katika karakana binafsi. Vile vile, TEMESA ilikamilisha miradi 81 ya usimikaji umeme ikilinganishwa na miradi 139 iliyosimikwa

mwaka 2022. Kupungua kwa idadi ya miradi kulitokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi iliyokuwa ikitekelezwa na Wakala, hususan kwenye majengo yaliyoko kwenye mji wa Serikali Dodoma.

**Mfuko wa Barabara**

268. Mwaka 2023, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilikusanya shilingi bilioni 906.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,475 zilizokusanywa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 38.5. Hii ilitokana na kupungua kwa mapato yaliyotokana na tozo ya mafuta kulikosababishwa na kupungua kwa kiasi cha mafuta yaliyoingizwa nchini kufuatia kupungua kwa matumizi ya mafuta katika kuzalisha umeme. Vile vile, Bodi ilifanya ukaguzi wa miradi 838 ya barabara ikilinganishwa na miradi 1,279 iliyokaguliwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 34.5. Upungufu huo ulitokana na ukaguzi maalum wa miradi 548 uliofanywa na TARURA katika mtandao wa barabara za wilaya.

**Nyumba na Majengo ya Serikali**

269. Mwaka 2023, Wakala wa Majengo Tanzania uliendelea kusanifu na kusimamia ujenzi wa miradi 110 ya nyumba na majengo ya Serikali ikilinganishwa na miradi 109 iliyosimamiwa mwaka 2022. Aidha, Wakala ulikarabati nyumba na majengo 132 mwaka 2023 ikilinganishwa na nyumba na majengo 335 yaliyokarabatiwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 60.6. Upungufu huo ulitokana na Serikali kuwekeza raslimali fedha nyingi zaidi katika ujenzi wa majengo mapya pamoja na kuendelea na shughuli za ukarabati

270. Mwaka 2023, nyumba 6,493 zilipangishwa kwa wapangaji wa kibiashara na watumishi wa umma kama ilivyokuwa mwaka 2022. Kati ya nyumba zilizopangishwa, nyumba 2,382 zilipangishwa kwa watumishi wa umma na nyumba 4,111 zilipangishwa kibiashara.

**Usajili wa Makandarasi**

271. Mwaka 2023, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilisajili makandarasi 1,807 ikilinganishwa na makandarasi 1,341 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 34.8. Hii ilitokana uhamasishwaji uliofanywa na Bodi na uzingatiaji wa sheria ya usajili wa makandarasi. Usajili huo uliwezesha makandarasi waliosajiliwa kufikia 15,841 Desemba 2023. Aidha, miradi 4,539 ya ujenzi ilisajiliwa na Bodi mwaka 2023 ikilinganishwa na miradi 4,013 iliyosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 13.1. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa shughuli za ujenzi nchini.

272. Mwaka 2023, miradi 3,354 ilikaguliwa na Bodi ikilinganishwa na miradi 3,728 iliyokaguliwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 10.0. Hii ilitokana na kupungua kwa kaguzi za dharura za miradi ya ujenzi kuendana na mpangokazi na ukomo wa bajeti.

Kati ya miradi iliyokaguliwa, miradi 2,334 ilikidhi vigezo na miradi 1,020 haikukidhi vigezo. Miradi kutokidhi vigezo kulisababishwa na kutekelezwa na watu wasiosajiliwa, miradi kutosajiliwa, kutokuweka bango la mradi, kutozingatia sheria ya usalama wa wafanyakazi na makandarasi kutekeleza miradi iliyo juu ya kiwango chao. Aidha, hatua mbalimbali za kisheria zilichukuliwa kwa miradi isiyokidhi vigezo zikiwemo kutozwa faini kwa makandarasi na kusimamisha ujenzi wa baadhi ya miradi. Vile vile, Bodi ilipeleka mahakamani mashauri 64 ya makosa mbalimbali ikiwemo kutekeleza miradi kwa kutumia kampuni au wataalam wasio makandarasi mwaka 2023 ikilinganishwa na mashauri 40 mwaka 2022.

**Usajili wa Wahandisi**

273. Mwaka 2023, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili wahandisi 2,981 wa fani mbalimbali ikilinganishwa na wahandisi 2,846 waliosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 4.7. Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyoendelea kutolewa kuhusu umuhimu wa usajili kwa wataalam wa kada ya uhandisi. Hadi Desemba 2023, wahandisi waliosajiliwa walifikia 37,345. Kati ya wahandisi hao, wahandisi 2,783, sawa na asilimia 93.4 walikuwa watanzania na wahandisi 198 walitoka nje ya nchi. Aidha, Bodi ilisajili mafundi sanifu 348 mwaka 2023 ikilinganishwa na mafundi sanifu 463 waliosajiliwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 24.8. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya wahandisi kutoka nje kuondoka nchini baada ya kukamilisha miradi waliyokuwa wakiitekeleza. Hadi Desemba 2023, idadi ya mafundi sanifu waliosajiliwa ilifikia 1,590.

274. Hadi Desemba 2023, kampuni za ushauri zilizosajiliwa na Bodi zilifikia 421 kutoka kampuni 405 mwaka 2022. Aidha, Bodi ilisajili wahandisi washauri 31 mwaka 2023 ikilinganishwa na wahandisi washauri 12 waliosajiliwa mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na mwamko wa wataalamu wa kada ya uhandisi wa ndani kushiriki katika fursa zilizopo kwenye sekta ya ujenzi. Kati ya hao, wahandisi washauri 24 walikuwa watanzania na wahandisi washauri saba (7) walikuwa wa kigeni. Hadi Desemba 2023, wahandisi washauri waliosajiliwa walifikia 659.

275. Mwaka 2023, Bodi ilisajili maabara 11 za vifaa vya ujenzi na uhandisi ikilinganishwa na maabara moja iliyosajiliwa mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini - TARURA kuanzisha Maabara zake katika mikoa. Hadi Desemba 2023, maabara za vifaa vya ujenzi na uhandisi zilizosajiliwa zilifikia 51.

276. Mwaka 2023, wahandisi waliopata mafunzo walikuwa 1,704 ikilinganishwa na wahandisi 1,488 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.5. Hadi Desemba 2023, idadi ya wahandisi waliopata mafunzo ilifikia 13,170. Kati ya hao, wahandisi 364 walihitimu na kusajiliwa kama wahandisi wataalamu mwaka 2023 ikilinganishwa na wahandisi 289 mwaka 2022. Kwa upande mwingine, Bodi ilisajili miradi 795 ya ujenzi

mwaka 2023 ikilinganishwa na miradi 716 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.0. Ongezeko hilo lilitokana na matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika usajili wa miradi ya ujenzi. Aidha, Bodi ilikagua miradi 185 mwaka 2023 ikilinganishwa na miradi 106 iliyokaguliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 74.5. Ongezeko hilo lilitokana na ufuatiliaji na kaguzi maalum za kikanda zilizofanyika katika miradi.

**Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

277. Mwaka 2023, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili wataalamu 140 ikilinganishwa na wataalamu 128 waliosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.4. Hii ilitokana na wataalamu kuendelea kujisajili kupitia mfumo wa kielektroniki wa Bodi. Kati ya waliosajiliwa, wataalamu 139 ni watanzania na mtaalamu mmoja alitoka nje ya nchi. Hadi Desemba 2023, wataalamu wa ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi waliosajiliwa walifikia 1,442. Aidha, wahitimu 230 walishiriki mafunzo kwa vitendo katika fani za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi mwaka 2023 ikilinganishwa na wahitimu 212 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.5. Hii ilitokana na ongezeko la miradi ya ujenzi lililowezesha upatikanaji wa nafasi za mafunzo kwa vitendo katika sekta ya ujenzi.

278. Mwaka 2023, Bodi ilisajili kampuni 32 za ushauri wa ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi ikilinganishwa na kampuni 16 zilizosajiliwa mwaka 2022. Hii ilitokana na upatikanaji wa kazi za ushauri elekezi kufuatia kuongezeka kwa miradi ya ujenzi pamoja na matumizi ya mifumo ya kielekektroniki katika usajili wa kampuni. Hadi Desemba 2023, kampuni za ushauri elekezi zilizosajiliwa na Bodi zilifikia 439. Aidha, kampuni zilizosajiliwa na Bodi mwaka 2023 zote zilikuwa za watanzania.

279. Mwaka 2023, Bodi ilisajili miradi 1,396 ya ujenzi wa majengo ikilinganishwa na miradi 1,097 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 27.3. Ongezeko hilo lilitokana na ukaguzi wa miradi na udhibiti wa waendelezaji wa majengo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria Na.4 ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya mwaka 2010. Aidha, Bodi ilikagua miradi 4,885 ya ujenzi wa majengo mwaka 2023 ikilinganishwa na miradi 3,362 iliyokaguliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 45.3. Hii ilitokana na ufanisi wa ukaguzi uliochangiwa na kuongezeka kwa rasilimali za kufanyia ukaguzi. Kati ya miradi iliyokaguliwa, miradi 4,139 (asilimia 84.7) ilikidhi matakwa ya Sheria Na.4 ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya mwaka 2010 na miradi 746 (asilimia 15.3) haikukidhi.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

280. Mwaka 2023, Baraza la Taifa la Ujenzi lilitoa ushauri wa kiufundi kwa wadau nane (8) wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau saba (7) mwaka 2022. Aidha, Baraza lilisuluhisha migogoro 247 ya ujenzi mwaka 2023 ikilinganishwa na migogoro 111 mwaka

2022. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ufanisi wa kuratibu mashauri ya usuluhishi wa migogoro.

281. Mwaka 2023, Baraza kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania liliandaa mapitio ya viwango 83 vya ubora wa vifaa vya ujenzi ikilinganishwa na viwango 19 mwaka 2022. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mapitio ya viwango vya ubora. Aidha, Baraza liliendesha kozi tano (5) kwa wadau wa sekta ya ujenzi mwaka 2023.

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi**

282. Mwaka 2023, Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ilitoa mafunzo ya stashahada kwa wanafunzi 208 ikilinganishwa na wanafunzi 140 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 48.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa maombi ya washiriki kulikochangiwa na juhudi za Taasisi kuendelea kujitangaza kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Katika kipindi hicho, Taasisi ilitoa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa mafundi sanifu 12 ikilinganishwa na mafundi sanifu 16 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 25.0. Aidha, washiriki 290 kutoka katika vikundi vya wanawake na vijana walipata mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi katika kukarabati na kutengeneza barabara mwaka 2023 ikilinganishwa na washiriki 99 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, Taasisi ilihamasisha matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa wadau 177 wa barabara kutoka TARURA na baadhi ya halmashauri ikilinganishwa na wadau 116 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 52.6.

## MAENDELEO YA ARDHI

### Utayarishaji wa Hatimiliki, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Utatuzi wa Migogoro

283. Mwaka 2023, hatimiliki za viwanja na mashamba zilizoandaliwa kwa ajili ya usajili zilikuwa 133,944 ikilinganishwa na hatimiliki 94,832 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 41.2. Aidha, hatimiliki za kimila 74,830 zilitolewa kwa wananchi mwaka 2023 ikilinganishwa na hatimiliki 38,575 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 94.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa viwanja na mashamba yaliyopimwa kufuatia utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi - LTIP; Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; na uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kumiliki ardhi kisheria. Vile vile, vyeti 149 vya ardhi za vijiji vilitolewa na kufikisha jumla ya vijiji 11,969 vilivyopatiwa vyeti kati ya vijiji 12,319 vilivyosajiliwa nchini. Kwa upande mwingine, migogoro ya ardhi 2,503 ilitatuliwa kiutawala mwaka 2023 ikilinganishwa na migogoro 2,684 mwaka 2022. Kupungua kwa migogoro kulitokana na utaratibu wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi kupitia kliniki za ardhi.

### Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria

284. Mwaka 2023, hatimiliki na nyaraka za kisheria zilizosajiliwa zilikuwa 200,318 ikilinganishwa na nyaraka 183,072 zilizosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la

asilimia 9.4. Hii ilitokana kuendelea kwa utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi; Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; kliniki za ardhi; na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria kwa matumizi mbalimbali.

**Jedwali Na 11.3: Usajili wa Hatimilki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria Mwaka 2019 - 2023**

| **Hati Zilizosajiliwa** | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Hati za kumiliki ardhi zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura 334 | 47,948 | 57,180 | 61,527 | 83,195 | 90,408 |
| Hati za Sehemu ya Jengo chini ya Sheria ya Usajili wa Hati za Sehemu ya Jengo (Unit Title Act No.17/2008). | 321 | 924 | 232 | 380 | 294 |
| **Jumla Hatimilki** | **48,269** | **58,104** | **61,759** | **83,575** | **90,702** |
| **Miamala na Nyaraka Zilizosajiliwa** | | | | | |
| Miamala iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura 334 | 15,018 | 35,477 | 39,252 | 51,413 | 57,395 |
| Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura 117 | 26,096 | 33,938 | 36,354 | 42,112 | 44,655 |
| Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya mali zinazohamishika, Sura 210 | 3,129 | 5,698 | 4,265 | 5,972 | 7,566 |
| **Jumla Nyaraka za Kisheria** | **44,243** | **75,113** | **79,871** | **99,497** | **109,616** |
| **Jumla Kuu: Hatimilki na Nyaraka za Kisheria** | **92,512** | **133,217** | **141,630** | **183,072** | **200,318** |

**Chanzo**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Uthamini wa Mali na Upimaji wa Mashamba na Viwanja**

285. Mwaka 2023, Serikali iliidhinisha taarifa 94,551 za uthamini wa kawaida na fidia ikilinganishwa na taarifa 67,621 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 39.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa miamala ya ardhi, hususan katika maeneo ya uhamisho wa milki, uhuishaji wa milki, mikopo, uthamini kwa ajili ya mizania ya kimahesabu na fidia katika miradi ya kimkakati.

286. Mwaka 2023, ramani zenye viwanja 314,977 na mashamba 2,564 ziliidhinishwa ikilinganishwa na ramani zenye viwanja 430,640 na mashamba 1,386 mwaka 2022. Kupungua kwa idadi ya viwanja vilivyoidhinishwa kulitokana na baadhi ya kampuni za upangaji na upimaji zilizokasimiwa jukumu hilo kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati na kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kufutiwa usajili.

**Jedwali Na 11.4: Viwanja na Mashamba Yaliyoidhinishwa Mwaka 2022 - 2023**

| Na. | Mikoa | 2022 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Viwanja | Mashamba | Viwanja | Mashamba |
| 1 | Arusha | 12,159 | 13 | 5,836 | 1541 |
| 2 | Dar es Salaam | 38,993 | - | 25,765 | - |
| 3 | Dodoma | 52,668 | 5 | 21,461 | 520 |
| 4 | Geita | 6,725 | - | 4,631 | - |
| 5 | Iringa | 11,902 | 20 | 10,670 | 16 |
| 6 | Kagera | 5,733 | 52 | 2,225 | 20 |
| 7 | Katavi | 5,449 | - | 5,963 | - |
| 8 | Kigoma | 8,033 | 76 | 5,794 | 129 |
| 9 | Kilimanjaro | 3,786 | 325 | 1,617 | 27 |
| 10 | Lindi | 5,985 | 16 | 5,731 | 15 |
| 11 | Manyara | 19,031 | 26 | 17,870 | 44 |
| 12 | Mara | 21,735 | - | 17,001 | 1 |
| 13 | Mbeya | 54,507 | 3 | 55,558 | 3 |
| 14 | Morogoro | 22,623 | 66 | 23,652 | 157 |
| 15 | Mtwara | 9,807 | - | 7,129 | 9 |
| 16 | Mwanza | 9,521 | 2 | 8,010 | 9 |
| 17 | Njombe | 8,306 | 30 | 7,359 | 23 |
| 18 | Pwani | 31,459 | 33 | 19,580 | - |
| 19 | Rukwa | 1,900 | 3 | 2,472 | 12 |
| 20 | Ruvuma | 11,672 | 1 | 8,449 | 2 |
| 21 | Shinyanga | 15,135 | - | 7,579 | - |
| 22 | Simiyu | 12,782 | - | 4,664 | - |
| 23 | Singida | 9,657 | 693 | 9,938 | 20 |
| 24 | Songwe | 1,949 | 2 | 4,148 | 3 |
| 25 | Tabora | 17,696 | - | 13,340 | 9 |
| 26 | Tanga | 31,427 | 20 | 18,535 | 4 |
| | **Jumla** | **430,640** | **1,386** | **314,977** | **2,564** |

**Chanzo**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

287. Mwaka 2023, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 734 iliandaliwa katika wilaya 47 ikilinganishwa na vijiji 97 katika wilaya 20 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi; Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; na ushiriki wa wadau wa maendeleo katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

**Jedwali Na 11.5: Vijiji Vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi Mwaka 2023**

| Na. | Mkoa | Halmashauri ya Wilaya | Mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji | Idadi ya Vijiji |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Pwani | Rufiji | Kipugira, Mtanza-Msona, Ndundu-Nyikanza, Nyaminywili, Kipo, Mwasemi mibuyu saba, Kitapi, Mbwara, Tari, Mohoro-Mashariki, Mohoro-Magharibi, Chumbi A, Chumbi B, Chumbi C, Mbunju-Mvuleni, Ruwe, Mkongo Kaskazini, Mkongo-Kusini, Ngorongoro Mashariki, na Ngorongoro- Magharibi. | 20 |
| | | Kisarawe | Kihare, Koresa, Kwala, Mafumbi, na Cholesamvula | 5 |
| 2 | Dodoma | Chamwino | Ikombo, Malecela, Manda, Zajilwa, Chinugulu, Huzi, Magungu, Mondomela, Mpyayungu, Muheme, Ng'Hambaku, Segala, Umoja, na Chikola. | 14 |
| | | Bahi | Nghulugano, Uhelela, Mapinduzi, Chikola, Mpinga, Chipanga A, Chipanga B, Bahi Makulu, Nagulo Bahi, na Chimendeli. | 10 |
| 3 | Singida | Mkalama | Tumuli, Milade, Kitumbili, na Kinyangiri. | 4 |
| | | Iramba | Mgungia, Kyengege, Misuna, Kikonge, Mugundu, Mbelekese, Usure, Kitukutu, Tulya, Nkonkilangi, Kisonga-Shelui, Doromoni, Shelui II, Migilango, Ntwike na Mgongo. | 16 |
| | | Singida | Mvae, Kinyeto, Mgori, Munkhola, Sughana, Unyampanda, Mughunga, Lamba, Ghata, Mughamo, Mpipiti, Ughandi A, Ughandi B, Mwarufyu, Mjughuda, Msimihi, Mwachambia, Merya, Ikhanoda, na Msange. | 20 |
| 4 | Rukwa | Sumbawanga | Katoo, Nkwilo, Kizungu, Mnazimmoja, Asilia, Ilembo, Kilembo, Lusaka, Mulombo, Kapewa, Kaoze, Msanda Muungano A, Liwelyamvula, Mshani, Msanda Muungano B, Lyanza, Nankanga C. Kazi, Itela, Mkunda, Katonto, Nankanga, Kapenta, Nsanga, na Mkusi. | 24 |
| | | Nkasi | Itindi | 1 |
| 5 | Tabora | Igunga | Mgazi, Mwazizi, Bukoko, Migongwa, Mwalamo, Ntigu, Itumba, Bukama, Kitangili, Lugubu, Mwalala, Ussongo, Kaumbu, Ipumbulya, Nguvumoja, Mwabakima, Mbutu, Ganyawa, Ibutamisuzi, Kidalu, Jogohya, Kining’inila, Hindishi, Mwanyagula, Iyogelo, Mwamashimba, Chagana, Mtungulu, Igoweko, Mwina, Buhekela, Mwamashinga, Mwamala, Ntobo, Imalilo, na Matinje. | 36 |
| | | Uyui | Ipululu, Igalula, Goweko, Tambukareli, Imalakaseko, Kamama, Mpumbuli, Kimungi, Vumilia, Isenefu, Kawekapina, Nsololo, Kizengi, Gengesita, Ntalasha, na Nyauwanga. | 16 |
| 6 | Mwanza | Kwimba | Shushi, Isunga, Goloma, Ibindo, Mhulya, Solwe, Ishingisha, Bungulwa, Ngulla, Ngogo, Mhulula, Manawa, Mwagin'hi, Mwitambu, Mwandu, Kinoja, Isabilo, Mwankuba,Talaga, na Kitunga. | 20 |
| | | Misungwi | Budutu, Gambajiga, Mwakalima, Mamaye, Ibongoya A, Ibongoya B, Mwasubi, Bugomba, Magaka, Mwalwigi, Mwagagala, Lubuga, Mwamaguha, Ikoma, Ndinga, na Mhungwe. | 16 |
| | | Magu | Lubugu, Bubinza, Kisamba, Misungwi, Sayaka, Kitongo, Kayenze B, Chandulu, Bugatu, Salama, Kisesa B, Mwamanga, Mwabulenga, Ng’washepi, Nhobola, Igombe, Langi, na Itandula. | 18 |
| | | Buchosa | Mgogo, Isenyi, Luhiza, Chanika, Bugoro, Nyachitale, Kabanga, Nyakasasa, Nyamisiwi, Buhama, Nyamkolechilwa, Nyakabanga, Nyagalamila, Igwanzozu, Mwamanyili, Lumeya, Bilulumo, Kisisa, Humulumo, Kasela, Lusolelo, Kamisa, Isegeng’he, na Luharanyonga. | 24 |
| 7 | Simiyu | Meatu | Butuli, Malwilo Mnadani, Mwageni, Nyanza, Bulyandulu, Semu, Tindabuligi, Ming’ongwa, Mwasungura, Mwamashimba, Mwagwila, Mwabusungu, Mwajidalala, Isengwa, Mbugayabanhya, Mbalagane, Mwangudo, Buganza, Iramba Ndogo, Sungu, Makao, Mwanyahina, Mwabagimu, Shushuni, Jinamo, Sapa, Mbushi, na Lukale. | 28 |
| | | Itilima | Mwamakili, Mbogo, Ng’walali, Nding’ho, Lung’wa, Nyantugutu, Pijulu, Longalombogo, na Shishani. | 9 |
| | | Maswa | Gumali, Igongwa, Isageng'He, Isulilo, Mwasayi, Sulu, Zabazaba, Buhangija, Mwandang'ombe, Bugarama, Busamuda, Bushitala, Funika, Isanga, Masela, Mwabuki, Mwadila, Wigelekelo, Ikungu, Jihu, Kidema, Muhida, Ngongwa, na Nyashimba. | 24 |
| | | Busega | Lunguku, Mwabayanda, Mwakiloba, na Kijilishi. | 4 |

| **Jedwali Na 11.5 Linaendelea** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **Mkoa** | **Halmashauri ya Wilaya** | **Mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji** | **Idadi ya Vijiji** |
| 8 | Shinyanga | Shinyanga | Ihalo, Masekelo, Imesela, Mwamanyuda, Puni, Bunonga, Nyika, Nyashimbi, Ishololo, Zobogo, Kazuni, Kasingili, Maskati, Bukene, Nyida, Sumbigu, Welezo, Nsalala, Nshishundo, Mwamkanga, Amani, Mwiseme, Sayu, Nzoza, Mwakatola, Mwaduntu, Shilabela, Mwamadilanha, Bulambila, Ng'hama, Mwang'osha, na Kituli. | 32 |
| | | Kishapu | Dulisi, Mipa, Ng'wigumbi, Ng'wagankulu, Ng'washinon'gela, Sekeididi, Seseko, Songwa, Busangwa, Kabila, Mwamasololo, Mwanima, Mwajipugira, Mwajiningu, Sekebugoro, na Wishiteleja. | 16 |
| | | Ushetu | Nsunga, Mliza, Nhimbo, Ngokolo, Mhulidede, Mhuge, Kabanga, Bulima, Itumbo, Itumbili, Iwilo, Igalula, Chibiso, Nshimba, Kigwa, Mbuta, Sofi, Igunda, Bunasani, na Ilemve. | 20 |
| 9 | Tanga | Korogwe | Torontombugani, Kwetonge, Mkwajuni, Mabogo, Ngomeni, Mswaha majengo, Mgila, Mwenga, Gombero, Kwamkole, Makumba, Mkokola, Gombalamu, Manga mikocheni, Manga mtindiro, na Mazinde ngua. | 16 |
| | | Handeni | Msomera | 1 |
| | | Kilindi | Lengusero, na Saunyi. | 2 |
| 10 | Kilimanjaro | Moshi | Mwangaria | 1 |
| 11 | Kigoma | Buhigwe | Kigogwe, Kshanga, Janda, Bukuba, Songambele, Munzeze, Bukuye, Kirungu, Kasumo, Kinazi, Bulimanyi, Ndoha, Kimara, Rusaba, Mnyegera, na Kibwigwa. | 16 |
| 12 | Mara | Tarime | Kiongera, Nyakalima, Muriba, Kikomori, Nyasicha, Kubiterere, Korotambe, Nyamohonda, Borega-A, Kimusi, Matamankwe, Nyantira, Tagare, Keisangora, Ntagacha, Gwitare, Kitenga, Kwisarara, na Turugeti. | 19 |
| | | Bunda | Manchimweru, Bigegu, Nyaburundu, Mihingo, Mekomariro, Kurusanga, Sarawe, Mahanga, Tiring'ati, Nyangere, Salama Kati, Salama 'A', Sanzate, Nyang'aranga, Marambeka, Rakana, Bukama, Kiloreri, Kambubu, Sikilo, Mugara, Mwiruruma, Isanju, Nyarugoma, Mumagunga, Namhura, Chingulubila, Kasahunga, Nakatuba, Karukekere, Namalebe, na Neruma. | 32 |
| | | Rorya | Ikoma, Kogaja, Panyakoo, Ng'ope, Ochuna, Nyamasanda, Nyamusi, Roche, Chereche, Tatwe, Burere, Irienyi, Oliyo, Kwibuse, Kuruya, Nyambiwe, Kirogo, Rabuor, Makongro, na Radienya. | 20 |
| | | Musoma | Kigera, Kwikuba, Maneke, Mmahare, Kasoma, Chumwi, Mabuimerafuru, Lyasembe, Buanga, Rusoli, Kwikerege, Butata, Bwasi, Kome, Bugunda, Bujaga, Bugwema, Musanja, Kaburabura, Masinono, Makojo, Chitale, Chimati, na Busungu. | 24 |
| | | Butiama | Ryamagubo, Songora, Nyarukoru, Nyanza, Nyabikwabi, Nyamikoma, Tonyo, Bisumwa, Busegwe, Kyamajoje, Nyakiswa, Bumangi, Kizaru, Bisarye, Nyasirori, Kwigutu, Mwibagi, Kwisaro, Ryamisanga, Kitasakwa, Buswahili, Kongoto, Kamgendi, na Kirumi. | 24 |
| 13 | Njombe | Makete | Bulongwa, Utanziwa, Ilolo, Idende, Imehe, Iyoka, Kilanji, Kitula, Madihani, Mahulu, Unyagala, Unyangogo, Iniho, Lumage, Kidope, Nkunga, Mahanji, Kinyika, Ndapo, Mbela, Mlondwe, Mpangala, Mang'oto, Ubiluko, Makeve, Ipelele, Mbanga, Malembuli, Lugao, Unenamwa, Uganga, Luwumbu, Usililo, Kigala, Mlengu, Ikowo, Matenga, Nkondo, Ikungula, Magoye, Igenge, Ng'onde, Makusi, Lugoda ,Ukange, Mbalatse, Ukwama, Ihanga, Kijyombo, Igumbilo, Malanduku, Lupila, Ilungu, Lupombwe, Ipepo, Udilu, Masisiwe, Maliwa Ikete, Ilevelo, Ihela, Usagatikwa, Utweve, na Igolwa. | 64 |
| | | Ludewa | Lihagule, Kingole, Liughai, Kimelembe, Nkomang'ombe, Ilela, Ngelenge, Mbongo, Luana, Mbwila, Mholo, Mfalasi, Kiyombo, Mkiu, Lupande, na Lupanga. | 16 |
| | | Wanging'ombe | Mapogoro | 1 |
| 14 | Kigoma | Kigoma Vijijini | Mkwanga, Nyamhoza, na Nyabigufa. | 3 |
| 15 | Kagera | Kyerwa | Murongo | 1 |
| 16 | Morogoro | Morogoro | Kichangani, Gomero, Nyarutanga, Mnganzi, Magogoni, na Kongwa. | 6 |
| | | Ulanga | Chilongola, Euga, Gombe, Nkongo, na Mzelezi. | 5 |
| 17 | Lindi | Liwale | Ndunyungu, Mitawa, Ngorongopa, Mpengere, Lubaba, na Nambinda. | 6 |
| | | Ruangwa | Chiundu, Namkatila, Nandandala, Namkonjela, Mkaranga, Nandanda, Mbecha, Chilangalile, Likwachu, Nambiranje, Nanjaru, Chikwale, Chikoko, Mibure, Nanganga, na Litama. | 16 |
| 18 | Ruvuma | Tunduru | Ngapa, Mnazimmoja, Chawisi, Muhuwesi, Jaribuni, Ligunga, Liwangula, Matemanga, Chingulungulu, Msagula, Majimaji, Chalinze, Magomeni, Namiungo, Mnenje, Nammanga, Mchengamoto, Mkowela, Tanga, Namatanda, Tinginya, Imani, Pachanne, Misufini, Kazamoyo, Nangolombe, Mitwana, na Mnazimmoja. | 28 |
| | | Mbinga | Mahenge, Mapipili, Ndembo, Kibanga, Kilanga Juu, Linda,Liyombo, Mahilo, Mbuji, Mhagawa, Mkalanga, Mzuzu, Silo, Mitambotambo, na Ulolela, Mawono, na Lituru . | 17 |
| 19 | Songwe | Songwe | Mpona, Wanzani, Chang'ombe, Galula, Ifuko, Isanzu, Iyovyo, Manda, Mbuyuni, Mheza, Mwagala, Nahalyongo, Namambo, Namkukwe, Ndanga, Rukwa, Some, Songambele, Totowe, na Magamba. | 20 |
| 20 | Iringa | Mufindi | Ihimbo, Isipii, Lwang'A, Mkalala, Mlevelwa, Ibwanzi, Igeleke, Ihegela, Ikanga, Ikaning'Ombe, Itona, Kitiru, Iyegeya, Luhunga, Lulanda, Mninga, Nyakipambo, Uhafiwa, na Ifupira. | 19 |
| | | | **Jumla** | **734** |

**Chanzo:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa**

288. Mwaka 2023, Serikali iliandaa na kuidhinisha michoro 492 ya mipango miji ikilinganishwa na michoro 2,101 mwaka 2022. Aidha, makazi 196,146 yasiyopangwa yalirasimishwa mwaka 2023 ikilinganishwa na makazi 452,805 mwaka 2022. Kupungua kwa makazi yaliyorasimishwa kulitokana na ushiriki mdogo wa wananchi katika utekelezaji wa miradi shirikishi ya urasimishaji.

**Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya**

289. Mwaka 2023, mashauri 35,635 (mapya 17,662 na 17,973 yanayoendelea kusikilizwa) yalikuwa kwenye Mabaraza 96 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ikilinganishwa na mashauri 49,905 mwaka 2022. Kati ya hayo, mashauri 21,039 yaliamuliwa na mashauri 14,596 yanaendelea kusikilizwa. Kupungua kwa mashauri hayo kulitokana na kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua Mabaraza 13 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

**Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara**

290. Mwaka 2023, Shirika la Nyumba la Taifa lilikamilisha ujenzi wa nyumba 524 na kuendelea na ujenzi wa nyumba 588 katika maeneo mbalimbali nchini ikilinganishwa na nyumba 215 zilizokamilika na nyumba 475 zilizoendelea na ujenzi mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kukamilika kwa miradi ya ujenzi wa nyumba katika maeneo ya *Morocco square* na Chamwino pamoja na utekelezaji wa Mradi wa *Samia Housing* na Iyumbu. Kati ya nyumba zilizokamilika, nyumba 303 zilikuwa za gharama nafuu na nyumba 221 za bei ya kati na juu mwaka 2023 ikilinganishwa na nyumba 405 za bei nafuu, na nyumba 235 za bei ya kati na juu mwaka 2022. Katika kipindi hicho, Kampuni ya Nyumba kwa Watumishi ilikamilisha ujenzi wa nyumba 45 za gharama nafuu na jengo moja la kibiashara katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.

# SURA YA 12

# UCHUKUZI NA UHIFADHI MIZIGO

## Usafiri wa Barabara

291. Mwaka 2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini - LATRA ilitoa leseni 298,270 za usafirishaji kwa vyombo vilivyosajiliwa kutoa huduma ya usafirishaji kibiashara ikilinganishwa na leseni 245,418 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 21.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wawekazaji wapya, hususan katika usafirishaji wa mizigo na pikipiki za magurudumu mawili na matatu.

**Jedwali Na. 12.1: Leseni za Usafirishaji Zilizotolewa Mwaka 2019 - 2023**

| Kundi la Leseni | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mabasi ya abiria | 60,344 | 52,081 | 53,451 | 50,452 | 50,316 | -0.3 |
| Magari ya mizigo | 123,460 | 142,559 | 133,428 | 142,154 | 183,392 | 29 |
| Bajaji/Pikipiki | 18,345 | 20,400 | 36,984 | 52,812 | 64,562 | 22.2 |
| **Jumla** | **202,149** | **215,040** | **223,863** | **245,418** | **298,270** | **21.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini

292. Mwaka 2023, ajali zilizotokana na vyombo vya usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara zilipungua kwa asilimia 28.2 na kufikia 1,009 ikilinganishwa na ajali 1,405 zilizotokea mwaka 2022. Kupungua kwa ajali kulitokana na kaguzi za mara kwa mara barabarani, matumizi ya mfumo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi ya masafa marefu pamoja na elimu iliyotolewa kwa wadau wa vyombo vya usafiri barabarani. Aidha, ajali za magari ya mizigo zilikuwa 300 ikilinganishwa na ajali 268 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.9. Hii ilitokana na uzembe wa madereva na uendeshaji hatarishi.

**Jedwani Na. 12.2: Ajali za Barabarani Mwaka 2019 - 2023**

| Aina ya Vyombo | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mabasi ya abiria | 442 | 330 | 365 | 357 | 335 | -6.2 |
| Magari ya Mizigo | 331 | 407 | 224 | 268 | 300 | 11.9 |
| Bajaji/Pikipiki | 567 | 415 | 463 | 780 | 374 | -52.1 |
| **Jumla** | **1,340** | **1,152** | **1,052** | **1,405** | **1,009** | **-28.2** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini

## Usafiri wa Reli

293. Mwaka 2023, Shirika la Reli Tanzania - TRC lilisafirisha shehena ya mizigo tani 382,289 kwa umbali wa kilometa 360,780,885 ikilinganishwa na tani 491,322 kwa umbali wa kilometa 485,141,822 kwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa mizigo iliyosafirishwa kwa asilimia 22.2. Upungufu huo ulisababishwa na uhaba wa vitendea kazi ikiwemo vichwa

vya treni  na mabehewa ya mizigo pamoja na kufungwa kwa njia ya reli kutokana na mvua iliyosababisha uharibifu wa miundombinu ya reli.

294. Mwaka 2023, Shirika lilisafirisha abiria 489,560 wa masafa marefu kwa umbali wa kilometa 370,748,514 ikilinganishwa na abiria 466,262 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometa 343,076,014 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezwa kwa mabehewa 22 ya abiria pamoja na ukarabati wa njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Isaka. Kwa upande wa huduma ya usafiri wa treni katika Jiji la Dar es Salaam, Shirika lilisafirisha abiria 2,560,891 kwa umbali wa kilomita 71,704,948 mwaka 2023 ikilinganishwa na abiria 2,668,294 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometa 74,712,232 mwaka 2022, sawa na upungufu wa abiria waliosafirishwa kwa asilimia 4.0. Upungufu huo ulisababishwa na abiria kushindwa kufika kwa urahisi katika vituo vya kupandia na kushukia kutokana na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa.

295. Mwaka 2023, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia - TAZARA ilisafirisha mizigo yenye jumla ya tani 301,040 ikilinganishwa na tani 188,782 zilizosafirishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 59.5. Hii ilitokana na Mamlaka kuingia ubia na kampuni binafsi ya Calabash inayosafirisha mizigo kwa kulipia tozo ya njia pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa daraja la reli la Chambeshi.

**Jedwali Na. 12.3: Shehena ya Mzigo Iliyosafirishwa Mwaka 2019 - 2023**

| Aina ya Mzigo | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kwenda nje ya nchi | 68,253 | 71,249 | 75,140 | 17,863 | 28,064 | 57.1 |
| Kutoka nje ya nchi | 86,240 | 75,271 | 73,843 | 59,155 | 63,936 | 8.1 |
| Ndani ya TAZARA | 21,106 | 19,901 | 50,146 | 88,891 | 73,973 | -16.8 |
| **Jumla Ndogo** | **175,599** | **166,421** | **199,129** | **165,909** | **165,973** | **0.04** |
| Kampuni binafsi | - | 166,676 | 192,952 | 22,873 | 135,067 | 490.5 |
| **Jumla Kuu** | **175,599** | **333,097** | **392,081** | **188,782** | **301,040** | **59.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia

296. Mwaka 2023, Mamlaka ilisafirisha abiria 2,710,104 ikilinganishwa na abiria 2,793,588 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 3.0. Kati ya hao, abiria 534,603 walikuwa wa safari ndefu (Dar es Salaam - Mbeya - Zambia), abiria 359,564 wa treni ya Udzungwa na abiria 1,815,937 wa treni ya jijini Dar es Salaam.

**Jedwali Na. 12.4: Abiria Waliosafirishwa Mwaka 2019 - 2023**

| Aina ya Abiria | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Njia ndefu | 494,059 | 493,799 | 432,981 | 514,382 | 534,603 | 3.9 |
| Udzungwa | 396.895 | 420,945 | 406,762 | 375,575 | 359,564 | -4.3 |
| Dar es salaam | 2,155,048 | 1,813,108 | 1,872,930 | 1,903,631 | 1,815,937 | -4.6 |
| **Jumla** | **3,046,002** | **2,727.85** | **2,712,673** | **2,793,588** | **2,710,104** | **-3.0** |


**Chanzo**: Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia

### Usafiri wa Anga

297. Mwaka 2023, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania - TCAA ilisajili ndege 31 ikilinganishwa na ndege 12 zilizosajiliwa mwaka 2022. Hii ilitokana na: kuendelea kuimarika kwa biashara ya usafiri wa Anga; maboresho ya viwanja na mitambo ya kuongozea ndege; na juhudi za Serikali katika kukuza utalii kupitia programu maalum ya "*Tanzania - The Royal Tour*". Katika kipindi hicho, Mamlaka ilikagua na kutoa vyeti vya ubora kwa ndege 120 ikilinganishwa na ndege 147 mwaka 2022. Hadi Desemba 2023, mashirika 25 ya ndege za kimataifa yalitoa huduma kwa utaratibu wa mikataba ya usafiri wa anga baina ya Tanzania na nchi nyingine - BASA ikilinganishwa na mashirika 23 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko la ndege za kimataifa lilichangiwa na kuendelea kukua kwa soko la usafiri wa anga nchini na hivyo kuvutia mashirika mapya.


298. Mwaka 2023, abiria waliosafiri kwa njia ya anga walikuwa 6,820,541 ikilinganishwa na abiria 5,718,395 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 19.3. Kati ya hao, abiria 3,801,252 walisafiri ndani ya nchi na abiria 3,019,289 walisafiri nje ya nchi.

**Kielelezo Na.12.1: Idadi ya Abiria Waliotumia Usafiri wa Anga Mwaka 2019 - 2023**



299. Mwaka 2023, safari za ndege zilikuwa 199,711 ikilinganishwa na safari 195,619 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 2.1. Aidha, mizigo iliyosafirishwa ilikuwa tani 36,265.01 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 35,115 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Kuongezeka kwa safari za ndege na mizigo kulitokana na kuimarika kwa biashara ya usafiri wa anga pamoja na ongezeko la idadi ya watalii nchini.

**Kielelezo Na. 12.2: Safari za Ndege Mwaka 2019 - 2023**




| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kimataifa | 247,803 | 17,885 | 26,414 | 39,559 | 41,090 |
| Ndani ya nchi | 44,302 | 103,370 | 126,908 | 156,060 | 158,621 |
| Jumla | 292,105 | 121,255 | 153,322 | 195,619 | 199,711 |

Kimataifa  Ndani ya nchi  Jumla

300. Mwaka 2023, Shirika la ndege Tanzania - ATCL liliendelea kutoa huduma katika vituo vya ndani 13 ikilinganishwa na vituo 14 mwaka 2022. Hii ilitokana na kusitishwa kwa safari katika kituo cha Mtwara kutokana na ukarabati wa uwanja. Aidha, vituo vya nje ya nchi viliendelea kubaki 10 kama ilivyokuwa mwaka 2022.

301. Mwaka 2023, Shirika lilisafirisha abiria 1,070,347 ikilinganishwa na abiria 1,021,117 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 4.8. Aidha, Shirika lilisafirisha tani 4,065 za mizigo ndani na nje ya nchi mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 3,190 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 27.4. Ongezeko la usafirishaji wa abiria na mizigo lilitokana na kununuliwa kwa ndege mpya mbili ambapo moja ni ya abiria na nyingine ya mizigo.

**Usafiri wa Majini**

302. Mwaka 2023, leseni za waendeshaji wa shughuli za bandari zilizotolewa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania - TASAC zilikuwa 11 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Hii ni kutokana na uhai wa leseni hizo kuwa wa kipindi cha miaka mitatu, mitano na 10 kulingana na ukubwa na aina ya shughuli za bandari. Katika kipindi hicho, mawakala 1,143 wa ugomboaji shehena ipitayo katika maeneo ya kiforodha walipewa leseni ikilinganishwa na mawakala 1,129 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 1.2. Aidha, leseni za

wakusanyaji/watawanyaji wa mizigo zilikuwa 54 ikilinganishwa na leseni 33 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 63.6. Ongezeko la leseni lilitokana na kukua kwa fursa za biashara ya majini.

303. Mwaka 2023, leseni 48 za wapimaji uzito wa makasha zilitolewa ikilinganishwa na leseni 47 zilizotolewa mwaka 2022. Aidha, leseni za bandari kavu zilizotolewa zilifikia 77 mwaka 2023 kutoka leseni 69 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.6. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutolewa kwa leseni za bandari kavu za magari. Vile vile, leseni za uwakala wa meli zilifikia 41 mwaka 2023 kutoka leseni 34 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 20.6.

**Jedwali Na. 12.5: Leseni Zilizotolewa kwa Watoa Huduma Mwaka 2019 - 2023**

| Na. | Aina ya leseni | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ugomboaji wa shehena | 824 | 903 | 947 | 1,129 | 1,143 | 1.2 |
| 2 | Uwakala wa meli | 27 | 24 | 24 | 34 | 41 | 20.6 |
| 3 | Ukusanyaji wa mizigo | 28 | 31 | 32 | 33 | 54 | 63.6 |
| 4 | Upimaji wa makasha | 41 | 47 | 54 | 47 | 48 | 2.1 |
| 5 | Bandari Kavu | 27 | 42 | 46 | 69 | 77 | 11.6 |

**Chanzo:** Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania

304. Mwaka 2023, vyombo vidogo 12,193 vya usafiri majini (chini ya mita 24) vilipewa leseni ikilinganishwa na vyombo vidogo 9,159 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 33.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuwa na leseni. Aidha, TASAC ilisajili vyombo vikubwa 94 vya usafiri majini vyenye urefu wa zaidi ya mita 24 mwaka 2023 ikilinganishwa na vyombo vikubwa 93 mwaka 2022.

305. Mwaka 2023, shehena zilizohudumiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania - TPA zilikuwa tani milioni 26.36 ikilinganishwa na tani milioni 22.89 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 15.2. Ongezeko hilo lilitokana na Mamlaka kuendelea kuboresha miundombinu na huduma pamoja na kujitangaza katika nchi za jirani ambazo ziliendelea kutumia Bandari ya Dar es Salaam kupitisha mizigo.

**Jedwali Na. 12.6: Shehena Zilizohudumiwa (Tani '000) Mwaka 2019 - 2023**

| Bandari | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bandari Kuu za Mwambao** | | | | | | |
| Dar es Salaam | 16,023.0 | 15,875.9 | 17,025.0 | 19,870.2 | 22,916.2 | 15.3 |
| Tanga | 571 | 475 | 844 | 968.6 | 976.1 | 0.8 |
| Mtwara | 122 | 189 | 213 | 1,222.00 | 1,671.1 | 36.7 |
| **Jumla ndogo** | **16,716.0** | **16,521.9** | **18,082.0** | **22,060.8** | **25,563.4** | **15.9** |
| **Bandari Ndogo na Bandari za Maziwa Makuu** | | | | | | |
| Kilwa, Lindi, Mafia, Bagamoyo na Pwani | 32 | 107 | 191 | 207.8 | 229.8 | 10.6 |
| Mwanza | 163 | 142 | 234 | 283.5 | 267.9 | -5.5 |
| Kigoma | 206 | 250 | 265 | 313.4 | 286.2 | -8.7 |
| Kyela | 1 | 17 | 11 | 13.7 | 11.6 | -15.4 |
| **Jumla ndogo** | **402** | **516** | **701** | **818.4** | **795.5** | **-2.8** |
| **Jumla Kuu** | **17,118.0** | **17,037.9** | **18,783.0** | **22,879.2** | **26,358.9** | **15.2** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

306. Mwaka 2023, Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara zilihudumia makasha 993,899 yenye urefu wa futi 20 ikilinganishwa na makasha 893,190 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.3. Kati ya hayo, Bandari ya Dar es Salaam ilihudumia makasha 978,649, Tanga makasha 7,299 na Mtwara makasha 7,951. Ongezeko la makasha lilitokana na Bandari ya Dar es Salaam kupokea na kuhudumia meli kubwa za makasha kufuatia maboresho ya miundombinu ikiwemo kuongezwa kwa kina cha gati namba 1 hadi 7 pamoja na kuimarishwa kwa lango la bahari la kuingia na kutoka kwenye Bandari.

**Jedwali Na. 12.7: Shehena ya Makasha Yenye Urefu wa Futi 20 Mwaka 2019 - 2023**

| Bandari | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Dar es Salaam** | | | | | | |
| *Terminal 1* | 121,429 | 108,227 | 110,732 | 169,771 | 814,695 | 13.8 |
| *Terminal 2* | 605,002 | 601,654 | 606,169 | 715,707 | 163,954 | -3.4 |
| **Jumla ndogo** | 726,431 | 709,881 | 716,901 | 885,478 | 978,649 | 10.5 |
| Tanga | 6,334 | 7,401 | 5,817 | 7,712 | 7,299 | -5.4 |
| Mtwara | 3,695 | 19 | 90 | 0 | 7,951 | - |
| **Jumla ndogo** | 10,029 | 7,420 | 5,907 | 7,712 | 15,250 | 97.7 |
| **Jumla Kuu** | **736,460** | **717,301** | **722,808** | **893,190** | **993,899** | **11.3** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

307. Mwaka 2023, abiria 3,864,140 walihudumiwa na Mamlaka ikilinganishwa na abiria 3,999,657 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 3.4. Hii ilitokana na kusitishwa kwa huduma ya meli ya abiria katika bandari ya Tanga kwa ajili ya matengenezo.

**Jedwali Na. 12.8: Abiria Waliohudumiwa Mwaka 2019 - 2023**

| Bandari | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 1,994,809 | 1,639,683 | 2,303,471 | 2,300,228 | 2,302,998 | 0.1 |
| Tanga | 67,699 | 55,403 | 49,246 | 98,374 | 26,599 | 73.0 |
| Mwanza | 541,121 | 1,176,918 | 1,461,900 | 1,394,654 | 1,257,947 | 9.8 |
| Kigoma | 2,148 | 1,781 | 43,364 | 168,836 | 206,423 | 22.3 |
| Kyela | 3,790 | 5,670 | 17,209 | 37,565 | 70,173 | 86.8 |
| **Jumla** | **2,609,567** | **2,879,455** | **3,875,190** | **3,999,657** | **3,864,140** | **3.4** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

### Muda wa Meli Kukaa Bandarini

308. Mwaka 2023, muda wa meli kukaa bandarini ulikuwa wastani wa siku 10.6 ikilinganishwa na wastani wa siku 10.7 mwaka 2022. Aidha, muda wa meli kukaa bandarini kwa meli za makasha na shehena ya kawaida ulikuwa siku 9.0 na 8.0 mwaka 2023 ikilinganishwa na siku 10.4 na 7.4 mtawalia mwaka 2022. Vile vile, muda wa meli za mafuta kukaa bandarini uliongezeka na kufikia siku 14.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na siku 14.3 mwaka 2022.

**Jedwali Na. 12.9: Muda wa Meli Kukaa Bandarini (Siku) Mwaka 2019 - 2023**

| Kitengo/Meli | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Makasha | 3.5 | 3.3 | 3.8 | 10.4 | 9.0 |
| Shehena ya kawaida | 3.6 | 3.1 | 3.7 | 7.4 | 8.0 |
| Mafuta | 5.8 | 5.6 | 6.5 | 14.3 | 14.7 |
| **Wastani** | **4.3** | **4.0** | **4.7** | **10.7** | **10.6** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

### Shehena za Nchi Jirani

309. Mwaka 2023, shehena za nchi jirani zilizopita Bandari ya Dar es Salaam zilikuwa tani 8,871,438 ikilinganishwa na tani 8,239,112 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.7. Ongezeko hilo lilitokana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kuendelea kutangaza fursa za bandari kupitia ofisi za masoko katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (D.R. Congo), Zambia, Rwanda, na Burundi, pamoja na kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya bandari.

**Jedwali Na. 12.10: Shehena za Nchi Jirani (Tani) Mwaka 2019 - 2023**

| Nchi | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zambia | 1,763,052 | 1,159,013 | 1,507,746 | 1,975,793 | 2,311,278 | 17.0 |
| D.R. Congo | 1,914,138 | 1,840,657 | 2,357,867 | 3,379,124 | 3,726,938 | 10.3 |
| Burundi | 453,280 | 476,807 | 507,017 | 520,714 | 385,975 | -25.9 |
| Rwanda | 1,238,540 | 1,239,238 | 1,366,290 | 1,483,175 | 1,677,505 | 13.1 |
| Malawi | 336,714 | 407,472 | 471,385 | 557,826 | 581,981 | 4.3 |
| Uganda | 140,960 | 153,995 | 138,805 | 192,912 | 113,630 | -41.1 |
| Nyinginezo | 25,203 | 63,104 | 72,488 | 127,546 | 74,131 | -41.9 |
| **Jumla** | **5,871,887** | **5,340,287** | **6,421,598** | **8,239,112** | **8,871,438** | **7.7** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania
**Nyinginezo:** Msumbiji, Sudani, Kenya, Comoro, Angola na Zimbabwe

### Uchukuzi Kwenye Maziwa

310. Mwaka 2023, Kampuni ya Huduma za Meli - MSCL ilisafirisha abiria 279,566 ikilinganishwa na abiria 294,114 waliosafirishwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 4.9. Upungufu huo ulitokana na abiria wengi kuamua kutumia usafiri kwa njia ya barabara. Aidha, katika kipindi hicho, Kampuni ilisafirisha tani 44,598.70 za mizigo ikilinganishwa na tani 25,897.4 zilizosafirishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 72.2. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa kwa kitengo cha masoko na biashara na kuendelea kutoa huduma kwa meli za New Victoria, New Butiama, MV Umoja na MV Clarias katika Ziwa Victoria, pamoja na MV Mbeya II katika Ziwa Nyasa.

### Kampuni ya Meli ya China na Tanzania

311. Mwaka 2023, Kampuni ya Meli ya China na Tanzania - SINOTASHIP ilisafirisha tani 619,870 za shehena ikilinganishwa na tani 610,774 zilizosafirishwa mwaka 2022. Aidha, makasha 73,599 yalihudumiwa na Kampuni katika Bandari ya Dar es Salaam mwaka 2023, ikilinganishwa na makasha 63,529 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 15.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa biashara ya uwakala na meli zinazoleta na kuondosha mizigo katika bandari ya Dar es Salaam.

### Huduma za Hali ya Hewa

312. Mwaka 2023, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania - TMA ilihudumia ndege 48,516 ikilinganishwa na ndege 45,891 zilizohudumiwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 5.7. Aidha, Mamlaka ilihudumia meli/boti 131,749 mwaka 2023 ikilinganishwa na meli/boti 66,002 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 99.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa kuhusu umuhimu wa taarifa za hali ya hewa kwa watumiaji wa usafiri wa majini.

313. Mwaka 2023, Mamlaka ilihudumia wateja 1,420 wa huduma mahsusi ikilinganishwa na wateja 674 mwaka 2022. Aidha, kiwango cha usahihi wa utabiri kilifikia asilimia 86.4

ikilinganishwa na asilimia 88.5 mwaka 2022. Ongezeko la utoaji wa huduma mahsusi pamoja na kiwango cha usahihi wa utabiri limechangiwa na Serikali kuendelea kuwekeza katika mitambo na vifaa vya kisasa vya hali ya hewa. Kiwango kilichofikiwa ni zaidi ya asilimia 70 kinachokubalika Kimataifa na Shirika la Hali ya Hewa Duniani.

**Jedwali Na. 59: SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)+**

| Maelezo | Kipimo | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tani-Kilometa: | | | | | | | | | |
| Zilizokuwepo | 000 | 3,937 | 863,107 | 32,095 | 32,927 | 65,968 | 68,806 | 71,872 | 133,124 |
| Zilizotumika | 000 | 1,756 | 89,092 | 17,526 | 18,944 | 33,655 | 38,930 | 48,464 | 81,137 |
| Matumizi | % | 47 | 10 | 55 | 58 | 51 | 56.6 | 67 | 61 |
| **Viti - kilometa:** | | | | | | | | | |
| Vilivyokuwepo | 000 | 37,877 | 225,259 | 231,943 | 321,771 | 557,216 | 552,682 | 690,408 | 1,227,755 |
| Vilivyotumika | 000 | 20,692 | 122,532 | 158,203 | 220,433 | 347,101 | 417,706 | 552,968 | 788,162 |
| Matumizi | % | 56 | 54 | 68 | 69 | 62 | 75 | 80 | 64.2 |
| Abiria ++ | 000 | 28 | 129 | 279 | 627 | 434 | 657 | 929 | 1,066 |
| Mizigo ya ziada | Tani | 1 | 41 | 55 | 96 | 86 | 75 | 54 | 0 |
| Mizigo mingine | Tani | 7 | 50 | 220 | 696 | 438 | 526 | 3,030 | 2,992 |
| Shehena za Posta | Tani | - | 32 | 119 | 295 | 61 | 21 | 72 | 91 |

**Chanzo:** Shirika la Ndege Tanzania
+ Zinahusu "scheduled traffic" tu
++ Abiria waliolipa nauli kamili
- Takwimu hazikupatikana

# SURA YA 13

# HABARI, MAWASILIANO, SANAA NA BURUDANI

## MAWASILIANO

### Huduma za Posta

314. Mwaka 2023, Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua 1,146,627 ndani ya nchi ikilinganishwa na barua 1,476,336 zilizosafirishwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 22.3. Upungufu huo ulitokana na ushindani kutoka kwa wasafirishaji binafsi pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya njia za kidigitali katika mawasiliano. Katika kipindi hicho, barua 296,657 zilisafirishwa nje ya nchi ikilinganishwa na barua 232,504 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 27.6. Ongezeko hilo lilitokana na kurejea kwa shughuli za kiuchumi katika nchi mbalimbali kutokana na kupungua kwa maambukizi ya UVIKO - 19.

315. Mwaka 2023, vifurushi vilivyosafirishwa ndani ya nchi viliongezeka kwa asilimia 42.6 na kufikia 18,760 ikilinganishwa na vifurushi 13,159 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na wateja wakubwa ikiwemo, Benki ya CRDB, Benki ya NMB na kampuni ya mawasiliano ya Tigo kuendelea kutumia huduma zinazotolewa na Shirika pamoja na kukua kwa biashara kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya usafiri katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, vifurushi vilivyosafirishwa nje ya nchi mwaka 2023 vilikuwa 2,450 ikilinganishwa na vifurushi 1,158 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kurejea kwa shughuli za kiuchumi katika nchi mbalimbali kufuatia kupungua kwa maambukizi ya UVIKO - 19 pamoja na Shirika la World Vision na Compassion kutuma vifurushi vingi kwa mara moja.

316. Mwaka 2023, Shirika la Posta lilisafirisha rejesta 86,014 nchini ikilinganishwa na rejesta 72,595 zilizosafirishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 18.5. Ongezeko hilo lilitokana na kuwepo kwa taasisi zilizotoa matangazo ya ajira na kuelekeza maombi yatumwe kwa njia ya Posta. Kwa upande mwingine, rejesta 7,751 zilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2023 ikilinganishwa na rejesta 11,950 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 35.1. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya njia za kidigitali ikiwemo barua pepe katika mawasiliano.

317. Mwaka 2023, nyaraka na vipeto vilivyotumwa kwa njia ya haraka nchini vilipungua kwa asilimia 13.7 na kufikia 519,607 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 602,339 mwaka 2022. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa ushindani wa kibiashara na uchakavu wa vitendea kazi ikiwemo, magari na pikipiki. Aidha, nyaraka na vipeto 7,923 vilitumwa nje ya nchi kwa njia ya haraka mwaka 2023 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 8,454 vilivyotumwa nje ya nchi mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 6.3. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa ushindani wa biashara za usafirishaji. Vile vile, barua na

nyaraka 32,665 zilipokelewa na kusambazwa kwa njia ya huduma ya usambazaji wa barua za haraka ndani ya miji mwaka 2023 ikilinganishwa na barua na nyaraka 39,525 zilizopokelewa na kusambazwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 17.4. Upungufu huo ulitokana na ushindani mkubwa wa kibiashara, hususan huduma ya usambazaji wa barua za haraka ndani ya miji.

318. Mwaka 2023, miamala ya fedha 24,197 ilifanyika kupitia njia ya *Western Union* ikilinganishwa na miamala 37,757 iliyofanyika mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 35.9. Aidha, miamala 1,121 ya fedha ilifanyika kupitia njia ya Money Gram mwaka 2023 ikilinganishwa na miamala 3,305 iliyofanyika mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 66.1. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya ofisi kufungwa kwa ajili ya ukarabati na kuhuisha mfumo wa *Western Union Point of Sale* (WUPOS).

**Huduma za Simu**

319. Mwaka 2023, kadi za simu za kiganjani ziliongezeka kwa asilimia 16.7 na kufikia 70,215,144 kutoka kadi 60,192,331 mwaka 2022. Hii ilitokana na kukua kwa huduma za habari na mawasiliano, kuongezeka kwa miamala ya fedha mtandao na huduma nyingine za kimtandao. Aidha, kadi za simu za mezani zilipungua kwa asilimia 10.6 na kufikia 75,732 mwaka 2023 kutoka kadi 84,696 mwaka 2022. Hii ilitokana na kupungua kwa mahitaji kufuatia kurahisishwa kwa mawasiliano kupitia simu za kiganjani.

320. Mwaka 2023, wastani wa gharama za kupiga simu ndani ya mtandao zilikuwa shilingi 26 na nje ya mtandao shilingi 28 kwa dakika ikilinganishwa na wastani wa gharama ya shilingi 32 kupiga simu ndani na nje ya mtandao kwa dakika mwaka 2022. Mabadiliko hayo yalitokana na kuongezeka kwa ushindani katika soko la mawasiliano. Aidha, wastani wa gharama za kupiga simu ndani ya Afrika Mashariki zilikuwa shilingi 754 kwa dakika mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,151 kwa dakika mwaka 2022. Kupungua kwa gharama za kupiga simu ndani ya Afrika Mashariki kulitokana na kuongezeka kwa ushindani kwa watoa huduma za mawasiliano ndani ya Afrika Mashariki. Vile vile, wastani wa gharama za kupiga simu kwenda mataifa mengine zilikuwa shilingi 1,960 kwa dakika mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,889 kwa dakika mwaka 2022.

**Huduma za Intaneti**

321. Mwaka 2023, kadi za simu zinazotumia intaneti zilikuwa milioni 35.9 ikilinganishwa na kadi za simu milioni 31.2 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 15.1. Aidha, matumizi ya intaneti nchini yalikuwa Gigabaiti (GB) milioni 1,026 mwaka 2023 ikilinganishwa na Gigabaiti milioni 227.5 mwaka 2022. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa matumizi ya intaneti na maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya huduma za mtandao wa intaneti.

**Jedwali Na. 13.1: Huduma za Intaneti Nchini Mwaka 2019 - 2023**

| Aina ya Huduma | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| *Fixed Wireless* | 773,837 | 510,683 | 1,034,958 | 6,003 | 8,315 | 38.5 |
| *Mobile Wireless* | 24,762,778 | 27,371,350 | 25,176,367 | 31,100,860 | 35,815,632 | 15.2 |
| *Fixed Wired* | 257,946 | 588,472 | 3,647,434 | 65,681 | 61,645 | -6.1 |
| **Jumla** | **25,794,560** | **28,470,506** | **29,858,759** | **31,172,544** | **35,885,592** | **15.1** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

### Huduma za Utangazaji

322. Mwaka 2023, watumiaji wa huduma za utangazaji walifikia 3,678,199 kutoka watumiaji 3,455,323 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Kati ya hao, watumiaji wa huduma za utangazaji kupitia satelaiti walifikia 1,880,636 kutoka watumiaji 1,702,056 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 10.5. Aidha, watumiaji wa huduma za utangazaji kupitia mitambo iliyosimikwa ardhini walifikia 1,781,340 kutoka watumiaji 1,667,465 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Vile vile, watumiaji wa cable television walipungua na kufikia 16,223 mwaka 2023 kutoka watumiaji 85,802 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 81.1. Upungufu huo ulitokana na kukua kwa vyanzo vingine vya upashanaji habari ikiwemo mitandao ya kijamii, utangazaji kupitia satelaiti na mitambo iliyosimikwa ardhini.

**Jedwali Na. 13:2: Watumiaji wa Huduma za Utangazaji Mwaka 2022 - 2023**

| Aina ya Huduma | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mitambo iliyosimikwa ardhini - DTT | 1,432,398 | 1,472,317 | 1,613,031 | 1,667,465 | 1,781,340 | 6.8 |
| Satelaiti - DTH | 1,092,891 | 1,341,686 | 1,577,315 | 1,702,056 | 1,880,636 | 10.5 |
| *Cable Television* | 158,224 | 158,224 | 29,403 | 85,802 | 16,223 | 81.1 |
| **Jumla** | **2,236,577** | **2,769,841** | **3,219,749** | **3,455,323** | **3,678,199** | **6.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

### Utoaji wa Leseni za Mawasiliano

323. Mwaka 2023, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni 352 za huduma mbalimbali za mawasiliano ikilinganishwa na leseni 246 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 43.1. Ongezeko hilo lilitokana na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu utaratibu wa kuwasilisha maombi ya leseni kwa njia ya kielektroniki na punguzo la gharama za leseni kwa baadhi ya watoa huduma.

**Jedwali Na. 13.3: Leseni Zilizotolewa Mwaka 2019 - 2023**

| Na. | Aina ya Leseni | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Huduma za mawasiliano daraja B | 15 | 6 | 0 | 0 | 0 | - |
| 2 | Maudhui ya redio | 22 | 15 | 13 | 15 | 29 | 93.3 |
| 3 | Maudhui ya runinga | 6 | 7 | 9 | 9 | 5 | -44.4 |
| 4 | Ufungaji na utengenezaji wa vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki | 67 | 33 | 50 | 20 | 65 | 225 |
| 5 | Kuingiza nchini vifaa vya mawasiliano vya | 42 | 30 | 44 | 45 | 42 | -6.7 |
| 6 | Kusambaza nchini vifaa vya mawasiliano vya | 23 | 12 | 16 | 20 | 25 | 25 |
| 7 | Kuuza vifaa vya mawasiliano vya | 321 | 606 | 201 | 29 | 0 | - |
| 8 | Huduma za kusafirisha vifurushi na vipeto | 90 | 39 | 20 | 22 | 61 | 177.3 |
| 9 | V-sat | 571 | 57 | 21 | 69 | 11 | -84.1 |
| 10 | Maudhui ya mtandaoni | 330 | 305 | 151 | 0 | 109 | - |
| 11 | Maudhui kutokana na matumizi | 18 | 15 | 21 | 17 | 5 | -70.5 |
| | **Jumla** | **1,505** | **1,125** | **546** | **246** | **352** | **43.1** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

324. Hadi Desemba 2023, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulikuwa na urefu wa kilometa 11,436 zilizounganishwa kwenye mikoa 26 ikilinganishwa na kilometa 9,982 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.6. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa lengo la kuongeza wigo wa upatikanaji wa mawasiliano ya simu na intaneti nchini na nchi jirani ili kufikia mapinduzi ya kidigitali. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano yalikuwa ni shilingi milioni 56,966.00 ikilinganishwa na shilingi milioni 32,440.63 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 75.6.

**HABARI**

325. Hadi Desemba 2023, kulikuwa na magazeti 328, vituo vya redio 244 na vituo vya runinga 78 vilivyosajiliwa na kupewa leseni ikilinganishwa na magazeti 296, vituo vya redio 226 na vituo vya runinga 60 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa mahitaji ya kupashana habari na kupungua kwa gharama ya leseni kwa baadhi ya huduma kufuatia mabadiliko ya kanuni. Katika kipindi hicho, magazeti na majarida 32 yalisajiliwa ikilinganishwa na magazeti na majarida 46 yaliyosajiliwa mwaka 2022. Aidha, vituo vipya 18 vya redio vilisajiliwa mwaka 2023 ikilinganishwa na vituo 15 mwaka 2022. Vile vile,

vituo vipya 18 vya runinga vilisajiliwa mwaka 2023 ikilinganishwa na vituo tisa (9) mwaka 2022. Kwa upande mwingine, blogu 22 zilisajiliwa mwaka 2023 ikilinganishwa na blogu sita (6) mwaka 2022.

**Jedwali 13.4: Usajili wa Vyombo vya Habari Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Idadi ya Magazeti/Majarida | Idadi ya Vituo vya Redio | Idadi ya Vituo vya Runinga | Idadi ya Blogu |
|---|---|---|---|---|
| 2019 | 23 | 21 | 8 | 106 |
| 2020 | 24 | 15 | 1 | 40 |
| 2021 | 26 | 9 | 10 | 15 |
| 2022 | 46 | 15 | 9 | 6 |
| 2023 | 32 | 18 | 18 | 22 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

326. Mwaka 2022/2023, Shirika la Utangazaji Tanzania-TBC liliendelea kuongeza usikivu wa redio kwa kufunga mitambo ya masafa ya FM maeneo mbalimbali ya nchi. Katika kipindi hicho, Shirika lilifungua mitambo ya masafa katika wilaya 20 ikilinganishwa na wilaya 19 mwaka 2021/2022. Ongezeko hilo liliwezesha wilaya 137 kufikiwa na huduma za Shirika na hivyo, kuwezesha wananchi kupata matangazo ya redio ya taifa (TBC Taifa na TBC FM).

327. Hadi Desemba 2023, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote - UCSAF kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano ulifikisha huduma za mawasiliano katika kata 1,219 zenye vijiji 3,648 na wakazi 14,926,860 ikilinganishwa na kata 1,095 zilizokuwa na vijiji 3,392 na wakazi 13,391,794 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa Mradi wa Mawasiliano Vijijini. Katika kipindi hicho, minara 122 ilikamilika na kuanza kutoa huduma ya mawasiliano ya simu ikilinganishwa na minara 304 mwaka 2022. Kati ya minara hiyo, Halotel ilikuwa na minara 14, TTCL 51, Airtel 39, Vodacom 17 na Tigo (MIC) mmoja.

## SANAA NA BURUDANI

### Maendeleo ya Kiswahili Kitaifa na Kimataifa

328. Mwaka 2023, Baraza la Kiswahili la Taifa - BAKITA liliandaa na kurusha hewani vipindi 1,187 kuhusu sarufi na fasihi ya kiswahili kupitia redio na runinga ikilinganishwa na vipindi 1,064 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.6. Katika kipindi hicho, vitabu vya miswada ya ithibati ya lugha vilivyokusudiwa kutumika shuleni vilipungua kwa asilimia 72.7 na kufikia 30 ikilinganishwa na vitabu vya miswada 110 mwaka 2022. Upungufu huo ulitokana na uamuzi wa Serikali kutumia vitabu vya kiada na ziada vilivyochapishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania. Kwa upande mwingine, BAKITA ilisajili wataalamu 328 wa kiswahili katika kanzidata mwaka 2023 ikilinganishwa na wataalamu

316 waliosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Hii ilitokana na ongezeko la mahitaji ya wataalamu wa kiswahili kwa ajili ya kufundisha raia wa kigeni lugha ya Kiswahili.

329. Mwaka 2023, Baraza la Kiswahili la Taifa lilikuwa na vituo 44 vya kufundisha kiswahili kwa raia wa kigeni vilivyosajiliwa na kupewa ithibati ikilinganishwa na jumla ya vituo 20 vilivyosajiliwa mwaka 2022. Hadi Desemba 2023, watanzania wanaofundisha kiswahili nje ya nchi walifikia 203 kutoka watanzania 85 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Uhariri na Tafsiri ya Nyaraka**

330. Mwaka 2023, BAKITA ilitafsiri nyaraka 1,380 ikilinganishwa na nyaraka 1,375 mwaka 2022. Kati ya hizo, nyaraka 322 zilitafsiriwa kutoka lugha ya kiingereza kwenda lugha ya kiswahili, nyaraka 135 kutoka lugha ya kiswahili kwenda lugha ya kiingereza, nyaraka 209 kutoka lugha ya kifaransa kwenda lugha ya kiingereza na nyaraka 714 kutoka lugha ya kiarabu kwenda lugha ya kiingereza. Ongezeko hilo lilitokana na kutangaza huduma zinazotolewa na Baraza ikiwamo tafsiri. Aidha, Baraza liliratibu huduma ya ukalimani katika mikutano 11 ya kitaifa na kimataifa.

331. Mwaka 2023, Baraza lilihariri miswada 10 ikilinganishwa na miswada 20 iliyohaririwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 50. Hii ilitokana na kupungua kwa miswada kutoka kwa wahariri binafsi kulikosababishwa na kukosekana kwa soko la bidhaa za uandishi, pamoja na baadhi ya taasisi kutotumia uhariri wa lugha katika maandalizi ya nyaraka mbalimbali. Kwa upande mwingine, BAKITA ilibaini makosa 192 ya matumizi ya lugha ya kiswahili katika vyombo vya habari mwaka 2023 ikilinganishwa na makosa 1,005 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 80.9. Upungufu huo ulitokana na elimu ya matumizi ya lugha sahihi iliyotolewa na Baraza kupitia redio, televisheni, mitandao ya kijamii, magazeti na semina kwa waandishi.

**Jedwali Na. 13.5: Huduma Zilizotolewa na BAKITA Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Vipindi vya Redio na Runinga | Huduma ya Ithibati | Huduma ya Tafsiri | Huduma ya Ukalimani | Huduma ya Uhariri | Makosa ya Matumizi ya Lugha Vyombo vya Habari |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2019 | 780 | 38 | 5,061 | 2 | 7 | 1,081 |
| 2020 | 1,020 | 213 | 869 | 0 | 41 | 1,380 |
| 2021 | 1,008 | 203 | 1,148 | 0 | 23 | 1,205 |
| 2022 | 1,064 | 110 | 1,375 | 12 | 20 | 1,005 |
| 2023 | 1,187 | 30 | 1,380 | 11 | 10 | 192 |

**Chanzo:** Baraza la Kiswahili la Taifa

**Maendeleo ya Sanaa**

**Vibali vya Utayarishaji wa Filamu**

332. Mwaka 2023, Bodi ya Filamu Tanzania ilitoa vibali 276 vya utayarishaji wa filamu ikilinganishwa na vibali 272 vilivyotolewa mwaka 2022. Kati ya hivyo, vibali 201 vilitolewa kwa watayarishaji filamu wa Tanzania na vibali 75 vilitolewa kwa wageni. Kuongezeka kwa vibali hivyo kulitokana na kuendelea kwa utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria na kanuni kwa waandaaji wa filamu.

**Usajili wa Wabunifu na Kazi za Sanaa**

333. Mwaka 2023, Taasisi ya Hakimiliki Tanzania - COSOTA ilisajili wabunifu 518 wa kazi za sanaa ikilinganishwa na wabunifu 424 waliosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 22.2. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji kwa wanachama kusajili kazi zao kwa njia ya kielektroniki. Aidha, kazi za sanaa zilizosajiliwa na COSOTA zilikuwa 2,379 mwaka 2023 ikilinganishwa na kazi 3,904 zilizosajiliwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 39.1. Upungufu wa usajili wa kazi za sanaa ulitokana na baadhi ya vyombo vya habari kusitisha ununuzi wa filamu.

334. Mwaka 2023, COSOTA ilitoa vyeti 1,357 vya uthibitisho wa umiliki wa hakimiliki ikilinganishwa na vyeti 1,430 vilivyotolewa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 5.1. Aidha, leseni 360 za watumiaji wa kazi zenye hakimiliki zilitolewa mwaka 2023 ikilinganishwa na leseni 621 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 42. Upungufu huo ulitokana na uelewa mdogo wa wasanii na waandishi kuhusu mgawanyo wa majukumu ya usimamizi wa hakimiliki yaliyotokana na marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999.

**Jedwali Na. 13.6: Huduma Zilizotolewa na Taasisi ya Hakimiliki Tanzania Mwaka 2019 - 2023**

| **Na.** | **Huduma** | **Mwaka** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
| 1 | Usajili wa Wabunifu wa kazi za sanaa | 1378 | 1,436 | 2,066 | 424 | 518 |
| 2 | Usajili wa kazi za ubunifu | 0 | 1,431 | 3,827 | 3,904 | 2,379 |
| 3 | Vyeti vya Umiliki (Clearance Certificates) | 1241 | 1,431 | 3,835 | 1,430 | 1,357 |
| 4 | Leseni | 354 | 354 | 370 | 621 | 360 |

**Chanzo**: Taasisi ya Hakimiliki Tanzania

**Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo**

335. Mwaka 2023, vikundi 43 vya sanaa na utamaduni kutoka ndani na nje ya nchi vilishiriki katika Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ikilinganishwa na vikundi 46 vilivyoshiriki mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 6.5. Kati ya vikundi hivyo, vikundi 39 vilitoka ndani ya nchi na vinne (4) vilitoka nje ya nchi.

**Usajili wa Wasanii**

336. Mwaka 2023, Baraza la Sanaa la Taifa - BASATA liliendelea kurasimisha kazi za wasanii nchini ambapo wasanii binafsi 1,089 walisajiliwa ikilinganishwa na wasanii 472 waliosajiliwa mwaka 2022. Kati ya hao, wasanii 685 walikuwa wa muziki, sawa na asilimia 62.9, wasanii 179 walikuwa wa maonesho (asilimia 16.4) na wasanii 225 wa ufundi (asilimia 20.7). Ongezeko hilo lilitokana na elimu na hamasa iliyoendelea kutolewa kwa wasanii na wadau wa sanaa ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wa kutumia mfumo wa usajili wa kielektroniki.

**Jedwali Na. 13.7: Usajili wa Wasanii Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Ufundi | Maonesho | Muziki | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 2019 | 64 | 446 | 500 | 1,010 |
| 2020 | 34 | 172 | 171 | 377 |
| 2021 | 68 | 197 | 201 | 466 |
| 2022 | 87 | 178 | 207 | 472 |
| 2023 | 225 | 179 | 685 | 1,089 |

**Chanzo:** Baraza la Sanaa la Taifa

**Utoaji wa Tuzo za Kazi za Sanaa**

337. Mwaka 2022/23, tuzo 54 zilitolewa kwa wasanii wa muziki wa kitanzania ikilinganishwa na tuzo 61 zilizotolewa mwaka 2021/22, sawa na upungufu wa asilimia 11.5. Kati ya hizo, tuzo 44 zilikuwa za ndani ya nchi na tuzo 10 zilikuwa za nje ya nchi. Kupungua kwa tuzo zilizotolewa kulitokana na maboresho katika vipengele vilivyotumika katika utoaji wa tuzo.

**Jedwali Na. 13.8: Tuzo za Muziki kwa Wasanii wa Kitanzania Mwaka 2018/19 - 2022/23**

| Mwaka | Idadi ya Tuzo za Ndani | Idadi ya Tuzo za Nje | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2018/19 | 10 | 4 | 14 |
| 2019/20 | 8 | 2 | 10 |
| 2020/21 | 15 | 13 | 28 |
| 2021/22 | 47 | 14 | 61 |
| 2022/23 | 44 | 10 | 54 |

**Chanzo:** Baraza la Sanaa la Taifa

338. Mwaka 2023, tuzo 56 zilitolewa kwa wadau wa filamu ikilinganishwa na tuzo 63 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 11.1. Upungufu huo ulichangiwa na maboresho katika vipengele vilivyotumika katika utoaji wa tuzo. Kati ya hizo, tuzo 41 zilikuwa za ndani ya nchi na tuzo 15 zilikuwa za nje ya nchi.

**Jedwali Na. 13.9: Tuzo za Filamu Mwaka 2019 - 2023**

| Tuzo | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Tuzo za Ndani | 22 | 2 | 33 | 50 | 41 |
| Tuzo za Nje | 2 | 2 | 3 | 13 | 15 |
| **Jumla** | **24** | **4** | **36** | **63** | **56** |

**Chanzo:** Bodi ya Filamu Tanzania

**Maendeleo ya Michezo**

339. Mwaka 2023, Baraza la Michezo la Taifa - BMT lilisajili vilabu vya michezo 154 ikilinganishwa na vilabu 178 vilivyosajiliwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 13.5. Hadi Desemba 2023, vilabu vya michezo vilivyosajiliwa vilifikia 9,823 kutoka vilabu 9,669 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, vyama vya michezo vilivyosajiliwa vilifikia 552 mwaka 2023 kutoka vyama 518 vilivyosajiliwa mwaka 2022. Vile vile, wakuzaji/mawakala waliosajiliwa walifikia 247 mwaka 2023 kutoka wakuzaji/mawakala 188 mwaka 2022. Aidha, vituo/shule za michezo 28 zilisajiliwa mwaka 2023 ikilinganishwa na vituo/shule 33 zilizosajiliwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 15.2. Upungufu huo ulitokana na mwitikio mdogo wa wadau wa michezo katika kusajili vituo/shule za michezo.

**Jedwali Na. 13.10: Usajili wa Wadau wa Michezo Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Vilabu vya Michezo | Vyama vya Michezo | Vituo/shule za Michezo | Wakuzaji /Mawakala wa Michezo | Taasisi za Michezo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2019 | 231 | 18 | 21 | 19 | 0 | 289 |
| 2020 | 110 | 12 | 5 | 26 | 10 | 163 |
| 2021 | 216 | 15 | 22 | 60 | 9 | 322 |
| 2022 | 178 | 15 | 33 | 40 | 10 | 276 |
| 2023 | 154 | 34 | 28 | 59 | 0 | 275 |

**Chanzo:** Baraza la Michezo la Taifa

## Jedwali Na. 60: HUDUMA ZA POSTA

| Maelezo | Kipimo | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ofisi Ndogo Posta | Namba | 65 | 65 | 66 | 57 | 46 | 40 | 29 | 29 | 29 |
| Franchised Post Offices | Namba | 90 | 90 | 87 | 87 | 79 | 72 | 70 | 70 | 70 |
| Ofisi Kubwa | Namba | 158 | 158 | 154 | 157 | 139 | 132 | 144 | 144 | 144 |
| **Jumla** | Namba | **313** | **313** | **307** | **301** | **264** | **244** | **243** | **243** | **243** |
| Masanduku Binafsi | 000 | 160 | 160 | 161 | 161 | 145 | 126 | 126 | 126 | 152 |
| Masanduku Yaliokodishwa | 000 | 138 | 138 | 143 | 157 | 126 | 125 | 125 | 125 | 119 |
| Maombi Yasiotimizwa | 000 | 4 | 1 | 1 | 3 | 1 | 1 | 2 | 0 | - |
| Mifuko Pekee Iliyokodishwa | Namba | 180 | 180 | 342 | 675 | 442 | 291 | 240 | 180 | 60 |
| Barua Zilizotumwa bila Vifurushi | Mill. | 10 | 4 | 5 | 9 | 11 | 6 | 4 | 2 | 2 |
| Regista na Barua za Amana | 000 | 402 | 297 | 269 | 280 | 186 | 65 | 45 | 50 | 25 |
| Vifurushi Nchini | 000 | 17 | 36 | 51 | 63 | 32 | 4 | 6 | 10 | 7 |
| Vifurushi Nje | 000 | 9 | 2 | 3 | 4 | 3 | 2 | 2 | 1 | 6 |
| Leseni za kuuza stamp | Namba | - | - | 4,635 | 6,027 | 5,570 | 2,803 | 1,726 | 1,374 | 463 |
| **Huduma za Haraka, barua na vifurushi** | " | | | | | | | | | |
| Ndani ya Nchi | " | 416,007 | 452,827 | 560,710 | 655,927 | 511,274 | 466,029 | 627,822 | 481,588 | 354,746 |
| Nje ya Nchi | " | 308,288 | 6,364 | 9,534 | 14,346 | 13,742 | 7,080 | 11,642 | 5150 | 6,254 |
| EMS Money Fax | " | 748 | 272 | 18 | - | - | 52 | - | - | - |
| EMS Fax (Fax message received) | " | 3,844 | 2,518 | 129 | - | - | - | - | 0 | - |
| **Overnight Mail Services** | " | - | - | - | - | - | - | - | 0 | - |
| Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa | " | 53,639 | 57,605 | 24,966 | 14,553 | 19,598 | 46,093 | 30,339 | 24889 | 26,171 |
| Vifurushi vya magazeti vilivyosafirishwa | " | 9,130 | 113,448 | 2,120 | 5,346 | 7,800 | - | - | 0 | - |
| **Huduma za gari ndogo** | | | | | | | | | | |
| Idadi ya Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa | " | 9,576 | - | - | 2,919 | 2,518 | 5,651 | 3,293 | 6377 | 5,178 |
| Amna za Haraka Zilizotolewa | " | 58,423 | 272 | 127 | 104 | 109 | 52 | | 0 | - |
| Amana za Haraka Zilizolipwa | | - | - | - | | - | - | - | 0 | - |
| **Amana za Haraka za Nje ya Nchi** | | | | | | | | | | |
| Zilizotumwa | " | 221 | 220 | 8 | 11 | 26 | - | - | 0 | - |
| Zilizopokelewa | " | 283 | 116 | 43 | 37 | - | - | - | 0 | - |
| Amana za Posta zilizouzwa | " | 251 | 107 | 45 | 2 | - | - | - | 0 | - |
| Amana za Posta Zilizolipwa | " | 25 | 18 | 8 | - | - | - | - | 0 | - |
| **Benki ya Akiba (Transaction)** | | | | | | | | | | |
| Uwekaji Amana (Deposit) | " | 21,541 | 261,423 | 59,249 | 108,972 | 91,567 | 56,064 | 94,689 | 96,959 | 70,110 |
| Uchukuaji Amana (Withdrawal) | " | 18,098 | 45,449 | 76,926 | 133,531 | 103,958 | 75,065 | 69,203 | 94,374 | 106,845 |

**Chanzo**: Shirika la Posta

**Jedwali Na. 61: IDADI YA KADI ZA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI**

| Kampuni | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A. Simu za Kiganjani** | | | | | | | | |
| Mobitel/Tigo | 11,044,520 | 12,583,640 | 12,572,826 | 13,032,073 | 13,369,276 | 15,940,373 | 19,698,263 | 23.6 |
| Vodacom | 12,714,297 | 14,143,657 | 15,672,390 | 15,621,457 | 15,913,553 | 18,180,904 | 21,272,484 | 17.0 |
| Airtel | 10,571,110 | 10,954,621 | 12,722,224 | 13,823,756 | 14,700,426 | 16,616,488 | 19,146,016 | 15.2 |
| Zantel | 934,991 | 1,153,623 | 1,170,085 | 1,021,409 | 1,107,504 | - | - | - |
| Benson/Smart | 131,501 | 132,292 | | - | - | - | - | - |
| TTCL Mobile | 175,717 | 587,191 | 981,072 | 963,384 | 1,813,719 | 1,495,577 | 1,644,194 | 9.9 |
| Smile | | | 1,222 | 12,395 | 11,600 | 15547 | - | - |
| Hallotel | 3,799,691 | 3,942,237 | 4,641,701 | 6,818,228 | 7,200,140 | 8,028,138 | 8,529,919 | 6.3 |
| **Jumla Ndogo** | **39,371,827** | **43,497,261** | **47,761,520** | **51,292,702** | **54,116,218** | **60,277,027** | **70,290,876** | **16.6** |
| **B. Simu za Mezani** | | | | | | | | |
| TTCL | 127,009 | 124,220 | 76,288 | 72,469 | - | - | - | |
| Zantel | 85 | 18 | | - | - | - | - | |
| **Jumla Ndogo** | **127,094** | **124,238** | **76,288** | **72,469** | - | - | - | |
| Mobile Network | | 43,497,261 | 47,685,232 | 51,220,233 | 54,044,384 | 60,192,331 | 70,215,144 | 16.7 |
| Fixed Network | | 124,298 | 76,288 | 72,834 | 71,834 | 84696 | 75,732 | -10.6 |
| **Jumla Ndogo** | | **43,621,559** | **47,761,520** | **51,293,067** | **54,116,218** | **60,277,027** | **70,290,876** | **16.6** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

# SURA YA 14

## NISHATI

**Ufuaji wa Umeme**


340. Mwaka 2023, uwezo wa uzalishaji wa umeme ulikuwa megawati 1,887.50 ikilinganishwa na megawati 1,733.4 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.9. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza kufanya kazi kwa miradi ya Rusumo na Kinyerezi I Extension ambayo pia imeongeza umeme unaozalishwa nchini. Aidha, hadi kufikia mwezi Desemba, 2023, ujenzi wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Julius Nyerere wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 ulikuwa umefikia asilimia 95.8. Vile vile, kufikia mwezi Machi 2024, mtambo mmoja kati ya mitambo tisa ulianza kufanyiwa majaribio ya kuzalisha umeme ambapo megawati 235 zinazozalishwa zimeanza kuingizwa katika Gridi ya Taifa. Katika kipindi hicho, umeme uliotumika kwa matumizi ya nyumbani (D1 na T1) ulikuwa saa za kilowati 3,668,634,262.40, viwandani saa za kilowati 3,669,847,892 na Zanzibar saa za kilowati 588, 096,751.

341. Mwaka 2023, umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali ulikuwa saa za gigawati 10,379.56 ikilinganishwa na saa za gigawati 9,064.9 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.5. Kati ya umeme uliozalishwa, saa za gigawati 10,110.61 zilizalishwa katika Gridi ya Taifa, saa za gigawati 71.59 zilizalishwa katika vituo nje ya Gridi ya Taifa na saa za gigawati 197.36 zilinunuliwa kutoka nchi jirani. Umeme uliozalishwa katika Gridi ya Taifa ulitokana na vyanzo vifuatavyo: mitambo ya nguvu za maji saa za gigawati 2,699.10; gesi saa za gigawati 7,369.91; mafuta mazito na dizeli saa za gigawati 31.20; na tungamotaka saa za gigawati 10.40. Aidha, umeme uliozalishwa na mitambo inayomilikiwa na TANESCO ulikuwa saa za gigawati 8,651.32 mwaka 2023 ikilinganishwa na saa za gigawati 7,320.1 uliozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 18.2. Vile vile, umeme uliozalishwa na kampuni binafsi ulipungua kwa asilimia 3.5 na kufikia saa za gigawati 1,530.88 mwaka 2023 ikilinganishwa na saa za gigawati 1,585.9 mwaka 2022.

342. Mwaka 2023, umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali ulikuwa saa za gigawati 8,232 ikilinganishwa na saa za gigawati 7,729.6 zilizouzwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Katika kipindi hicho, umeme uliopotea ulikuwa asilimia 14.63 ya umeme uliozalishwa ikilinganishwa na upotevu wa asilimia 14.53 mwaka 2022. Upotevu huo ulitokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme, urefu wa miundombinu ya kusambaza umeme na kuzidiwa kwa mashineumba. Hadi Desemba 2023, Serikali kupitia Mradi wa Usambazaji wa Nishati Vijijini iliunganisha umeme katika vijiji 11,720 kati ya vijiji 12,318 vya Tanzania Bara, sawa na asilimia 95.2 ya vijiji vyote.

343. Mwaka 2023, miundombinu ya kusafirisha umeme nchini ilifikia urefu wa kilometa 7,745.38 kutoka kilometa 6,267 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 23.6. Aidha, miundombinu ya kusambaza umeme ilifikia kilometa 176,750.88 mwaka 2023 kutoka kilometa 173,425 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 1.9. Vile vile, wateja waliounganishwa na umeme nchini walifikia 4,714,129 mwaka 2023 kutoka wateja 4,247,806 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.0. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuendelea kutumika kwa mfumo mpya wa maombi ya umeme wa Nikonekt, utekelezaji wa miradi ya Wakala wa Nishati Vijijini, hususan miradi ya ujazilizi (densification) na miji ya pembezoni mwa miji (peri- urban).

**Kielelezo Na. 14.1: Uzalishaji Umeme katika Vyanzo Mbalimbali Mwaka 2023**




## Gesi Asilia

344. Mwaka 2023, gesi asilia iliyozalishwa ilikuwa futi za ujazo milioni 85,173.2 ikilinganishwa na futi za ujazo milioni 79,059.9 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.7. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na mauzo ya gesi asilia katika vitalu vya Songosongo na Mnazi Bay yalikuwa dola za Marekani milioni 124.53 ikilinganishwa na mapato ya dola za Marekani milioni 71.3 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 75.0. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya gesi, hususan katika uzalishaji wa nishati ya umeme, matumizi majumbani, hotelini, viwandani na kwenye magari.

345. Mwaka 2023, mtandao wa usambazaji wa gesi asilia ulifikia kilometa 170.72 kutoka kilometa 143.38 mwaka 2022. Hadi Desemba 2023, nyumba 1,511, viwanda 56, taasisi 13 na vituo vitano (5) vya kujaza gesi asilia kwenye magari viliunganishwa kwenye miundombinu ya gesi asilia. Aidha, takriban magari 4,500 yaliunganishwa na mfumo wa gesi asilia mwaka 2023 ikilinganishwa na magari 2,000 mwaka 2022.

**Jedwali Na. 14.1: Uzalishaji wa Gesi Asilia (Futi za Ujazo Milioni) Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Songosongo | Mnazi Bay | Jumla | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| 2019 | 37,619.76 | 26,201.52 | 63,821.28 | 8.3 |
| 2020 | 33,149.94 | 23,934.21 | 57,084.15 | -10.6 |
| 2021 | 35,095.18 | 29,828.96 | 64,924.14 | 13.7 |
| 2022 | 46,116.99 | 32,942.96 | 79,059.95 | 21.8 |
| 2023 | 45,976.38 | 39,196.81 | 85,173.19 | 7.7 |

**Chanzo:** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

**Jedwali Na. 14.2: Mapato ya Mauzo ya Gesi Asilia (Dola za Marekani) Mwaka 2019 - 2023**

| Mwaka | Songosongo | Mnazi Bay | Jumla | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| 2019 | 28,097,086 | 35,952,953 | 64,050,039 | 1.5 |
| 2020 | 20,995,963 | 34,122,450 | 55,118,413 | -13.9 |
| 2021 | 16,018,066 | 42,886,054 | 58,904,120 | 6.9 |
| 2022 | 26,933,872 | 44,355,811 | 71,269,683 | 21.0 |
| 2023 | 45,264,440 | 79,265,141 | 124,529,581 | 75.0 |

**Chanzo:** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

### Uagizaji Mafuta

346. Mwaka 2023, mafuta yaliyoingizwa nchini yalikuwa lita za ujazo milioni 4,010.3 ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 4,174.7 zilizoingizwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 3.9. Hii ilitokana na jitihada za Serikali kuendelea kuhimiza matumizi ya nishati mbadala zinazopatikana nchini hususani gesi asilia ili kupunguza gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje. Kati ya kiasi kilichoigizwa, mafuta ya dizeli yalikuwa lita za ujazo milioni 2,216.8, petroli lita za ujazo milioni 1,557.5, mafuta ya taa lita za ujazo milioni 4.3, mafuta ya ndege lita za ujazo milioni 213.8 na mafuta mazito lita za ujazo milioni 18.0. Katika kipindi hicho, akiba ya mafuta nchini iliendelea kuwa juu ya wastani wa siku 15 kulingana na matakwa ya leseni ya biashara ya mafuta. Aidha, akiba ya mafuta ya petroli ilikuwa siku 14, dizeli siku 17, mafuta ya ndege siku 32 na mafuta ya taa siku 45.

347. Mwaka 2023, mafuta ya ndege yaliyoingizwa nchini yaliongezeka kwa asilimia 13.6 kutokana na kuongezeka kwa safari za ndege. Aidha, mafuta ya petroli yaliyoingizwa nchini yaliongezeka kwa asilimia 4.6 kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi. Kwa upande mwingine, mafuta ya dizeli yaliyoingizwa nchini yalipungua kwa asilimia 10.0 na mafuta mazito kwa asilimia 31.3. Kushuka kwa uagizaji wa mafuta mazito kulitokana na kupungua kwa matumizi ya nishati hiyo katika uzalishaji wa umeme. Vile vile, mafuta ya taa yaliyoingizwa nchini yalipungua kwa asilimia 43.2 kutokana na Serikali kuendelea kudhibiti uchakachuaji wa petroli na dizeli pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya nishati mbadala maeneo ya vijijini, ikiwemo umeme wa jua.

**Jedwali na. 14.3: Mafuta Yaliyoingizwa Nchini kwa Matumizi ya Ndani Mwaka 2023 (Lita za Ujazo)**

| Mwezi | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Taa | Mafuta ya Ndege | Mafuta Mazito | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 125,179,002 | 92,599,784 | - | 21,414,352 | - | 239,193,138 |
| Februari | 199,051,846 | 82,358,367 | 656,793 | 19,696,669 | 4,195,487 | 305,959,162 |
| Machi | 143,488,531 | 155,503,018 | 382,093 | 18,665,745 | 3,142,485 | 321,181,872 |
| Aprili | 158,016,459 | 85,859,875 | 379,044 | 16,534,497 | - | 260,789,875 |
| Mei | 136,612,008 | 105,741,020 | - | 22,622,565 | - | 264,975,593 |
| Juni | 114,441,315 | 115,921,775 | - | - | - | 230,363,090 |
| Julai | 116,560,262 | 100,710,704 | 266,016 | 14,404,980 | - | 231,941,962 |
| August | 275,632,425 | 157,958,761 | 253,570 | 35,765,159 | 4,126,957 | 473,736,872 |
| Septemba | 181,118,532 | 136,479,933 | - | 19,120,084 | - | 336,718,549 |
| Octoba | 215,993,307 | 149,368,483 | 894,002 | 24,147,819 | - | 390,403,612 |
| Novemba | 255,720,595 | 149,133,554 | - | - | 4,183,379 | 409,037,527 |
| Desemba | 139,493,887 | 121,560,151 | 268,072 | 21,112,117 | - | 282,434,226 |
| Jumlisha Mafuta ya nje yaliyouzwa ndani ya nchi (Localized Transit) | 155,472,012 | 104,350,176 | 1,160,762 | 282,756 | 2,325,551 | 263,591,256 |
| **Jumla Kuu 2023** | **2,216,780,181** | **1,557,545,600** | **4,260,353** | **213,766,743** | **17,973,859** | **4,010,326,735** |
| Mwaka 2022 | 2,463,360,290 | 1,489,481,164 | 7,494,822 | 188,175,209 | 26,169,652 | 4,174,681,137 |
| **Badiliko (Asilimia)** | **-10** | **4.6** | **-43.2** | **13.6** | **-31.3** | **-3.9** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani**

348. Mwaka 2023, lita za ujazo milioni 4,721.6 za mafuta ziliingia nchini kwenda nchi jirani ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 4,014.6 zilizoingizwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 17.6. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika nchi jirani. Kati ya kiasi kilichoagizwa, mafuta ya dizeli yalikuwa lita za ujazo milioni 3,241.4, petroli lita za ujazo milioni 1,256.4, mafuta ya ndege lita za ujazo milioni 219.7, na mafuta ya taa lita za ujazo milioni 3.9.

**Jedwali Na. 14.4: Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani Mwaka 2023 (Lita za Ujazo)**

| Mwezi | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Taa | Mafuta ya Ndege | Jumla |
|---|---:|---:|---:|---:|---:|
| Januari | 239,841,584 | 94,100,123 | 2,080,506 | 16,779,092 | 352,801,305 |
| Februari | 346,623,282 | 94,407,124 | 786,345 | 24,649,833 | 466,466,584 |
| Machi | 293,121,782 | 117,371,727 | 789,557 | 16,798,395 | 428,081,461 |
| Aprili | 204,141,441 | 72,448,197 | - | 21,112,106 | 297,701,744 |
| Mei | 314,700,436 | 139,493,087 | - | 30,706,260 | 484,899,783 |
| Juni | 160,511,097 | 118,976,178 | - | - | 279,487,275 |
| Julai | 221,302,081 | 146,335,734 | 801,204 | 15,121,857 | 383,560,876 |
| August | 292,871,734 | 89,383,403 | - | 30,366,144 | 412,621,282 |
| Septemba | 253,962,640 | 119,685,431 | - | 23,307,769 | 396,955,840 |
| Octoba | 416,577,521 | 144,862,704 | - | 23,765,023 | 585,205,248 |
| Novemba | 369,810,349 | 86,737,960 | - | - | 456,548,309 |
| Desemba | 283,445,178 | 136,987,456 | 670,179 | 17,403,723 | 438,506,537 |
| Kutoa Mafuta ya nje yaliyouzwa ndani ya nchi (Localized Transit) | 155,472,012 | 104,350,176 | 1,160,762 | 282,756 | 261,265,706 |
| **Jumla Kuu 2023** | **3,241,437,112** | **1,256,438,949** | **3,967,029** | **219,727,447** | **4,721,570,538** |
| Mwaka 2022 | 2,458,487,206 | 1,335,819,566 | 24,888,781 | 185,878,850 | 4,014,613,196* |
| **Badiliko (Asilimia)** | **31.8** | **-5.9** | **-84.1** | **18.2** | **17.6** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati
*Inajumuisha mafuta mazito Lita za Ujazo 9,538,794

**Mwenendo wa Bei za Mafuta**

349. Mwaka 2023, wastani wa bei ya mafuta katika soko la dunia kwa tani ulikuwa dola za Marekani 777 kwa petroli, dola za Marekani 770 kwa dizeli na dola za Marekani 805 kwa mafuta ya taa ikilinganishwa na dola za Marekani 912, dola za Marekani 972 na dola za Marekani 962 mtawalia mwaka 2022. Bei hizo zilipungua kwa asilimia 14.8 kwa mafuta ya petroli, asilimia 20.8 mafuta ya dizeli na asilimia 16.3 mafuta ya taa kutokana na ongezeko la uzalishaji wa mafuta kutoka katika nchi ambazo si wanachama wa Jumuiya ya Nchi Zinazozalisha Mafuta - OPEC pamoja na kushuka kwa mahitaji ya mafuta kwenye soko la dunia.

350. Mwaka 2023, wastani wa bei za ukomo za mafuta kwa lita katika soko la ndani uliongezeka hadi shilingi 2,999 kwa mafuta ya petroli, shilingi 3,058 kwa mafuta ya dizeli na shilingi 3,015 kwa mafuta ya taa ikilinganishwa na shilingi 2,894 mafuta ya petroli, shilingi 2,927 mafuta ya dizeli na shilingi 3,009 kwa mafuta ya taa mwaka 2022. Ongezeko hilo ni sawa na wastani wa asilimia 3.6 kwa mafuta ya petroli, asilimia 4.5 kwa mafuta ya dizeli na asilimia 0.2 kwa mafuta ya taa. Licha ya kupungua kwa bei ya mafuta katika soko

la dunia, wastani wa bei ya mafuta katika soko la ndani uliongezeka kutokana na gharama kubwa za kuagiza mafuta kutokana na uhaba wa fedha za kigeni (hususan dola za Marekani) pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi ikilinganishwa na mwaka 2022.

**Jedwali Na. 14.5: Wastani wa Bei za Mafuta Katika Soko la Dunia Mwaka 2019 - 2023 (Dola za Marekani kwa Tani)**

| Aina ya Mafuta | Petroli | | | | Dizeli | | | | Mafuta ya Taa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwezi/ Mwaka** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
| Januari | 592 | 496 | 808 | 787 | 552 | 443 | 738 | 836 | 574 | 448 | 743 | 880 |
| Februari | 580 | 562 | 912 | 787 | 571 | 504 | 826 | 781 | 585 | 504 | 826 | 820 |
| Machi | 578 | 617 | 1,069 | 776 | 551 | 513 | 1,040 | 739 | 572 | 513 | 1,038 | 754 |
| Aprili | 529 | 618 | 1,030 | 797 | 475 | 506 | 1,094 | 710 | 484 | 512 | 1,044 | 739 |
| Mei | 397 | 644 | 1,168 | 703 | 402 | 548 | 1,117 | 635 | 291 | 555 | 1,098 | 675 |
| Juni | 214 | 680 | 1,168 | 723 | 249 | 586 | 1,117 | 662 | 291 | 589 | 1,098 | 692 |
| Julai | 261 | 720 | 949 | 775 | 300 | 595 | 1,054 | 740 | 291 | 600 | 1,035 | 766 |
| Agosti | 389 | 697 | 879 | 847 | 367 | 564 | 1,013 | 870 | 291 | 570 | 1,015 | 903 |
| Septemba | 389 | 732 | 761 | 866 | 369 | 614 | 936 | 916 | 333 | 617 | 929 | 952 |
| Oktoba | 405 | 793 | 749 | 773 | 359 | 710 | 1,004 | 856 | 333 | 721 | 956 | 876 |
| Novemba | 394 | 775 | 764 | 767 | 320 | 679 | 924 | 778 | 333 | 690 | 931 | 825 |
| Desemba | 386 | 718 | 686 | 720 | 321 | 634 | 802 | 722 | 301 | 644 | 830 | 781 |
| **Wastani wa Bei** | **426** | **671** | **912** | **777** | **403** | **575** | **972** | **770** | **390** | **580** | **962** | **805** |
| **Badiliko (Asilimia)** | **-28.2** | **57.5** | **35.9** | **-14.8** | **-29** | **42.6** | **69.2** | **-20.7** | **-33.8** | **48.8** | **65.8** | **-16.3** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Jedwali Na. 14.6: Wastani wa Bei za Mafuta Katika Soko la Ndani Mwaka 2023 (Shilingi/Lita)**

| Mwezi | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| Januari | 2,819 | 3,295 | 3,203 |
| Februari | 2,819 | 3,105 | 3,061 |
| Machi | 2,968 | 3,130 | 3,098 |
| Aprili | 2,781 | 2,847 | 2,929 |
| Mei | 2,871 | 2,871 | 2,830 |
| Juni | 2,873 | 2,662 | 2,829 |
| Julai | 2,736 | 2,544 | 2,829 |
| Agosti | 3,199 | 2,935 | 2,668 |
| Septemba | 3,213 | 3,259 | 2,943 |
| Oktoba | 3,281 | 3,448 | 2,943 |
| Novemba | 3,274 | 3,374 | 3,423 |
| Desemba | 3,158 | 3,226 | 3,423 |
| **Wastani Mwaka 2023** | **2,999** | **3,058** | **3,015** |
| Wastani Mwaka 2022 | 2,894 | 2,927 | 3,009 |
| **Badiliko (Asilimia)** | **3.6** | **4.5** | **0.2** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Nishati Jadidifu**

**Nishati mbadala ya Gesi inayotokana na Petroli**

351. Mwaka 2023, gesi inayotokana na petroli (Liquefied Petroleum Gas - LPG) iliyoagizwa kutoka nje kwa matumizi mbalimbali ilikuwa tani za ujazo 364,982 ikilinganishwa na tani za ujazo 250,200 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 45.9. Ongezeko hilo lilichangiwa na juhudi za Serikali na sekta binafsi kuhamasisha matumizi ya gesi inayotokana na petroli ambayo ni moja ya nishati safi za kupikia na rafiki kwa mazingira.

**Jedwali Na. 62: UWEZO WA MITAMBO YA KUFUA UMEME NCHINI NA UPATIKANAJI WA UMEME MWAKA 2023**

| Jina la Kituo | Uwezo (MW) | Umeme Uliozalishwa (GWh) |
|---|---|---|
| **Umeme kutokana na Maji** | | |
| Kidatu | 204 | 1,157.04 |
| Kihansi | 180 | 703.08 |
| Mtera | 80 | 463.9 |
| Hale | 21 | 31.86 |
| Nyumba ya Mungu | 8 | 27.08 |
| New Pangani Falls | 68 | 236.53 |
| Uwemba | 0.84 | 2.55 |
| Mwenga | 4 | 17.23 |
| Yovi | 0.95 | 5.23 |
| Tulila | 5 | 30.78 |
| Andoya | 1 | 0.67 |
| Darakuta | 0.32 | 1.41 |
| Matembwe (Ikondo) | 0.59 | 0.15 |
| Luponde | 0.9 | 5.17 |
| Rusumo | 27 | 16.42 |
| **Jumla Ndogo - Maji** | **601.6** | **2,699.10** |
| **Umeme kutokana na Gesi Asilia** | | |
| Ubungo Gas PP- I | 102 | 413.6 |
| Tegeta Gas PP | 45 | 273.74 |
| Ubungo Gas PP - II | 129 | 954.06 |
| Kinyerezi I | 150 | 785.4 |
| Kinyerezi II | 248.22 | 1,798.21 |
| Songas | 189 | 1,459.68 |
| Somanga | 7.5 | 9.87 |
| Mtwara | 30.6 | 121.76 |
| Ubungo Gas PP - III | 112.5 | 734.57 |
| Kinyerezi I Ext | 135 | 819.02 |
| **Jumla Ndogo -Gesi** | **1,148.80** | **7,369.90** |
| **Umeme kutokana na Mafuta** | | |
| Zuzu | 7.4 | 2.87 |
| Biharamulo | 4.14 | - |
| Ngara | 2.5 | - |
| Nyakato | 63 | 28.33 |
| Ludewa | 1.27 | - |
| Songea | 5.77 | - |
| Mbinga | 2 | - |
| Liwale | 0.85 | - |
| Madaba | 0.48 | - |
| Namtumbo | 0.34 | - |
| **Jumla Ndogo - Mafuta** | **87.75** | **31.2** |
| **Umeme kutokana na Tungamotaka (Biomass)** | | |
| TPC | 9 | 10.05 |
| TANWAT | 1.5 | 0.35 |
| **Jumla Ndogo - Tungamotaka** | **10.5** | **10.4** |
| **Jumla - Gridi ya Taifa** | **1,848.70** | **10,110.60** |
| **Umeme nje ya Mfumo wa Gridi ya Taifa (Off-Grid)** | | |
| Bukoba | 2.56 | 0.65 |
| Inyonga | 0.82 | 1.86 |
| Kasulu | 3.75 | 4.5 |
| Kibondo | 2.5 | 7.66 |
| Kigoma | 8.75 | 28.08 |
| Loliondo | 2.25 | 6.89 |
| Mafia | 3.2 | 12.84 |
| Mpanda | 5 | 8.87 |
| Sumbawanga | 5 | 0.08 |
| Solowazi - Kigoma | 5 | 0.16 |
| **Jumla - Nje ya Gridi ya Taifa** | **38.8** | **71.6** |
| **Umeme kutoka Nchi Jirani** | | |
| Uganda | - | 141.71 |
| Zambia | - | 55.65 |
| **Jumla - Umeme kutoka Nje** | **-** | **197.36** |
| **Jumla Kuu** | **1,887.5** | **10,379.56** |

**Chanzo:** Shirika la Ugamvi wa Umeme Tanzania

**Jedwali Na. 63: MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI MWAKA 2023 (Saa za Gigawati)**

| Mwaka | Tanzania Bara | | | Zanzibar | Jumla | Umeme Uliozalishwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wateja wadogo (D1) | Wateja wa Kati (T1) | Wateja Wakubwa (T2,T3 & T8) | T5+T7 | | |
| 2013 | 280.6 | 1,747.0 | 2560.4 | 218.7 | 4,806.7 | 5,946.2 |
| 2014 | 217.0 | 1,891.0 | 2595.0 | 348.5 | 5,051.5 | 6,186.8 |
| 2015 | 148.8 | 2,082.7 | 2721.1 | 344.6 | 5,297.1 | 6,416.9 |
| 2016 | 345.3 | 2,263.4 | 2887.2 | 375.6 | 5,871.5 | 7,092.2 |
| 2017 | 301.5 | 2,371.0 | 2893.3 | 390.4 | 5,956.2 | 7,115.3 |
| 2018 | 319.8 | 2,481.9 | 3075.0 | 414.0 | 6,290.7 | 7,354.8 |
| 2019 | 307.2 | 2,655.9 | 3198.1 | 481.5 | 6,642.8 | 7,804.9 |
| 2020 | 325.8 | 2,668.6 | 3205.1 | 474.9 | 6,674.3 | 7,862.9 |
| 2021 | 339.9 | 2,900.0 | 3527.0 | 546.3 | 7,313.2 | 8,580.8 |
| 2022 | 351.0 | 3,063.1 | 3730.6 | 584.9 | 7,729.6 | 9,064.9 |
| 2023 | 393.6 | 3,313.2 | 3864.2 | 661.0 | 8,232.0 | 10,379.6 |

**Chanzo:** Shirika la Ugamvi wa Umeme Tanzania

**Jedwali Na. 64: MAUZO YA UMEME KWA MIKOA MWAKA 2023 (GWh)**

| Mkoa | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 150.4 | 161 | 179.7 | 177.7 | 228.7 | 249.3 | 297.2 |
| Arusha | 365.9 | 383.3 | 406.3 | 385.6 | 395.6 | 413.9 | 452.1 |
| Manyara | 31.9 | 32.4 | 34.8 | 35.2 | 53.5 | 59 | 67.3 |
| Kilimanjaro | 179.4 | 181.7 | 185.2 | 183.9 | 195.2 | 206.3 | 218.7 |
| Tanga | 330.4 | 353.9 | 351.3 | 342.2 | 375.5 | 408.7 | 391.5 |
| Morogoro | 242.8 | 274.9 | 268 | 266.8 | 298.5 | 307.5 | 329.7 |
| Pwani | 302.1 | 393.1 | 450.7 | 517.9 | 597.9 | 635.7 | 714.8 |
| Dar-es-Salaam | 2,412.5 | 2,481.6 | 2,596.5 | 2,534.0 | 2,652.0 | 2,805.9 | 2,932.0 |
| Lindi | 22.9 | 25.8 | 29.7 | 30.5 | 33.8 | 36.2 | 41.5 |
| Mtwara | 48.3 | 52.8 | 55.9 | 55.9 | 58.6 | 60.9 | 66.5 |
| Ruvuma | 35.4 | 41.9 | 50.3 | 53.7 | 56.9 | 59.4 | 66.5 |
| Iringa | 98.4 | 103.7 | 108.9 | 109.1 | 117.3 | 123.8 | 133.6 |
| Mbeya | 177.6 | 186.9 | 201.6 | 209.9 | 226.9 | 231.5 | 231.8 |
| Singida | 43.8 | 45.7 | 49.5 | 53.1 | 58.1 | 65.1 | 69.5 |
| Tabora | 55.9 | 60.7 | 68.4 | 69.7 | 76.4 | 77.9 | 80.9 |
| Rukwa | 27 | 25.9 | 27.3 | 28.6 | 31.1 | 32.5 | 39 |
| Kigoma | 34.8 | 40.2 | 40.3 | 41 | 47.5 | 52.3 | 59.6 |
| Shinyanga | 371.9 | 339.5 | 354.1 | 352.2 | 421.7 | 411.2 | 395.3 |
| Kagera | 76.9 | 90.6 | 80.3 | 79.2 | 96.8 | 108.1 | 119.2 |
| Mwanza | 283.2 | 287.7 | 295.2 | 300.9 | 325.6 | 344.5 | 348.4 |
| Mara | 156.9 | 165.8 | 163.9 | 188.1 | 195.5 | 215.1 | 241.2 |
| Njombe | 35.6 | 35.4 | 39.1 | 42 | 45.7 | 47.8 | 53 |
| Katavi | 10.8 | 11.2 | 13.6 | 16.3 | 21.8 | 24 | 27.8 |
| Geita | 42.7 | 49.2 | 53 | 60.8 | 77.7 | 83 | 96.9 |
| Simiyu | 18.2 | 22.4 | 24.2 | 24.8 | 28.6 | 31 | 34.3 |
| Songwe | 10.1 | 29.3 | 33.2 | 40.4 | 50.2 | 54.4 | 62.8 |
| **Jumla Tanzania Bara** | **5,565.8** | **5,876.7** | **6,161.1** | **6,199.4** | **6,766.9** | **7,144.8** | **7,571.0** |
| Zanzibar | 390.4 | 414.0 | 481.5 | 474.9 | 546.3 | 584.9 | 661.0 |
| **Jumla** | **5,956.2** | **6,290.7** | **6,642.6** | **6,674.3** | **7,313.2** | **7,729.7** | **8,232.0** |

**Chanzo:** Shirika la Umeme Tanzania
GWh Giga Watt-Hour (Saa za GigaWati) = Million KWh

## SURA YA 15

## MAJI

### Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

352. Mwaka 2023, kiwango cha rasilimali za maji kinachofaa kwa matumizi kiliendelea kuwa wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka kama kilivyokuwa mwaka 2022. Kati ya kiwango hicho, mita za ujazo bilioni 105 zilikuwa juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 zilikuwa chini ya ardhi. Aidha, kiwango cha upatikanaji wa maji safi na salama kiliendelea kuwa mita za ujazo 2,105 kwa mtu kwa mwaka kama ilivyokuwa mwaka 2022. Kiwango hicho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa.

353. Mwaka 2023, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini yalikadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 66 kwa mwaka ikilinganishwa na mita za ujazo bilioni 64 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii zikichagizwa zaidi na ongezeko la idadi ya watu.

354. Mwaka 2023, vyanzo 908 vya maji vilitambuliwa na kufikia vyanzo 3,265 kutoka vyanzo 2,357 mwaka 2022. Kati ya hivyo, vyanzo 316 viliwekewa mipaka ili visiharibiwe na shughuli za kibinadamu ikilinganishwa na vyanzo 213 vilivyowekewa mipaka mwaka 2022.

355. Mwaka 2023, vituo vipya sita (6) vya kufuatilia mwenendo wa maji juu na chini ya ardhi vilijengwa na kufikia vituo 1,205 vinavyofanya kazi kutoka vituo 1,199 mwaka 2022. Vituo hivyo vinajumuisha: vituo 342 vya hali ya hewa; vituo 380 vya kufuatilia maji katika mito, maziwa na mabwawa; vituo 95 vya maji chini ya ardhi; vituo 33 vya kufuatilia mchanga kwenye mito; na vituo 355 vya ubora wa maji. Aidha, vituo 86 vilikarabatiwa mwaka 2023 ili kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa mwenendo wa maji.

### Ubora wa Maji

356. Mwaka 2023, sampuli 6,490 za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ubora ikilinganishwa na sampuli 6,344 zilizohakikiwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 2.3. Ongezeko hilo lilitokana na ununuzi wa vifaa vya uchunguzi wa ubora wa maji katika maabara za Mtwara, Singida, Morogoro na Tanga, pamoja na matengenezo yaliyofanyika kwenye vifaa vya uchunguzi wa ubora wa maji katika maabara ya Dar es Salaam. Kati ya sampuli zilizokusanywa, sampuli 5,764 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya majumbani; sampuli 233 ufuatiliaji wa mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji; sampuli 71 utafiti; sampuli 242 matumizi ya viwandani; sampuli 24 umwagiliaji; sampuli 49 ujenzi; na sampuli 107 kupima uwezo wa utendaji kazi wa maabara.

357. Mwaka 2023, matokeo ya uhakiki wa ubora wa maji katika sampuli 5,764 za matumizi ya majumbani yalionesha kuwa sampuli za maji 3,365 (asilimia 58.4) zilikidhi viwango vya ubora na usalama wa maji vinavyokubalika kimataifa na sampuli 2,399 hazikukidhi viwango. Kutokidhi viwango kwa sampuli kulitokana na uwepo wa kiasi kikubwa cha rangi, tope, ugumu wa maji, madini ya chumvi, nitrate, fluoride, manganese na chuma katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, uwepo kwa vimelea vya vijidudu katika skimu za usambazaji maji zisizokuwa na miundombinu ya kutibu maji pamoja na uwepo wa kiasi kidogo cha dawa ya chlorine baki katika skimu za usambazaji maji zenye miundombinu ya kutibu maji kulichangia kutofikiwa kwa viwango vya ubora na usalama wa maji unaotakiwa.


358. Mwaka 2023, sampuli zote 315 za maji kwa ajili ya shughuli za viwandani, umwagiliaji, ujenzi, utafiti na upimaji wa uwezo wa utendaji kazi wa maabara zilifanyiwa uhakiki na kukidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kwa matumizi husika. Aidha, matokeo ya uhakiki wa sampuli 233 kutoka katika vyanzo vya maji yalionesha kuwa havikuathiriwa na hali ya miamba ya asili, shughuli za kibinadamu, jiografia ya eneo na mabadiliko ya tabianchi na hivyo, kuwa rafiki kwa mazingira na viumbe hai vilivyomo.

359. Mwaka 2023, sampuli 377 za majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira zilikusanywa na kuhakikiwa ubora ikilinganishwa na sampuli 446 zilizohakikiwa ubora mwaka 2022. Matokeo ya uhakiki yalionesha kuwa sampuli 122, sawa na asilimia 32.4 hazikukidhi viwango vya ubora kutokana na kuwepo kwa *Chemical Oxygen Demand* (COD), *Biological Oxygen Demand* (BOD), *Nitrate* na *Phosphate* kuliko kiwango kinachohitajika kwa ajili ya maji hayo kurudishwa kwenye mazingira.

**Huduma ya Maji Vijijini**

360. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kuboresha miundombinu ya maji safi vijijini kwa kukamilisha miradi 711 yenye vituo vya kuchotea maji 8,751 vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 4,178,368 ikilinganishwa na miradi 689 yenye vituo vya kuchotea maji 8,667 na uwezo wa kuhudumia wananchi 1,585,336 mwaka 2022. Hadi Desemba 2023, idadi ya vituo vinavyofanya kazi na kutoa huduma ilifikia 151,643 ikilinganishwa na vituo 142,892 katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali kuendelea kusogeza huduma ya maji karibu na wananchi katika maeneo ya vijijini. Aidha, kaya zilizounganishwa na huduma ya maji zilikuwa 207,498 ikilinganishwa na kaya 180,341 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 15.1. Kwa ujumla, wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ulikuwa asilimia 79.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 77.0 mwaka 2022.

**Kielelezo Na. 15.1: Mwenendo wa Wastani wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini waka 2019 - 2023**





**Huduma ya Maji Mijini**


361. Mwaka 2023, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini ilifikia wastani wa asilimia 90 ikilinganishwa na asilimia 88.0 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kukamilika kwa miradi ya maji inayohudumia wakazi wa maeneo ya mijini. Katika kipindi hicho, jumla ya miradi ya maji mijini iliyokamilika ilikuwa 70 ikilinganishwa na miradi 105 mwaka 2022.

362. Mwaka 2023, wateja 1,990,206 waliunganishwa na huduma ya majisafi ikilinganishwa na wateja 1,843,329 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa ukarabati wa miundombinu ya maji, kuunganisha wateja kwenye miradi iliyokamilika katika miji mikuu ya mikoa na wilaya pamoja na utekelezaji wa miradi ya kitaifa.

**Kielelezo Na. 15.2: Mwenendo wa Wastani wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji Mijini Mwaka 2019 - 2023**




**Kielelezo Na. 15.3: Mwenendo wa Wastani wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji Mijini na Vijijini Mwaka 2019 - 2023**




363. Mwaka 2023, uzalishaji wa maji (unaojumuisha miji mikuu ya mikoa, mamlaka za maji za miradi ya kitaifa na miji mikuu na midogo ya wilaya) ulikuwa mita za ujazo milioni 395.9 ikilinganishwa na mita za ujazo milioni 383.6 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.2. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na mauzo ya majisafi na salama

yalifikia shilingi bilioni 383.9 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 383.5 mwaka 2022.

**Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa**

364. Mwaka 2023, visima 1,188 vilichimbwa katika maeneo mbalimbali ikilinganishwa na visima 1,092 mwaka 2022. Kati ya hivyo, visima 513 vilichimbwa na Serikali na visima 675 vilichimbwa na sekta binafsi. Kuongezeka kwa idadi ya visima vilivyochimbwa kulitokana na juhudi za Serikali na uwekezaji wa sekta binafsi katika kuwapatia wananchi huduma ya majisafi na salama. Visima hivyo vilichimbwa katika mabonde yafuatayo: Bonde la Maji la Ziwa Tanganyika visima 14; Bonde la Maji la Ziwa Rukwa (263); Bonde la Maji la Ziwa Nyasa tisa (9); Bonde la Maji la Pangani (260); Bonde la Kati (165); Bonde la Maji la Rufiji (80); Bonde la Maji la Ruvuma na Pwani ya Kusini (61), Bonde la Maji la Wami/Ruvu (67); na Bonde la Maji la Ziwa Victoria (269).

365. Mwaka 2023, Serikali iliendelea na ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua ili kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya mabwawa tisa (9) yalijengwa katika maeneo yafuatayo: Engukument II (Wilaya ya Monduli); Uhelera na Bahimakuru (Bahi); Igumangobo na Ilambambasa (Maswa); Ng'walukwa (Shinyanga); Ngofila (Kishapu); Qang'dend (Karatu); na Horohoro (Mkinga).

**Uondoaji wa Majitaka**

366. Mwaka 2023, mtandao wa majitaka ulikuwa na urefu wa kilomita 1,503.4 ikilinganishwa na kilomita 1,411.42 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Katika kipindi hicho wateja waliounganishwa katika mtandao wa majitaka waliongezeka na kufikia 115,269 ikilinganishwa na wateja 114,366 mwaka 2022. Kwa upande mwingine, huduma ya usafi wa mazingira katika miji ambayo haina mtandao wa majitaka iliendelea kutolewa kupitia mfumo usiounganishwa na mtandao katika uondoshaji wa majitaka kwa kutumia magari maalumu ya kubeba majitaka. Hadi Desemba 2023, Mamlaka 12 za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Sumbawanga, Kahama, Bukoba, Musoma, Geita, Nansio, Sengerema, Kigoma, Magu, Misungwi, Lindi na Lamadi zilikuwa zinatumia mfumo huo. Aidha, huduma ya uondoshaji majitaka katika miji mingine iliendelea kutolewa na halmashauri kwa kushirikiana na wadau.

## Jedwali Na. 65: UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYONA MAJI MIJINI

**A. MAMLAKA ZA MAJI ZA MIJI MIKUU YA MIKOA (RWSSA)**

| Mamlaka ya Maji | 2022 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|
| | Uzalishaji (Mita za Ujazo) | Mapato (Shilingi) | Uzalishaji (Mita za Ujazo) | Mapato (Shilingi) |
| Arusha | 20,017,280 | 21,390,953,209 | 29,033,530 | 22,414,906,277 |
| Babati | 3,565,668 | 3,912,484,932 | 4,111,770 | 4,299,991,437 |
| Bukoba | 2,529,815 | 2,945,302,438 | 2,876,972 | 3,126,973,721 |
| Dodoma | 21,265,094 | 25,264,352,439 | 21,998,770 | 21,013,601,786 |
| DAWASA | 146,048,955 | 141,740,399,828 | 141,097,720 | 142,034,738,371 |
| Geita | 1,690,698 | 1,917,029,001 | 1,900,004 | 1,873,449,388 |
| Iringa | 5,712,001 | 8,652,023,414 | 6,365,079 | 8,904,401,229 |
| Kigoma | 3,586,158 | 3,002,913,540 | 1,906,628 | 955,509,319 |
| Lindi | 878,539 | 1,063,216,234 | 3,586,158 | 2,779,730,026 |
| Mpanda | 1,169,650 | 869,585,385 | 894,474 | 1,028,659,374 |
| Mbeya | 13,494,530 | 14,955,836,127 | 14,037,363 | 14,465,894,142 |
| Morogoro | 11,930,636 | 13,572,675,386 | 11,081,500 | 13,052,443,221 |
| Moshi | 15,029,184 | 12,279,254,328 | 14,513,727 | 11,564,651,416 |
| Mtwara | 4,962,060 | 8,139,364,788 | 4,585,970 | 4,456,114,662 |
| Musoma | 5,740,568 | 4,519,829,547 | 6,588,171 | 4,694,349,536 |
| Mwanza | 29,339,889 | 28,199,968,444 | 30,808,692 | 31,296,954,665 |
| Njombe | 1,167,132 | 1,126,900,128 | 1,167,132 | 1,247,612,800 |
| Bariadi | 509,159 | 293,937,466 | 587,861 | 281,000,789 |
| Kahama | 4,792,959 | 8,619,593,156 | 5,489,976 | 8,163,134,057 |
| Singida | 3,419,772 | 4,266,723,312 | 5,171,242 | 8,993,680,073 |
| Songea | 3,061,519 | 3,426,864,913 | 3,572,570 | 3,714,319,686 |
| Sumbawanga | 2,142,137 | 1,946,293,862 | 3,168,035 | 3,625,873,850 |
| Tabora | 6,419,230 | 6,864,622,193 | 2,626,954 | 1,605,691,901 |
| Shinyanga | 4,962,060 | 8,139,364,788 | 6,043,371 | 7,731,582,765 |
| Tanga | 11,849,467 | 16,598,821,831 | 12,427,071 | 15,238,912,081 |
| Vwawa-Mlowo | 318,817 | 175,935,327 | 465,324 | 179,390,823 |
| **JUMLA - RWSSA** | **325,602,976** | **343,884,246,016** | **336,106,064** | **338,743,567,395** |

**B. MAMLAKA ZA MAJI ZA MIRADI YA KITAIFA (NWP)**

| Mamlaka ya Maji | 2022 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|
| | Uzalishaji (Mita za Ujazo) | Mapato (Shilingi) | Uzalishaji (Mita za Ujazo) | Mapato (Shilingi) |
| Wanging'ombe | 1,290,180 | 506,423,815 | 769,160 | 478,777,525 |
| Kahama Shinyanga | 20,421,916 | 11,874,703,921 | 21,320,537 | 15,907,526,430 |
| Mugango Kiabakari | 83,700 | 158,836,548 | 797,070.00 | 87,931,281.50 |
| Masasi Nachingwea | 304,971 | 501,528,108 | 304,971 | 3,066,700,000 |
| Makonde | 807,475 | 441,582,968 | 1,110,799 | 577,101,267 |
| Maswa | 1,667,474 | 584,453,331 | 1,674,963 | 720,559,301 |
| HTM | 1,708,333 | 1,077,810,939 | 1,301,273 | 774,307,500 |
| **JUMLA - NWP** | **26,284,049** | **15,145,339,630** | **27,278,773** | **21,612,903,304.50** |

**Jedwali Na. 65: Linaendelea**

| C. MAMLAKA ZA MAJI ZA MIJI MIKUU NA MIDOGO YA WILAYA (DTWSSA) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mamlaka ya Maji** | **2022** | | **2023** | |
| | **Uzalishaji (Mita za Ujazo)** | **Mapato (Shilingi)** | **Uzalishaji (Mita za Ujazo)** | **Mapato (Shilingi)** |
| Karatu | 399,336 | 434,436,314 | 1,542,730 | 1,033,678,521 |
| Kondoa | 1,105,200 | 798,458 | 1,026,791 | 438,234,820 |
| Mpwapwa | 722,047 | 381,085,701 | 781,334 | 376,061,939 |
| Ludewa | 306,499 | 26,459,980 | 399,330 | 56,283,412 |
| Makete | 327,840 | 137,255,466 | 327,840 | 155,575,654 |
| Mafinga | 995,973 | 509,329,446 | 992,558 | 494,079,542 |
| Makambako | 1,030,817 | 751,365,577 | 774,438 | 663,048,409 |
| Biharamulo | 388,118 | 417,216,769 | 380,372 | 332,382,119 |
| Ngara | 501,977 | 370,089,014 | 633,585 | 382,372,406 |
| Kasulu | 924,620 | 207,796,173 | 924,620 | 239,296,172 |
| Same-Mwanga | 835,149 | 566,159,784 | 835,149 | 453,965,789 |
| Kilwa Masoko | 451,494 | 315,010,876 | 537,592 | 330,774,544 |
| Loliondo | 147,201 | 225,214,356 | 142,816 | 193,029,014 |
| Kiteto Kibaya | 63,760 | 60,938,469 | 121,592 | 87,583,788 |
| Mbulu | 618,864 | 232,464,108 | 622,042 | 288,966,069 |
| Bunda | 1,068,510 | 941,382,540 | 1,068,510 | 1,124,825,262 |
| Orkesumet | 133,545 | 288,312,242 | 245,742 | 396,208,712 |
| Sengerema | 1,663,105 | 1,334,149,905 | 1,753,457 | 1,486,271,589 |
| Chunya | 150,535 | 140,456,330 | 105,711 | 93,317,128 |
| Itumba Isongele | 561,370 | 68,034,929 | 319,442 | 60,516,128 |
| Kyela-Kasumulu | 1,797,684 | 95,257,668 | 1,797,684 | 95,151,875 |
| Mbarali Rujewa | 722,880 | 147,242,713 | 722,880 | 124,993,361 |
| Rungwe Tukuyu | 2,147,888 | 283,724,401 | 2,183,067 | 285,691,030 |
| Ifakara | 181,181 | 85,070,617 | 234,002 | 101,438,817 |
| Kilosa | 519,697 | 272,963,850 | 498,482 | 312,097,280 |
| Mahenge | 126,768 | 145,128,781 | 13,133 | 121,621,229 |
| Morogoro Mikumi | 272,166 | 237,786,072 | 234,547 | 265,759,895 |
| Rufiji Utete | 163,689 | 102,492,516 | 179,552 | 148,630,131 |
| Namtumbo | 218,000 | 78,724,010 | 352,755 | 99,558,414 |
| Kahama | 4,792,959 | 8,619,593,156 | 5,171,242 | 8,993,680,073 |
| Kishapu | 138,211 | 251,572,943 | 160,435 | 251,289,017 |
| Maganzo | 89,701 | 158,173,273 | 230,265 | 130,447,372 |
| Mwanhuzi | 253,086 | 252,957,700 | 105,852 | 172,259,845 |
| Maswa | 1,667,474 | 584,453,331 | 252,115 | 225,647,984 |
| Manyoni | 480,205 | 518,290,173 | 480,205 | 601,229,730 |
| Korogwe | 701,707 | 526,283,225 | 480,205 | 433,949,873 |
| Lushoto | 677,595 | 142,922,137 | 691,876 | 253,726,203 |
| Korogwe Mombo | 226,920 | 66,519,061 | 579,254 | 148,250,389 |
| Songe | 32,365 | 76,883,168 | 258,420 | 47,095,986 |
| Igunga | 1,530,809 | 1,466,801,512 | 1,530,809 | 1,831,6 86,105 |
| Nzega | 1,142,502 | 1,679,815,542 | 1,598,960 | 1,705,317,300 |
| Turiani | 1,091,880 | 287,516,320 | 1,243,590 | 1,806,130,380 |
| **JUMLA - DTWSSA** | **31,371,327** | **23,488,128,606** | **32,534,981** | **23,524,165,612** |
| **JUMLA KUU (A+B+C)** | **383,258,352** | **382,517,714,252** | **395,919,818** | **383,880,636,311** |

**Chanzo:** Wizara ya Maji

**Jedwali Na. 66: MAHITAJI NA KIWANGO CHA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI MWAKA 2023**

| Mamlaka ya Maji | Mwaka 2023 | |
|---|---|---|
| | Mahitaji ya Maji (Mita za Ujazo) | Wastani wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji (Asilimia) |
| Arusha | 49,189,222.0 | 78.0 |
| Babati | 11,616,315.0 | 79.0 |
| Bukoba | 3,985,203.0 | 79.0 |
| Dodoma | 133,845.0 | 91.0 |
| DAWASA | 678,961.0 | 92.0 |
| Iringa | 7,835,090.0 | 90.0 |
| Mpanda | 4,081,584.0 | 76.0 |
| Kigoma | 690,000.0 | 81.0 |
| Lindi | 2,699,703.0 | 45.0 |
| Mbeya | 32,850,000.0 | 80.0 |
| Morogoro | 24,486,390.0 | 70.0 |
| Moshi | 26,058,080.0 | 89.0 |
| Mtwara | 8,184,000.0 | 61.0 |
| Musoma | 38,100,000.0 | 58.0 |
| Mwanza | 58,400,000.0 | 62.0 |
| Geita | 22,560.0 | 72.0 |
| Bariadi | 3,454,848.0 | 33.0 |
| Shinyanga | 583,500.0 | 82.0 |
| Kahama | 6,229,000.0 | 85.0 |
| Singida | 2,849,810.0 | 79.0 |
| Songea | 20,366.0 | 90.0 |
| Sumbawanga | 3,679,455.5 | 91.0 |
| Tabora | 10,864,447.0 | 82.0 |
| Tanga | 16,988,775.0 | 92.0 |
| Vwawa - Mlowo | 4,745,000.0 | 51.0 |
| **Jumla** | **818,790,139.5** | **75.5** |

**Chanzo:** Wizara ya Maji

# SURA YA 16

# ELIMU MAFUNZO YA UFUNDI NA TEKNOLOJIA

**Elimu ya Awali**

367. Mwaka 2023, idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika elimu ya awali walikuwa 1,679,542 ikilinganishwa na wanafunzi 1,543,843 walioandikishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Kati ya hao, wasichana walikuwa 825,535 na wavulana walikuwa 854,007. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuimarika kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo utekelezaji wa programu ya elimu bila ada pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu. Kati ya walioandikishwa mwaka 2023, wanafunzi 6,919 (wasichana 3,018 na wavulana 3,901) walikuwa na mahitaji maalum ikilinganishwa na wanafunzi 6,120 wenye mahitaji maalum mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 13.1. Aidha, wanafunzi walioandikishwa katika shule za Serikali walikuwa 1,562,286 mwaka 2023 sawa na asilimia 93.0 ya wanafunzi wote walioandikishwa ikilinganishwa na wanafunzi 1,435,735 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Kati ya hao, wasichana walikuwa 768,595 na wavulana 793,691. Vile vile, wanafunzi walioandikishwa katika shule zisizo za Serikali nao waliongezeka kwa asilimia 8.5 na kufikia 117,256 mwaka 2023 ikilinganishwa na wanafunzi 108,108 walioandikishwa mwaka 2022.

368. Mwaka 2023, idadi ya walimu katika shule za awali za Serikali ilipungua na kufikia 9,608 (wanawake 6,618 na wanaume 2,990) kutoka walimu 10,093 (wanawake 6,867 na wanaume 3,226) mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 4.8. Kati ya hao, walimu wenye sifa wanaofundisha elimu ya awali walikuwa 7,958 mwaka 2023 ikilinganishwa na walimu 8,600 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 7.5. Kupungua kwa walimu katika ngazi hii kulitokana na baadhi ya walimu kupanda daraja na kupangiwa majukumu ya kufundisha katika madarasa ya shule za msingi. Aidha, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi wa elimu ya awali ulifikia 1:163 mwaka 2023 ikilinganishwa na uwiano wa 1:167 mwaka 2022. Uwiano huo ulizidi kiwango cha uwiano wa 1:25 unaokubalika kitaifa.

**Elimu ya Msingi**

369. Mwaka 2023, idadi ya shule za msingi zilifikia 19,733 kutoka shule 19,261 mwaka 2022. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 17,463 ikilinganishwa na shule 17,405 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Serikali kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na shule ya msingi. Aidha, shule zisizo za Serikali zilifikia 2,270 mwaka 2023 kutoka shule 2,268 mwaka 2022.

370. Mwaka 2023, idadi ya wanafunzi katika shule za elimu ya msingi ilifikia 11,425,482 (wavulana 5,616,919 na wasichana 5,808,563) kutoka wanafunzi 11,420,973 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za elimu ya msingi walikuwa 74,295 (wasichana 32,075 na wavulana 42,220) ikilinganishwa na wanafunzi

66,372 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.9. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali ilikuwa 10,824,374 (wasichana 5,506,034 na wavulana 5,318,340) mwaka 2023 ikilinganishwa na wanafunzi 10,872,508 mwaka 2022. Vile vile, idadi ya wanafunzi katika shule zisizo za Serikali ilikuwa 601,108 (wasichana 302,529 na wavulana 298,579) mwaka 2023 ikilinganishwa na wanafunzi 548,465 mwaka 2022.

371. Mwaka 2023, idadi ya watahiniwa 1,356,392 (wasichana 726,078 na wavulana 630,314) walifanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba ikilinganishwa na watahiniwa 1,350,881 mwaka 2021. Kati ya hao, watahiniwa 1,092,960 (wasichana 585,040 na wavulana 507,920) walifaulu, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 80.6 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 79.5 mwaka 2022.

372. Mwaka 2023, idadi ya walimu katika shule za elimu ya msingi za Serikali ilifikia 176,540 (wanawake 87,173 na wanaume 89,367) kutoka walimu 173,276 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, idadi ya walimu katika shule za elimu ya msingi zisizo za Serikali ilifikia 30,783 mwaka 2023 (wanawake 12,741 na wanaume 18,042) kutoka walimu 28,396 mwaka 2022. Kwa upande mwingine, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi wa shule za elimu ya msingi za Serikali na zisizo za Serikali uliendelea kubaki katika uwiano wa 1:57 mwaka 2023 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Aidha, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika shule za Serikali ulikuwa 1:61 ikilinganishwa na uwiano wa 1:63 mwaka 2022. Uwiano huo ulizidi kiwango halisi cha uwiano wa 1:45 unaokubalika kitaifa.

**Elimu ya Sekondari**

373. Mwaka 2023, idadi ya shule za sekondari ilifikia 5,926 kutoka shule 5,540 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.0. Kati ya hizo, shule 4,578 zilikuwa za Serikali na shule 1,348 zilikuwa za sekta binafsi ikilinganishwa shule 4,211 za Serikali na shule 1,329 za sekta binafsi mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali za kuongeza idadi ya madarasa na shule mpya za sekondari ili kukabiliana na idadi kubwa ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza.

374. Mwaka 2023, idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita ilikuwa 3,077,355 ikilinganishwa na wanafunzi 2,823,588 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.0. Kati ya hao, wasichana walikuwa 1,608,202 na wavulana 1,469,153. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari za Serikali ilikuwa 2,774,947 (wasichana 1,450,857 na wavulana 1,324,090) mwaka 2023 ikilinganishwa na wanafunzi 2,529,699 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.7. Vile vile, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne ilikuwa 2,881,335 ikilinganishwa na wanafunzi 2,645,115 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.9. Kati ya hao, wanafunzi katika shule za Serikali walikuwa 2,618,325 ikilinganishwa na wanafunzi 2,387,525 katika shule za Serikali mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.7.

Ongezeko hilo lilitokana na idadi kubwa ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza kufuatia utekelezaji wa programu ya elimu msingi bila ada.

375. Mwaka 2023, idadi ya watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne walikuwa 529,596 (wasichana 284,893 na wavulana 244,703) ikilinganishwa na watahiniwa 522,217 waliofanya mtihani mwaka 2022. Kati ya hao, watahiniwa 471,427 (wasichana 250,147 na wavulana 221,280) walifaulu, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 89.0 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 87.8 mwaka 2022. Aidha, watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha sita mwaka 2023 walikuwa 96,319 (wasichana 43,366 na wavulana 52,953) ikilinganishwa na watahiniwa 84,870 (wasichana 37,468 na wavulana 47,402) mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 13.5. Kati ya hao, watahiniwa 96,010 (wasichana 43,268 na wavulana 52,742) walifaulu, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 99.90 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 99.87 mwaka 2022.

376. Mwaka 2023, idadi ya walimu katika shule za sekondari za Serikali ilifikia 96,130 (wanawake 33,253 na wanaume 62,877) kutoka walimu 91,537 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Hii inatokana na jitihada za Serikali kuendelea kuongeza ajira mpya za walimu. Aidha, idadi ya walimu katika shule za sekondari zisizo za Serikali ilifikia 21,779 mwaka 2023 (wanawake 4,934 na wanaume 16,845) kutoka walimu 21,668 mwaka 2022.

**Elimu katika Vyuo vya Ualimu**

377. Mwaka 2023, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu ilikuwa 23,162 (wanawake 11,119 na wanaume 12,043) ikilinganishwa na wanachuo 22,085 kwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 4.9. Katika kipindi cha mwaka 2022/23 wanachuo waliodahiliwa walikuwa 13,051 ikilinganishwa na wanachuo 9,497 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 37.4. Aidha, wanachuo waliofanya mtihani wa kuhitimu mafunzo ya ualimu katika ngazi ya stashahada na astashahada walikuwa 7,901 mwaka 2023 ikilinganishwa na wanachuo 8,284 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 4.6. Kati ya hao, wanachuo 7,694 walifaulu na kuhitimu mafunzo ya ualimu mwaka 2023, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 97.4 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 94.8 mwaka 2022. Kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu kulitokana na juhudi za kuboresha miundombinu ya vyuo vya ualimu vya Serikali pamoja na kuvipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia, hususan katika masomo ya sayansi na TEHAMA.

**Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

378. Mwaka 2022/23, Serikali iliendelea kufanya kaguzi katika shule na vyuo vya ualimu kwa lengo la kuhakikisha kuwa ubora wa elimu inayotolewa unazingatiwa katika ngazi zote za elimu. Katika kipindi hicho, taasisi 6,649 za elimu zilikaguliwa ikilinganishwa na taasisi 6,524 zilizokaguliwa mwaka 2021/22. Kuongezeka kwa taasisi zilizokaguliwa kulitokana na

juhudi za Serikali katika kuimarisha mazingira ya utendaji kazi katika Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule za Kanda na Wilaya.

**Jedwali Na. 16.1 Ukaguzi wa Taasisi za Elimu Mwaka 2021/22 - 2022/23**

| Taasisi/Shule/ Vituo/Vyuo | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---:|---:|
| Shule za Awali na Msingi | 5,332 | 5,623 |
| Shule za Sekondari | 1,162 | 986 |
| Vyuo vya Ualimu | 30 | 40 |
| **Jumla** | **6,524** | **6,649** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Elimu ya Ufundi na Mafunzo**

379. Mwaka 2022/23, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ilikuwa 193,343 ikilinganishwa na wanafunzi 185,818 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 4.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya elimu ya ufundi katika soko la ajira. Kati ya wanafunzi hao, wanawake walikuwa 94,370 (asilimia 48.8) na wanaume walikuwa 98,973. Aidha, idadi ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo vilifikia 474 mwaka 2022/23 kutoka vyuo 459 mwaka 2021/22.

**Elimu ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

380. Mwaka 2022/23, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ufundi stadi vinavyomilikiwa na VETA ilikuwa 69,347 (wanawake 17,577 na wanaume 51,770) ikilinganishwa na wanafunzi 64,142[1] mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 8.1. Hii ilitokana na ujenzi, upanuzi na ukarabati wa vyuo vya ufundi stadi pamoja na miundombinu ya mafunzo ikiwemo: kumbi za mihadhara katika Chuo cha Utalii na Ukarimu Njiro (VETA Hotel and Tourism Training Institute); ujenzi wa mabweni katika chuo cha VETA Simanjiro; mabwalo ya chakula, Namtumbo, Itilima na Ileje; ukarabati wa vyuo vya VETA Dar es Salaam, Dodoma, Newala; na uboreshaji wa mitaala 18 inayoendana na mahitaji ya soko la ajira. Aidha, wanafunzi 14,897 ( wanawake 5,027 na wanaume 9,870) walihitimu mafunzo ya ufundi stadi kwa kozi za muda mrefu katika vyuo vinavyomilikiwa na VETA mwaka

[1] Kupungua kwa idadi ya wanafunzi walioripotiwa mwaka 2022 kunatokana na mabadiliko ya Sheria ya VETA ya Mwaka 1994 iliyofanyiwa marekebisho Mwaka 2022 ambapo jukumu la Urekebu lilihamishiwa NACTVET. Hivyo, takwimu hii haijumuishi vyuo binafsi vya ufundi ambavyo usimamizi wake ulihamishiwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi - NACTVET

2022/23 ikilinganishwa na wanafunzi 15,780 mwaka 2021/22, sawa na upungufu wa asilimia 5.6. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya wanafunzi waliojisajili kwenye programu za Mitihani ya Taifa ya Biashara - NABE ambayo muda wake umekwisha na kupungua kwa idadi ya wanafunzi katika Programu ya uanagenzi (Apprenticeship Programe) inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

381. Mwaka 2022/23, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya maendeleo ya wananchi ilikuwa 17,695 (wanawake 7,352 na wanaume 10,343) ikilinganishwa na wanafunzi 16,457 mwaka 2021/22. Aidha, wanafunzi 13,527 walihitimu mafunzo katika vyuo vya maendeleo ya wananchi mwaka 2023 ikilinganishwa na wanafunzi 12,665 waliohitimu mwaka 2022. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi kulitokana na ujenzi, upanuzi pamoja na ukarabati wa vyuo 55 vya maendeleo ya wananchi.

**Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

382. Mwaka 2023, Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha ilidahili wanafunzi 168 (wanawake 55 na wanaume 113) ikilinganishwa na wanafunzi 151 waliodahiliwa mwaka 2022. Katika kipindi hicho, wanafunzi 131 (wanawake 45 na wanaume 86) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 78 waliohitimu mwaka 2022. Hii ilitokana na uhitimu wa wanafunzi wengi waliofadhiliwa na Mradi wa Vituo vya Umahiri (African Centres of Excellence - ACE II).

383. Mwaka 2023, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilidahili wanafunzi 9,664 (wanawake 7,439 na wanaume 2,225) ikilinganishwa na wanafunzi 8,398 waliodahiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 15.1. Aidha, wanafunzi 1,978 (wanawake 1,437 na wanaume 541) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 2,203 waliohitimu mwaka 2022.

384. Mwaka 2023, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanafunzi 7,130 (wanawake 1,697 na wanaume 5,433) ikilinganishwa na wanafunzi 5,475 waliodahiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 30.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mitaala na ndaki zilizochangia kuongezeka kwa kozi mpya.

385. Mwaka 2023, Chuo cha Ufundi Arusha kilidahili wanafunzi 2,887 (wanawake 635 na wanaume 2,252) ikilinganishwa na wanafunzi 3,031 waliodahiliwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 4.8. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya wanafunzi waliopangwa kulikosababishwa na upungufu wa hosteli ambapo Serikali inaendelea na ujenzi wa majengo mapya ya hosteli.

**Elimu ya Juu**

386. Mwaka 2022/23, wanafunzi katika vyuo vikuu nchini walikuwa 274,438 (wanawake 121,909 na wanaume 152,529) ikilinganishwa na wanafunzi 229,049 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 19.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wanafunzi wanaohitimu elimu ya sekondari, wanafunzi wanaojiunga kutokana na kupata sifa katika vyuo vya elimu ya kati, upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu pamoja na kuongezeka kwa programu zinazotolewa.

387. Mwaka 2022/23, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 657 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 611.3 iliyotolewa mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Katika kipindi hicho, wanafunzi 202,016 walinufaika na mikopo hiyo ikilinganishwa na wanafunzi 176,763 walionufaika mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Kati ya hao, wanafunzi wa mwaka wa kwanza walikuwa 73,077 na wanafunzi 128,939 waliokuwa wanaendelea na masomo. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wanafunzi wanaoendelea na masomo walionufaika na mikopo kwa mara ya kwanza. Aidha, mikopo kutoka kwa wanufaika kiasi cha shilingi bilioni 169.8 ilirejeshwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi bilioni 182.5 zilizorejeshwa mwaka 2021/22, sawa na upungufu wa asilimia 7.0. Hii ilitokana na Serikali kusitisha adhabu na tozo za kulinda thamani ili kuwapa ahueni walipaji wa mikopo.

**Udhibiti wa Mionzi**

388. Mwaka 2023, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania ilipokea na kutathmini maombi 842 ya leseni za matumizi na umiliki wa vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na maombi 782 ya leseni mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.7. Aidha, maombi 767 yalipata leseni baada ya kukidhi vigezo mwaka 2023 ikilinganishwa na maombi 542 mwaka 2022. Hadi Desemba 2023, vituo vinavyomiliki na kutumia mionzi vilifikia 1,425 kutoka vituo 1,188 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, vituo 971 vilikaguliwa ili kudhibiti usalama wa wagonjwa na wafanyakazi mwaka 2023 ikilinganishwa na vituo 670 vilivyokaguliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 44.9.

389. Mwaka 2022/23, Tume ilipima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,120 katika vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na wafanyakazi 2,064 waliopimwa mwaka 2021/22. Matokeo ya vipimo yalibainisha kuwa viwango vya mionzi wanavyopata wafanyakazi vipo katika viwango vinavyokubalika. Kwa upande mwingine, Tume ilipima viwango vya mionzi katika sampuli 41,544 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na sampuli 37,433 mwaka 2021/22. Kati ya hizo, sampuli 10,559 zilikuwa za vyakula kutoka nje, sampuli 29,824 za vyakula vilivyosafirishwa nje ya nchi, sampuli 383 za mbolea, sampuli 660 za tumbaku, sampuli 39 kutoka kwa wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa za vyakula ndani ya nchi na

sampuli 79 kutoka vyanzo vya maji na bidhaa nyingine. Matokeo yalionesha kuwa sampuli zote zilizopimwa hazikuwa na uchafuzi wa viasili vya mionzi.

**Jedwali Na. 67: SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO**

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2007 | 401,011 | 218,060 | 105,770 | 70,796 | 21,789 | 11,668 | 829,094 |
| 2008 | 395,930 | 332,393 | 175,353 | 95,214 | 25,240 | 11,743 | 1,035,873 |
| 2009 | 480,529 | 308,131 | 159,789 | 167,355 | 31,201 | 12,695 | 1,159,700 |
| 2010 | 382,207 | 398,870 | 293,519 | 279,995 | 26,065 | 20,674 | 1,401,330 |
| 2011 | 403,873 | 396,724 | 380,528 | 279,117 | 30,265 | 25,164 | 1,515,671 |
| 2012 | 457,321 | 386,250 | 355,740 | 343,376 | 31,206 | 28,859 | 1,602,752 |
| 2013 | 444,532 | 506,036 | 193,901 | 302,963 | 30,581 | 26,698 | 1,504,711 |
| 2014 | 479,089 | 506,170 | 356,787 | 178,246 | 33,619 | 26,899 | 1,580,810 |
| 2015 | - | - | - | - | - | - | - |
| 2016 | 467,982 | 366,396 | 263,981 | 278,690 | 45,533 | 47,007 | 1,469,589 |
| 2017 | 491,535 | 443,614 | 296,034 | 236,775 | 53,749 | 43,494 | 1,565,201 |
| 2018 | 587,186 | 480,327 | 358,960 | 278,239 | 57,287 | 52,687 | 1,814,686 |
| 2019 | 637,335 | 555,087 | 388,029 | 334,284 | 52,428 | 56,042 | 2,023,205 |
| 2020 | 659,661 | 588,561 | 454,139 | 360,356 | 58,402 | 51,138 | 2,172,257 |
| 2021 | 718,592 | 616,791 | 498,703 | 422,403 | 66,576 | 56,880 | 2,379,945 |
| 2022 | 784,061 | 648,525 | 499,958 | 454,981 | 77,873 | 64,301 | 2,529,699 |
| 2023 | 952,657 | 719,377 | 486,848 | 459,443 | 82,069 | 74,553 | 2,774,947 |
| **Badiliko (Asilimia) 2022 - 2023** | **21.5** | **10.9** | **-2.6** | **1.0** | **5.4** | **15.9** | **9.7** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia
- Takwimu Hazikupatikana

**Jedwali Na. 68: SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO**

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2007 | 47,437 | 46,927 | 41,340 | 35,746 | 11,299 | 8,667 | 191,416 |
| 2008 | 42,971 | 43,232 | 43,177 | 35,980 | 12,576 | 8,594 | 186,530 |
| 2009 | 44,255 | 36,384 | 37,064 | 34,061 | 11,851 | 9,096 | 172,711 |
| 2010 | 56,620 | 57,876 | 50,778 | 46,820 | 12,269 | 13,006 | 237,369 |
| 2011 | 63,282 | 67,205 | 65,859 | 54,521 | 11,083 | 11,926 | 273,876 |
| 2012 | 65,058 | 69,403 | 64,453 | 61,209 | 9,684 | 11,713 | 281,520 |
| 2013 | 70,060 | 77,407 | 67,998 | 65,637 | 8,592 | 9,651 | 299,345 |
| 2014 | 109,784 | 96,732 | 76,574 | 66,898 | 8,865 | 7,686 | 366,539 |
| 2015 | - | - | - | - | - | - | - |
| 2016 | 70,844 | 81,499 | 72,970 | 73,231 | 21,091 | 17,731 | 337,366 |
| 2017 | 71,160 | 79,548 | 77,168 | 72,056 | 24,146 | 19,578 | 343,656 |
| 2018 | 64,844 | 71,685 | 74,932 | 74,848 | 24,030 | 23,441 | 333,780 |
| 2019 | 63,629 | 64,488 | 68,064 | 74,121 | 22,050 | 22,900 | 315,252 |
| 2020 | 63,232 | 64,727 | 64,328 | 67,255 | 20,032 | 21,675 | 301,249 |
| 2021 | 61,784 | 64,901 | 64,889 | 63,481 | 17,917 | 19,010 | 291,982 |
| 2022 | 66,052 | 62,741 | 65,172 | 63,625 | 18,989 | 17,310 | 293,889 |
| 2023 | 68,757 | 67,294 | 62,761 | 64,198 | 20,653 | 18,745 | 302,408 |
| **Badiliko (Asilimia) 2022 - 2023** | **4.1** | **7.3** | **(3.7)** | **0.9** | **8.8** | **8.3** | **2.9** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
- Takwimu Hazikupatikana

**Jedwali Na. 69: IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA**

| Elimu ya msingi | 2022 | | | 2023 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Waume | Wake | Jumla | Waume | Wake | Jumla |
| Jumla ya wanafunzi wote walioandikishwa Darasa la I-VII | 5,636,996 | 5,783,977 | 11,420,973 | 5,616,919 | 5,808,563 | 11,425,482 |
| Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za Serikali Darasa la I-VII | 5,363,454 | 5,509,054 | 10,872,508 | 5,318,340 | 5,506,034 | 10,824,374 |
| Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa la I-VII | 273,542 | 274,923 | 548,465 | 298,579 | 302,529 | 601,108 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi | 103,854 | 97,818 | 201,672 | 107,409 | 99,914 | 207,323 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi za Serikali | 87,110 | 86,166 | 173,276 | 89,367 | 87,173 | 176,540 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi za binafsi | 16,744 | 11,652 | 28,396 | 18,042 | 12,741 | 30,783 |
| **Elimu ya Sekondari** | | | | | | |
| Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI | 1,347,219 | 1,476,369 | 2,823,588 | 1,469,153 | 1,608,202 | 3,077,355 |
| Wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali, kidato I-VI | 1,206,820 | 1,322,879 | 2,529,699 | 1,324,090 | 1,450,857 | 2,774,947 |
| Wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI | 140,399 | 153,490 | 293,889 | 145,063 | 157,345 | 302,408 |
| Idadi ya walimu katika shule za Serikali | 59,520 | 32,017 | 91,537 | 62,723 | 33,407 | 96,130 |
| Idadi ya walimu katika shule za binafsi | 16,852 | 4,816 | 21,668 | 16,999 | 4,780 | 21,779 |
| Jumla ya Walimu katika shule za Sekondari | 76,372 | 36,833 | 113,205 | 79,722 | 38,187 | 117,909 |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
- Takwimu Hazikupatikana

**Jedwali Na. 70: IDADI YA TAASISI ZA ELIMU**

| Aina ya Taasisi | 2022 | | | 2023 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Binafsi | Jumla | Serikali | Binafsi | Jumla |
| Shule za Msingi | 17,181 | 2,080 | 19,261 | 17,463 | 2,270 | 19,733 |
| Shule za Sekondari | 4,211 | 1,329 | 5,540 | 4,578 | 1,348 | 5,926 |
| Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari) | - | - | - | 35 | 30 | 65 |
| Elimu ya Ufundi na Mafunzo | - | - | - | 304 | 857 | 1,161 |
| **Jumla** | **21,392** | **3,409** | **24,801** | **22,380** | **4,505** | **26,885** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
- Takwimu hazikupatikana

## SURA YA 17

## AFYA NA MAENDELEO YA JAMII

### AFYA

### Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

390. Mwaka 2023, vituo vya kutolea huduma za afya vinavyofanya kazi viliongezeka kwa asilimia 6.9 na kufikia vituo 11,805 ikilinganishwa na vituo 11,041 mwaka 2022. Kati ya hivyo, vituo vilivyokuwa vinamilikiwa na Serikali vilikuwa 7,091, sekta binafsi vituo 3,638 na mashirika ya dini vituo 1,076. Ongezeko hilo lilitokana na kufunguliwa kwa vituo vipya, kuimarika kwa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa taarifa za vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na usajili wa vituo vipya vya binafsi.

**Jedwali Na. 17.1: Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Mwaka 2022 - 2023**

| Aina ya Vituo | 2022 | | | | 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Serikali** | **Mashirika ya Dini** | **Sekta Binafsi** | **Jumla** | **Serikali** | **Mashirika ya Dini** | **Sekta Binafsi** | **Jumla** |
| Hospitali | 217 | 119 | 82 | 418 | 228 | 121 | 87 | 436 |
| Vituo vya Afya | 725 | 162 | 129 | 1,016 | 831 | 163 | 132 | 1,126 |
| Zahanati | 5,719 | 692 | 1,036 | 7,447 | 6,010 | 714 | 1,080 | 7,804 |
| **Jumla ndogo** | **6,661** | **973** | **1,247** | **8,881** | **7,069** | **998** | **1,299** | **9,366** |
| Poly clinic | 3 | 32 | 284 | 319 | 0 | 44 | 321 | 365 |
| *Nyinginezo (Kliniki, maabara | 17 | 35 | 1,716 | 1,768 | 21 | 34 | 1,935 | 1,990 |
| Martenity/Nursing ho | 1 | 1 | 71 | 73 | 1 | 0 | 83 | 84 |
| **Jumla kuu** | **6,682** | **1,041** | **3,318** | **11,041** | **7,091** | **1,076** | **3,638** | **11,805** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya

*Nyinginezo inajumuisha kliniki, maabara na vituo vya uchangiaji wa damu

391. Mwaka 2023, wagonjwa waliohudumiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya hospitali, vituo vya afya na zahanati walikuwa 45,164,482 ikilinganishwa na wagonjwa 42,971,561 waliohudumiwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 5.1. Ongezeko hilo lilitokana na uboreshwaji wa huduma za afya ikiwemo ununuzi wa dawa, upatikanaji wa vifaa na vifaa tiba pamoja na kusogeza vituo vya kutolea huduma za afya karibu na wananchi. Kati ya waliohudumiwa, wagonjwa wa nje walikuwa 43,407,242 na wagonjwa wa kulazwa walikuwa 1,757,240. Aidha, vitanda vya wagonjwa vilifikia 125,500 mwaka 2023 kutoka vitanda 104,687 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 19.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na vitanda kufuatia kukamilika kwa majengo ya vyumba vya wagonjwa mahututi na vyumba vya kutolea huduma za dharura.

**Dawa na Vifaa Tiba**

392. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kipindi hicho, upatikanaji wa bidhaa za afya katika ngazi zote za vituo vya kutolea huduma za afya ulikuwa wa wastani wa asilimia 75.6 ikilinganishwa na asilimia 67.8 mwaka 2022. Ongezeko hili lilitokana na juhudi za Serikali katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya ikiwemo upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

**Jedwali Na. 17.2: Upatikanaji wa Dawa katika Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Mwaka 2023**

| Na. | Aina ya Kituo | Idadi ya Aina za Dawa zinazotakiwa | Hali ya upatikanaji wa Dawa (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| 1. | Hospitali ya Taifa, Maalum, Kanda | 290 | 91 |
| 2. | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa | 284 | 95 |
| 3. | Hospitali ya Wilaya | 253 | 70 |
| 4. | Kituo cha Afya | 219 | 62 |
| 5. | Zahanati | 141 | 60 |
| | **Wastani** | | **75.6** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya

393. Mwaka 2023, Serikali ilikamilisha ufungwaji wa mashine ya *PET CT- Scan* moja kwa ajili ya uchunguzi na matibabu ya saratani katika Taasisi ya Saratani Ocean Road pamoja na *Angio Suite* moja katika Taasisi ya Mifupa-MOI na *Mini Angio-Suite* moja katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa ajili ya uchunguzi na matibabu ya mishipa ya damu. Aidha, mashine za Magnetic *Resonance Imaging* (MRI) zilifikia 13, mitambo ya kisasa ya *CT–Scan* 45, *Digital X–Ray* 346, mashine za uchunguzi wa moyo saba (7), *Ultrasound Machine* 512 na *Fluoroscopy* 13.

**Afya ya Uzazi na Mtoto**

394. Mwaka 2023, wajawazito 2,597,643 walihudhuria kliniki ikilinganishwa na wajawazito 2,442,407 mwaka 2022. Kati ya hao, wajawazito 1,053,738 (asilimia 40.6) walifanya hudhurio la kwanza kabla ya majuma 12 mwaka 2023 ikilinganishwa na wajawazito 947,654 (asilimia 38.8) mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na utolewaji wa elimu ya afya kwa umma kupitia redio na televisheni kuhusu umuhimu wa kuhudhuria kliniki mapema.

395. Mwaka 2023, wajawazito waliohudhuria kliniki angalau mara nne (4) walikuwa asilimia 117 ya makadirio ikilinganishwa na asilimia 110.6 mwaka 2022. Aidha, wajawazito waliohudhuria kliniki na kupima Virusi Vya Ukimwi (VVU) walikuwa asilimia 98.1 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 98.9 mwaka 2022. Kati ya hao, asilimia 0.77 ya wajawazito waligundulika kuwa na VVU ikilinganishwa na asilimia 1.0 mwaka 2022. Vile vile,

asilimia 96.4 ya wajawazito waliogundulika kuwa na VVU walianzishiwa matibabu ya kufubaza VVU ikilinganishwa na asilimia 97.5 mwaka 2022.

396. Mwaka 2023, wanawake 601,922 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi ikilinganishwa na wanawake 669,755 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 10.1. Kati ya hao, wanawake 20,392 (asilimia 3.4) waligundulika kuwa na saratani ya mlango wa kizazi na wanawake 15,778 (asilimia 2.6) waligundulika kuwa na mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi. Kwa upande mwingine, chanjo za kuwakinga wasichana wenye umri kati ya miaka 9 hadi 14 dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi ziliendelea kutolewa. Wasichana waliochanjwa HPV 1 walikuwa 943,551 sawa na asilimia 114 na HPV 2 walikuwa 758,320 (asilimia 91) mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 75.0 na asilimia 76.0, mtawalia mwaka 2022.

397. Mwaka 2023, huduma za dharura za afya ya uzazi na mtoto mchanga ziliendelea kuboreshwa kwa kuongeza idadi ya vituo vya afya vinavyofanya upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni - CEmNOC. Aidha, vituo vya kumtoa mtoto tumboni vilifikia 523 ikilinganishwa na vituo 388 mwaka 2022. Vile vile, vyumba/wodi za watoto wachanga mahtuti na wanaozaliwa kabla ya wakati viliongezeka hadi vyumba/wodi 189 mwaka 2023 kutoka vyumba 125 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 51.2. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Serikali kuendelea kuboresha huduma za dharura za afya ya uzazi na mtoto mchanga kwa lengo la kupunguza vifo vya mama na watoto wachanga.

**Huduma za Chanjo kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja**

398. Mwaka 2023, idadi ya watoto waliozaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya iliongezeka kwa asilimia 6.5 na kufikia watoto 2,105,713 ikilinganishwa na watoto 1,976,433 waliozaliwa mwaka 2022. Aidha, watoto 2,615,399 wenye umri chini ya mwaka mmoja walitarajiwa kupata chanjo mbalimbali ambapo watoto waliopata chanjo ya PENTA - 3 walikuwa asilimia 103, Surua Rubella - 1 (asilimia 101), Surua Rubella - 2 (asilimia 97), OPV - 3 (asilimia 100), Rota - 2 (asilimia 99) na PCV - 3 (asilimia 100). Ongezeko la viwango vya uchanjaji ni matokeo ya utekelezaji wa zoezi maalum la *Periodic Intensification of Routine Immunization* (PIRI) lililolenga kuwatafuta watoto wasiochanjwa au wasiokamilisha ratiba za chanjo.

**Huduma za Matibabu ya Kibingwa**

399. Mwaka 2023, huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ziliendelea kutolewa katika hospitali maalum nchini. Katika kipindi hicho, wagonjwa 124 walipandikizwa figo ikilinganishwa na wagonjwa 98 mwaka 2022. Aidha, huduma ya upandikizaji wa uroto ilitolewa kwa wagonjwa 15 mwaka 2023 ikilinganishwa na wagonjwa 11 mwaka 2022. Vile vile, wagonjwa 166 waliwekewa puto ili kupunguza unene uliokithiri ikilinganishwa na wagonjwa 11 mwaka 2022.

400. Mwaka 2023, wagonjwa 2,239 walifanyiwa upasuaji wa moyo kwa kutumia mtambo maalum (Catheterization Laboratory) ikilinganishwa na wagonjwa 1,618 mwaka 2022. Aidha, watoto waliopandikiziwa vifaa vya usikivu waliongezeka na kufikia 61 mwaka 2023 kutoka watoto 49 mwaka 2022. Vile vile, wagonjwa 31 walipata huduma ya upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye sakafu ya ubongo kupitia tundu la pua ikilinganishwa na wagonjwa 28 mwaka 2022.

401. Mwaka 2023, huduma mpya za kibingwa na ubingwa bobezi za upandikizaji wa nyonga na magoti zilitolewa kwa wagonjwa 78 na upasuaji wa moyo wa kupandikiza mishipa bila kusimamisha moyo kwa wagonjwa wanne (4). Aidha, wagonjwa 380 walipata matibabu ya kuondoa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa kutumia mawimbi mshtuko (Extracorporeal Shock Wave Lithotripsy).

**Udhibiti wa Malaria**

402. Mwaka 2023, vipimo 24,171,900 vya vitendanishi vya malaria na vichupa 1,755,363 vya dawa ya malaria ya sindano vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na vipimo 22,578,350 na vichupa 2,890,242 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, visa vipya vya malaria vilikuwa 58 kwa kila watu 1,000 kama ilivyokuwa mwaka 2022. Aidha, vyandarua 9,575,639 vyenye dawa vilinunuliwa na kusambazwa ikilinganishwa na vyandarua 6,119,732 mwaka 2022.

403. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutekeleza afua ya ufuatiliaji na matibabu ya wagonjwa wa malaria hadi ngazi ya kaya, hususan kwenye mikoa yenye kiwango kidogo cha maambukizi ya malaria. Afua hiyo ilitekelezwa katika mikoa mitano (5) ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Njombe na Iringa ikilinganishwa na mikoa minne (4) mwaka 2022. Aidha, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu - NIMR ilifanya uchambuzi wa mbu 8,772 waliokusanywa katika vituo 32 mwaka 2022. Matokeo ya utafiti uliofanyika mwaka 2023 yalionesha kuwa asilimia 42.3 ya mbu walikuwa aina ya *Anopheles Fenestus* na asilimia 57.7 walikuwa *Anopheles Gambiae s.s*. Vile vile, utafiti huo ulionyesha uwezo wa mbu kueneza vimelea vya malaria kwa mtu kwa mwaka ulipungua na kufikia asilimia 0.10 mwaka 2023 kutoka asilimia 0.97 mwaka 2022. Upungufu huo ulitokana na utekelezaji wa afua mbalimbali ikiwemo: ugawaji wa vyandarua kwa makundi maalumu (mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano, wafungwa, watu wanaoishi na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na wazee); upuliziaji wa viuadudu vya kibaiolojia katika mazalia ya mbu; na kuelimika kwa jamii kuhusu umuhimu wa kufanya usafi wa mazingira ili kuharibu vyanzo vya mazalia ya mbu.

**Udhibiti wa Kifua Kikuu**

404. Mwaka 2023, wagonjwa 93,184 wa kifua kikuu waligundulika na kuanzishiwa matibabu ikilinganishwa na wagonjwa 100,747 mwaka 2022. Aidha, wagonjwa 337 wa kifua kikuu sugu waligundulika; kati ya hao, wagonjwa 312, sawa na asilimia 92.6 walianzishiwa matibabu. Katika kipindi hicho, vituo vya kutolea huduma za uchunguzi na tiba ya kifua kikuu vilifikia 1,773 kutoka vituo 1,752 mwaka 2022. Vile vile, vituo vya kutoa huduma za afya vyenye uwezo wa kuanzisha matibabu ya kifua kikuu sugu vilifikia 314 mwaka 2023 kutoka vituo 304 mwaka 2022.

**Lishe**

405. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe (2021/22 - 2025/26) ili kukabiliana na athari za lishe duni na kuimarisha ukuaji wa mwili na akili kwa watoto. Katika kipindi hicho, asilimia 87.0 ya watoto 9,421,026 walio chini ya umri wa miaka mitano walipatiwa matone ya Vitamini A ikilinganishwa na watoto 9,456,436 (asilimia 99.0) mwaka 2022. Aidha, watoto waliozaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya na kunyonyeshwa ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa walikuwa asilimia 89.0 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 91.3 mwaka 2022. Kwa upande mwingine, asilimia 1.8 ya wajawazito waliopimwa wingi wa damu katika hudhurio la kwanza walikuwa na upungufu wa damu mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 1.1 ya wajawazito waliopimwa mwaka 2022.

406. Mwaka 2023, watoto waliozaliwa na uzito pungufu walikuwa asilimia 5.5 ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2022. Hii ilitokana na kuendelea na utekelezaji wa afua mbalimbali za lishe kwa wajawazito ikiwemo utoaji wa vidonge vya madini chuma, utoaji wa elimu ya lishe, kuhamasisha ulaji wa vyakula vilivyoongezwa virutubishi na kuhudhuria kliniki kwa wakati.

**Mafunzo katika Kada za Afya**

407. Mwaka 2023, wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya afya katika ngazi ya astashahada na stashahada walikuwa 24,463 (wanawake 13,091 na wanaume 11,372) ikilinganishwa na wanafunzi 25,393 waliodahiliwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 3.7. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya vyuo kufungiwa na NACTVET kwa kukosa ubora wa uendeshaji wa mafunzo ya afya na kusitishwa kwa baadhi ya kozi. Aidha, wanafunzi waliohitimu walikuwa 14,974 (wanawake 7,572 na wanaume 7,402) ikilinganishwa na wanafunzi 10,231 (wanaume 5,385 na wanawake 4,846) mwaka 2022.

**Jedwali Na. 17.3: Wanafunzi Waliodahiliwa na Kuhitimu Mafunzo ya Afya Mwaka 2023**

| Na | Kozi | Waliodahiliwa | | | Waliohitimu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Wanaume | Jumla | Wanawake | Wanaume | Jumla |
| 1 | Utabibu wa Kinywa na Meno | 117 | 184 | 301 | 46 | 91 | 137 |
| 2 | Utabibu | 2,866 | 4,251 | 7,117 | 2,139 | 3,125 | 5,264 |
| 3 | Rediografia | 19 | 29 | 48 | 0 | 0 | 0 |
| 4 | Sayansi ya Afya ya Mazingira | 40 | 78 | 118 | 47 | 118 | 165 |
| 5 | Sayansi ya Taarifa za Afya | 46 | 30 | 76 | 21 | 22 | 43 |
| 6 | Teknolojia ya Utunzaji wa Kumbukumbu na Taarifa za Afya | 19 | 20 | 39 | 25 | 33 | 58 |
| 7 | Sayansi ya Maabara za Tiba | 437 | 665 | 1,102 | 270 | 366 | 636 |
| 8 | Uuguzi na Ukunga | 2,144 | 1,337 | 3,481 | 2,228 | 1,761 | 3,989 |
| 9 | Optometria | 27 | 37 | 64 | 19 | 20 | 39 |
| 10 | Sayansi ya Ufamasia | 7,308 | 4,669 | 11,977 | 2,748 | 1,825 | 4,573 |
| 11 | Fisiotherapia | 68 | 64 | 132 | 29 | 41 | 70 |
| 12 | Elimu kwa Watumishi wa Afya | 0 | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| 13 | Usimamizi wa Afya Wilayani | 0 | 4 | 4 | 0 | 0 | |
| | **Jumla** | **13,091** | **11,372** | **24,463** | **7,572** | **7,402** | **14,974** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya

## MAENDELEO YA JAMII

### Ustawi wa Jamii

408. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutekeleza kampeni ya kuchochea hamasa ya ujenzi wa nyumba bora kwa gharama nafuu zinazotumia teknolojia rahisi na ya kisasa. Kampeni hiyo iliyowezesha wananchi kujenga nyumba bora 6,151 ikilinganishwa na nyumba 5,732 zilizojengwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.3.

### Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

409. Mwaka 2023, wanafunzi 11,574 (wanawake 7,639 na wanaume 3,935) walidahiliwa katika taasisi na vyuo vya maendeleo ya jamii ikilinganishwa na wanafunzi 11,139 (wanawake 6,965 na wanaume 4,174) waliodahiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.9. Aidha, katika kipindi hicho, wanafunzi 9,803 walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 9,404 mwaka 2022.

**Jedwali Na. 17.4: Udahili wa Wanafunzi katika Taasisi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

| Taasisi | Ngazi ya Elimu | 2022 | | | 2023 | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | |
| Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | Stashahada | 709 | 901 | 1,610 | 560 | 924 | 1,484 | -7.8 |
| | Astashahada | 1,380 | 2,265 | 3,645 | 1,419 | 2,613 | 4,032 | 10.6 |
| | **Jumla ndogo** | **2,089** | **3,166** | **5,255** | **1,979** | **3,537** | **5,516** | **5** |
| Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru | Astashahada | 410 | 926 | 1,336 | 446 | 915 | 1,361 | 1.9 |
| | Stashahada | 185 | 430 | 615 | 149 | 378 | 527 | -14.3 |
| | Shahada | 342 | 549 | 891 | 102 | 169 | 271 | -69.6 |
| | Stashahada ya Juu | – | – | – | 313 | 459 | 772 | – |
| | Shahada ya Uzamili | 46 | 30 | 76 | 42 | 46 | 88 | 15.8 |
| | **Jumla ndogo** | **983** | **1,935** | **2,918** | **1,052** | **1,967** | **3,019** | **3.5** |
| Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama | Astashahada | 427 | 609 | 1,036 | 318 | 840 | 1,158 | 11.8 |
| | Stashahada | 329 | 561 | 890 | 65 | 152 | 217 | -75.6 |
| | Shahada | 311 | 636 | 947 | 521 | 1,143 | 1,664 | 75.7 |
| | Stashahada ya Juu | 4 | 3 | 7 | - | - | - | - |
| | Shahada ya Uzamili | 31 | 55 | 86 | - | - | - | - |
| | **Jumla ndogo** | **1,102** | **1,864** | **2,966** | **904** | **2,135** | **3,039** | **2.5** |
| | **Jumla Kuu** | **4,174** | **6,965** | **11,139** | **3,935** | **7,639** | **11,574** | **3.9** |

**Chanzo:** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

410. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Uanagenzi kwa kuwaunganisha wanafunzi na wahitimu wa taaluma ya maendeleo ya jamii kwenye mashirika, taasisi, na kampuni ili kupata mafunzo kwa vitendo. Katika kipindi hicho, wahitimu 1,421 wa taaluma ya maendeleo ya jamii walipata mafunzo kwa vitendo ikilinganishwa na wahitimu 1,078 mwaka 2022.

### Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

411. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kuratibu utoaji wa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Katika kipindi hicho, vituo 340 vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo 254 mwaka 2022. Aidha, watoto 198,432 (wavulana 97,011 na wasichana 101,421) waliandikishwa katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana mwaka 2023 ikilinganishwa na watoto 179,394 mwaka 2022. Vile vile, vituo vilikuwa na walezi 1,589 ikilinganishwa na walezi 1,151 mwaka 2022.

### Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto

412. Mwaka 2023, watoto 45 (wasichana 24 na wavulana 21) walio katika mazingira hatarishi walipata huduma za malezi ya kambo ikilinganishwa na watoto 48 (wasichana 21 na wavulana 27) mwaka 2022. Aidha, mwaka 2023 watoto walioasiliwa walikuwa 40 (wasichana 23 na wavulana 17) ikilinganishwa na watoto 56 walioasiliwa mwaka 2022.

413. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanaoishi katika makao ya watoto ya Taifa Kurasini - Dar es Salaam na Kikombo - Dodoma. Katika kipindi hicho, watoto 209 (wasichana 86 na wavulana 123) walipatiwa huduma hizo ikilinganishwa na watoto 127 mwaka 2022. Aidha, watoto 13,036 (wasichana 6,407 na wavulana 6,629) walipatiwa huduma za msingi kupitia makao ya watoto ya binafsi mwaka 2023 ikilinganishwa na watoto 25,493 mwaka 2022.

414. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutoa huduma za ustawi katika mahabusu tano (5) za watoto zilizopo Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Katika kipindi hicho, watoto 325 (wasichana 18 na wavulana 307) walio katika mkinzano na sheria waliwezeshwa kupata huduma za msingi ikiwemo chakula, mavazi, malazi, matibabu na elimu ikilinganishwa na watoto 428 mwaka 2022.

415. Mwaka 2023, watoto 48 (wasichana 2 na wavulana 46) waliokuwa katika mkinzano na sheria walichepushwa kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na familia zao ikilinganishwa na watoto 54 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, wavulana tisa (9) walihukumiwa na kupelekwa katika Shule ya Maadilisho Irambo, Mbeya ikilinganishwa na watoto 13 wavulana mwaka 2022. Kupungua kwa watoto waliohukumiwa kulitokana na Programu ya Marekebisho ya Tabia inayotekelezwa katika ngazi ya halmashauri.

**Ukatili wa Kijinsia**

416. Mwaka 2023, Serikali iliendelea na juhudi za kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto. Katika kipindi hicho, matukio 38,314 ya ukatili wa kijinsia yalitolewa taarifa ikilinganishwa na matukio 30,566 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 25.3. Matukio hayo ni pamoja na ubakaji, mauaji ya vikongwe, kujeruhi, shambulio la aibu, ukeketaji na lugha za matusi. Aidha, matukio 17,969 ya ukatili dhidi ya watoto yalitolewa taarifa mwaka 2023 ikilinganishwa na matukio 12,163 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 47.7. Matukio hayo ni pamoja na ubakaji, ulawiti, kutupa watoto, utelekezaji wa familia, shambulio la aibu na mimba za utotoni. Makosa ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yaliyotolewa taarifa yaliongezeka kutokana na juhudi za Serikali na wadau mbalimbali za kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa za matukio ya ukatili ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

**Huduma za Ustawi kwa Wazee**

417. Mwaka 2023, huduma za msingi ikiwemo chakula, malazi, mavazi na huduma za afya ziliendelea kutolewa kwa wazee wasiojiweza wanaoishi katika makazi 14 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali. Katika kipindi hicho, wazee 245 (wanawake 145 na wanaume 100) walipatiwa huduma za msingi ikilinganishwa na wazee 272 mwaka 2022.

**Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

418. Mwaka 2023, Serikali ilisajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,484 ikilinganishwa na Mashirika 1,351 yaliyosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Ongezeko hilo lilitokana na matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika usajili wa Mashirika. Kati ya Mashirika yaliyosajiliwa, Mashirika 63 yalikuwa ya kimataifa, 1,357 ngazi ya Taifa, 38 ngazi ya mkoa na 26 ngazi ya wilaya.

419. Mwaka 2023, utendaji kazi wa Mashirika 2,824 Yasiyo ya Kiserikali ulifuatiliwa ikilinganishwa na mashirika 1,605 mwaka 2022. Kati ya hayo, Mashirika 397 yalitembelewa na Mashirika 2,427 yalifikiwa kupitia mkutano. Ufuatiliaji huo ulibaini kuwa, Mashirika mengi yalitekeleza miradi yenye tija kwa jamii ikiwemo: ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo kwa shule za msingi na sekondari; ujenzi wa vituo vya afya; elimu kuhusu haki ya wanawake kumiliki ardhi na rasilimali; kuongeza thamani katika mazao ya kilimo; uwezeshaji wananchi kiuchumi; elimu ya afya, ulinzi na usalama wa mtoto; na utoaji wa bima ya afya ya jamii. Aidha, mikataba 500 ya fedha ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ilikaguliwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mikataba 955 mwaka 2022. Vile vile, ukaguzi wa mikataba ya fedha ulibaini kuwa shilingi bilioni 671.44 zilipokelewa mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,081.50 mwaka 2022.

**Jedwali Na. 71: IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA**

| Mwaka | Wagonjwa wa Nje | | | | Jumla ya Wagonjwa waliolazwa | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hospitali | Zahanati | Vituo vya Afya | Jumla Wagonjwa wa nje | | |
| 2007 | 1,842,671 | 28,328,093 | 4,520,026 | 34,690,790 | 2,979,115 | 37,669,905 |
| 2008 | 1,934,805 | 29,744,498 | 4,746,027 | 36,425,330 | 3,128,071 | 39,553,401 |
| 2009 | 2,128,286 | 32,718,948 | 5,220,630 | 40,067,864 | 3,440,870 | 43,508,734 |
| 2010 | 2,341,114 | 35,990,843 | 5,742,693 | 44,074,650 | 3,784,957 | 47,859,607 |
| 2011 | 2,622,048 | 39,917,117 | 6,431,816 | 48,970,981 | 4,239,152 | 53,210,133 |
| 2012 | 2,815,529 | 41,333,522 | 6,657,817 | 50,806,868 | 4,388,108 | 55,194,976 |
| 2013 | 2,903,275 | 42,682,479 | 6,873,056 | 52,458,810 | 4,529,971 | 56,988,781 |
| 2014 | 5,910,725 | 14,008,692 | 475,295 | 20,394,712 | 1,665,935 | 22,060,647 |
| 2015 | 4,480,781 | 25,072,487 | 6,006,466 | 35,559,734 | 1,858,956 | 37,418,690 |
| 2016 | 4,984,645 | 20,859,281 | 6,515,219 | 32,359,145 | 1,775,835 | 34,134,980 |
| 2017 | 5,266,252 | 21,115,639 | 7,050,725 | 33,432,616 | 1,650,224 | 35,082,840 |
| 2018 | 4,675,045 | 27,473,506 | 8,903,461 | 41,052,012 | 1,359,264 | 42,411,276 |
| 2019 | 9,821,148 | 26,500,182 | 10,153,322 | 46,474,652 | 1,852,720 | 48,327,372 |
| 2020 | 10,150,504 | 22,154,653 | 9,741,820 | 42,046,977 | 1,852,720 | 43,899,697 |
| 2021 | 11,348,037 | 19,705,594 | 9,219,985 | 40,273,616 | 1,651,001 | 41,924,617 |
| 2022 | 27,290,723 | 1,486,649 | 12,567,881 | 41,345,253 | 1,626,308 | 42,971,561 |
| 2023 | 14,047,587 | 9,399,664 | 19,959,991 | 43,407,242 | 1,757,240 | 45,164,482 |

**Chanzo:** Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,Jinsia, Wazee na Watoto

**Jedwali Na. 72: IDADI YA VITANDA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NCHINI**

| Aina ya Vituo | 2022 | | | | 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Shirika la kujitolea/ Dini | Binafsi | Jumla | Serikali | Shirika la kujitolea/ Dini | Binafsi | Jumla |
| Hospitali ya Taifa | 1,731 | - | - | 1,731 | 1,731 | - | - | 1,731 |
| Hospitali Maalum za Kibingwa | 1,396 | - | - | 1,396 | 1,305 | - | - | 1,305 |
| Hospitali za Rufaa za Kanda | 1,059 | 860 | - | 1,919 | 1,446 | - | - | 1,446 |
| Hospitali za Mikoa | 6,688 | - | - | 6,688 | 14,226 | - | - | 14,226 |
| Hospitali za Wilaya | 3,033 | 7,425 | - | 10,458 | 16,541 | - | - | 16,541 |
| Hospitali nyingine | 14,510 | 1,086 | 21,412 | 37,008 | 680 | 17,396 | 5,001 | 23,077 |
| Vituo vya Afya | 17,151 | 1,695 | 5,968 | 24,814 | 23,066 | 5,380 | 2,334 | 30,780 |
| Zahanati | 14,811 | 158 | 5,704 | 20,673 | 27,750 | 4,896 | 3,748 | 36,394 |
| **Jumla** | **60,379** | **11,224** | **33,084** | **104,687** | **86,745** | **27,672** | **11,083** | **125,500** |

**Chanzo:** Wizara ya Afya



## Sehemu ya Tatu

# Maendeleo Katika Maeneo Mengine

# SURA YA 18

## MASUALA MTAMBUKA NA MAENDELEO YA WATU

### MASUALA MTAMBUKA

**Mazingira**

420. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 kwa kufanya mapitio ya Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2022 na kuhamasisha uwekezaji katika biashara ya kaboni. Aidha, kampuni za uwekezaji kwenye biashara ya kaboni zilifikia 35 mwaka 2023 kutoka kampuni 6 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na mapitio ya Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2022, uwepo wa Mwongozo wa Biashara ya Kaboni na elimu kwa wawekezaji kuhusu umuhimu na faida ya biashara ya kaboni. Hadi Desemba 2023, shilingi bilioni 33 zilipatikana katika biashara ya kaboni.

421. Mwaka 2023, miradi 1,260 ilipata hati ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa ikilinganishwa na miradi 1,079 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 16.8. Hii ilitokana na matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa maombi ya vyeti vya TAM uliowezesha kupunguza muda uliotumika kupata cheti kutoka siku 90 hadi siku 60. Aidha, hati tatu (3) za Tathmini ya Athari kwa Mazingira Kimkakati (TMK) zilitolewa mwaka 2023 ikilinganishwa na hati mbili (2) zilizotolewa mwaka 2022. Vile vile, vyeti 281 vya ukaguzi wa mazingira vilitolewa mwaka 2023 ikilinganishwa na vyeti 199 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 41.2.

**Jedwali Na. 18.1: Vyeti vya Tathmini na Ukaguzi wa Mazingira Mwaka 2022 - 2023**

| Na. | Aina ya Vyeti | 2022 | 2023 |
|---|---|---:|---:|
| 1 | Vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira Kimkakati | 2 | 3 |
| 2 | Vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira | 1,079 | 1,260 |
| 3 | Vyeti vya ukaguzi wa mazingira | 199 | 281 |
| | **Jumla** | **1,280** | **1,544** |

**Chanzo:** Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

422. Mwaka 2023, vibali 256 vilitolewa kwa wafanyabiashara wanaojihusisha na ukusanyaji, uhifadhi, usafirishaji na uingizaji wa taka hatarishi ambazo hurejelezwa na kutumika kama malighafi katika shughuli za uzalishaji viwandani ikilinganishwa na vibali 204 vilivyotolewa mwaka 2022.

423. Mwaka 2023, miti iliyopandwa iliongezeka kwa asilimia 43.8 na kufikia miti 266,970,203 kutoka miti 185,636,155 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, miti 211,805,184 ilistawi, sawa na asilimia 79.3. Ongezeko la upandaji miti lilitokana na elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

**Ulinzi na Usalama wa Raia**

424. Mwaka 2023, makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa na wananchi yalikuwa 53,640 ikilinganishwa na makosa 54,123 mwaka 2022. Kupungua kwa makosa ya jinai kulitokana na Serikali kuendelea kufanya doria, misako na operesheni za kubaini, kuzuia, kutanzua na kupambana na uhalifu katika maeneo ya mijini, vijijini, barabara kuu na mipakani pamoja na elimu inayoendelea kutolewa kwa umma kuhusu utekelezaji wa dhana ya ulinzi shirikishi katika kudhibiti uhalifu. Kati ya hayo, makosa 13,748 yalikuwa dhidi ya binadamu, makosa 22,552 ya kuwania mali, makosa 862 ya uhalifu wa kifedha na makosa 16,478 yalikuwa dhidi ya maadili ya jamii. Aidha, makosa madogo yaliyotolewa taarifa yalikuwa 563,462 mwaka 2023 ikilinganishwa na makosa 520,758 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Makosa yaliyotolewa taarifa yalifanyiwa kazi kulingana na sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

425. Mwaka 2023, matukio ya ajali yaliyotolewa taarifa yalikuwa 1,759 (barabarani 1,733, majini 22 na angani 4) ikilinganishwa na matukio 1,732 mwaka 2022. Kuongezeka kwa ajali kulitokana na ubovu wa vyombo vya usafiri, uzembe wa madereva barabarani na sababu za kimazingira. Aidha, matukio ya ajali 1,118 yalisababisha vifo vya watu 1,647 na majeruhi 2,716 mwaka 2023 ikilinganishwa na matukio ya ajali 1,064 yaliyosababisha vifo vya watu 1,545 na majeruhi 2,278 mwaka 2022. Hatua mbalimbali ziliendelea kuchukuliwa kupunguza ajali za barabarani ikiwemo: ukaguzi rasmi na usio rasmi katika vituo vya mabasi, magari makubwa na madogo; kufanya doria katika barabara kuu na operesheni endelevu; ukaguzi wa shule za udereva ili kuhakikisha zinakidhi viwango vya taaluma kwa madereva wa vyombo vya moto; na kuendelea kushirikiana na wadau wa usalama barabarani ili kuimarisha usimamizi wa sheria.

426. Mwaka 2023, wafungwa na mahabusu katika magereza yote nchini walifikia 26,994 (wafungwa 18,245 na mahabusu 8,749) ikilinganishwa na wafungwa na mahabusu 32,058 mwaka 2022. Idadi hiyo inaendana na uwezo wa magereza wa kuhifadhi wafungwa na mahabusi 29,902. Kupungua kwa wafungwa na mahabusu kulitokana na kupungua kwa vitendo vya kiuhalifu sambamba na kuachiwa huru kwa wafungwa 2,244 kupitia msamaha wa Rais na kutolewa kwa vifungo vya nje kwa wafungwa 621 mwaka 2023 ikilinganishwa na wafungwa 5,457 walioachiwa huru na wafungwa 1,052 waliotumikia vifungo vya nje mwaka 2022.

427. Mwaka 2023, miito 2,079 ya matukio ya moto ilipokelewa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ikilinganishwa na miito 2,059 iliyopokelewa mwaka 2022. Aidha, miito ya maokozi iliyopokelewa ilikuwa 1,242 ikilinganishwa na miito 635 mwaka 2022. Hii ilichangiwa na elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya namba ya simu 114 ya dharura. Vile vile, elimu ya kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto ilitolewa kupitia vipindi 482 vya redio na vipindi 125 vya luninga. Kwa upande mwingine, kaguzi za kinga na

tahadhari dhidi ya moto zilifanyika katika maeneo 60,482 mwaka 2023 ikilinganishwa na maeneo 60,182 yaliyofanyiwa kaguzi mwaka 2022.

428. Mwaka 2023, wageni walioingia nchini kwa vibali halali walifikia 1,727,486 ikilinganishwa na wageni 1,392,939 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 24.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za utalii na uwekezaji kulikochagiwa na Programu Maalum ya Tanzania - *The Royal Tour* sambamba na kuimarishwa kwa mazingira ya kuvutia uwekezaji wa nje. Aidha, wageni 1,564,277 walitoka nchini kwenda nchi mbalimbali duniani kwa vibali halali mwaka 2023 ikilinganishwa na wageni 1,237,984 mwaka 2022. Vile vile, hati za kusafiria zilizotolewa na Idara ya Uhamiaji kwa watanzania zilikuwa 151,774 ikilinganishwa na hati 107,130 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 41.7. Ongezeko hilo lilichangiwa na jitihada za Serikali katika kufungulia uchumi na uhitaji wa watanzania kwenda nje ya nchi kwa ajili ya biashara, masomo, mikutano, ajira pamoja na matibabu.

429. Mwaka 2023, wageni 304 walipewa uraia na Idara ya Uhamiaji ikilinganishwa na wageni 150 waliopewa uraia mwaka 2022. Aidha, wahamiaji haramu 26,542 walikamatwa ikilinganishwa na wahamiaji haramu 23,902 waliokamatwa mwaka 2022. Hii ni kutokana na, kukamata wahamiaji walioingia nchini kwa njia zisizo rasmi, kuishi na kufanya kazi bila kufuata sheria, taratibu na kanuni za uhamiaji kama vile kuishi na kibali kilichoisha muda wa matumizi, kufanya kazi bila kuwa na vibali stahiki au kujishughulisha na kazi yoyote kinyume na kibali walichopewa. Vile vile, hati 20,191 za ukaazi zilitolewa mwaka 2023 ikilinganishwa na hati za ukaazi 16,894 zilizotolewa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 19.5. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa uwekezaji, hususan kwenye sekta ya uzalishaji. Kwa upande mwingine, wakimbizi 19,416 walirejeshwa katika nchi zao kwa hiari kutokana na kuimarika kwa hali ya amani katika nchi hizo mwaka 2023 ikilinganishwa na wakimbizi 5,808 waliorejeshwa nchini mwao mwaka 2022. Katika kipindi hicho, wakimbizi 7,890 walihamishiwa nchi ya tatu ikilinganishwa na wakimbizi 3,522 waliohamishiwa nchi ya tatu mwaka 2022.

**Utambuzi na Usajili wa Watu**

430. Hadi Desemba 2023, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa - NIDA ilikuwa imesajili na kutambua watu 24,376,028 ikilinganishwa na watu 23,630,813 waliotambuliwa na kusajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.2. Aidha, Mamlaka ilitoa namba za utambulisho 20,608,213 ikilinganishwa na namba za utambulisho 19,885,966 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Ongezeko hilo lilitokana na mkakati wa kuhakikisha kila mwananchi anayesajiliwa anapata namba ili kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali. Hadi Desemba 2023, vitambulisho 18,982,537 vilizatolewa ikilinganishwa na vitambulisho 11,201,666 vilivyotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la

asilimia 69.5. Ongezeko hilo lilitokana na upatikanaji wa kadighafi kwa ajili ya kuzalishia vitambulisho vya Taifa.

431. Hadi Desemba 2023, ofisi 153 za usajili katika ngazi ya wilaya ziliunganishwa na Kituo Kikuu cha Kanzidata ikilinganishwa na ofisi 141 za usajili ngazi ya wilaya katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.5. Aidha, taasisi 93 (taasisi za umma 43 na taasisi binafsi 50) ziliunganishwa katika Mfumo wa Usajili na Utambuzi ikilinganishwa na taasisi 70 zilizounganishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 32.9. Hii ilitokana na watoa huduma kuendelea kujiunga na Mfumo wa Mamlaka kwa lengo la kurahisisha uhakiki wa taarifa za watu ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma na kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi.

**Udhibiti wa Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu**

432. Mwaka 2023, waathirika 133 wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu waliokolewa na kutafutiwa hifadhi na baadhi yao kuunganishwa na familia zao ikilinganishwa na waathirika 151 waliookolewa mwaka 2022. Aidha, kesi za usafirishaji haramu wa binadamu zilizofunguliwa mwaka 2023 zilikuwa tano (5) ikilinganishwa na kesi 13 zilizofunguliwa mwaka 2022. Kati ya hizo, kesi mbili (2) zilitolewa hukumu ikilinganishwa na kesi tatu (3) mwaka 2022.

**Usajili wa Jumuiya**

433. Mwaka 2023, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya iliendelea kusajili na kusimamia uendeshaji wa jumuiya za kidini na jumuiya zisizo za kidini kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337 kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 3 ya Mwaka 2019. Jumuiya hizo ni muungano wa watu kumi au zaidi ulioanzishwa kwa ajili ya kutimiza malengo ya kitaaluma, kijamii, kiutamaduni, kidini au kiuchumi yenye kulenga kuwanufaisha au kuwastawisha wanachama wake. Katika kipindi hicho, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya ilisajili jumla ya jumuiya 412 ikilinganishwa na jumuiya 452 zilizosajiliwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 8.8. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa vigezo vya usajili, uendeshaji na usimamizi wa Jumuiya kwa lengo la kudhibiti uwezekano wa Jumuiya kutenda makosa ya jinai kama vile utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa biashara haramu ya silaha.

**Usajili, Ufilisi na Udhamini**

434. Mwaka 2023, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini - RITA ilisajili vizazi 1,444,795 ikilinganishwa na vizazi 1,361,608 vilivyosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko wa asilimia 6.1. Katika kipindi hicho, watoto 863,206 walisajiliwa kupitia Mpango wa Usajili kwa Watoto Walio Chini ya Umri wa Miaka Mitano ikilinganishwa na watoto 643,943 waliosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 34.1. Aidha, Wakala ulisajili matukio ya vifo 35,663 mwaka 2023 ikilinganishwa na matukio 35,183 ya

vifo yaliyosajiliwa mwaka 2022. Vile vile, maombi 205,693 ya usajili na uhakiki wa nyaraka yalipokelewa kupitia mfumo wa usajili wa vizazi na vifo na uhakiki wa nyaraka (e - HUDUMA) mwaka 2023 ikilinganishwa na maombi 205,666 yaliyopokelewa mwaka 2022.

435. Mwaka 2023, Wakala ulisajili hati za viapo vya ndoa 45,455 ikilinganishwa na hati za viapo vya ndoa 51,011 mwaka 2022. Aidha, hati za talaka 866 zilisajiliwa mwaka 2023 ikilinganishwa na hati za talaka 447 zilizosajiliwa mwaka 2022. Vile vile, hati za watoto wa kuasili 32 zilisajiliwa mwaka 2023 ikilinganishwa na hati 19 zilizosajiliwa mwaka 2022. Katika kipindi hicho, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Uandikishaji Vizazi na Vifo, Sura 108 ili kuruhusu watoto wa kuasili kupata vyeti vya kuzaliwa vikiwa na majina ya wazazi waliowaasili na kuepusha unyanyapaa kwa watoto hao.

436. Mwaka 2023, Wakala ulitoa hati 84 za miunganisho ya wadhamini ikilinganishwa na hati 40 zilizotolewa mwaka 2022. Aidha, bodi za wadhamini 5,987 zilisajiliwa katika mfumo wa usajili wa kielektroniki mwaka 2023 ikilinganishwa na bodi za wadhamini 5,594 zilizosajiliwa mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kuanzishwa kwa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa bodi za wadhamini. Vile vile, wosia 156 ziliandikwa na kuhifadhiwa mwaka 2023 ikilinganishwa na wosia 139 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa kampeni ya elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuandika na kutunza wosia kama sehemu ya kuepusha migogoro ya wanafamilia pindi mwenye mali anapofariki.

**Maendeleo ya Sheria na Mahakama**

437. Mwaka 2023, miswada 26 ya mapendekezo ya kutungwa kwa sheria mpya iliandaliwa. Kati ya hiyo, miswada 14 ilipitishwa kuwa sheria ikilinganishwa na miswada 11 iliyopitishwa mwaka 2022. Aidha, sheria ndogo 569 ziliandaliwa na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali mwaka 2023 ikilinganishwa na sheria ndogo 785 zilizoandaliwa na kuchapishwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 27.5. Upungufu huo ulitokana na uboreshwaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kuondoa taratibu zinazokwamisha au kuchelewesha uanzishaji wa biashara. Vile vile, afua nyingine zilizotekelezwa kwa lengo la kuimarisha mfumo wa sheria zilikuwa: kutafsiri sheria kutoka lugha ya kiingereza kwenda lugha ya kiswahili; kufanya mapitio ya sheria zote kuu kwa ajili ya urekebu wa sheria hizo; na kurahisisha utumiaji wa sheria hizo ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kutokana na ufasaha wa sheria zenyewe.

438. Mwaka 2023, mikataba 1,812 ya kitaifa na kimataifa ilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na mikataba 1,878 iliyofanyiwa upekuzi mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 3.5. Aidha, Hati za Makubaliano 511 zilifanyiwa upekuzi mwaka 2023 ikilinganishwa na Hati za Makubaliano 265 zilizofanyiwa upekuzi mwaka 2022, sawa na

ongezeko la asilimia 92.8. Mikataba hiyo ilihusisha masuala ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo pamoja na utoaji wa huduma za jamii kama vile, ujenzi wa shule, hospitali na barabara.

439. Mwaka 2023, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipokea majalada 1,024 ya uchunguzi wa tuhuma za rushwa na matumizi mabaya ya madaraka kutoka TAKUKURU. Kati ya hayo, majalada 475 sawa na asilimia 46.4 yaliandaliwa hati za mashtaka ili kuziwasilisha mahakamani, majalada 129 (asilimia 12.6) yalifungwa na majalada 343 (asilima 33.5) yalirejeshwa kwa upelelezi zaidi. Aidha, kati ya kesi za rushwa 126 zilizokuwa mahakamani mwaka 2023, kesi 45 zilisikilizwa na kuamuliwa mahakamani na kesi 81 ziliendelea kusikilizwa na mahakama. Vile vile, kesi 6,990 zinazohusu makosa ya nyara za Serikali, madini, maliasili nyingine, madawa ya kulevya, utakatishaji wa fedha na uhalifu wa mtandaoni ziliendeshwa mahakamani. Kati ya hizo, kesi 4,409 ziliamuliwa na washitakiwa 2,951 walitiwa hatiani na kupewa adhabu za vifungo na faini na washtakiwa 475 waliachiwa huru.

440. Mwaka, 2023 Mahakama ya Tanzania iliendelea kusogeza huduma za mahakama karibu na wananchi kwa: kukamilisha ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kwimba na Wilaya ya Liwale; kukamilisha ujenzi wa mahakama za mwanzo za Usevya (Mlele), Nyakibimbili (Bukoba), Mahenge (Kilolo) na Luilo (Ludewa); na kuendelea na ukarabati wa jengo la Mahakama Kuu Dodoma. Aidha, Mahakama ya Tanzania, iliboresha mfumo wa utoaji huduma kwa njia za kielektroniki unaolenga kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa huduma za Mahakama kwa umma. Vile vile, Mahakama ilikamilisha ujenzi wa mfumo wa Akili Mnemba/Bandia ili kurahisisha usikilizaji wa mashauri na utoaji wa hukumu kwa wakati.


**Utawala Bora**

441. Mwaka 2023, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilifanya chambuzi 806 za mifumo ya utendaji kazi na utoaji wa huduma ikilinganishwa na chambuzi 746 zilizofanyika mwaka 2022. Aidha, TAKUKURU ilikagua miradi ya maendeleo 1,800 ikilinganishwa na miradi 988 iliyokaguliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 82.2. Miradi hiyo ilijumuisha sekta za utawala, nishati, ujenzi, maji, fedha, elimu, afya, kilimo, usafirishaji, na viwanda. Ukaguzi huo, ulibaini miradi 171 kuwa na kasoro kwenye utekelezaji na kuanzishiwa uchunguzi.

442. Mwaka 2023, TAKUKURU ilifungua kesi za rushwa 600 katika mahakama mbalimbali nchini ikilinganishwa na kesi 1,306 zilizofunguliwa mwaka 2022. Aidha, kesi 496 ziliamuliwa mahakamani mwaka 2023 ambapo Jamhuri ilishinda kesi 336 ikilinganishwa na kesi 822 zilizoamuliwa mahakamani na Jamhuri kushinda kesi 482 mwaka 2022.

443. Taarifa ya *Transparency International* (TI) ya mwaka 2023 inaonesha kuwa Tanzania ilipata alama 40 kati ya alama 100 ya Fahirisi ya Rushwa mwaka 2023 ikilinganishwa na alama 38 mwaka 2022. Aidha, alama ilizopata Tanzania ipo katika nafasi nzuri zaidi ikilinganishwa na wastani wa alama 33 ambazo Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zilipata. Vile vile, nafasi ya Tanzania katika kupambana na vitendo vya rushwa iliimarika na kufikia nafasi ya 87 kati ya nchi 180 mwaka 2023 ikilinganishwa na nafasi ya 94 mwaka 2022.

**Kielelezo Na. 18.1: Mwenendo wa Fahirisi ya Rushwa katika Sekta ya Umma Mwaka 2012 - 2023**




**HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU**

444. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutekeleza sera, programu na miradi mbalimbali yenye lengo la kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo ya watu. Jitihada hizo zinaongozwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

**Jitihada za Kupunguza Umaskini**

445. Mwaka 2023, Serikali iliendelea na kuboresha ustawi wa jamii na kupunguza umaskini uliokithiri kupitia programu mbalimbali ikiwemo Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini - TASAF. Utekelezaji wa Mpango huo, ulihusisha uhawilishaji wa fedha kwa kaya maskini; kutoa ajira za muda mfupi kwa kaya za walengwa; na kuhamasisha uundaji wa vikundi vya kuweka akiba, kukopeshana na kuwekeza kwenye miradi ya uzalishaji mali kupitia vikundi hivyo.

446. Hadi Desemba 2023, kaya zinazonufaika na Mpango zilikuwa 1,371,916 zenye wanufaika 6,938,481 ikilinganishwa na kaya 1,371,038 zenye wanufaika 6,596,820 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na marekebisho ya taarifa kwa baadhi ya kaya zilizokuwa kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya tathmini ya Mpango. Kati ya wanufaika wa Mpango, wanawake walikuwa 3,600,267 (asilimia 51.9) na wanaume 3,338,214 (asilimia 48.1). Aidha, watoto wenye umri wa hadi miaka mitano (miaka 0-5) ambao wanatakiwa kuhudhuria kliniki walikuwa 763,233, sawa na asilimia 11.0 ya wanufaika wote. Vile vile, wanufaika waliokuwa shule za msingi na sekondari wenye umri kati ya miaka 6 hadi 18 walikuwa 2,914,162 (asilimia 42.0) na wanufaika wenye umri stahiki wa kushiriki katika shughuli za uzalishaji (miaka 19 - 60) walikuwa 2,567,238 (asilimia 37.0). Katika kipindi hicho, wanufaika wenye umri wa zaidi ya miaka 60 walikuwa 693,848, sawa na asilimia 10.0 ya wanufaika wote.

**Jedwali Na. 18.2: Wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Mwaka 2022 - 2023**

| **Jinsia** | **Idadi ya Wanufaika** | | **Idadi ya Wanufaika (Umri)** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2022** | **2023** | **0 - 5** | **Jun-18** | **19 - 60** | **Zaidi ya 60** |
| Wanaume | 3,240,199 | 3,338,214 | 406,778 | 1,606,407 | 1,064,053 | 260,976 |
| Wanawake | 3,356,621 | 3,600,267 | 356,455 | 1,307,755 | 1,503,185 | 432,872 |
| **Jumla** | **6,596,820** | **6,938,481** | **763,233** | **2,914,162** | **2,567,238** | **693,848** |
| **Asilimia ya wanufaika wote** | | | **11.0** | **42.0** | **37.0** | **10.0** |

**Chanzo:** Mfuko wa Maendeleo ya Jamii


447. Hadi Desemba 2023, shilingi bilioni 1,834.33 zilitolewa kupitia uhawilishaji fedha kwa wanufaika wote ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,312.80 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 39.7. Hii inatokana na kuongezeka kwa idadi ya wanufaika.

448. Hadi Desemba 2023, vikundi 56,518 vyenye wanachama 778,940 viliundwa kutoka katika kaya maskini ikilinganishwa na vikundi 43,302 vyenye wanachama 587,397 vilivyoundwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la vikundi kwa asilimia 30.5. Ongezeko hilo lilitokana na wananchi kuhamasika kuunda vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali. Aidha, shilingi bilioni 3.8 zilikopeshwa kwa wanachama wa vikundi kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3.1 zilizokopeshwa mwaka 2022. Vile vile, kaya 605,227 zilianzisha miradi midogo ya kujiongezea kipato kupitia ruzuku na mikopo iliyotolewa ili kujikwamua kiuchumi.

**Maendeleo ya Watu**

449. Kwa mujibu wa Taarifa ya Dunia ya Maendeleo ya Watu ya Mwaka 2023 iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa - UNDP, Tanzania ilishika nafasi ya 167 kati ya nchi 193 katika maendeleo ya watu mwaka 2022 ikilinganishwa na nafasi ya 160 mwaka 2021. Hii ilichangiwa na kupungua kwa baadhi ya viashiria muhimu vya maendeleo ya watu ikiwemo wastani wa pato la mtu kwa kuzingatia uwezo wa kufanya manunuzi (kwa kizio cha mwaka 2017), miaka inayotarajiwa kwa mwanafunzi kuwa shuleni na wastani wa miaka ya kuwa shuleni. Aidha, Fahirisi ya Maendeleo ya Watu - HDI ilifikia 0.532 mwaka 2022 ikilinganishwa na 0.529 mwaka 2021. Fahirisi hii inapimwa kwa kiwango cha kuanzia sifuri ambacho ni kiwango cha chini kabisa cha maendeleo ya watu hadi 1.0 ambacho ni kiwango cha juu sana cha maendeleo ya watu. Kuongezeka kwa fahirisi ya maendeleo ya watu kulitokana na Serikali kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za msingi ikiwemo afya, elimu na maji pamoja na kuboresha viwango vya maisha ya watanzania. Vile vile, wastani wa umri wa kuishi kwa mtanzania ulikuwa miaka 66.8 mwaka 2022 ikilinganishwa na miaka 66.2 mwaka 2021.

**Kielelezo Na. 18.2: Mwenendo wa Fahirisi ya Maendeleo ya Watu, Mwaka 1990 - 2022**



## SURA YA 19

## UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

### Usajili wa Miradi ya Uwekezaji

450. Mwaka 2023, Kituo cha Uwekezaji Tanzania - TIC kilisajili miradi 526 ikilinganishwa na miradi 293 iliyosajiliwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 79.5. Kati ya hiyo, miradi 182 ilikuwa ya watanzania, miradi 214 ya wageni na miradi 130 ya ubia kati ya watanzania na wageni. Aidha, thamani ya miradi iliyosajiliwa ilikuwa dola za Marekani milioni 5,720.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,537.7 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 26.1. Ongezeko la thamani na idadi ya miradi iliyosajiliwa lilichangiwa na juhudi za Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji, ikiwemo kutungwa kwa sheria mpya ya uwekezaji Namba 10 ya mwaka 2022. Sheria hiyo imeweka vivutio vya uwekezaji kwa miradi ya ukarabati na upanuzi ambapo kati ya miradi 526 iliyosajiliwa mwaka 2023, miradi 57 ilikuwa ya ukarabati na upanuzi. Vile vile, miradi iliyosajiliwa ilikuwa na fursa za ajira 137,010 mwaka 2023 ikilinganishwa na fursa za ajira 40,889 mwaka 2022.

### Mgawanyiko wa Usajili wa Miradi Kisekta

451. Mwaka 2023, sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa kusajili miradi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 1,688.51 ikifuatiwa na sekta ya usafirishaji mizigo dola za Marekani milioni 1,322.53 na sekta ya ujenzi wa majengo ya biashara dola za Marekani milioni 1,054.21. Katika kipindi hicho, sekta iliyosajili idadi kubwa ya miradi ilikuwa uzalishaji viwandani miradi 208 ikifuatia usafirishaji mizigo miradi 111 na utalii miradi 58.

**Jedwali Na. 19.1: Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa Mwaka 2023**

| Na. | Sekta | Miradi Iliyosajiliwa | | | | Fursa za ajira | Thamani (Dola za Marekani milioni) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Watanzania | Wageni | Ubia | Jumla | | |
| 1 | Kilimo | 14 | 21 | 13 | 48 | 30,718 | 793.1 |
| 2 | Mawasiliano | 0 | 1 | 1 | 2 | 43 | 28.52 |
| 3 | Utalii | 23 | 19 | 16 | 58 | 4,103 | 188.648 |
| 4 | Uzalishaji viwandani | 49 | 111 | 48 | 208 | 26,563 | 1,688.51 |
| 5 | Ujenzi majengo ya biashara | 14 | 29 | 14 | 57 | 3,596 | 1,054.21 |
| 6 | Usafirishaji mizigo | 66 | 22 | 23 | 111 | 18,780 | 1,322.53 |
| 7 | Huduma | 4 | 7 | 9 | 20 | 1,832 | 282.66 |
| 8 | Rasilimali Watu | 3 | 1 | 2 | 6 | 443 | 7.08 |
| 9 | Madini | 4 | 0 | 2 | 6 | 495 | 47.52 |
| 10 | Nishati | 1 | 1 | 1 | 3 | 118 | 58.22 |
| 11 | Miundombinu ya kiuchumi | 4 | 2 | 1 | 7 | 50,319 | 249.38 |
| | **Jumla** | **182** | **214** | **130** | **526** | **137,010** | **5,720.38** |

**Chanzo**: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

**Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa**

452. Mwaka 2023, Mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa kuvutia asilimia 40.5 ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa, ikifuatiwa na Pwani (asilimia 16.9), Arusha (asilimia 5.7), Mwanza (asilimia 4.4) na Dodoma (asilimia 4.2). Hii ilitokana na mikoa hiyo kuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji, hususan miundombinu bora pamoja na uwepo wa Ofisi za Kanda za Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

**Jedwali Na. 19.2: Mgawanyiko wa Miradi Iliyosajiliwa Kimkoa Mwaka 2023**

| Mkoa | Sekta | | | | | | | | | | | Jumla ya Miradi Kimkoa | Asilimia ya Mgawanyo kimkoa (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kilimo | Ujenzi wa Majengo ya Biashara | Miundombinu ya Uchumi | Nishati | Rasilimali watu | Uzalishaji Viwandani | Madini na Petroli | Huduma | Mawasiliano ya Simu | Utalii | Usafirishaji mizigo | | |
| Arusha | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 15 | 7 | 30 | 5.7 |
| Pwani | 10 | 9 | 0 | 0 | 0 | 55 | 1 | 1 | 0 | 4 | 9 | 89 | 16.9 |
| Dar es Salaam | 3 | 32 | 6 | 0 | 4 | 69 | 0 | 12 | 2 | 12 | 73 | 213 | 40.5 |
| Dodoma | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 13 | 0 | 0 | 0 | 3 | 5 | 22 | 4.2 |
| Geita | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 8 | 1.5 |
| Iringa | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 3 | 9 | 1.7 |
| Kagera | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 8 | 1.5 |
| Katavi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0.4 |
| Kigoma | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0.4 |
| Kilimanjaro | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 4 | 5 | 17 | 3.2 |
| Lindi | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 7 | 1.3 |
| Manyara | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 8 | 1.5 |
| Mara | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 10 | 1.9 |
| Mbeya | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 9 | 1.7 |
| Morogoro | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 9 | 1.7 |
| Mtwara | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | | 4 | 0.8 |
| Mwanza | 3 | 3 | 0 | 0 | 1 | 12 | | 2 | | 1 | 1 | 23 | 4.4 |
| Njombe | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0.6 |
| Rukwa | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0.4 |
| Ruvuma | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 1 | 0 | 1 | 2 | 10 | 1.9 |
| Shinyanga | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 10 | 1.9 |
| Simiyu | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 6 | 1.1 |
| Singida | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 | 0.8 |
| Songwe | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0.4 |
| Tabora | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0.4 |
| Tanga | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 2 | 0 | 2 | 2 | 17 | 3.2 |
| **Jumla** | **48** | **57** | **7** | **3** | **6** | **208** | **6** | **20** | **2** | **58** | **111** | **526** | **100.0** |

**Chanzo**: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

**Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje**

453. Kwa mujibu wa Taarifa ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2023, uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 9.1 na kufikia dola za Marekani milioni 20,644.4 mwaka 2022 kutoka dola za Marekani milioni 18,924.3 mwaka 2021. Kati ya uwekezaji huo, uwekezaji wa moja kwa moja ulifikia dola za Marekani milioni 17,137.4, sawa na asilimia 83.0 ya uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje, uwekezaji wa hisa ulifikia dola za Marekani 135.1 (asilimia 0.7) na uwekezaji mwingine dola za marekani 3,371.8 (asilimia 16.3). Aidha, mitaji iliyowekezwa na sekta binafsi kutoka nje ya nchi kwa bei za miaka husika ilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,745.8 mwaka 2022 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,186.8 zilizowekezwa mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 47.1.

**Jedwali Na. 19.3: Uwekezaji kwenye Sekta Binafsi kutoka Nje ya Nchi (Dola za Marekani Milioni) Mwaka 2018 - 2022**


| Aina ya uwekezaji | Kiasi kilichowekezwa | | | | | Limbikizo lililowekezwa | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
| Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka Nje | 971.6 | 1,217.2 | 943.8 | 1,190.5 | 1,437.6 | 14,092.0 | 14,762.9 | 15,612.6 | 15,741.1 | 17,137.4 |
| Uwekezaji wa Hisa | 1.6 | 5.5 | 1.8 | 4.9 | 0.2 | 30.6 | 104.6 | 124.8 | 126.8 | 135.1 |
| Uwekezaji mwingine | 241.3 | 17.3 | -85.5 | -8.6 | 308.1 | 5,233.7 | 2,810.0 | 2,724.5 | 3,056.5 | 3,371.8 |
| **Jumla** | **1,214.4** | **1,240.0** | **860.1** | **1,186.8** | **1,745.8** | **19,356.3** | **17,677.5** | **18,461.9** | **18,924.3** | **20,644.4** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje**

454. Mwaka 2022, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ulikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,437.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,190.5 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 20.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato na muunganiko na ununuzi wa kampuni za kimataifa pamoja na kuimarika kwa ugharamiaji wa miradi ya kimataifa. Aidha, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliongezeka katika mabara yote ambapo nchi za OECD zilikuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wa asilimia 42.7 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 18.9 mwaka 2021. Vile vile, mchango wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje nchi za EAC na SADC ulikuwa asilimia 18 kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 10.9 mwaka 2021.

**Kielelezo Na. 19.1: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje Mwaka 2016 - 2022**




**Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi**

455. Mwaka 2022, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliendelea kujikita zaidi katika shughuli za uchimbaji madini na mawe, fedha na bima pamoja na uzalishaji viwandani. Shughuli hizo zilichangia wastani wa asilimia 88.0 ya uwekezaji wote wa moja kwa moja kutoka nje. Shughuli za uchimbaji madini na mawe ziliongoza kwa kuwa na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje wenye thamani ya dola za Marekani milioni 847.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 596.3 mwaka 2021. Aidha, shughuli za fedha na bima zilifuatia kwa kuwa na uwekezaji wenye thamani ya dola za Marekani milioni 238.4 mwaka 2022 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 132.8 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 79.5. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kukua kwa sekta ya fedha na bima. Vile vile, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje katika shughuli za uzalishaji viwandani ulikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 180.1 mwaka 2022 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 352.0 mwaka 2021.

**Jedwali Na. 19.4: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi Mwaka 2018 - 2022 (Dola za Marekani Milioni)**

| Shughuli za kiuchumi | Kiasi kilichowekezwa | | | | | Limbikizo lililowekezwa | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
| Malazi na Huduma za Chakula | 63.4 | 6.3 | -7.5 | -0.3 | 36.3 | 301.3 | 380.9 | 372.2 | 356.9 | 409.1 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 12.7 | 8.0 | -12.0 | 2.0 | -3.7 | 59.5 | 70.2 | 61.2 | 78.1 | 77.0 |
| Kilimo | 19.0 | 30.3 | 15.5 | 20.8 | 14.3 | 327.9 | 1,582.4 | 1,596.4 | 579.5 | 588.6 |
| Sanaa na Burudani | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.7 | 0.8 | 0.6 | 0.6 | 2.1 | 2.7 |
| Ujenzi | 85.7 | 81.2 | -2.3 | -15.4 | 15.5 | 478.9 | 290.7 | 286.1 | 305.8 | 318.9 |
| Elimu | 4.5 | 3.2 | 0.8 | -2.2 | -0.1 | 8.6 | 9.8 | 10.5 | 9.7 | 7.6 |
| Umeme na Gesi | -0.7 | 8.9 | -22.8 | -2.3 | 1.5 | 20.3 | 59.7 | 36.7 | 13.9 | 24.3 |
| Fedha na Bima | 124.6 | 162.9 | 85.4 | 132.8 | 238.4 | 1,591.8 | 1,274.9 | 1,321.7 | 1,463.7 | 1,695.4 |
| Afya na Huduma za Jamii | -0.7 | 1.3 | -1.2 | 11.3 | -4.4 | 58.6 | 61.6 | 60.0 | 92.7 | 88.0 |
| Habari na Mawasiliano | 199.7 | 274.7 | 60.3 | 34.5 | 89.5 | 1,934.9 | 1,463.2 | 1,517.2 | 1,204.6 | 1,291.3 |
| Uzalishaji Viwandani | 330.5 | 225.5 | 176.2 | 352.0 | 180.1 | 2,827.9 | 2,221.4 | 2,375.1 | 2,412.1 | 2,582.3 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 30.7 | 384.5 | 614.2 | 596.3 | 847.1 | 5,634.6 | 6,589.4 | 7,205.0 | 8,509.1 | 9,312.9 |
| Shughuli za kiataalamu na kisayansi | -0.5 | 1.2 | 1.0 | 0.6 | 0.0 | 21.0 | 19.1 | 20.1 | 0.2 | 0.2 |
| Upangishaji Majengo | -1.9 | -3.3 | -4.0 | -1.2 | -0.2 | 117.5 | 66.8 | 58.3 | 83.5 | 83.3 |
| Usafirishaji na Uhifadhi Mizigo | 12.4 | 13.0 | 26.6 | 18.1 | 12.1 | 150.0 | 191.2 | 213.6 | 129.5 | 141.9 |
| Biashara | 92.3 | 19.3 | 13.4 | 43.5 | 10.7 | 558.5 | 481.0 | 477.9 | 499.8 | 513.8 |
| **Jumla** | **971.6** | **1,217.2** | **943.8** | **1,190.5** | **1,437.6** | **14,092.0** | **14,762.9** | **15,612.6** | **15,741.1** | **17,137.4** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

## Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

456. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI). Katika kipindi hicho, utekelezaji wa Mpango uliwezesha kufutwa au kupunguzwa kwa tozo na ada 66 ikilinganishwa na tozo na ada 39 zilizofutwa au kupunguzwa mwaka 2022. Aidha, mfumo wa *Government Enterprises Service Bus* (GovESB) umeendelea kuwezesha mifumo ya Serikali kuwasiliana kwa urahisi na kubadilishana taarifa na hivyo, kuokoa gharama, muda pamoja na kurahisisha utoaji wa huduma kwa mwananchi na wawekezaji kwa kuwa taarifa zote zinapatikana katika dirisha moja. Hadi Desemba 2023, mifumo 90 ya taasisi 83 za umma iliunganishwa katika mfumo wa GovESB ikilinganishwa na mifumo 50 ya taasisi za umma 45 iliyounganishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

457. Mwaka 2023, Mfumo wa Kieletroniki wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini - GePG ambao umerahisisha taratibu za ulipaji wa ada na tozo mbalimbali za Serikali kwa kuondoa ulazima wa wananchi kufika ofisi mbalimbali kwa ajili ya kufanya malipo na kupunguza muda wa kufanya malipo pamoja na kuongeza uwazi katika ukusanyaji wa mapato uliendelea kuboreshwa. Hadi Desemba 2023, watoa huduma 983 waliunganishwa katika mfumo wa GePG kutoka watoa huduma 900 waliounganishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.2.

458. Mwaka 2023, Serikali ilifanya marekebisho ya sheria mbalimbali zilizolenga kuweka unafuu katika mazingira ya biashara na uwekezaji zilizoidhinishwa na Bunge kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Miscellaneous Amandements) ya mwaka 2023. Sheria zilizofanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 zilikuwa: Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147; Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438; Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290; Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya Mwaka 2015; Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura ya 306; Sheria ya Ardhi, Sura ya 113; Sheria ya Madini, Sura ya 123; Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, Sura ya 82; Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41; Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196; na Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399. Aidha, Sheria zilizofanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Miscellaneous Amandements) zilikuwa: Sheria ya Maendeleo ya Biashara, Sura ya 155; Sheria ya Wakala wa Vipimo, Sura ya 340; Sheria ya Taifa ya Leseni za Viwanda, Sura ya 46; Sheria ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, Sura ya 112; Sheria ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura ya 373; Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Sura ya 420; Sheria ya Nguvu ya Atomu, Sura ya 188; Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Sura ya 159; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147; Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399; Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura ya 263, na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

459. Mwaka 2023, Serikali ilikamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji - *Tanzania Electronic Investment Window* (TelW). Mfumo huo unamuwezesha mwekezaji kusajili mradi popote alipo na kupata vibali vya uwekezaji ndani ya siku tatu (3) kwa kuzingatia vigezo. Katika kipindi hicho, Mfumo huo uliunganishwa na mifumo ya taasisi saba (7) zinazohusika na utoaji wa vibali ambazo ni: Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; Idara ya Uhamiaji; Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni; Mamlaka ya Mapato Tanzania; na Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

460. Mwaka 2023, Baraza la Taifa la Biashara - TNBC liliratibu Mkutano wa 14 wa Baraza uliofanyika tarehe 9 Juni, 2023 kwa kuwakutanisha wadau wa sekta ya umma na sekta binafsi. Mkutano huo ulilenga kuimarisha mahusiano ya sekta ya umma na binafsi na kujadili mikakati ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Mkutano huo ulioongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara. Mkutano huo uliazimia yafuatayo: taarifa ya utekelezaji wa MKUMBI iwasilishwe na kujadiliwa kila

robo mwaka kupitia Vikao vya Kamati Tendaji ya TNBC; kufanya tathmini na kutoa mapendekezo ya maboresho ya sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya taasisi ili kuondoa vikwazo katika ukuaji wa uwekezaji na biashara nchini; kuwepo Mfumo wa Pamoja wa Malipo kwa Taasisi za Udhibiti (Single Payment System) kwa lengo la kupunguza upotevu wa muda, urasimu na gharama za kufanya biashara nchini; na kuongeza idadi ya Vituo vya Huduma vya Pamoja vya Kidijiti (Digital One-Stop Centres).

461. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inaendelea kutekeleza maazimio hayo ambapo Taarifa ya Utekelezaji wa MKUMBI imeendelea kuwasilishwa TNBC katika kila robo mwaka ikionesha utekelezaji wa masuala ya mbalimbali. Aidha, taarifa hiyo huwasilishwa na kujadiliwa katika kila kikao cha Kamati Tendaji ya TNBC ikiwa ni Maandalizi ya Kikao cha Baraza la Biashara la Taifa ambacho mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

462. Serikali imeendelea na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha inaweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara wote wa ndani na nje ili waweze kufanya biashara bila usumbufu na kulipa kodi stahiki kwa hiari kwa mujibu wa sheria kwa kurekebisha sheria mbalimbali. Aidha, Serikali imeanza kufanyia kazi utumiaji wa mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu za taasisi za udhibiti (Single Window Payment System). Vile vile, Serikali imeendelea kupitia na kurekebisha mifumo ya taasisi ambazo zina sura moja ya utoaji wa huduma za malipo na kuanza kulipa kwa kutumia namba moja ya malipo (control number). Baadhi ya maeneo ambayo yameanza kutumia namba moja ya malipo kwa malipo ni katika biashara za mifugo minadani ambapo taasisi zilizokuwa zinahusika na ukusanyaji mapato yaani Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) na Wizara ya Mifugo kwa kila moja kutoa namba yake ya malipo zinatumia namba moja. Hii imewapunguzia wafanyabiashara usumbufu wa kulipa malipo ya Serikali kwa mamlaka zaidi ya moja.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

463. Mwaka 2023, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi liliratibu na kufuatilia utekelezaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Katika kipindi hicho, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 743.7 ilitolewa kwa wajasiriamali 6,064,957 (wanawake 3,288,186 na wanaume 2,776,771) ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 713.8 iliyotolewa kwa wajasiriamali 2,203,838 mwaka 2022, sawa na ongezeko la mikopo kwa asilimia 4.2. Hii ilitokana na wananchi kukidhi matakwa na masharti ya mikopo yanayotolewa. Jitihada pia zimeendelea kufanywa na Serikali za kuhakikisha riba za mikopo ya mifuko ya uwezeshaji zinapungua ili kuwezesha wananchi walio wengi kukopesheka. Miongoni mwa mifuko hiyo ni Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao riba kwa muda wa mkopo imepungua kutoka asilimia 10 kwa mwaka 2022 hadi kufikia riba ya asilimia tano (5) kwa mwaka 2023.

464. Kati ya kiasi kilichotolewa, mifuko inayotoa mikopo ya moja kwa moja na dhamana ilitoa shilingi bilioni 430.5 kwa wanufaika 932,442 na shilingi bilioni 313.2 zilitolewa kwa wanufaika 5,132,515 kupitia mifuko inayotoa ruzuku. Vile vile, fedha zilizotolewa zilizalisha ajira 7,764,975 (wanawake 4,208,616 na wanaume 3,556,359) mwaka 2023 ikilinganishwa na ajira 3,122,104 zilizozalishwa mwaka 2022. Kati ya ajira zilizotokana na mifuko ya uwezeshaji, ajira 5,500,894 sawa na asilimia 70.8 ni za wanufaika wa ruzuku za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii. Mikopo iliyotolewa mwaka 2023 ilielekezwa zaidi katika shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi kwa asilimia 45.7 ikifuatiwa na shughuli za viwanda na biashara asilimia 15.1 na elimu asilimia 11.8.

**Jedwali Na. 19.5: Mikopo iliyotolewa kwa Shughuli za Kiuchumi Mwaka 2022 - 2023**

| Na. | Sekta | 2022 | | | 2023 | | | Mchango Katika Shughuli za Kiuchumi (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiasi kilichotolewa Shilingi '000 | Marejesho Shilingi '000 | % | Kiasi kilichotolewa Shilingi '000 | Marejesho Shilingi '000 | % | |
| 1 | Afya | 48,510,000 | 35,425,000 | 73.0 | 19,776,201 | 15,456,000 | 78.2 | 2.7 |
| 2 | Elimu | 82,370,000 | 65,718,235 | 79.8 | 87,683,998 | 70,125,500 | 80.0 | 11.8 |
| 3 | Madini | 67,914,000 | 54,219,820 | 79.8 | 54,564,450 | 47,650,000 | 87.3 | 7.3 |
| 4 | Kilimo, mifugo na uvuvi | 221,760,000 | 202,356,000 | 91.3 | 339,875,130 | 216,435,000 | 63.7 | 45.7 |
| 5 | Utalii | 85,336,924 | 69,794,000 | 81.8 | 67,176,945 | 58,210,000 | 86.7 | 9.0 |
| 6 | Viwanda na biashara | 145,530,000 | 128,236,000 | 88.1 | 112,211,356 | 104,301,000 | 93.0 | 15.1 |
| 7 | Nishati | 41,580,000 | 30,959,514 | 74.5 | 43,512,600 | 32,450,000 | 74.6 | 5.9 |
| 8 | Nyinginezo | 20,790,000 | 18,731,000 | 90.1 | 18,859,948 | 14,380,000 | 76.2 | 2.5 |
| **Jumla** | | **713,790,924** | **605,439,569** | 84.8 | **743,660,628** | **559,007,500** | 75.2 | **100** |

**Chanzo:** Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

465. Mwaka 2023, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iliendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na vya Kati - SANVN. Katika kipindi hicho, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.38 ilitolewa katika viwanda 17 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.80 iliyotolewa kwa viwanda 59 mwaka 2022. Aidha, marejesho ya mikopo iliyotolewa yalikuwa na thamani ya shilingi bilioni 1.95 ikilinganishwa na marejesho ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.49 kwa mwaka 2022. Marejesho ya mikopo yanajumuisha kipindi chote cha mpango wa SANVN ulioanza kutekelezwa mwaka 2020.

466. Ajira zilizozalishwa kutokana na utekelezaji wa Mpango zilikuwa 10,308 (wanawake 6,647 na wanaume 3,661) mwaka 2023 ikilinganishwa na ajira 6,887 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 49.7. Hii ilitokana na hamasa ya wanufaika kukidhi vigezo ili kutumia fursa za uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati kupitia Mpango katika shughuli za kiuchumi.

467. Mwaka 2023, Baraza liliratibu utoaji wa mafunzo kwa wajasiriamali 490,199 (wanawake 274,748 na wanaume 215,451) ikilinganishwa na wajasiriamali 431,419 waliopata mafunzo mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 13.6. Hii ilitokana na wananchi wanaojihusisha na shughuli za kiuchumi, hususan wajasiriamali kuhamasika kushiriki katika mafunzo.

468. Hadi Desemba 2023, vituo vya uwezeshaji wananchi vilikuwa 20 kama ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, vituo vya uwezeshaji vilitoa huduma kwa wananchi 40,657 (wanawake 15,903 na wanaume 24,754) mwaka 2023 ikilinganishwa na wananchi 34,441 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 18.0. Ongezeko hilo lilitokana na uelewa wa wananchi kutembelea vituo ili kupata huduma za mafunzo, ushauri wa kibiashara, urasimishaji wa biashara, mikopo, ruzuku na dhamana. Vile vile, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 11.3 ilitolewa kupitia vituo vya uwezeshaji kwa wajasiriamali 5,218 (wanawake 2,237 na wanaume 2,981) mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9.4 zilizotolewa kwa wajasiriamali 4,017 mwaka 2022. Marejesho ya mikopo yalikuwa kiasi cha shilingi bilioni 10.6 sawa na asilimia 93.9 ya mikopo iliyotolewa ikilinganishwa na shilingi bilioni 7.1 sawa na asilimia 75.7 kwa mwaka 2022. Urejeshaji mzuri wa mikopo ulitokana na jitihada za vituo kutembelea miradi ya wanufaika wa mikopo, fursa za mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi wa fedha na utunzaji wa kumbukumbu. Serikali inaendelea kuhimiza wajasiriamali kushiriki kwa wingi katika maonesho ya mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

**Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati**

469. Mwaka 2023, miradi ya kimkakati na uwekezaji katika sekta mbalimbali ilizalisha ajira 162,968 za moja kwa moja ikilinganishwa na ajira 101,353 zilizozalishwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 58.7. Kati ya ajira zilizozalishwa, ajira 156,661 zilikuwa za watanzania na ajira 6,307 za wageni mwaka 2023 ikilinganishwa na ajira 95,831 za watanzania na ajira 5,522 za wageni mwaka 2022. Kuongeza kwa ajira za watanzania kulitokana na juhudi za Serikali kuongeza fursa za ajira kupitia urithishaji wa ujuzi na uhaulishaji wa teknolojia kwa kuhakikisha mikataba inayoingiwa inaweka vipengele vya ushiriki wa watanzania.

470. Mwaka 2023, makandarasi wa miradi ya kimkakati waliingia mikataba na kampuni 3,360 kwa ajili ya kandarasi 1,032, kazi za ushauri elekezi 104 na huduma 2,224 za chakula, ulinzi, usafiri, bima na bidhaa za ujenzi ikilinganishwa na kampuni 2,827 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Aidha, idadi ya wakandarasi wa kitanzania waliosajiliwa walikuwa ni 1,690 na wakandarasi walioingia ubia ni 64 wa kutoa huduma katika miradi ya kimkakati.

**Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

471. Mwaka 2023, Serikali ilipokea na kuchambua miradi 10 inayotarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi - PPP ikilinganishwa na miradi mitano (5) iliyopokelewa na kuchambuliwa mwaka 2022. Hadi Desemba 2023, miradi minne (4) ilikuwa katika hatua za ununuzi wa mbia ikilinganishwa na miradi mitano (5) mwaka 2022. Miradi hiyo ni: Mradi wa barabara ya tozo kutoka Kibaha hadi Chalinze kilometa 78.9; Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Ujenzi wa Kituo cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; na Mradi wa Uendeshaji wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza ambapo Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka ilikuwa katika hatua ya kusaini mkataba na mwekezaji. Aidha, maandiko 72 ya miradi yalikuwa katika hatua mbalimbali za uchambuzi ikilinganishwa na maandiko 57 mwaka 2022.

472. Mwaka 2023, Serikali iliendelea kutoa mafunzo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi na taasisi za fedha kuhusu dhana ya PPP, Sheria ya PPP na Kanuni zake. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wadau 555 mwaka 2023 ikilinganishwa na wadau 247 mwaka 2022. Aidha, mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wadau katika uibuaji, uandaaji, ugharamiaji na utekelezaji wa miradi ya PPP.

**Jedwali Na. 73: KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA: MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA MWAKA 2022 - 2023**

| Sekta | 2022 | | | | | | | | 2023 | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | A | B | C | D | E | F | G | H | A | B | C | D | E | F | G | H |
| Kilimo | 29 | 29 | 0 | 7 | 13 | 9 | 3,199 | 78.4 | 48 | 43 | 5 | 14 | 21 | 13 | 30,718 | 793.1 |
| Mawasiliano | 2 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 85 | 176.9 | 2 | 2 | - | 0 | 1 | 1 | 43 | 28.52 |
| Utalii | 23 | 23 | 0 | 4 | 9 | 10 | 1,109 | 66.3 | 58 | 48 | 10 | 23 | 19 | 16 | 4,103 | 188.648 |
| Uzalishaji Viwandani | 141 | 141 | 0 | 46 | 56 | 39 | 23,341 | 3,277 | 208 | 193 | 15 | 49 | 111 | 48 | 26,563 | 1,688.51 |
| Majengo ya biashara | 14 | 14 | 0 | 9 | 3 | 2 | 772 | 184.2 | 57 | 54 | 3 | 14 | 29 | 14 | 3,596 | 1,054.21 |
| Usafirishaji Mizigo | 58 | 58 | 0 | 28 | 17 | 13 | 9,838 | 647.7 | 111 | 87 | 24 | 66 | 22 | 23 | 18,780 | 1,322.53 |
| Huduma | 13 | 13 | 0 | 1 | 8 | 4 | 1,271 | 28.7 | 20 | 20 | - | 4 | 7 | 9 | 1,832 | 282.66 |
| Rasilimali Watu | 9 | 9 | 0 | 2 | 2 | 5 | 1,038 | 46.4 | 6 | 6 | - | 3 | 1 | 2 | 443 | 7.06 |
| Madini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 6 | 0 | 4 | 0 | 2 | 495 | 47.52 |
| Nishati | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 10 | 3 | 3 | - | 1 | 1 | 1 | 118 | 58.22 |
| Miundombinu ya Kiuchumi | 3 | 3 | 0 | 2 | 1 | 0 | 233 | 22.1 | 7 | 7 | - | 4 | 2 | 1 | 50,319 | 249.38 |
| **Jumla** | **293** | **293** | **0** | **99** | **112** | **82** | **40,889** | **4,537.7** | **526** | **469** | **57** | **182** | **214** | **130** | **137,010** | **5,720.4** |

**Chanzo:** Kituo cha Uwekezaji Tanzania
A Jumla ya Miradi Iliyosajiliwa
B Miradi Mipya
C Miradi ya Maendeleo
D Miradi ya Wazawa
E Miradi ya Wageni
F Miradi ya Ubia
G Jumla ya Ajira
H Jumla ya Thamani ya Uwekezaji (USD Milioni)
- Takwimu Hazikupatikana



## Sehemu ya Nne

# Suala Maalumu Kimaendeleo

## SURA YA 20

## MABORESHO YA MFUMO WA ELIMU WA TANZANIA

**Utangulizi**

473. Elimu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha kuwa Taifa linakuwa na wananchi wenye weledi na uwezo wa kuchangia katika maendeleo ya nchi yao. Mwaka 2015 hadi 2023, sekta ya elimu Tanzania imekuwa ikiongozwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Sera ya Elimu na Mafunzo ni mwongozo unaoainisha mikakati mbalimbali ya kutatua changamoto za sekta ya elimu ili kuhakikisha kuwa elimu na mafunzo yanatolewa kwa ufanisi nchini na hivyo kufikia maendeleo endelevu ya jamii na Taifa kwa ujumla. Aidha, ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia, pamoja na kuongeza ubora wa elimu na mafunzo nchini, Serikali imefanya maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Maboresho hayo yamewezesha kupatikana kwa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023.

474. Sura hii inatoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ikibainisha mafanikio, changamoto na tathmini iliyofanyika kuboresha Sera hiyo. Aidha, Sura hii inabainisha mikakati iliyoanza kutekelezwa ili kuboresha mfumo wa elimu, umuhimu wa kufanya maboresho hayo nchini pamoja na maboresho yatakayoendelea kufanyika kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023.

**Mfumo wa Elimu Kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014**

475. Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ililenga kunyumbua mfumo wa elimu na mafunzo ili utoe fursa za kutosha kwa watu kujielimisha. Aidha, mfumo huo ulilenga kutoa elimu na mafunzo yenye ubora unaokubalika na kutambulika kitaifa, kikanda na kimataifa. Kwa sababu hiyo, mfumo wa elimu ulijielekeza kuandaa rasilimali watu ya kutosha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ajira pamoja na mabadiliko yanayotokea ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia.

476. Muundo wa elimu kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ulikuwa 1+6+4+2+3+ ambao ulilenga kumuwezesha mhitimu kumaliza mzunguko wa masomo kwa muda mfupi. Kupitia muundo huo, elimu ya awali ilipendekezwa kutolewa kwa mwaka mmoja kwa watoto wenye umri wa miaka kati ya mitatu (3) hadi mitano (5) na elimumsingi kwa miaka 10 (miaka sita (6) kwa elimu ya msingi na miaka minne (4) elimu ya sekondari ngazi ya chini). Umri wa kuanza darasa la kwanza ulipendekezwa kuwa miaka minne (4) hadi sita (6) kulingana na maendeleo na uwezo wa mtoto kumudu masomo katika ngazi husika. Aidha, Sera hii ilitilia mkazo kujumuishwa kwa mikondo ya ufundi kwenye elimu ya msingi na sekondari ili wahitimu wapate ujuzi utakaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa pamoja na elimumsingi katika mfumo wa umma kutolewa bila ada.

**Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014**

477. Kwa mujibu wa tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, maoni ya wadau wa elimu yanaonesha kuwa Serikali ilitekeleza mfumo wa elimu ya awali kwa mwaka mmoja kupitia mwongozo unaozitaka shule za msingi za Serikali kuwa na darasa la elimu ya awali na sekta binafsi kuanzisha shule za awali. Aidha, Serikali ilianzisha na kusimamia uendeshaji wa vituo shikizi ili kupunguza umbali ambao watoto wanatembea kutoka mahali wanapoishi kwenda shule mama. Kutokana na jitihada hizo, kiwango cha uandikishwaji wa wanafunzi wa elimu ya awali kiliongezeka na kufikia wanafunzi 1,679,542 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 1,069,823 mwaka 2015. Vile vile, idadi ya wanafunzi waliojiunga na darasa la kwanza iliongezeka na kufikia 1,916,878 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 1,568,378 mwaka 2015.

478. Kutokana na elimu ya msingi na sekondari ngazi ya chini kuwa ya lazima, Serikali iliondoa ada kwa shule za msingi na sekondari kupitia Waraka wa Elimu Na. 3 wa Mwaka 2016. Aidha, Serikali iliondoa ada kwa kidato cha tano na sita katika mfumo wa umma kupitia Waraka wa Elimu Na. 5 wa Mwaka 2022. Utekelezaji wa afua hizo uliwezesha kiwango cha wanafunzi walioandikishwa katika elimu ya msingi kuongezeka na kufikia 5,616,919 mwaka 2023 ikilinganishwa na wanafunzi 4,265,714 mwaka 2016. Vile vile, idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika elimu ya sekondari ngazi ya chini iliongezeka na kufikia wanafunzi 2,881,335 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 1,675,593 mwaka 2016 **(Jedwali Na. 20.1).** Hii ni sawa na kiwango cha uandikishwaji wa wanafunzi wa rika lengwa cha asilimia 98.2 na asilimia 52.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 93.5 na asilimia 42.6 mwaka 2016 kwa shule za msingi na sekondari ngazi ya chini mtawalia **(Jedwali Na. 20.2).**

**Jedwali Na. 20.1: Idadi ya Wanafunzi Walioandikishwa Mwaka 2016 - 2023**

| Mwaka | Shule za Msingi | | | Sekondari Ngazi ya Chini | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana | Wasichana | Jumla | Wavulana | Wasichana | Jumla |
| 2016 | 4,265,714 | 4,373,488 | 8,639,202 | 824,767 | 850,826 | 1,675,593 |
| 2017 | 4,629,215 | 4,688,576 | 9,317,791 | 863,718 | 904,172 | 1,767,890 |
| 2018 | 5,046,571 | 5,065,100 | 10,111,671 | 965,305 | 1,025,714 | 1,991,019 |
| 2019 | 5,300,782 | 5,304,648 | 10,605,430 | 1,045,441 | 1,139,596 | 2,185,037 |
| 2020 | 5,443,914 | 5,481,982 | 10,925,896 | 1,103,810 | 1,218,449 | 2,322,259 |
| 2021 | 5,557,707 | 5,639,081 | 11,196,788 | 1,192,225 | 1,319,319 | 2,511,544 |
| 2022 | 5,636,996 | 5,783,977 | 11,420,973 | 1,248,118 | 1,396,997 | 2,645,115 |
| 2023 | 5,616,919 | 5,808,563 | 11,425,482 | 1,361,152 | 1,520,183 | 2,881,335 |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI


**Jedwali Na. 20.2: Uandikishaji wa Wanafunzi, Mwaka 2016 - 2023 (Asilimia)**

| | Shule za Msingi | | | Sekondari Ngazi ya Chini | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Jumla** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Jumla** |
| 2016 | 92.4 | 94.5 | 93.5 | 41.9 | 43.3 | 42.6 |
| 2017 | 96.4 | 97.4 | 96.9 | 40.8 | 41.8 | 41.3 |
| 2018 | 104.9 | 106 | 105.4 | 42.7 | 44.6 | 43.7 |
| 2019 | 110.1 | 110.5 | 110.3 | 42.1 | 45.7 | 43.9 |
| 2020 | 109.9 | 111.2 | 110.6 | 43.8 | 48.1 | 46 |
| 2021 | 108.6 | 110.7 | 109.7 | 45 | 49.9 | 47.4 |
| 2022 | 106.7 | 110.4 | 108.5 | 45.3 | 51.2 | 48.2 |
| 2023 | 96.6 | 99.8 | 98.2 | 49.7 | 55.8 | 52.7 |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI


479. Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,356,392 walifanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba mwaka 2023 ikilinganishwa na watahiniwa 844,938 mwaka 2013. Hii ilichangiwa na utolewaji wa elimumsingi bila ada pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu nchini. Aidha, watahiniwa waliofaulu mtihani wa kuhitimu darasa la saba walikuwa 1,073,402 mwaka 2023 ikilinganishwa na watahiniwa 427,606 mwaka 2013. Vile vile, watahiniwa wa darasa la saba waliojiunga na kidato cha kwanza walikuwa 1,019,879 mwaka 2022 ikilinganishwa na watahiniwa 439,626 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 132.0. Kwa ujumla katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2023, tofauti kati ya watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba na wahitimu waliojiunga na kidato cha kwanza imekuwa ikipungua. Hata hivyo, katika kipindi hicho cha mapitio, wastani wa wahitimu 274,140 hawakupata fursa ya kujiunga na kidato cha kwanza. **Kielelezo Na. 20.1)**.

**Kielelezo Na. 20.1: Mwenendo wa Wahitimu wa Shule za Msingi Mwaka 2009 - 2022**




480. Watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne waliongezeka na kufikia 529,596 mwaka 2023 ikilinganishwa na watahiniwa 352,614 mwaka 2013. Aidha, watahiniwa waliofaulu mtihani wa kuhitimu kidato cha nne waliongezeka na kufikia 471,427 mwaka 2023 ikilinganishwa na watahiniwa 235,227 mwaka 2013. Vile vile, watahiniwa wa kidato cha nne waliojiunga na kidato cha tano walikuwa 102,722 mwaka 2021 ikilinganishwa na watahiniwa 39,173 mwaka 2013 (**Kielelezo Na. 20.2)**. Kwa ujumla, ikilinganishwa na mwaka 2013 tofauti kati ya watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne na wahitimu waliojiunga na kidato cha tano ilipungua. Hata hivyo, wastani wa wahitimu 298,604 hawakupata fursa ya kujiunga na kidato cha tano katika kipindi cha mapitio. Tofauti ya kiwango cha wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza ni kubwa ikilinganishwa na kiwango cha wanafunzi wanaojiunga na kidato cha tano (**Kielelezo Na. 20.3**). Kutokana na tofauti hiyo, kuna umuhimu wa kuwajengea wanafunzi ujuzi stahiki kwa ajili ya soko la ajira kwa kuweka kipaumbele katika stadi za amali.

**Kielelezo Na. 20.2: Mwenendo wa Wahitimu katika Ngazi ya Sekondari ya Chini Mwaka 2009 - 2022**




| | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Waliojiunga na kidato cha tano | 39,173 | 42,484 | 66,090 | 77,895 | 76,254 | 78,272 | 84,261 | 96,651 | 102,722 | |
| Waliofanya mtihani wa kidato cha nne | 352,614 | 240,410 | 384,300 | 349,524 | 317,777 | 360,510 | 422,722 | 435,654 | 487,730 | 522,217 |
| Waliofaulu | 235,227 | 167,643 | 240,996 | 244,762 | 245,274 | 284,126 | 340,914 | 373,958 | 422,388 | 456,975 |

**Kielelezo Na. 20.3: Mlinganisho wa Kiwango cha Wanafunzi Wanaojiunga na Kidato cha Kwanza na Kidato cha Tano (Asilimia), Mwaka 2009 - 2021[2]**




481. Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika shule za msingi ulikuwa 1:57 mwaka 2023 ikilinganishwa na uwiano wa 1:42 mwaka 2016. Kwa upande wa shule za Serikali, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi ulikuwa 1:61 mwaka 2023 ikilinganishwa na uwiano wa 1:43 mwaka 2016 (**Kielelezo Na. 20.4**). Uwiano huu unaweza kuwa ulichangiwa na sera ya elimumsingi bila ada iliyosababisha ongezeko kubwa la wanafunzi katika shule za msingi. Aidha, uwiano huo umezidi kiwango cha 1:45 kinachokubalika kitaifa. Kutokana na hilo, Serikali inaendelea na juhudi za kuajiri walimu ili kuhakikisha uwiano sahihi wa mwalimu kwa wanafunzi.

[2] Asilimia ya wanafunzi waliojiunga na kidato cha kwanza (I) pamoja na asilimia ya wanafunzi waliojiunga na kidato cha tano (V). Huu ni uwiano wa wanafunzi walioandikishwa kidato cha kwanza (I) kwa wanafunzi walioandikishwa darasa la saba (7) pamoja na uwiano wa wanafunzi walioandikishwa kidato cha tano (V) kwa wanafunzi walioandikishwa kidato cha nne (IV) (transition rate to form I and form V).

**Kielelezo Na. 20.4: Uwiano wa Mwalimu kwa Wanafunzi katika Shule za Msingi Mwaka 2016 - 2023**





482. Kwa Mujibu wa taarifa kutoka katika Mfumo wa kukusanya, kuchambua na kutoa taarifa ya takwimu za Elimu Msingi (Basic Education Management Information System - BEMIS), katika kipindi cha Machi 2021 hadi Machi 2022, jumla ya wanafunzi 206,600 wa shule za msingi (wavulana 119,442 na wasichana 85,158), sawa na asilimia 0.018 ya wanafunzi 11,196,788 waliokuwepo shuleni mwaka 2021 walikatiza masomo kwa sababu mbalimbali. Aidha, jumla ya wanafunzi 130,647 wa shule za sekondari (wavulana 68,355 na wasichana 62,292), sawa na asilimia 0.049 ya wanafunzi 2,671,927 waliokuwepo shuleni mwaka 2021 walikatiza masomo katika kipindi hicho. Vile vile, taarifa ya BEMIS inaonesha kuwa katika kipindi cha Machi 2022 hadi Machi 2023, jumla ya wanafunzi 193,605 wa shule za msingi (wavulana 112,366 na wasichana 811,239), sawa na asilimia 0.017 ya wanafunzi 11,420973 waliokuwepo shuleni mwaka 2022 walikatiza masomo. Kwa upande mwingine, jumla ya wanafunzi 136,313 wa shule za sekondari (wavulana 69,847 na wasichana 66,466), sawa na asilimia 0.048 ya wanafunzi 2,823,588 waliokuwepo shuleni mwaka 2022 walikatiza masomo yao. Kukatiza masomo kwa wanafunzi hao kulichangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo: hali ya umaskini iliyosababisha familia zao kushindwa kikidhi mahitaji ya shule; majanga ya asili kama vile ukame, mafuriko yaliyoathri upatikanaji wa huduma za msingi; ajira za utotoni hususan maeneo ya migodini, mashamba makubwa, maeneo ya uvuvi na sehemu za masoko; kukosekana kwa mazingira rafiki ya ufundishaji na kujifunzia; na kutokuwepo kwa mazingira wezeshi ya uendelezaji wa vipaji au vipawa vya wanafunzi.

483. Katika kukabiliana na changamoto hizo Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi ikiwemo kuboresha miundombinu kwa kuongeza idadi ya shule na kuajiri walimu wenye sifa na pamoja na kutekeleza sera ya elimumsingi bila ada. Kutokana na hilo, kiwango cha wanafunzi wanaoacha shule


kilipungua na kufikia asilimia 1.7 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.9 mwaka 2013 (**Kielelezo Na. 20.5)**. Hii ilichangiwa na kupungua kwa utoro, mimba za utotoni, mila potofu, pamoja na kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Kupungua kwa wanafunzi wanaoacha shule kunaenda sambamba na kuongezeka kwa kiwango cha wanafunzi wanaomaliza shule na kuongeza wastani wa muda unaotarajiwa kwa mwanafunzi kuwa shuleni, hivyo kuimarika kwa maendeleo ya watu.

**Kielelezo Na. 20.5: Kiwango cha Kuacha Shule katika Shule za Msingi Mwaka 2011 - 2022**




484. Wanafunzi wa shule ya msingi waliorudia madarasa katika shule za Serikali na zisizo za Serikali walikuwa 399,511 mwaka 2023 ikilinganishwa na wanafunzi 55,302 mwaka 2013(Kielelezo Na. 20.6). Ongezeko hilo linatokana na ufaulu usioridhisha unaoweza kuwa ulichangiwa na uwiano mkubwa kati ya mwalimu na wanafunzi, hususan katika shule za msingi za Serikali. Kwa upande wa elimu ya sekondari, wanafunzi waliorudia darasa walikuwa 52,274 mwaka 2023 ikilinganishwa na wanafunzi 85,057 mwaka 2013, sawa na upungufu wa asilimia 38.5.

**Kielelezo Na 20.6: Wanafunzi Wanaorudia Darasa katika Shule za Msingi Mwaka 2012 - 2023**




**Jedwali Na 20.4: Wanafunzi Wanaorudia Darasa katika Sekondari Ngazi ya Chini Mwaka 2012 - 2023**

| Mwaka | Shule za Serikali | Shule Zisizo za Serikali | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2012 | 20,117 | 4,833 | 24,950 |
| 2013 | 77,798 | 7,259 | 85,057 |
| 2014 | 23,512 | 2,475 | 25,987 |
| 2015 | - | - | - |
| 2016 | 24,203 | 2,825 | 27,028 |
| 2017 | 21,908 | 2,415 | 24,323 |
| 2018 | 26,125 | 2,393 | 28,518 |
| 2019 | 26,637 | 2,237 | 28,874 |
| 2020 | 29,742 | 1,916 | 31,658 |
| 2021 | 29,966 | 2,124 | 32,090 |
| 2022 | 27,157 | 1,805 | 28,962 |
| 2023 | 50,166 | 2,108 | 52,274 |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI

- Takwimu hazikupatikana

**Utofauti wa Idadi ya Wahitimu na Fursa za Ajira**

485. Kwa mujibu wa utafiti wa REPOA wa mwaka 2019, wahitimu kati ya 800,000 na 1,000,000 huingia katika soko la ajira kila mwaka. Hata hivyo, kwa wastani uchumi wa Tanzania unaweza kutengeneza ajira 250,000 kwa mwaka na wahitimu wengi hutumia muda wa wastani wa miaka 5.5 kupata ajira[3]. Aidha kulingana na takwimu za elimu, wastani wa wahitimu 274,140 hawajapata fursa ya kujiunga na kidato cha kwanza, na wastani wa wahitimu 298,604 hawajapata fursa ya kujiunga na kidato cha tano. Vile vile, wastani wa wanafunzi 171,851 wa shule za msingi na wanafunzi 97,436 wa sekondari ngazi ya chini waliacha shule katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2022. Hivyo, kwa makadirio zaidi ya wanafunzi 800,000 huingia katika soko la ajira kila mwaka Kwa upande mwingine, kulingana na takwimu za ajira katika sekta rasmi zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kulikuwa na ajira mpya 308,951 mwaka 2016 ikilinganishwa na ajira mpya 414,795 mwaka 2017. Hii inaashiria kuwa kuna utofauti mkubwa kati ya uwezo wa uchumi kutoa ajira na idadi ya wahitimu wanaoingia katika soko la ajira. Kutokana na hilo, kipaumbele cha Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023 cha kuwajengea wanafunzi ujuzi stahiki kwa ajili ya soko la ajira kwa kuweka stadi za amali katika kila ngazi ya elimu kunaweza kupunguza tofauti kati ya utoaji wa ajira na idadi ya wahitimu.

486. Pamoja na mafanikio katika viashiria vingi vya elimu, utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ulikuwa na mapungufu yafuatayo: baadhi ya maeneo ya Sera kukosa ufafanuzi wa kutosha hivyo kutoa mwanya wa tafsiri tofauti katika baadhi ya maeneo ya msingi, kama vile, muundo wa elimu, lugha ya kufundishia na kutokuwa na umri mahsusi wa kuanza elimu ya awali na elimu ya msingi; baadhi ya maeneo ya Sera kutotekelezwa mathalan, kuendelea kutumika kwa muundo wa elimu wa 2+7+4+2+3+ badala ya 1+6+4+2+3+ ambapo elimu ya msingi imeendelea kuwa ya miaka saba (7) badala ya miaka sita (6) iliyokusudiwa na Sera; elimu ya lazima imeendelea kuwa ya miaka saba (7) badala ya miaka 10 iliyokusudiwa na Sera; kutokuwepo kwa sheria ya elimumsingi na sekondari; kukosekana kwa utaratibu wa kuwezesha maendeleo ya wanafunzi wenye vipaji, vipawa na mahitaji maalum; kukosekana kwa utaratibu na utambuzi wa maarifa, ujuzi, na stadi zinazopatikana nje ya mfumo wa shule; na baadhi ya maeneo muhimu kutozingatiwa

[3] REPOA, 2019. *Does obtaining a lot of schooling guarantee a quick transition to employment? Evidence from TVET graduates in Tanzania*

kwenye Sera kama vile, malengo ya jumla ya elimu na malengo kwa kila ngazi ya elimu na mafunzo.

**Changamoto za Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014**

487. Utekelezaji wa Sera ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo:

i. Mfumo wa elimu na mafunzo kutotoa fursa kulingana na uwezo, vipaji na vipawa. Mfumo umetawaliwa na muundo wa kitaaluma wenye dhana ya kuchuja wahitimu ili kupata wachache wenye uwezo mkubwa na watakaosoma hadi kumaliza chuo kikuu. Hali hii inatokana na nafasi za elimu na mafunzo ngazi za juu kuwa chache.

ii. Mfumo kutokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia na hivyo, kutoa wahitimu ambao hawana umahiri wa kutosha kuhimili ushindani katika ulimwengu wa soko la ajira;

iii. Mfumo usio fanisi wa udhibiti na ithibati ya elimu na mafunzo katika ngazi zote;

iv. Upungufu wa nguvukazi ya kutosha yenye maarifa, stadi na ujuzi unaohitajika kwa ajili ya sekta mbalimbali;

v. Mfumo usio na ufanisi wa usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo;

vi. Mfumo usio wa uhakika na endelevu wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo wenye vyanzo anuai na endelevu; na

vii. Kutozingatiwa kwa masuala yanayoibuka ambayo yanaathiri utoaji wa elimu na mafunzo.

**Malengo na Mahitaji ya Kuboresha Sera ya Elimu**

488. Moja ya malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo ya Taifa 2011/12 - 2024/25 ni kuhakikisha kuwa kuna maendeleo ya haraka ya rasilimali watu ili kuchochea maendeleo na kuiwezesha Tanzania kuingia uchumi wa kati na shindani ifikapo mwaka 2025. Malengo hayo yatafikiwa kwa kutayarisha idadi ya kutosha ya watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi. Kwa muktadha huo, kuna umuhimu wa kufanya maboresho ya mfumo wa elimu ili kuchochea utekelezaji wa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

**Malengo ya Kuboresha Sera ya Elimu na Mafunzo 2014**

489. Sera imejielekeza katika kuwajengea wanafunzi ujuzi stahiki kwa ajili ya soko la ajira kwa kuweka kipaumbele katika stadi za amali kwa kila ngazi ya elimu. Aidha, lengo la kuboresha Sera linatokana na hitaji la nchi kuwa na mfumo wa elimu na mafunzo wenye kumuandaa mtanzania mwenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaomuwezesha kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

**Mahitaji ya Kuboresha Sera ya Elimu 2014**

490. Msukumo wa kuboresha Sera ya Elimu 2014 ulitokana na masuala yafuatayo:

i. **Maoni ya wadau mbalimbali wa Elimu:** Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, wadau wa elimu walitoa maoni mbalimbali kuhusu utoshelevu na uhalisia wa maudhui katika mitaala ya ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Hoja kubwa za wadau wa elimu ni kuwa Sera haina utoshelevu stahiki kukidhi mahitaji ya utoaji wa elimu na mafunzo kwa sasa na siku zijazo. Aidha, maudhui ya mitaala hayajakidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia.

ii. **Matokeo ya Tafiti:** Matokeo ya tafiti mbalimbali yalithibitisha maoni ya wadau kuhusu umuhimu wa kuboresha Sera ya Elimu ili kuipa utoshelevu stahiki na kuiwezesha kukidhi mahitaji ya jamii kwa sasa na siku zijazo. Aidha, Tume ya Mipango ilifanya Utafiti wa Hali ya Soko la Ajira Mwaka 2014 kwa lengo la kubaini maendeleo ya ujuzi utakaoiwezesha Tanzania kuwa na uchumi imara na shindani ifikapo mwaka 2025. Utafiti huo ulibainisha umuhimu wa kutatua changamoto ya utofauti kati ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira na ujuzi unaotolewa na taasisi za elimu na mafunzo. Vile vile, utafiti ulibaini kuwa viwango vya ujuzi vya watafuta ajira viko chini ya viwango vinavyohitajika katika soko la ajira. Kwa upande mwingine, tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ilibaini changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya elimu zinazohitaji kutatuliwa kwa kuwa na mwelekeo mpya wa kisera na mikakati mipya.

iii. **Hitaji la Kujumuisha Mabadiliko Yaliyojitokeza Katika Kipindi cha Utekelezaji wa Sera:** Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, mabadiliko mengi yalitokea katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kiteknolojia na kijamii ndani na nje ya nchi. Mabadiliko hayo, hayakujumuishwa katika mfumo wa elimu na mafunzo wa zamani, na kusababisha changamoto mpya za kielimu ambazo zinahitaji mwelekeo mpya wa sera ili kuzitatua.

iv. **Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:** Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 mjini Dodoma alisema: "*Tutajielekeza katika kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na kufanya marekebisho kwenye mitaala iliyopo ili ijielekeze kwenye kutoa elimu ujuzi kulingana na mazingira ya nchi na soko la ajira*". Mwisho wa kunukuu.

**Maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014**

491. Maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo yamejielekeza katika kuboresha mfumo wa elimu, kuwianisha elimu na mahitaji ya soko la ajira, pamoja na kuchochea uvumbuzi na

uhawilishaji wa teknolojia ili kuhakikisha kuwa Taifa linapata rasilimali watu yenye ujuzi stahiki na toshelevu kwa mahitaji ya maendeleo ya nchi. Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 yamewezesha kupatikana kwa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023. Toleo jipya la Sera limejielekeza katika kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya elimu kwa kufanya maboresho ya kisera yafuatayo:

i. **Mfumo na Muundo wa Elimu na Mafunzo**

Serikali imewezesha upatikanaji wa fursa ya elimu kwa watoto wa jinsi zote kwa kuandikisha kiwango kikubwa cha wanafunzi katika elimu ya msingi. Hata hivyo, elimu baada ya elimu ya msingi imeendelea kuwa na changamoto mbalimbali ikiwemo mfumo uliopo kutegemea zaidi utaratibu wa kuchuja wanafunzi kwa ajili ya kuendelea na masomo, badala ya kutoa fursa ya kuwaendeleza kadiri ya uwezo, vipaji na vipawa vyao. Aidha, mfumo uliopo hautoi fursa anuai za elimu na mafunzo ambazo zinaweza kumfanya kila anayehitimu kupata ujuzi na maarifa kwa ajili ya ulimwengu wa kazi kulingana na uwezo, matakwa na malengo yake utakaomsaidia pindi anaposhindwa kuendelea kitaaluma na kuchaguliwa kujiunga na elimu ya mafunzo ya amali. Katika muktadha huo, maboresho ya mfumo wa elimu yamejikita katika kuweka utaratibu wa kubaini na kuendeleza wanafunzi wenye vipaji na vipawa mbalimbali, pamoja na kuweka mfumo nyumbufu wa elimu na mafunzo utakaowezesha wananchi wengi zaidi kujielimisha na kuwa huru kutafuta elimu katika fani wanayopenda.

Maboresho mengine yalifanyika katika muundo wa mfumo rasmi wa elimu na mafunzo na kuwa 1+6+4+2/3+3+, ikimaanisha mwaka mmoja (1) wa elimu ya awali, miaka sita (6) ya elimu ya msingi, miaka minne (4) ya elimu ya sekondari ngazi ya chini, miaka miwili (2) ya elimu ya sekondari ngazi ya juu au miaka mitatu (3) ya amali sanifu, na miaka isiyopungua mitatu (3) ya elimu ya juu. Aidha, katika maboresho hayo, umri wa kuanza elimu ya awali utakuwa miaka mitano (5), umri wa kuanza darasa la kwanza kuwa miaka sita (6), elimu ya lazima kuwa miaka 10, ikijumuisha elimu ya msingi ya miaka sita (6) na elimu ya sekondari ya chini ambayo itatolewa kwa miaka minne (4). Vile vile, elimu ya sekondari kugawanyika katika mikondo miwili (2) ambayo ni mkondo wa elimu jumla na mkondo wa elimu ya amali. Elimu ya amali itatolewa kuanzia kidato cha kwanza kwa lengo la kuwapatia wahitimu ujuzi stahiki na kuwajengea uwezo wa kuhimili ushindani katika ulimwengu wa kazi.

ii. **Ubora wa Elimu na Mafunzo**

Katika kuboresha mfumo wa elimu nchini, yafuatayo yatatekelezwa: elimu ya ualimu itaanza kutolewa kwa wahitimu waliomaliza kidato cha sita (6) na kuendelea; mafunzo ya ualimu yatakuwa na mwendelezo wa kitaaluma na kitaalamu kati ya ngazi moja na nyingine; mafunzo ya ualimu yatajumuisha mwaka mmoja wa mafunzo chini ya uangalizi baada ya kuhitimu mafunzo tarajali; somo la historia ya

Tanzania na maadili litaanzishwa na kufundishwa kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi chuo kikuu kwa lugha ya Kiswahili ili kujenga na kuendeleza maadili, mila, desturi na utamaduni wa mtanzania; mitaala ya elimu na mafunzo itaboreshwa ili kukidhi mahitaji ya ulimwengu wa kazi na kuhimili ushindani; utaratibu wa uwili katika utoaji wa elimu na mafunzo kwa kushirikiana na viwanda, mashamba na sekta nyingine za uzalishaji na utoaji huduma utaimarishwa; na Serikali itaboresha mfumo wa ajira ya walimu wakufunzi, na wahadhiri kwa kuhakikisha kuwa wenye sifa na viwango stahiki wanaajiriwa baada ya kufanya mitihani na kufaulu kama sehemu ya usaili.

**iii. Elimu ya Sayansi na Teknolojia**

Elimu ya sayansi na teknolojia ni muhimu katika kumwezesha mwananchi kumudu mazingira yake na kuchangia katika maendeleo ya Taifa. Kwa muktadha huo, mfumo wa elimu umefanyiwa maboresho kwa kufanya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kufundishwa kama somo katika ngazi zote kuanzia elimu ya awali. Aidha, matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa elimu na mafunzo yataimarishwa katika ngazi zote kulingana na mahitaji.

**iv. Matumizi ya Lugha katika Mawasiliano na Lugha ya Kufundishia**

Ubora wa elimu na mafunzo kwa kiasi kikubwa unategemea uelewa wa lugha kwa walimu na wanafunzi katika kufikisha na kupokea maarifa. Lugha za kiswahili na kiingereza, na lugha nyingine za kigeni zinafundishwa kama masomo katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Aidha, Lugha ya Alama Tanzania (LAT), Lugha ya Alama Mguso na Maandishi ya Breli ni masomo yanayofundishwa katika vyuo vya ualimu.

Kwa kutambua umuhimu wa lugha, Serikali iliendelea kuboresha ufundishaji wa masomo ya lugha katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Pamoja na juhudi hizo, bado kuna changamoto ya mawasiliano inayotokana na uelewa mdogo wa lugha. Sehemu kubwa ya changamoto hizo inatokana na mbinu duni, miundombinu na vifaa hafifu vya kufundishia na kujifunzia, ukosefu wa walimu mahiri wa lugha na matumizi madogo ya lugha za kigeni katika mazingira ya kawaida. Katika kuimarisha matumizi ya lugha mbalimbali katika mawasiliano, Serikali itaimarisha ufundishaji wa programu za lugha ambapo lugha ya kiswahili, kiingereza na nyingine za kigeni zitafundishwa kwa ufasaha na ufanisi. Aidha, lugha ya kiswahili itatumika kufundishia ngazi ya awali na msingi, isipokuwa kwa shule zitakazoruhusiwa kutumia kiingereza. Vile vile, lugha ya kiingereza itatumika kufundishia kuanzia elimu ya sekondari hadi chuo kikuu, isipokuwa kwa shule na vyuo vitakavyoruhusiwa kutumia lugha ya kiswahili.

v. **Maboresho Mengine**

Maboresho mengine yaliyofanyika katika mfumo wa elimu nchini ni: kutolewa kwa elimu bila ada katika shule za umma kuanzia ngazi ya awali hadi kidato cha sita; kufutwa kwa mtihani wa darasa la saba, ambapo wanafunzi watafanya mtihani wa upimaji wa kitaifa wa darasa la sita; kuimarishwa kwa utoaji wa mafunzo kazini kwa walimu, wakufunzi na wahadhiri; kuwekwa kwa utaratibu wa kuongeza ushindani wa taasisi za elimu ya juu kwa kuwavutia na kuwabakiza wahadhiri wenye hadhi ya kimataifa kwa kuzingatia uwezo wao katika utafiti, machapisho na huduma za kitaalamu; na kuimarishwa kwa utafiti wa kielimu ili kuwezesha maamuzi muhimu katika sekta kufanyika kwa kuzingatia matokeo ya tafiti.

**Hatua za Utekelezaji wa Maboresho ya Mfumo wa Elimu**

492. Katika kuhakikisha Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023 inatekelezwa kwa ufanisi, Serikali imechukua hatua mbalimbali kuandaa mazingira stahiki ya utekelezaji wa mfumo mpya wa elimu ikiwemo: kuandaa mitaala kuendana na soko la ajira kwa kukamilisha maboresho ya mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari, na elimu ya ualimu; kuandaa na kusambaza vitabu vya elimu ya awali, darasa la kwanza na la tatu kwa kuzingatia mtaala mpya; kuandaa na kusambaza vitabu (moduli) kwa ajili ya utoaji wa elimu ya amali kwa shule za sekondari zilizoidhinishwa kuanza kutoa mafunzo hayo; kutoa mafunzo kwa wasimamizi na walimu kuhusu mtaala mpya; na kuanza utekelezaji wa mtaala mpya kwa ngazi ya awali, darasa la kwanza na la tatu.

493. Katika ngazi ya sekondari ya chini, mafunzo ya amali yameanza kutolewa kwa shule 96 zilizopewa idhini ya kutoa mafunzo hayo kwa kidato cha kwanza. Aidha, Serikali inapanga kuandaa Mwongozo wa Mfumo Mpya wa Elimu kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa pamoja na kuendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 ili iendane na mwelekeo wa Sera. Hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na: kuendelea kuhuisha Mfumo wa Tuzo wa Taifa ili uendane na mabadiliko ya Sera; kuendelea kufanya mapitio ya mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi ya vyuo vya kati na elimu ya juu ili iendane na mwelekeo wa Sera na soko la ajira; kuendelea na ujenzi/ukarabati wa miundombinu ya madarasa na karakana katika shule za sekondari zilizoidhinishwa kutoa elimu ya amali; kuendelea kuwezesha upatikanaji wa vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia ikiwemo, vifaa vya karakana katika shule 96 za mkondo wa elimu ya amali; na kuendelea na ujenzi wa shule za sekondari za amali 26 za mikoa kwa ajili ya wasichana.

**Utaratibu wa Utekelezaji wa Maboresho ya Mfumo wa Elimu**

494. Utekelezaji wa maboresho ya mfumo wa elimu utafanyika kwa awamu kwa kuzingatia mipango na mahitaji ya kibajeti. Mathalan, utelekezaji wa sera ya elimu ya lazima kwa ngazi ya sekondari ya chini utaanza mwaka 2027. Utekelezaji wa mtaala

ulioboreshwa umeanza kwa elimu ya awali, darasa la kwanza na la tatu. Kwa ngazi ya sekondari ya chini, utekelezaji wa mtaala mpya umeanza kwa mkondo wa elimu ya amali kwenye shule 96 (28 za Serikali na 68 zisizo za Serikali). Shule hizi zimeidhinishwa kwa awamu ya kwanza ya majaribio kabla ya utekelezaji kamili kuanza. Aidha, Serikali imezifanyia maboresho shule 28 kwa kufanya ukarabati wa miundombinu ya madarasa, ujenzi wa karakana na kuzipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia michepuo ya fani zitakazofundishwa. Vile vile, Serikali imeajiri walimu wa fani za amali kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo ya amali yanatolewa kwa ufanisi. Katika ngazi ya sekondari ya juu, utekelezaji wa mtaala mpya utaanza kwa kidato cha tano na mafunzo ya ualimu yataanza kwa walio mwaka wa kwanza.

**Umuhimu wa Maboresho ya Mfumo wa Elimu katika Kujenga Nchi**

495. Maboresho ya mfumo wa elimu yana mchango mkubwa katika kuhakikisha malengo na mipango ya nchi inafikiwa. Manufaa tarajiwa ya maboresho ya mfumo wa elimu ni pamoja na:

i. **Kuchochea ukuaji wa uchumi na jamii nchini:** Maboresho ya mfumo wa elimu yamejielekeza katika kuongeza uwiano wa rasilimali watu mahiri. Maendeleo hayo ya rasilimali watu ni muhimu katika kuliletea Taifa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii na kuliweka kwenye uchumi shindani hasa katika soko la ajira ndani na nje ya nchi;

ii. **Kukuza hali ya maisha ya watu na kupunguza utofauti wa kipato:** Maboresho ya mfumo yamejielekeza katika kuongeza fursa za elimu kwa watanzania kwa kuzingatia uwezo, vipawa na vipaji, pamoja na kuwapatia wahitimu ujuzi stahiki ili waweze kujiajiri na kuhimili ushindani katika soko la ajira. Hii inatokana na kuwa maboresho ya mfumo wa elimu yanahusisha kuanzishwa kwa stadi za amali ili kuwajengea wahitimu uwezo wa kujitegemea kwa kujiajiri au kuajiriwa na hatimaye kuongeza kipato;

iii. **Kuiwezesha Tanzania kushindana katika soko la ajira duniani:** Maboresho ya mfumo wa elimu yanalenga kutoa elimu na mafunzo yanayotambulika kikanda na kimataifa na yanayokidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa. Maboresho hayo yatawezesha kufanyika kwa mapitio ya mitaala ya elimu na mafunzo na kuiboresha kulingana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisayansi ili ikidhi mahitaji ya ulimwengu wa kazi. Mitaala hiyo itawajengea wahitimu uwezo wa kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi;

iv. **Kukuza teknolojia nchini:** Mfumo unatoa fursa ya matumizi ya TEHAMA katika elimu na mafunzo. TEHAMA itafundishwa kama somo katika ngazi zote kuanzia elimu ya awali. Aidha, matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa elimu na mafunzo yataimarishwa kulingana na mahitaji katika ngazi zote. Vile vile, maboresho ya

mfumo yamejielekeza katika kuongeza wigo wa wananchi walioelimika katika sayansi, hisabati na teknolojia na wanaomudu kuitumia katika kuboresha maisha yao ya kila siku; na

v. **Kukuza na kulea vipaji kuanzia ngazi za awali:** Maboresho ya mfumo yanalenga katika kukuza na kulea vipaji kuanzia ngazi ya awali. Uendelezaji wa vipaji na vipawa unachangia katika kujenga Taifa kwa njia mbalimbali, ikiwemo: kuimarisha nidhamu, amani na mshikamano; kukuza ukakamavu, ujasiri na kujiamini; kuongeza kipato cha wananchi; na kulitambulisha Taifa nje ya mipaka.

**Hitimisho**

496. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, hali ya utoaji wa elimu nchini haijafikia kiwango kilichokusudiwa. Kutokana na hilo, maboresho ya mfumo wa elimu yanalenga katika kutatua changamoto mbalimbali ikiwemo: mfumo wa elimu kujikita zaidi kwenye elimu ya jumla na kukosa fursa anuai za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji; mitaala katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kutokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia; upungufu wa nguvukazi ya kutosha yenye maarifa, stadi na ujuzi unaohitajika kwa ajili ya sekta mbalimbali; mfumo usio wa uhakika na endelevu wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo wenye vyanzo anuai na endelevu; na kutozingatiwa kwa masuala yanayoibuka ambayo yanaathiri utoaji wa elimu na mafunzo.


497. Maboresho hayo ni muhimu kwani yatawezesha nchi kufikia malengo ambayo imejiwekea katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, mipango na mikakati ya maendeleo, pamoja na kuendana na mabadiliko ya ulimwengu, hususan katika uchumi, sayansi na teknolojia. Maboresho hayo yataiwezesha nchi kufikia malengo yanayohusu elimu katika Ajenda 2030 na kufikia maendeleo endelevu. Hivyo, ni muhimu kwa wadau wote wa sekta binafsi na Serikali kushirikiana katika kutekeleza maboresho yaliyofanyika katika mfumo wa elimu ili kuwezesha malengo tarajiwa kufikiwa.



Uzinduzi: “Jambo letu la SGR kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma linaenda kuanza”



Ujazaji wa maji katika Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere




Idadi ya Watalii waliotembelea hifadhi za Taifa nchini kwa Mwaka 2023


**Wizara ya Fedha**
**Mji wa Serikali - Mtumba**
**S.L.P 2802**
**Dodoma**
**http://www.mof.go.tz**